# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 3 Mei, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, Kikao cha Ishirini na Moja. Naomba niwasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**WABUNGE FULANI:** Kazi iendelee!

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**
Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omar Kipanga. Nakushukuru sana.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama,Kamati nyeti. Karibu Mheshimiwa kwa niaba ya Kamati.

**MHE. VINCENT P. MBOGO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mwanakamati, Mheshimiwa Vincent Mbogo. Tunakushukuru sana kwa niaba ya Kamati. *(Makofi)*

Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, Dar es Salaam.

Na. 168

**Kuimarisha Elimu ya Awali**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Utaratibu wa watoto kuingia darasa la kwanza ni lazima awe amepitia shule za awali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha madarasa ya elimu ya awali?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo; mpango wa Serikali wa kuimarisha elimu ya awali. Swali la Kibunge, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, elimu ya awali ni muhimu katika kumwandaa na kumjengea msingi mwanafunzi wakati wote atakapokuwa anaendelea na masomo katika ngazi zote. Kwa kuzingatia suala hili, Serikali ilitoa maagizo kuwa kila shule ya msingi nchini iwe na darasa la awali ili kuwapokea wanafunzi walio na umri kati ya miaka minne hadi mitano ikiwa ni maandalizi ya kujiunga na darasa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanda Mtaala wa Elimu ya Awali unaoendana na aina ya ujifunzaji unaotakiwa kwa watoto wa elimu ya awali. Mtaala huo umezingatia ujifunzaji kwa kutumia michezo. Hadi Februari 2021, walimu 70,712 wanaofundisha darasa la awali, la Kwanza na la Pili wamepatiwa mafunzo ya namna ya utumiaji wa mbinu sahihi za ufundishaji, ufaraguzi na utumiaji wa zana za kufundishia.

Hatua hii imeimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika madarasa ya awali nchini.

Mheshimiwa, Serikali imezielekeza Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa watoto wa Darasa la Awali, la Kwanza na la Pili wanapatiwa vyumba vya bora vya madarasa vinavyowawezesha kutengeneza mazingira bora ya kujifunzia kwa rika lao na kuhakikisha kuwa mtoto wa Darasa la Awali analindwa na kupata eneo zuri la kujifunzia kwa kucheza ndani na nje ya darasa. Hatua hii pia imehusisha kubadilisha madarasa haya kwa kuweka zana za ujifunzaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu na kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha Elimu ya Awali katika shule zote nchini kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, Viswahili vingine vugumu; katika majibu yako unasema ufaraguzi. Sasa hapa taabu, unatuacha njiani.

Mheshimiwa Mariam Kisangi, uliza swali lako.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa katika Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa kuandikisha watoto kuingia darasa la kwanza kunakuwa na sharti la Watoto kwamba ni lazima waje na *certificate* ya kumaliza elimu ya awali; na changamoto hii imekuwa ni kubwa sana katika maeneo ya pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam katika shule kama za Mbande, Majimatitu, Charambe, Nzasa na maeneo mengi ya Mkoa wa Dar es Salaam:-

Je, Serikali inatoa kauli gani sasa kuondoa changamoto hii kwa wananchi au wazazi ambao wanapeleka watoto wao kuwaandikisha darasa la kwanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa uwiano wa darasa la kwanza utakuta kuna mikondo minne au mitano ya lakini darasa la awali linakuwa moja tu, jambo ambalo ni changamoto kubwa kwa watoto wote ambao wanaanza darasa la kwanza kwenda kujiunga na elimu ya awali katika shule husika:-

Je, Serikali imejipangaje sasa kuweka bajeti ya kutosha katika kuimarisha elimu ya awali katika shule zote za msingi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiona swali lenyewe lilivyokuwa limeandikwa tu, ni sentensi moja; la Kibunge, lakini pia maswali ya nyongeza mazito kabisa. Hongera sana Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Majibu ya maswali hayo muhimu, Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, kwamba kuingia darasa la kwanza lazima mtu aje na cheti kutoka awali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali hapa kwamba kumekuwa na sharti la *certificate* ya Elimu ya Awali; na anataka kufahamu Serikali inatoa kauli gani? Kwanza nieleze tu kabisa kwamba katika ngazi ya awali, Serikali haina utaratibu wa *certificate.* Hizo ni taratibu ambazo watu wamejitungia huko chini. Mara nyingi sana ni hizo shule za *private* zaidi ndiyo wamefanya hivyo, lakini huo utaratibu haupo.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali ni moja tu; *certificates* zilizopo ni za darasa la saba, kidato cha nne, kidato cha sita na kuendelea, lakini kwa shule za awali *certificate* hakuna. Huo ni utaratibu ambao Serikali haiutambui. Kwa hiyo, hiyo ndiyo kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, uwiano wa wanafunzi, hususan darasa la kwanza na shule ya awali; na kwa sababu hiyo niseme tu kwamba kutokana na umuhimu

wa kuongeza wanafunzi katika shule za awali, ndiyo maana sasa hivi katika mipango yote ya Serikali ambayo tunayo, ikiwemo *EP4R, Boost, Lens, RISE,* miradi yote, tumehakikisha kabisa kwenye kila mradi tunaweka na *component* ya kujenga madarasa ya shule za awali ili kuhakikisha watoto wetu wanapata madarasa bora na tunaongeza madarasa ili watoto hao waweze kupata mazingira bora ya kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Ummy! Aah, majibu ya nyongeza, ahsante Mheshimiwa Waziri, nimekuona.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na vile vile nampongeza Mheshimiwa Mariam Kisangi. Nataka tu kuendelea kutoa tamko la kisera; ni marufuku shule kudai *certificate* ya awali kwa wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba bado hatujafanya vizuri katika kuongeza *access* ya watoto kuanza elimu ya awali. Kwa hiyo, haileti mantiki kusema kila mtoto ili aanze Darasa la Kwanza awe na *certificate* ya awali. Tunawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwenda kuweka nguvu za kuboresha watoto wetu hususan wa masikini kupata elimu ya awali, hususan katika maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona niweke hiyo; na wote ambao wanadai *certificate* ya elimu ya awali wajue kwamba wanatenda kinyume na maelekezo na miongozo ya Serikali.

**SPIKA:** Kwa kweli jibu hili ni la kutia moyo sana. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, maana hii imekuwa shida sasa.

Bado tuko katika Wizara hiyo hiyo ya TAMISEMI, Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Singida Kaskazini, kule Mtinko, Ilongero. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 169

**Kumaliza Ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Makuro na Ngimu – Singida Kaskazini**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa maboma ya vituo vya afya yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika Kata za Makuro na Ngimu?

**SPIKA:** Majibu ya swali la Singida Kaskazini, Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Singida shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, hospitali hiyo imetengewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wa wodi tatu na shilingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya Zahanati Minyeye, Mnung'una na Msikii katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya kukamilisha maboma matano ya zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na wananchi katika kujenga na kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya huduma za afya katika Jimbo la Singida Kaskazini zikiwemo Kata za Makuro, Ngimu na nchini kote ili kuendelea kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naipongeza Serikali kwa juhudi hizi za kuboresha huduma za afya katika Jimbo la Singida Kaskazini ikiwemo maendeleo yanayofanyika kwenye hii Hospitali ya Wilaya pamoja na vifaa tiba na upanuzi wa wodi.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Halmashauri ya Wilaya ya Singida inakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa watumishi wa Idara ya Afya, hasa wauguzi pamoja na madaktari: Je, Serikali ina mpango au mkakati gani wa kuhakikisha inaleta watumishi wa kada hii katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ili kuhakikisha huduma za afya zinapatikana ipasavyo?

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali ilijenga Kituo cha Afya cha Mgori pale ambapo hata wewe ulifika siku ile ulipokuja kuniombea kura; lakini hospitali hii hadi sasa haijaanza kufanya kazi pamoja na kwamba kituo hiki kimekamilika kwa asilimia 100 kwa maana ya majengo; hapana vifaa tiba wala gari la kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inapeleka fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba pamoja na ununuzi wa *ambulance* kwa ajili ya kubebea wagonjwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani kwa ufuatiliaji wa karibu sana katika miradi ya maendeleo katika Jimbo lake hili la Singida Kaskazini ikiwepo miradi hii ya afya. Kimsingi ni kweli tunafahamu baada ya kazi kubwa sana iliyofanywa na Serikali ya kujenga miundombinu ya huduma za afya kwa maana ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali mpya za Halmashauri, *automatically* tumekuwa na uhitaji mkubwa pia wa watumishi wakiwemo Waganga, Madaktari pamoja na Wauguzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuweka mipango ya kuendelea kuajiri watumishi hawa ili sasa vituo hivi ambavyo vimejengwa na kukamilika vianze kutoa huduma; na katika mwaka ujao wa fedha, Serikali imeomba vibali vya ajira kwa ajili ya wataalam hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ighondo kwamba pamoja na maeneo mengine kote nchini, Serikali itahakikisha inawapangia watumishi katika Halmashauri ya Singida likiwemo Jimbo hili la Singida Kaskazini ili vituo vya afya viendelee kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Mgori kimekamilika muda mrefu na sasa kinahitaji kupata watumishi kama ambavyo nimeongea kwenye swali langu la msingi, pia gari la wagonjwa na vifaa tiba. Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba kwa ajili ya Vituo vya Afya na Hospitali za Halmashauri mpya ambazo zinaendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakipa kipaumbele sana Kituo cha Afya cha Mgori ili na chenyewe kipate vifaa tiba na kuhakikisha kwamba kinaanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na magari ya wagonjwa, utaratibu wa Serikali tunaendelea kuandaa mipango ya kupata magari ya wagonjwa katika Vituo vya

Afya na Hospitali za Halmashauri kwa awamu kwa kadri ambavyo tutapata fedha. Hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hicho pia ni kipaumbele na Serikali itakwenda kukitimiza.

**SPIKA:** Waheshimiwa, kwa sababu ya muda, tunaendelea na Wizara ya Maji. Swali lanaulizwa na Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Gwambina. Mbunge wa Misungwi, uliza swali lako tafadhali.

Na. 170

**Mpango wa Kupeleka Maji Mji wa Usagara**

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji kwenye Mji wa Usagara?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Eng.* Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji Wilayani Misungwi ni asilimia 73. Katika juhudi za kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa maeneo hayo, katika mwaka 2021/2022, Serikali kupitia Programu ya *Lake Victoria Water and Sanitation* imepanga kutekeleza mradi wa maji katika maeneo ya Usagara, Buswelu, Kisesa na Buhongwa. Mradi huu utahusisha ujenzi wa vituo vya kusukuma maji viwili, mifumo ya usafirishaji na usambazaji maji yatakayozalishwa na Chanzo kipya cha Maji Butimba, ulazaji wa mabomba makubwa yenye ukubwa wa kuanzia milimita 50 hadi 600 kwa umbali wa kilomita 50, ujenzi wa matanki manne ya ukubwa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo utanufaisha maeneo yote ya Mji wa Usagara ikiwemo Usagara, Fela, Nyang'homango, Idetemya, Ukiliguru, Ntende, Sanjo, Isamilo, Mayolwa, Bukumbi na Kigongo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyeti, swali la nyongeza.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Majibu haya anayonipa Naibu Waziri wa Maji ni majibu ambayo yametolewa mwaka 2002 swali lilipoulizwa na Mheshimiwa Dalali Shibiliti, majibu hayo hayo; miaka kumi baadaye akauliza Mheshimiwa Charles Kitwanga akapewa majibu hayo hayo; nami nauliza miaka kumi baadaye napewa majibu haya haya.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, maji Usagara yanakwenda lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyeti na mimi ni shahidi yako, alipouliza Shibiliti nilikuwepo, alipouliza mawe matatu Kitwanga, nilikuwepo na unapouliza wewe nipo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Winfred Mahundi, Naibu Waziri kero hii ya Usagara itaisha lini? Tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnyeti Mbunge wa Misungwi. Awali ya yote Mheshimiwa Mnyeti pamoja na wananchi wote wa Misungwi poleni sana kwa adha hii ambayo imewapata kwa muda mrefu. Mheshimiwa Mbunge kama anavyofahamu Awamu hii ya Sita, ni awamu ambayo inakwenda kumaliza kama sio kupunguza kwa sehemu kubwa tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tulivyomsikia Mheshimiwa Rais, yeye mwenyewe akiwa hapa ndani kwa kutumia Bunge lako hili Tukufu aliahidi kuweka nguvu kubwa ya kuona kwamba matatizo ya maji yanakwenda kutatuliwa. Hivyo kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, kwenye bajeti

yetu ya mwaka 2021/2022, tunakuja Misungwi kuhakikisha tatizo hili sasa linabaki kuwa historia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tumalizie na hili swali lingine maana yake nalo ni la maji la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyangh'wale.

Na. 171

**Mradi wa Maji kutoka Nyamtukuza - Bukwimba**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza.

Je, ni lini mradi wa maji wa kutoka Nyamtukuza, Kakora, Kharumwa, Izunya, Kayenze hadi Bukwimba utakamilika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tupo Wizara ya Maji, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nassor Amar Hussein, Mbunge wa Nyangh'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa Maji wa Nyamtukuza uliopo Wilaya ya Nyang'hwale unalenga kuhudumia Vijiji 12 vya Nyamtukuza, Kakora, Bugombela, Nyarubele, Kitongo, Ikatangala, Kharumwa, Busengwa, Izunya, Kayenze, Bukwimba na Igeka. Hadi mwezi Machi, 2021, vijiji vinane (8) vimepata maji. Vijiji vilivyopata maji ni Nyamtukuza, Kakora, Kitongo, Ikatangala, Kharumwa, Busengwa, Nyarubele na Bugombela vimeanza kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, mradi umepangwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2021 na vijiji vyote 12 vitapata huduma ya maji ambapo wananchi wapatao 51,500 watanufaika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza nianze kuishukuru Serikali kwa kukamilisha kwenda kukamilisha mradi huu ambao ni wa kihostoria.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa sababu unaenda kukamilika mradi huu ambao utahudumia zaidi wananchi 51,500,000 mradi huu unaenda kukamilishwa mwezi Juni. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa yupo tayari kuambatana nami kwa ajili ya kwenda kuukabidhi mradi huo na kufanya sherehe kwa sababu mradi ule ni wa kihistoria kuanzia mwaka 1975? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuendelea kusambaza maji baada ya kukamilisha vijiji hivyo 12 katika kata zifuatazo: Kata ya Nyugwa, Nyijundu, Kaboha, Shabaka, Nyangh'wale na Busolwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kusambaza maji katika kata hizo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Amar Nassor Hussein, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nipende kupokea pongezi za shukrani kutoka kwako na pia suala la kuambatana na Mheshimiwa Mbunge, mimi na yeye tayari tulishafika pale Nyangh'wale, basi nitatoa nafasi hii kwa majimbo mengine ila nikishakamilisha nitaweza kutafuta nafasi ya kuja sasa kusheherekea.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kusambaza maji katika kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge upo tayari kwenye mipango mikakati ya mwaka ujao wa fedha. Hivyo

naomba tuendelee kuvuta Subira, tutakwenda mwaka ujao wa fedha kuona maji sasa yanaendelea kuwasogelea wananchi katika makazi yao.

**SPIKA:** Ahsante sana. Hebu twende Singida, tupate swali la nyongeza, Mheshimiwa Aysharose.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naishukuru sana Serikali kwa kutuchimbia visima katika Jimbo la Ikungi Mashariki na Ikungi Magharibi. Hata hivyo, visima hivi havina kabisa mtandao wa maji. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha visima hivi vinakuwa na mtandao wa maji ili kuwawezesha wananchi wa majimbo haya mawili la Ikungi Mashariki na Ikungi Magharibi kuweza kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Aysharose unauliza maswali ya Ikungi Mashariki lile Jimbo la yule jamaa aliyekimbilia Ubelgiji ambalo lilitelekezwa, halina mtu wa kulishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri Maji majibu tafadhali ya maji kule. Maana yake Jimbo lilikuwa halina mwakilishi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali ya nyongeza ya Mheshimiwa Aysharose, Mbunge Viti Maalum kutoka Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua kazi kubwa ambayo Wizara imefanya kuchimba visima vya kutosha na kwa sasa hivi kazi inayofuata ni kuona mtandao unakwenda kuwafikia wananchi. Hivyo Serikali huwa tunaangalia kwanza kupata chanzo na uhakika wa chanzo ukishapatikana tunajenga vituo vya kuchotea maji. Sasa tupo kwenye utaratibu wa kuona kwamba mtandao huu unaendelea kuwasogelea wananchi kadri mahitaji yanavyohitajika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hebu twende Mara, Mheshimiwa Ester Bulaya, tafadhali.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Wewe ni shahidi Mradi wa Maji Bunda sasa hivi unachukua takribani miaka kumi na tatu, najua kuna awamu ya tanki imekalimilika. Awamu nyingine ilikuwa ni kuhakikisha wanasambaza mabomba na kueneza mtandao wa maji katika kata zote 14. Hivi ninavyozungumza ni kata saba tu tayari ndiyo zimeanza kusambaza mradi wa maji na wana uhakika wa kupata maji angalau kwa asilimia 50. Je, ni lini sasa Wizara itahakikisha kata zote 14 za Bunda Mjini zinapata maji na ukizingatia humu ndani mimi ndiyo nawasemea hakuna anayewasemea. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Bunda jiandae swali la nyongeza. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kupokea pongezi kwa kuona kwamba tanki limekamilika na angalau asilimia hamsini ya usambazaji umeshakuwa katika utekelezaji. Kwa sababu tuna kata 14 na kata saba tayari utekelezaji unaendelea hiyo ndiyo kazi ya Wizara ya Maji.

Vilevile kama ambavyo umemtaja Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo kazi hii imefanyika kwa usimamizi madhubuti. Mbunge wa Jimbo amekuwa akifuatilia mara nyingi na kwa sababu Mbunge wa Jimbo amekuwa akiwasiliana na Wizara mara kwa mara ndiyo maana maji kata saba, kati ya kata 14 yameweza kutolewa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Bunda Mjini. Wizara ya Uchukuzi, tunaendelea na Mheshimiwa Regina Ndege. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Hapana Mheshimiwa wa Bunda Mjini, Bunda Mjini.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo mimi, ndiyo wa Bunda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, uliza swali lako.

Na. 172

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege - Manyara**

**MHE. REGINA N. QWARAY** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanja cha Ndege cha Mwada Mkoani Manyara?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu wa Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *yaani TAA* na kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara wameainisha eneo la Mwada katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege katika mkoa huo. Aidha, Serikali imeendelea na taratibu za kutwaa eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja hicho cha ndege. Baada ya hatua hii, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi yaani Sekta ya Ujenzi kupitia *TANROADS*,

itatangaza zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo hapo juu, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali ina nia thabiti na imejipanga kikamilifu katika kuhakikisha kuwa uwanja huo unajengwa ili kuweza kutoa huduma muhimu katika Mkoa huo wa Manyara na maeneo ya jirani. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina, nimekuona uliza swali.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi uliyonipa ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, Mkoa wetu wa Manyara ni miongoni mwa mikoa yenye vivutio vingi kama vile Hifadhi ya Wanyama Tarangile, tuna Mlima Hanang, tuna Ziwa Babati. Kutokana na ukosefu wa Kiwanja cha Ndege katika mkoa wetu watalii wengi wanapokuja katika mkoa wetu hutumia Uwanja wa Ndege uliopo Manyara kule Mto wa Mbu umbali wa kilometa 160, hutumia Uwanja wa Ndege uliopo KIA kilometa takribani 200, hutumia Uwanja wa Ndege wa Arusha kilometa zaidi 164. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Serikali haiwezi sasa kuweka msukumo wa pekee kusogeza huduma ya Uwanja wa Ndege katika Mkoa huu wa Manyara ili kuchochea shughuli za maendeleo katika mkoa wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa tayari eneo hili limekwishatengwa kule Mwada, ni lini sasa Serikali itaona kuboresha ili kuweka *airstrip* katika eneo hilo litumike wakati tunaendelea kusubiri ujenzi wa Uwanja wa Ndege katika mkoa wetu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kutoka kwa Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum, Manyara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Regina Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kufanya kazi za kibunge wa Mkoa, kwa sababu nina uhakika uwanja huo ukijengwa na kukamilika huduma itakuwa ya mkoa na mikoa ya jirani. La pili naomba nimuhakikishie kwamba jambo hili Mheshimiwa Pauline Gekul Mbunge wa Babati Mjini na wengine wenye majimbo wamekuwa wakifuatilia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali ni kwamba *tuna-engage* Mkandarasi Mshauri tuelekeze fedha katika eneo hili, tunajua umuhimu wake na vitu vyote katika Mkoa wa Manyara ukamilike.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali lake la pili linalohusu wazo lake la kutengeneza *airstrip* katika eneo hili, tunalipokea na tutalifanyia kazi ili huduma iweze kupatikana katika eneo hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jeremiah Amsabi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Takwimu mbalimbali za wataalam zimeonesha kama Uwanja wa Ndege wa Serengeti ukiboreshwa utakuwa uwanja pekee katika Kanda ya Ziwa utakaoleta tija kubwa kiuchumi, kiuhifadhi na kijamii kwa wananchi wa Serengeti na Tanzania kwa ujumla. Kwa kuwa mpaka sasa tayari wadau mbalimbali na wananchi wamekwishachangia ujenzi wa uwanja huu. Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa uwanja huu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli Uwanja wa Serengeti ni muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi ya nchi lakini pia katika eneo la Serengeti na Mkoa wa Mara kwa ujumla. Pia naomba nitambue kwamba ni kweli wananchi na Mheshimiwa Mbunge amejiunga, wametengeneza *group* la *WhatsApp,* wanachangisha fedha na Mheshimiwa Mbunge leo ameomba *appointment* watu wakija awapokee tuzungumze.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwelekeze Mkurugenzi wa Viwanja vya Ndege atume watalaam wetu katika eneo hili ili juhudi nzuri za wananchi zisipotee, atuongezee utalaam wa Wizara yetu kazi hii ifanyike na uwanja ujengwe ili watalii wasizunguke Zaidi, washuke pale karibu na tutape huduma na fedha iongezeke.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini kati.

Na.173

**Daraja la Mto Bubu – Kondoa Mjini**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Daraja la Mto Bubu ili wananchi wa upande wa pili wa mto waweze kuvuka na kupata huduma mbalimbali za kijamii?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo bado tupo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Daraja la Mto Bubu lijulikanalo kama Munguri B lipo katika barabara ya Kondoa – Nunguri – Mtiriangwi – Gisambalang – Nangwa yenye jumla ya urefu wa kilomita 81.4. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Manyara kupitia Wilaya za Kondoa na Hanang.

Mheshimiwa Spika, mvua kubwa zilizonyesha mwaka 2019/2020 zilisababisha Mto Bubu kutanuka na kufanya Daraja la Munguri B kutopitika wakati wa mvua. Kwa kutambua changamoto hii, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADs)* imetenga fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021 kwa ajili ya kufanya usanifu wa Daraja jipya katika Mto Bubu.

Mheshimiwa Spika, taratibu za ununuzi wa kumpata Mhandisi Mshauri zipo katika hatua za mwisho ambapo kazi hiyo inatarajiwa kuanza Juni, 2021. Aidha, katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, daraja hili limetengewa shilingi bilioni sita kwa ajili ya kukamilisha kazi ya usanifu. Baada ya usanifu kukamilika, ujenzi wa daraja hili utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa muda wa kuuliza swali la nyongeza, nina swali moja tu. Sasa kwa sababu zoezi la ukamilishaji wa ujenzi litachukua muda mrefu kwa kuzingatia majibu ya Mheshimiwa Waziri. Sasa je, Serikali haioni haja sasa ya kujenga japo daraja la dharura kwa kupitia vyombo vyetu vya jeshi ili kunusuru kesi za vifo pamoja na upotevu wa mali za wananchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia changamoto za wananchi wake wa Jimbo lake waliompigia kura kumleta hapa Bungeni. La pili, naomba nimwambie kwamba jambo hili tumelipokea, kabla ya kwenda kuomba vyombo vyetu vya Jeshi kuna taratibu zake, naomba nimwelekeze Katibu Mkuu Ujenzi atume mtaalam wetu katika eneo hili ili tuone kama kuna haja ya kujenga daraja la dharura kwa wakati huu na tuweze kulifanyia kazi wananchi wetu waendelee kupata huduma kama ilivyo matarajio ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Mheshimiwa Mohamed Suleiman Omar, Mbunge wa Malindi, lakini nadhani hayupo, sasa namwomba Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, kwa niaba yake. Mheshimiwa Soud.

Na.174

**Hitaji la Askari na Vitendea Kazi - Polisi Zanzibar**.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH (K.n.y. MHE. MOHAMED SULEIMAN OMAR)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Askari wapya Pamoja na kuleta vitendea kazi vya kutosha kwa Polisi Zanzibar inayokabiliwa na upungufu mkubwa wa Askari kutokana na wengi kufikia umri wa kustaafu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Suleiman Omar, Mbunge wa Malindi kutoka Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa rasilimali watu na vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi pamoja na mambo mengine huzingatia hali ya uhalifu wa eneo husika, jiografia ya eneo, idadi ya watu wanaohudumiwa na Jeshi la Polisi na ikama ya watumishi sambamba na upatikanaji wa vitendea kazi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa askari wa Jeshi la Polisi kwa Raia kimataifa ni askari mmoja kwa raia mia nne hamsini (1:450) hata hivyo kwa upande wa Zanzibar takwimu zinaonesha kuwa uwiano ni askari mmoja kwa raia mia tatu na tisini na mbili (1:392). Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 hii inamaanisha kuwa idadi ya Polisi Zanzibar ni wengi ukilinganisha na mahitaji katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vitendea kazi, napenda kukiri kuwa kama ilivyo maeneo mengine ya nchi, kuna uhaba wa vitendea kazi. Serikali itaendelea kuongeza ikama ya watumishi na vitendea kazi kadri nafasi za ajira na fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningeomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa vile tokea mwaka 2012 hadi leo hii ni miaka tisa imepita na idadi ya askari polisi imeendelea kupungua kutokana na askari wengi kustaafu katika maeneo ya Zanzibar.

Vilevile kuongeza kwa vitendo vya uhalifu katika baadhi ya maeneo, je, Mheshimiwa Waziri au Serikali haioni haja ya kuajiri askari zaidi katika maeneo ya Zanzibar na hasa mashambani ili kuweza kuziba hilo pengo kwa haraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili, kwa vile askari jamii katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar, wamekuwa ni msaada mkubwa na tayari kuna *good practices* katika baadhi ya maeneo. Je, Serikali haioni haja ya kuweza kupanua wigo wa askari jamii kwa kuwapatia mafunzo na motisha, ili kuweza kufanya kazi na kuweza kusaidia kupunguza vitendo vya uhalifu katika maeneo ya Zanzibar? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu Mheshimiwa Hamza Hamis Hamis, kuongeza askari kule Zanzibar mashambani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufanya uajiri kuna mambo lazima tuyaangalie. La kwanza, lazima tuhakikishe kwamba, tumepata kibali cha kufanya uajiri kitu ambacho nataka nimuambie Mheshimiwa Mbunge, tumeshakifanya na tumo mbioni kuhakikisha kwamba, tunapata ruhusa ya kufanya uajiri.

Mheshimiwa Spika, lingine ili tuweze kufanya uajiri maana yake lazima tuhakikishe kwamba tuna bajeti ya kutosha kwasababu tukisha waajiri lazima tuwalipe. Sasa kikubwa ambacho nataka nitoe wito hapa leo kwa Waheshimiwa Wabunge, hasa Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali na Waheshimiwa Wabunge leo tukijaaliwa hapa tunaenda kupitisha bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba bajeti hii tuipitishe kwasababu, ndani ya bajeti hii imezungumzwa taarifa za ajira za vijana hasa kwenye jeshi la polisi. Kwa hiyo, nawaomba tupitishe hii bajeti ili sasa tuweze kufanya hizo harakati za uajiri.

Mheshimiwa Spika, nimeulizwa pia suala kuhusu namna bora ya kuweza kuwaboresha askari jamii. Nimuambie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi tunavyozungumza tayari Kamishna anayeshughulika na masuala ya askari jamii na ulinzi shirikishi Zanzibar kwanza,

anachokifanya ni kutoa mafunzo kwa masheha na kamati za ulinzi na usalama za shehia na vijiji, ili lengo na madhumuni ni kuona namna bora ya kuweza kuwashirikisha wananchi katika kupata ulinzi. Lakini tayari kuna mfumo mzuri, mwongozo mzuri ambao umeshatolewa umeshaanza kutumika Unguja na Pemba *soon inshalah* utaanza kutumika. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa twende Liwale, Mheshimiwa Mbunge wa Liwale swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Liwale ni Wilaya ambayo iko mbali sana na makao makuu ya Mkoa ambako ni Lindi. Na pale Liwale hakuna kituo cha polisi kwa maana ya jengo hawana kabisaa, wanaishi kwenye nyumba ambayo ilipangwa na benki mpaka leo hii. Lakini, mwenyewe ni muhanga katika hili, mwaka huu mimi nimechomewa nyumba mbili na magari matatu wakati wa uchaguzi. Kimechangiwa sana na uhaba wa askari polisi na hatuna msaada wa karibu kutoka Liwale mpaka Nachingwea ni zaidi ya kilomita 120 mpaka Lindi zaidi ya kilomita 300. Sasa, je, Serikali ina mkakati gani kwanza, kutuongezea polisi Wilaya ya Liwale ikiwepo pamoja na majengo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, swali ni moja tu, Mheshimiwa Naibu Waziri sijui kama umewahi kutembelea Liwale! Ningekushauri utembelee. Majibu tafadhali zamani walikuwa polisi kwenye jeshi la gofu lile la Mjerumani, bado wapo hapo, hatari kubwa. Majibu Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niko tayari kama ambavyo umenishauri kwenda kutembea Liwale, bahati mbaya kidogo sijafika Liwale. Lakini najitahidi katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti tunaweza tukatenga siku moja tukaenda Liwale kwenda kuangalia hiyo hali, halafu tutarudi tuje tuone sasa namna ya kufanya tathmini kuona namna ya kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini, suala hili la uhaba wa askari mimi nadhani tuje pale pale, tuhakikishe kwamba tunaipitisha bajeti yetu, bajeti ambayo imezungumza suala zima la uajiri wa polisi, vijana hawa wa polisi, ili tuweze kuajiri. Tukikwamisha hii maana yake tutakuwa hatuna namna ya kufanya. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa wenye maswali kuhusu mambo ya ndani leo ndio bajeti ya Wizara, Mheshimiwa Waziri mwenyewe anajiandaa pale, Mheshimiwa Simbachawene. Kwa hiyo, baadaye mnaweza mkapata nafasi ya kuchangia hata kwa dakika chache na wale ambao hamtapata nafasi basi muanze kuandika, ili muanze kumpelekea mapema aweze *ku-take note* kuhusu *consults* zenu za mambo ya ndani ya nchi.

Sasa ni Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mbunge wa Makunduchi. Mheshimiwa Ravia tafadhali.

Na. 175

**Vyama Vya Michezo Kubadili Katiba Kukidhi Matakwa Binafsi**

**MHE: RAVIA IDARUS FAINA** aliuliza.

Je, Kwa nini Vyama vya Michezo ikiwemo *TFF* na *TOC* vimekuwa vikibadili Katiba zao kwa lengo la kulinda viongozi waliopo madarakani na kudhibiti watanzania wengine wasigombee nafasi katika vyama hivyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mheshimiwa Pauline Philip Gekul nadhani ni mara ya kwanza anajibu kwa Wizara hii sina hakika sana, karibu sana kwa majibu yako Mheshimiwa Pauline Gekul. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa uhai siku ya leo tukaendelea kutimiza wajibu wetu sisi Wabunge wa Bunge hili. Lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kuniamini tena na kunifanya Naibu katika Wizara hii. Mheshimiwa Rais nakushukuru sana. Lakini la tatu pia, niwatakie kila la kheri wanahabari wote kote nchini na duniani pia katika maadhimisho ya siku yao ya uhuru wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, Mbunge wa Makunduchi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Michezo Tanzania vinasajiliwa kwa Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa na 12 ya Mwaka 1967 na marekebisho yake Na. 6 Mwaka 1971 pia namba 3 ya Mwaka 2018; pamoja na kanuni za msajili za Mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mahitaji ya kubadili katiba za vyama kujitokeza na kufanyika katiba hizo haziwezi kuanza kufanya kazi, mpaka zisajiliwe upya na Msajili wa Vyama vya Michezo ambaye hupitia upya, kuona kama kanuni zinazosimamia Michezo na Sheria zingine za nchi zimeangaliwa. Iwapo msajili atabaini kuwa suala ambalo limeingizwa katika katiba halina maslahi kwa Chama na Taifa ikiwemo masuala ya utawala bora; Msajili amepewa mamlaka ya kisheria kukataa usajili huo kwa mujibu wa Kanuni za Usajili za Mwaka 1999, kifungu 11(3)(a) na (b).

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Shirikisho la *TFF* na *TOC* haijawahi kubadili katiba zao kwa lengo la kulinda viongozi walioko madarakani kwa kuwa, mabadiliko hayo yote ya kikatiba ni lazima yakidhi vigezo vya usajili vinavyosimamiwa na msajili wa vyama na vilabu vya Michezo nchini, ikiwemo utawala bora na ukomo wa muda wa uongozi chini ya *BMT*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Idarus Ravia Idarus una swali la nyongeza?

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini kwenye *TFF* ukomo wa uongozi ni vipindi vitatu vya miaka minne minne. Lakini, kwenye *TOC* hakuna ukomo. Je. haoni inazuia uhuru wa watu wengine kugombea? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ukomo katika uongozi wa *TFF* na kutokuwa na ukomo katika uongozi wa *TOC* hakuzuii watanzania wengine kugombea? Ndio swali lake. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TFF* wao wamekwenda vizuri kama alivyosema lakini *TOC* wanaendelea kufanya marekebisho katika katiba yao. Katiba yao Mwaka 2019 walirekebisha, 2020 msajili aliweza kuipitisha Novemba na katika marekebisho ambayo amefanya sasa, wameweka kipengele cha kwamba, mtu akigombea nafasi ya Urais basi ahudumu kwa *term* 3 akishahudumu kwa *term* 3 ya miaka minne minne ya miaka 12, baada ya hapo asirudie kugombea nafasi hiyo bali sasa apande juu aende *IOC* au kwenye nafasi zingine. Kwa hiyo, wameendelea kuboresha vile vipengele ambavyo vinaminya uhuru wa watu wengine na wengine kuendelea kugombea. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa wanamichezo wengi hapa lakini namuona promota wa masumbwi Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, uliza swali lako tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kama ilivyo kwa Chama cha *TFF* kwenye eneo la ngumi kumekuwa na ubabaishaji mwingi sana kwa kitu kinachoitwa Rais wa ngumi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusimamia uongozi huu unaokaa kwa muda mrefu bila kufuata katiba kama inavyosema? Ahsante kwa kunipa hiyo nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, tafadhali. Na hawa watu wa michezo wanapenda sana kujiita Rais, Rais unakuta Rais wa Yanga, Rais! Sasa kwani mkijiita mwenyekiti shida nini? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara kupitia *BMT* lakini kupitia kwa Msajili, tunaendelea kufuatilia hizi katiba ambazo wamechomeka vipengele ambavyo vinawafanya watu kuendelea kukaa madarakani. Mheshimiwa Mwakagenda suala lako tunalipokea na pia nitafanya ziara katika maeneo hayo na tutapitia katiba yao pia kwa upya tuone ni wapi wameweka vipengele hivyo. Nikuhakikishie kupitia msajili tutaangalia na tutashauri lakini pia wanachama, mtushauri pale ambako mnaona hizi katiba zinakandamiza uhuru wenu katika vyombo hivyo ambavyo mnashiriki vya kimichezo. Tuko tayari kupokea ushauri wenu.

**SPIKA:** Ahsante kwasababu ya muda Waheshimiwa Wabunge mtaona tunakimbiza muda tunaenda Wizara ya Madini, swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, uliza swali lako Mheshimiwa Hawa tafadhali.

Na. 176

**Madhara ya Madini ya Zebaki**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza: -

Je, ni kwa kiasi gani Serikali inafahamu madhara yatokanayo na madini ya zebaki?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu. Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya, tafadhali athari za zebaki.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma (Mbunge wa Viti Maalum) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali inatambua madhara makubwa ya kiafya kwa binadamu, mimea na mazingira yanayosababishwa na matumizi ya kemikali ya zebaki na hasa katika shughuli za uchenjuaji wa madini. Na miongoni mwa madhara ya kemikali hiyo kwa binadamu, ni kuathiri mifumo ya fahamu, uzazi, upumuaji na kusababisha magonjwa mbalimbali kama vile ya figo, moyo na saratani. Aidha, kemikali hiyo pia, huathiri viumbe hai vya majini na nchi kavu pindi zebaki inapotiririka na kuingia kwenye vyanzo vya maji ambavyo hutumiwa kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na shughuli za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, na njia zinazopelekea kemikali ya zebaki kuingia mwilini ni kushika, kuvuta hewa na kula vyakula vyenye viambata vya kemikali hiyo. Pamoja na athari hizo kiafya, matumizi ya zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu yameonesha uwezo mdogo wa kutoa dhahabu ambao ni chini ya asilimia 30, hali ambayo imekuwa ikipelekea wachimbaji wadogo kushindwa kuzalisha kiwango cha kutosha na hivyo kupata faida kidogo.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu athari za kemikali hiyo na kutoa njia salama za utumiaji, ikiwa ni pamoja na usakafiaji wa mialo na utumiaji wa *retorts* kiswahili chake ni (vigida) wakati wa uchomaji. Aidha, Serikali kupitia *STAMICO* itaendelea kutoa elimu ya matumizi ya njia mbadala ya uchenjuaji dhahabu kupitia vituo vyetu vya mfano vilivyoko maeneo ya Lwamgasa, Katente pamoja na Itumbi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu kama una swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninalo ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, Serikali inayafahamu kwa kuyataja kabisa madhara yanayotokana na kemikali ya zebaki lakini pia kwa kuwa, kutumia njia hii kuchenjulia dhahabu tunapata

asilimia kidogo tu kama ambazo ametaja asilimia 30, ni kwanini sasa Serikali isitumie *cyanide* kuchenjulia madini hayo ya zebaki na kuachana na kemikali hatari ya zebaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, kibali cha *ku-import* kemikali ya zebaki nchini kinatolewa na Mkemia Mkuu wa Serikali. Wataalam kutoka Wizarani wanatuambia kwamba Mkemia Mkuu wa Serikali hakupokea maombi ya *ku-import* zebaki nchini. Cha ajabu ni kwamba, kemikali hiyo ipo ya kutosha tu huko mtaani, sasa ni nini kauli ya Serikali juu ya njia hizi za panya zinazoingiza kemikali hii kiholela? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Mchafu, umekuwa *consistent* katika suala hili la kupambana na masuala ya zebaki tunakupongeza sana. Majibu ya swali hilo muhimu sana, Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya, Naibu Waziri Madini, tafadhali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, *cyanide* pamoja na baadhi ya *acids* ndio njia sahihi ambayo inafaa kwa ajili ya uchenjuaji dhahabu kwa sasa na ndio teknolojia ambayo aaah! Kama Mheshimiwa Mchafu atakumbuka kwamba, ndio teknolojia mpya ambayo imetumika na ndio imeleta hasa manufaa kwa wachimbaji wadogo. Sema, kwa kutumia *cyanide* pamoja na *vat leaching* inakuwa inahitaji kidogo mtaji uwe mkubwa ili mchimbaji mdogo aweze kuitumia. Sasa kitendo cha kuhitaji mtaji mkubwa kidogo ndicho kinachofanya wengine bado wanaendelea kutumia *mercury.*

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli kwamba, wengi wameshaanza kuhama na ndio msisitizo wa Wizara tunawasisitiza watoke kule kwasababu ya madhara ambayo yanaonekana. Nikweli kwamba, kwa kutumia *vat leaching* ambayo inatumia *cyanide* ni kwamba, hata *recovery* inakuwa ni kubwa na kwa hiyo tumuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama Wizara tutaendelea kufanya jitihada za kutoa elimu. Kwanza, wachimbaji wadogo wajue madhara makubwa yanayotokana na kutumia *mercury,*

lakini pia ikiwezekana hata kama ni kujiunga kwa vikundi waende katika teknolojia ambayo inafanya *recovery* kubwa lakini pia haina madhara makubwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kweli kwamba *mercury* inapatikana kwa wachimbaji wadogo wakiitumia na kwasababu, kibali kilipaswa kutoka kwa Mkemia Mkuu kama ambavyo anatoa kuhusu kemikali zingine zozote zile. Lakini Mheshimiwa Mbunge anathibitisha kwamba sio kweli kwamba yeye ametoa vibali. Tulichukue kama Serikali kwasababu tunatamani kulinda mazingira yetu, tunatamani kuwalinda wachimbaji wetu ili tuingie katika mnyororo na ikiwezekana badala ya kutoa elimu kwenye matumizi, basi twende pia kuangalia hata *source* ya mahali ambapo zebaki inaingilia. Nadhani kwa jinsi hiyo tutaweza kuwasaidia maana yake ni kwamba tuanze udhibiti tangu kwenye *source* kuliko kule kwenye matumizi yenyewe kwa kujali afya na mazingira yetu. Ahsante *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, inabidi pia wafundishe matumizi ya *cyanide* maana yake hiyo nayo ni shughuli pevu pia. Aaah! Sio rahisi swali hili likapita bila kumruhusu msukuma hata mmoja maana yake ndio inasemekana… sasa hawa waliosimama msukuma ni nani? Nimekuona Mheshimiwa Kabula Shitobelo, uliza swali.

**MHE. KABULA E. SHITOBELO:** Mheshimiwa Spika, ahsante ukizingatia sisi ndio mama zako au bibi zako lazima uturuhusu ahsante sana. Kutokana na shughuli za uchimbaji madini Mkoani Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla, tatizo na ongezeko kubwa la kansa kwa Mkoa mzima wa Mwanza kumekuwa na tatizo kubwa la kansa na tunaamini kabisa hii zebaki ndio inayosababisha ongezeko hili la kansa. Je. Serikali ina mpango gani sasa wa kudhibiti kabisa uingiaji wa kemikali hizi, ili kunusuru wananchi wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante kwa swali hilo zuri. Mheshimiwa Waziri wa Madini mwenyewe. Mheshimiwa Doto Biteko, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Kabula kwa swali lake ambapo ameulizia kuhusiana na udhibiti.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, hatua ya kwanza tuliyochukua mahali ambako dhahabu inachenjuliwa, inaitwa mialo, mwanzo mialo ilikuwa holela, kila mahali mtu anajenga; sasa tumeamua kuidhibiti ile mialo yote iwekwe kwenye eneo maalum na jumla ya mialo 5,025 imesajiliwa kote nchini.

Mheshimiwa Spika, pili, Chama cha Wachimbaji Wadogo kinaitwa *FEMATA* pamoja na Mkemia Mkuu wa Serikali wanatengeneza *umbrella* moja ya namna ya kuagiza zebaki hapa nchini na Mkemia Mkuu wa Serikali ameshatoa hiyo *go-ahead* lakini changamoto tuliyonayo ni ndogo ndogo tu ya uratibu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndani ya miezi hii miwili uagizaji wa zebaki tutakuwa tumeudhibiti na tutakuwa na *source* inayoeleka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Afya sijui una mpango gani wa kufanya *cancer screening* kwa Wabunge Wanyamwezi na Wasukuma. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunahamia Wizara ya Kilimo na swali la Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Balozi, tafadhali.

Na. 177

**Kutafuta Soko la Uhakika la Zao la Mahindi**

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipanga vipi kutafuta Soko la uhakika la zao la mahindi kwa wakulima wa Mikoa ya Kusini hususan Mkoa wa Njombe?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo inatekeleza mikakati mbalimbali ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Viwanda na Biashara katika kuwatafutia wakulima masoko ya mazao ya kilimo ikiwemo kuwaunganisha wakulima wa mahindi na wasindikaji wa mahindi kwa ajili ya unga na chakula cha mifugo, kuondoa vikwazo na kupunguza gharama za biashara na kupunguza ukiritimba na kuanza kutoa vibali vya kuuza mazao nje bila ya kuwa-*charge*. Vilevile, Wizara ipo katika hatua za awali kuhakikisha kwamba inaanzisha Idara ya Masoko na sekta binafsi; Serikali kununua mahindi kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* na Bodi ya Mazao mchanganyiko na Serikali kufanya makubaliano ya kibiashara baina ya Tanzania na nchi zenye fursa ya masoko zikiwemo nchi za *DRC*, Kenya, Sudan ya Kusini, Rwanda, Burundi na kutumia njia mbadala kuhakikisha wasafirishaji wanapata huduma za usafirishaji ikiwemo vibali kiurahisi. Pia Mkoa wa Njombe kuunganishwa na wanunuzi ikiwemo Kampuni ya *Silverland* ambayo katika msimu wa 2020/2021 imenunua jumla ya wastani wa tani 40,000 za mahindi.

Mheshimiwa Spika, kupitia jitihada hizo, kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Desemba 2020 wakulima na wafanyabiashara wameuza tani 89,725 za mahindi nchini Kenya, Burundi na DRC. Bodi ya Mazao na Nafaka Mchanganyiko imenunua jumla ya tani 24,000 za mahindi kutoka kwa wakulima. Pia, kufikia mwezi Mei, 2020, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* amenunua jumla ya tani 73,000 za mahindi zenye thamani ya shilingi bilioni 48 kutoka kwa wakulima na vikundi mbalimbali kwenye kanda zote nane. Kati ya hizo, jumla ya tani 11,000 za mahindi

zimenunuliwa kutoka Kanda ya Makambako inayojumuisha Mkoa wa Njombe ambao ulizalisha tani 332,000 za mahindi katika mwaka wa 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2021, Wizara inaangalia uwezekano wa kuwa na maghala katika nchi zenye masoko makubwa ya mazao ikiwemo nchi za *DRC* na South Sudan kwa lengo la kuhifadhi na kutangaza mazao ya kilimo na hivyo kuyauza kwa urahisi katika nchi hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na mikakati yote hii ya Serikali ambayo ni mizuri kuhusiana na soko la mazao ya mahindi bado mahindi ni mengi sana kwa wakulima. Hivi sasa debe la mahindi limefikia Sh.3,000, mahindi yam waka jana wakulima bado wanayo na mwezi Juni tunavuna tena yataungana. Serikali inaweza kuiagiza *NFRA* waende msimu huu wakaokoe adha hii kwa wakulima kwa kununua mahindi haya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu sana, Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la moja la Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba wakulima ama wanunuzi bado wana mazao mengi ya nafaka na wakati huo huo yanakutana na msimu wa mavuno hivi karibuni, huu ni ukweli ambao hauwezi kufichika.

Hata hivyo, sasa hivi hatuwezi kutoa *commitment* kwamba *NFRA* waende wakanunue nafaka hizo lakni hatua za awali ambazo tunazichukua na naamini baada ya muda mfupi tutalitatua tatizo la biashara kati ya sisi na nchi ya Kenya ambayo imekuwa ikinunua mazao yetu ya mahindi kwa muda mrefu. Naamini kwamba soko hilo likifunguka

litaongeza idadi ya mahindi yanayokwenda nje. Vilevile sasa hivi tuna mazungumzo na wenzetu wa *WFP* ambao nao wameonesha *demand* ya kununua mahindi zaidi ya tani kama laki moja na nusu.

Mheshimiwa Spika, lakini hatua nyingine ya msingi ambayo tunachukua kama Wizara ni kwamba tunaongea na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kuruhusu taasisi zetu *NFRA* na *CPB* kuruhusiwa kupata vibali ziweze kuchukua fedha katika taasisi za fedha na kununua mazao mengi ya wakulima kwa sababu uwezo wetu wa hifadhi sasa hivi umefika zaidi ya *metric tons* laki tano na kiwango tunachokihifadhi hakizidi laki moja na nusu.

Kwa hiyo, wakipewa kibali kutoka Wizara ya Fedha wataweza kukopa na kununua mahindi mengi pale ambapo tunakumbana na *situation* kama hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaeleze Waheshimiwa Wabunge na niwaombe Watanzania wenzangu na wakulima wa nchi hii tunafanyia kazi jambo hili la kuijengea uwezo *NFRA* na *CPB.* Wakati huohuo tunaruhusu wafanyabiashara wa Kitanzania, yeyote anayepata soko popote duniani aje Wizara ya Kilimo tutampa kibali bure aweze kwenda kuuza mazao yake bila kuzuiliwa popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuziomba halmashauri zisizuie mahindi, mpunga au mchele unaouzwa popote nje ya mipaka yetu kwa sababu kufanya hivyo itakuwa ni kutomtendea haki mkulima na wala hatuhitaji ukiritimba wowote kwenye *trade* ya mazao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona na natamani niwape nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza lakini mtaona muda umekwisha kabisa, tunatakiwa tuishie saa nne kamili, nafikiri wote mkiangalia saa yetu mtaona nachokizungumza. Kwa hiyo, tuchukue swali la mwisho kwa siku ya leo la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi ambalo limelekezwa Wizara ya Katiba na Sheria, kwa niaba yake Mheshimiwa Justin Nyamoga.

Na. 178

**Hitaji la Mahakama Tarafa ya Mahenge - Kilolo**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA (K.n.y. MHE. NANCY H. NYALUSI)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama katika Tarafa ya Mahenge Wilayani Kilolo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Naibu Waziri, Mheshimiwa Geophrey Pinda, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Mahakama ya Tarafa ya Mahenge iliyopo Wilaya ya Kilolo ni miongoni mwa Mahakama za Mwanzo hapa nchini zitakazoanza kujengwa kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022.

Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupitisha Wizara ya Katiba na Sheria ambayo ndiyo inayokwenda kutekeleza ujenzi wa Mahakama hiyo. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge avumilie kidogo kuanzia Julai, Mahenge wanakwenda kushuhudia kuanzwa kwa ujenzi huo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga umeridhika?

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Wilaya ya Kilolo haina majengo ya Mahakama na hivi sasa majengo yanayotumika ni ya Mahakama ya Mwanzo. Je, ni lini Serikali itajenga majengo ya Mahakama ya Wilaya ya Kilolo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Tarafa ya Mazombe kuna Mahakama ambayo ilijengwa enzi za mkoloni na haijawahi kufanyiwa ukarabati wowote. Je, ni lini Serikali itakarabati majengo hayo ili yaweze kuendana na hadhi ya sasa na haki iweze kutolewa katika mazingira mazuri?

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo kwa kifupi Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Wilaya ya Kilolo itaingizwa kwenye mpango wa ujenzi Kwa kipindi cha mwaka 2022/2023. katika kipindi kijacho cha fedha tunajenga ile Mahakama ya Mwanzo ambayo ipo Tarafa ya Mahenge na kwa ile ya Wilaya tutaanza kuiweka kwenye mpango nilioutaja.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu ukarabati wa ile Mahakama ya Mazombe, hii nayo tutaiweka kwenye mpango wa 2022/2023. Hii itaendana na ukarabati wa maeneo mengine yote ambayo tumeendelea kuweka mikakati kwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kusema, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 baadhi ya miradi yetu ambayo itaendeshwa katika kipindi hicho tumeiainisha tayari na katika ngazi ya wilaya tutakuwa na Mahakama nyingi sana ingawa kwenye mpango huo wilaya yake haipo. Kutokana na muda ningeweza kuziorodhesha wilaya hizi lakini kwa sasa inatosha kusema hivyo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Katiba na Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, nina matangazo muhimu kidogo. Upande wangu wa kulia naomba tusikilizane.

Kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo kwa safari ya kikazi lakini shughuli za Serikali humu Bungeni zitaongozwa na Mheshimiwa Waziri William Lukuvi. Kwa hiyo, naomba tumpe ushirikiano Mheshimiwa Lukuvi kama kawaida yetu. *(Makofi)*

Kuhusiana na wageni tulionao Bungeni, tunaye Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ndugu Christopher Kadio na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ramadhani Kailima. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Inspekta Jenerali wa Polisi, Ndugu Simon Sirro. Karibu sana IGP na sisi kama Bunge tunakupa pole sana kwa msiba wa mama mzazi. Pole sana, pole sana. *(Makofi)*

Wapo pia Naibu Kamishna wa Magereza, Ndugu Jaremiah Katungu na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Makakala, ahsante sana. Huyu dada yetu kwa kweli ni katika akina mama ma-*pioneers* kabisa ambao wanajenga heshima ya mwanamke katika nchi yetu. Hongera sana Kamishna Jenerali wa Uhamiaji. (*Makofi/Vigelegele*)

Wageni wengine ni Kamishna Jenerali wa Zimamoto na uokoaji, Ndugu John Masunga na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Dkt. Arnold Kihaule. Tunawakaribisha sana na wengine wote mliopo hapo. *(Makofi)*

Wageni 39 wa Mheshimiwa Joseph Kamonga na Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana ni Madiwani na Maafisa Tarafa kutoka Ludewa, Mkoani Njombe wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Ndugu Wise Mgina. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani mjifunze kwa sababu mengi

mnayofanya kule mnafanya kwa kurandana na Bunge lenyewe ambalo ndilo lenye mamlaka yote. Ninyi mmekasimiwa sehemu tu ya hizo shughuli, hongereni sana, simamieni maendeleo ya Ludewa. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Tadayo ambao ni mtoto wake Ndugu Jonathan Tadayo na mtoto wa rafiki yake ndugu Vision Bagonza kutoka Dar es Salaam. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Martha Mariki ambaye ni mdogo wake kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Dianah Mariki. Dianah karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambaye ni mama yake mzazi kutoka Jijini Arusha, Mama Sifa Swai. Huyu Mama Sifa Swai ni Mweka Hazina Mstaafu wa CCM Taifa kwa miaka mingi sana na alitunza Hazina ya CCM kwa uaminifu bila senti moja kupotea. Tuige mfano huo akina mama ni waaminifu. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazie kwamba kesho kutakuwa na Iftar ya kukata na shoka na yenyewe itaandaliwa na rafiki na ndugu zetu wa Benki ya *CRDB* itakuwa hapa katika viwanja vya Bunge.

Kwa hiyo, kesho msiandae Iftar kule majumba, kwa kweli *CRDB* wamejiandaa. Wiki hii kutakuwa na Iftar za hakika msiwe na wasiwasi. Baada ya hii nitatangaza na nyingine, baada ya hiyo sasa itafika ya Spika. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Umoja wa Wabunge Waislam kutakuwa na kikao saa 7.00 mchana katika Jengo la Utawala, Chumba Na. 207

Leo ni Mambo ya Ndani ya Nchi tulitarajiwa tuwe na siku mbili, siku ya Ijumaa na leo lakini kama mnavyojua hali na muda haukuruhusu kwa hiyo tutakuwa nayo leo tu peke yake. Kwa jinsi hiyo napenda nipate wachangiaji wengi iwezekanavyo, kwa hiyo, tutachangia kwa dakika tano tano

ili wengi tufikishe ujumbe na mtakaobaki basi muweze kuandika. Nawaombeni sana tutoe ushirikiano huo.

Waheshimiwa Wabunge, pamekuwa na maneno mengi sana kwenye mitandao na mimi si kazi yangu kwa kweli kushughulika sana na mambo ya mitandao na huwa sipendi. Baadhi ya ndugu zetu Wapinzani wanapenda sana kulisifu Bunge la Tisa la kaka yangu Marehemu Mzee Sitta na kwa kweli Bunge hilo lilifanya kazi nzuri sana. Mimi wananichafuaga sana lakini sijaamua kujisemea na kuweka *record* yangu mezani, wengi hawaijui. Bunge hilo la Tisa mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Bunge, kwa hiyo, nilikuwa ni mmoja wa wasaidizi wa karibu kabisa wa Mzee Sitta. Kwa hiyo, mafanikio ya Bunge la Tisa haiwezekani ukayazungumza halafu na mimi nisiwepo au la Kumi au lingine lolote lile. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa maoni yangu kitu kimoja kikubwa kuliko vyote katika Bunge la Tisa ni kwamba tulipata Kanuni mpya zilizobadilisha utendaji ulivyokuwa kabla ya wakati ule kuja kwenye utendaji wa kisasa zaidi ambao ndiyo tumeuendeleza hata leo. Wakati ule ilikuwa kipindi cha mabadiliko ya Kanuni iliyotoa uhuru zaidi, ikaleta maswali kwa Waziri Mkuu, ukaleta mabadiliko mengi tunayoyaona leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, unajua sifa siku zote zinaenda kwa bosi, aliyezitengeneza zile Kanuni wale mliokuwepo alikuwa nani kama siyo Job Ndugai. Mimi ndiye niliyekwenda Mauritius, Zambia, South Africa, Uganda, Kenya, India pamoja na UK nikaangalia *best practices* kote huko, tuka-*compare* na tunavyoendelea tukatengeneza hii maneno hii. Ukitengeneza ukiwa Msaidizi sifa si anapata bosi? Sasa hawa jamaa zangu, sipendagi sana ni mapema nitakapofika mwisho nitakuja kushusha *contribution* yangu kwa Bunge hili na kwa Taifa langu. Sasa hivi siyo wakati wake ninyi endeleeni kuchafua tu ni sehemu ya siasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, majuzi yametokea maneno kidogo, mdogo wangu Mheshimiwa Nape yakamtoka

maneno kidogo na yamezunguka sana. Sasa kwa sababu ni Mbunge, mkifika mahali Mbunge na Spika muanze kuwa mnapishana nadhani haipendezi eh? Kwa hiyo, sitapitia hoja zake kwa sababu ana uhuru *after all* lakini kitu kimoja hana uhuru kwa sababu ya Kanuni ni kuwasema vibaya Wabunge wenzake. *(Makofi)*

Nafikiri hilo kanuni zinakataza. Hilo lazima nilikemee. Aliwataja kwa majina ya mitaani huko ambayo kwa kweli alikosea sana. Niliongea naye, naamini aliteleza. Kwa hiyo, sitamsimamisha hapa aseme chochote. Ninachowaomba Waheshimiwa mumsamehe bure. Mtu akikufanyia kosa kubwa sana, unachoweza kufanya ni kumsamehe bure. Aliwakosea sana, aliwakosea sana, aliwakosea sana.

Tuchunge sana midomo yetu tunapo-*deal* na binadamu wenzetu, hasa wanapokuwa labda wana mawazo tofauti na yetu. Ndiyo utamaduni ambao ni vizuri tukaujenga katika nchi yetu. Kubishana, kupingana, kutofautiana lakini kwa hekima na kwa heshima inatusaidia sana kujenga nchi ambayo ndiyo wenzetu wa upande ule mwingine wanakosaga sana hicho; subira ya kuheshimu mtu mwingine hata kwenye michango yao.

Mheshimiwa Nape hayuko hivyo, alikosea tu kidogo. Pia Mheshimiwa Nape mdogo wangu, unapo-*deal* na wanawake duniani kote, unaongea nao kwa heshima. Hiyo ndiyo *practice* ya dunia. Wale wote wasioelewa, hivyo ndivyo ilivyo. Wanawake ni mama zetu, ni dada zetu, ni mabinti zetu tunaowazaa, tunawapenda, yaani ni *world practice,* hata katika mila zetu. Hata ninyi wenyewe mtanikubalia. Unaposhughulika na mtoto wako wa kike na mtoto wa kiume kidogo ni tofauti na hasa kwa sisi wanaume. Mtoto wa kike ni mama, dada, ana heshima yake. Hatutoki tu kiume kama tunavyotoka wa kiume, *we have to be soft somehow.* Kwa hiyo, hilo nawaomba sana msiliendeleze, msichukulie hivyo. *(Makofi)*

*At this juncture* pia, niwaambie vyama vya siasa, jamani mimi ni Spika mzoefu. Nimekuwa hapa Bungeni miaka

mingi, sasa hivi ina miaka 20, naelekea 25. Nina uzoefu wa kutosha. Wako watu wanapiga kelele, Ndugai anavunja Katiba, yaani hawaelewi watendalo kabisa. Katibu Mkuu wa chama chochote unaponiandikia jambo lenye mgogoro ambao unahusu mambo ya kikatiba; mgogoro unaotoka kwako kule, usiniandikie kipeperushi, mimi fulani nasema kwamba Spika chukua hatua, fukuza fulani na fulani. Halafu wewe unayeandikiwa hivyo, ndio Mbunge ufukuzwe. Kazi yangu mojawapo ni kulinda Wabunge. *(Makofi)*

Mkiruhusu hayo, mtapa taabu Waheshimiwa. Katibu Mkuu wa Chama chochote huko ulikotoka, anaandika tu barua, kipeperushi kama hivi, halafu mimi nakufukuza, haiendi hivyo. Aandike barua, aambatanishe na Katiba yake ya Chama chake, maana mimi siwezi kujua Katiba ya *UPDP,* sijui, chama gani ambayo ni *prevailing;* mimi nitajuaje? Aniambatanishie na katiba yake, aniambatanishie na muhtasari wa hicho kikao kilichofanya hayo maamuzi. Inawezekana huyo Katibu Mkuu kaamka tu, kaandika, halafu na mimi nakurupuka nachukua hatua. Nitakuwa ni Spika au ni kitu cha ajabu!

Andika muhtasari wako ili ile barua yako niiangalie niwape wataalam. Ninao wataalam wa sheria wengi tu, waangalie kufuatana na Katiba yako. Kwa sababu natekeleza kufuatana na Katiba ya chama chako: Je, ni sawabsawa? Hao Wajumbe wa kikao kinachoitwa Kamati Kuu hiyo iliyokaa ndio Wajumbe halisi? Namwuliza Msajili wa Vyama. Hao walioorodheshwa hapa ndiyo hao? Inawezekana nusu ni mamluki, halafu inaitwa sijui Kamati Kuu, sijui inaitwa nini? Utafanyaje? Naangalia kwenye muhtasari ule: Je, hao Wabunge wanaotuhumiwa kufukuzwa, walipata nafasi hata ya kuhojiwa na kujieleza? Walipata *natural justice?* Walisikilizwa? Nifukuze watu ambao hawakusikilizwa popote! Ndiyo mnataka *precedence* hiyo? Yaani Mbunge hujawahi kusikilizwa, wanaandika tu, fukuza huyu! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Nape, mambo haya mazito. Viko vyama ndugu zangu vimejaa udikteta. Vimejaa mfumo dume; kundi la wanaume wanakaa wanafukuza wanawake. *Group* la

wanawake tupu, 19 kwa mpigo! Hata kama barua hiyo inatoka CCM, chama change, kinafukuza Wabunge wanawake 19 kwa mpigo, kwa barua tu, kipeperushi namna hii! Lazima nitawaambia, ah, *stop!* Ngoja kwanza, subiri. Hebu tuangalie kidogo mambo yako sawa sawa?

Pia Katiba yao ina mambo ndani yake. Hiyo hiyo Katiba yao; wamechukua hatua kwa Katiba yao, wamekata rufaa huko. Kwa Katiba yao kuna kitu kinaitwa Baraza Kuu, kwa Katiba yao ndiyo chombo cha mwisho chenye maamuzi juu ya *fate* ya jambo hilo. Hilo Baraza Kuu limekutana? Limefanya maamuzi ya mwisho? Sasa unaniambiaje kwamba nichukue hatua, wakati Katiba yako mwenyewe huiheshimu? Sasa mimi ni kazi yangu Mbowe kukusomea Katiba yako ili uweze kuelewa? Siyo kazi yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa endeleeni kuchapa kazi, msiwe na wasiwasi, mpo mikono salama na haijapangwa kwamba lazima Spika achukue hatua katika siku mbili, au katika siku nne. Ni busara yake, anakwenda taratibu anajiridhisha taratibu. Sasa kwa nini watu wananiingilia jamani! Mimi mzoefu wa mambo haya. Tutafika tu. *(Makofi)*

Mwisho, niwaambie ndugu zangu wa vyama mbalimbali, tabia ya kuonea wanawake lazima iishe katika nchi hii. Lazima iishe kwa kupambana na baadhi ya vyama ambavyo vimejaa mfumo dume, kama hiki chama cha ajabu ajabu. Nani asiyejua jinsi mabinti hawa walivyopambana? Nani asiyejua? Wanasema eti, wanatoa wito kwa uongozi huku tukae tutafute muafaka wa Kitaifa, sijui nini; wewe muafaka wa chama chako unakushinda, utakaa utafute muafaka wa Kitaifa upi? Wewe migogoro mitupu nyumbani kwako, uzungumze muafaka wa Kitaifa, unaelewa maana ya muafaka wa Kitaifa? Kama unaelewa, si umalize ya kwako kwanza? *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Spika hoyee! *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa. Basi baada ya hapo, Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Karibu sana Mheshimiwa George Simbachawene. Tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/2021 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, ninaomba hotuba yangu yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya njema pamoja na kuniwezesha kuwasilisha hotuba yangu katika Bunge hili la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021 nchi yetu ilimpoteza Mwana Mageuzi, mpendwa wa wananchi wa Tanzania na aliyekuwa mbeba maono wa maendeleo, Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia vyombo vyake vya usalama imekuwa ni miongoni mwa wanufaika wakubwa wa miradi iliyojengwa na inayoendelea kutekelezwa kutokana na juhudi za Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ikiwemo ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya vyombo hivyo na ujenzi wa makazi ya Askari. Wizara itaendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa

miradi inayoendelea kama ilivyokusudiwa ikiwa kumuenzi Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mwenyezi Mungu ampumzishe kwa amani. Amina.

Mheshimiwa Spika, tarehe 19 Machi, 2021 Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kumpongeza kwa dhati kushika nafasi hii ya juu katika uongozi wa nchi yetu. Namwomba Mwenyezi Mungu amwangazie baraka na neema zote ili aliongoze Taifa letu kwa amani, utulivu na mafanikio makubwa ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hotuba za Rais, Samia Suluhu Hassan alizozitoa tangu kushika madara ya Urais zimempambanua na kumwonesha ni namna gani alivyo na uzalendo, umahiri, ubunifu, uadilifu, ujasiri na uwezo mkubwa wa kuliongoza vyema Taifa letu. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inatumia nafasi hii kuahidi kutekeleza maelekezo na maagizo yake wakati wote.

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu pia nazitoa kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango kwa kupendekezwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi hiyo. Pongezi nyingine nazitoa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ushindi wa kihistoria wa asilimia 76.27 alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2020. Ushindi huo ni wa kihistoria na ameanza kuonesha nia na dhamira ya dhati ya kuibadilisha Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 902.63. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 481.5 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 382.84 ni matumizi mengineyo na shilingi bilioni 38.29 ni za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya shilingi bilioni 707.16

ilipokelewa na Wizara sawa na asilimia 78 ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezwaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2021, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha bidhaa za ngozi kilichopo gereza la Karanga, Moshi; kukamilika kwa Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Magereza katika eneo la Msalato Jijini Dodoma; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 79 za makazi zenye uwezo wa kukaa familia 152 katika Vituo vya Magereza nchini; na kukamilika nyumba 19 za kuhudumia familia 38 za Askari wa Jeshi la Polisi katika Mikoa ya Arusha, Geita na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kujengwa kwa kiwanda kipya cha ushonaji wa sare za Askari katika eneo la Kurasini, Dar es Salaam; kutekelezwa kwa asilimia 90 ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Chamwino Dodoma; kujengwa kwa kambi za mafunzo ya Idara ya Uhamiaji iliyopo eneo la Boma Kichakamiba; Wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga; kuzalishwa na kusambazwa vitambulisho 925,342; kuokolewa kwa wahanga 165 wa biashara haramu za kusafirisha binadamu; na kupatikana kwa suluhisho la kudumu kwa wakimbizi wapatao 1,047 waliopelekwa katika Mataifa mbalimbali. Mafanikio mengine kwa kirefu yapo katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeweka kipaumbele katika kutekeleza maeneo yafuatayo: kuendelea kudumisha amani na usalama nchini; ujenzi wa ofisi za makazi na Askari; usajili na utambuzi wa watu 1,438,735; kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani; kuendelea kutekeleza mkakati wa mapinduzi ya kilimo kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa na mahabusu; kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata ngozi katika eneo la Gereza la Karanga, Moshi; kukamilisha uunganishwaji wa mfumo wa udhibiti wa mipaka *(e-border)* katika Ofisi za

Uhamiaji za Mkoa na Wilaya na maeneo mengine ya kipaumbele yametajwa katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla nchi yetu imeendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu na usalama na kuwezesha wananchi kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Aidha, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama nchini viliwezesha Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwezi Oktoba, 2020 kufanyika kwa kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya makosa makubwa ya jinai yaliyojumuisha makosa dhidi ya binadamu, maadili ya jamii na kuwania mali yaliyotolewa taarifa katika vituo vya Polisi nchini yalikuwa 37,230 ikilinganishwa na makosa 44,277 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Hii inaonesha kuwa makosa 7,047 yamepungua sawa na asilimia 15.9. Kupungua kwa makosa hayo kumetokana na ushirikiano mzuri baina ya Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, wananchi pamoja na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama barabarani nchini imezidi kuimarika kutokana na usimamizi mzuri wa Jeshi la Polisi kuhusu sheria za usalama barabarani, ushirikiano wadau, kuongezeka kwa utii wa sheria bila shuruti kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara, hivyo kuwezesha kupungua kwa matukio ya ajali, vifo na majeruhi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya matukio makubwa ya ajali 1,228 yalitolewa taarifa katika vituo vya polisi ikilinganishwa na matukio 1,920 katika kipindi kama hicho mwaka 2020 ikiwa ni sawa na kupungua kwa matukio ya ajali asilimia 36.04.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu kwa Umma; kuchukua hatua kali kwa wanaokiuka sheria; kuanzisha kanzidata ya kuwatambua madereva wa bajaji na bodaboda na hivyo kuongeza ufanisi katika usimamizi wa usalama barabarani. Natoa wito kuendelea kutii sheria za barabarani ili kuhakikisha usalama wao na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti/kupambana na uhalifu wa aina zote hapa nchini, Jeshi la Polisi limefanya operesheni mbalimbali kwa kushirikiana na Taasisi nyingine. Katika operesheni hizo, risasi 280 na silaha 134 zilikamatwa. Aidha, jumla ya watuhumiwa 138 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani na kesi zao zinaendelea. Vile vile nyara za Serikali 986 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.37 zilikamatwa na watuhumiwa 441 walifikishwa Mahakamani. Jeshi la Polisi katika mwaka 2021/2022 litafanya ukaguzi kwa wamiliki wa silaha ili kujiridhisha kuwa wanatekeleza kwa ukamilifu matakwa ya sheria husika pamoja na kudhibiti wizi wa nyara za Serikali. Aidha, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine litaendelea kudhibiti vitendo vya uhalifu katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na makazi ya Askari, utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa ujenzi wa nyumba za makazi, Vituo vya Polisi na mejengo ya ofisi unaendelea. Ujenzi wa majengo mawili yaliyoko eneo la Mabatini Jijini Mwanza yenye uwezo wa kuhudumia familia 24 za Askari unaendelea, ambapo jengo moja limekamilika na lingine liko katika hatua ya umaliziaji. Shilingi milioni 310.78 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Miradi mingine ni kama inavyoonekana katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 2.917 kwa ajili ya Vituo vya Polisi na majengo ya ofisi. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.5 zitatumika kujenga mabweni na hospitali katika Chuo cha Polisi Kurasini, Dar es Salaam na kiasi kinachobaki cha shilingi bilioni 1.47 kitatumika kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja C Mkokotoni Kaskazini Unguja; ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja A katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma; ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja A Wilaya ya Kigamboni Mkoa wa Kipolisi Temeke; na kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja B Wilaya ya Mbalizi Mkoani Mbeya. Aidha, viko vituo vinne vya Polisi Daraja C ambavyo vimekamilika, vimetajwa kwenye kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Jeshi la Polisi limepanga kutekeleza miradi ya kipaumbele ambayo ni kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja A, Lushoto Mkoani Tanga kwa shilingi milioni 250; kumalizia ujenzi wa jengo la Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara kwa gharama ya shilingi milioni 450; kumalizia ujenzi wa kituo cha Polisi Daraja C Ludewa, Njombe kwa gharama ya shilingi milioni 300; kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja A Mtumba katika Mji wa Serikali Dodoma kwa gharama ya shilingi milioni 601.1; kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A" Kigamboni, Dar es Salaam utakaogharimu shilingi 899.48; kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "C'' Nyakanazi, Kagera kwa shilingi milioni 60; na kukarabati jengo la Ofisi ya Kikosi cha Anga kwa gharama ya shilingi milioni 120.

Kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A" Kigamboni, Dar es Salaam utakao gharimu Shilingi 899.48; Kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "C'' Nyakanazi, Kagera kwa 60,000,000/=; na Kukarabati jengo la ofisi Kikosi cha Anga kwa gharama ya 120,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, vilevile, miradi iliyoanza kutekelezwa kwa nguvu za wananchi itakamilishwa, ambapo 200,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya mradi wa nyumba 12 za makazi, Kaskazini Pemba na 200,000,000/= zitatumika katika mradi wa nyumba 14 za makazi Kusini Pemba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Polisi litaendelea kuwashirikisha wadau katika ujenzi wa Vituo vya Polisi, majengo ya ofisi na makazi ya Askari nchini kote, pamoja na kumalizia miradi ya ujenzi iliyosimama. Hivyo, natumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika ujenzi wa Vituo vya Polisi na nyumba za makazi ya Askari ili kuimarisha hali ya ulinzi na usalama nchini.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza; Hali ya Ulinzi na Usalama; Magereza imeendelea kuwapokea, kuwalinda na kuwapatia huduma muhimu wahalifu wanaoletwa magerezani kwa mujibu wa sheria za nchi. Hadi kufikia mwezi

Machi, 2021 jumla ya wafungwa na mahabusu 33,570 walikuwepo katika magereza yote nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani, Jeshi la Magereza limeendelea kutumia utaratibu wa kifungo cha nje ambapo katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya wafungwa 881 walitolewa magerezani kwa utaratibu wa kifungo cha nje. Aidha, wafungwa 3,319 waliachiliwa huru na msamaha wa Mheshimiwa Rais. Vilevile kupitia Programu ya Huduma kwa Jamii na Huduma za Uangalizi, jumla ya wafungwa 2,253 walihukumiwa kutumikia adhabu hizo kwenye jamii; na hivyo kufanya jumla ya wafungwa wote waliotoka gerezani katika kipindi hicho kufikia wafungwa 6,453.

Mheshimiwa Spika, Kujitegemea kwa Chakula cha Wafungwa na Mahabusu; Jeshi la Magereza limeendelea kutekeleza Mpango wa Mapinduzi ya Kilimo ambao mpango huo ni wa mwaka 2020/2021 – 2024/2025 kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa na mahabusu. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020 Jeshi la Magereza limefanikiwa kuvuna tani 4,720 za mahindi, tani 1,120 za mpunga, tani 298 za maharage na tani 43.6 za alizeti. Katika msimu wa mwaka 2020/2021, jumla ya ekari 11,185 zimelimwa ambapo ekari 5,465 zimepandwa mahindi, ekari 2,511 mpunga na ekari 1,331 maharage na ekari 1,490 zimepandwa alizeti kwa matarajio ya kuvuna tani 5,530.73 za mahindi, tani 1,478.63 za mpunga na tani 290 za maharage.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kazi, Jeshi la Magereza limekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu katika eneo la Msalato Dodoma ambayo ilizinduliwa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 4 Februari, 2021. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 2.5 zilitolewa kwa ajili ya kuendeleza kazi zote zilizobaki. Serikali pia ilitoa shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa nyumba 173 zenye uwezo wa kukaa familia 326 zilizokuwa zimeanza kujengwa kwa kutumia rasilimali zinazopatikana

katika maeneo ya magereza. Ujenzi huo utasaidia kupunguza changamoto ya nyumba za makazi ambapo kwa sasa zipo nyumba 5,057 ikilinganishwa na mahitaji ya nyumba 12,500 zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utendaji wa kazi wa Jeshi la Magereza, Serikali imelipatia Jeshi hilo magari tisa kwa ajili ya shughuli za utawala. Magari hayo yamesaidia kupunguza changamoto ya usafiri kwa Viongozi Waandamizi. Aidha, mwaka 2021/2022, cha Shilingi bilioni 4.6 zimetengwa kwa ajili ya kununua magari 23 kwa shughuli za Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Lengo la Uchumi wa Viwanda; katika kusaidia kufikiwa lengo la uchumi wa viwanda, Jeshi la Magereza linakamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kiwanda cha Samani Msalato na ufungaji wa mashine ambao umefikia asilimia 90 na utakamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi, ambapo limefanya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto katika magari na maeneo mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya maeneo 36,703 yalikaguliwa, ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 5.25 kilikusanywa kutokana na ukaguzi huo. Aidha, Jeshi hilo limefanikiwa kuzima moto na kufanya uokoaji katika matukio 2,172. Aidha kwa kutambua umuhimu wa huduma hiyo, wadau wametoa msaada wa magari 10 ya utawala. Katika mwaka 2021/2022, Jeshi limepanga kununua magari mengine nane ya utawala na magari mawili kwa ajili ya kuzimia moto na vifaa mbalimbali vya kuzima moto na uokoaji.

Mheshimiwa Spika, Miradi Inayotekelezwa na Jeshi la Zimamoto; katika mwaka 2020/2021, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maafisa na Askari Eneo la Kikombo Jijini Dodoma ambapo ujenzi wa majengo sita yenye ghorofa tano umekamilika na jumla ya Shilingi

bilioni 2.9 zimetumika. Pia, Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto, Wilaya ya Chamwino Dodoma umefikia asilimia 75. Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.19 iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mfumo wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji; Idara hii imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya utoaji wa huduma kwa wageni na raia kupitia mfumo wa kielektroniki. Kwa sasa usimikaji wa mfumo wa usimamizi na udhibiti wa mipaka *(e-border system)* umekamilishwa katika ofisi za Uhamiaji za Mikoa. Aidha, katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali, zoezi la kuunganisha mfumo wa kielektroniki wa malipo ya Serikali linaendelea katika ofisi za uhamiaji. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 mfumo huu umeunganishwa katika ofisi za uhamiaji za mikoa 29, vituo 16 vya kuingia na kutoka nchini na ofisi 44 za Ubalozi wa Tanzania. Katika mwaka 2021/2022, zoezi la uunganishaji wa mfumo huu litaendelea katika mikoa na vituo vya uhamiaji vilivyobaki.

Mheshimiwa Spika, Misako na Doria ya Uhamiaji; shughuli za misako na doria ya uhamiaji zimeendelea kufanyika katika maeneo ya mipakani, migodini, viwandani, mahotelini na kwenye mashamba makubwa. Lengo ni kudhibiti wahamiaji haramu ikiwa ni pamoja na kuwabaini wageni wanaofanya kazi kinyume na sheria. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, jumla ya watuhumiwa 15,786 wa makosa ya kiuhamiaji walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Katika kuimarisha shughuli za misako na doria Serikali imetoa magari 16 kwa Idara ya Uhamiaji. Aidha, ununuzi wa magari sita umekamilika na hadi kufikia mwezi Juni, 2021 magari yote yatakuwa yamepokelewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Uhamiaji itaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu Dodoma; Ujenzi wa majengo ya ofisi zilizopo katika Mikoa ya Geita kwa gharama ya shilingi milioni 813.49; Mtwara shilingi milioni 878.66; na Lindi shilingi milioni 297.32. Aidha, makazi ya

Maafisa na Askari wa Uhamiaji yataboreshwa na kufanya ukarabati wa nyumba katika Mikoa ya Tabora na Pwani ambapo shilingi milioni 300 zimetengwa. Maeneo mengine yatakayoshughulikiwa ni kama inavyoonekana katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa; hadi kufikia Machi, 2021 usajili wa wananchi umefikia watu 22,345,948 ikilinganishwa na lengo la kusajili watu 25,237,954. Pia, Namba za Utambulisho 18,762,822 zimezalishwa na kugawiwa kwa wananchi. Aidha, *NIDA* imezalisha na kusambaza vitambulisho 925,342 na hivyo kufanya idadi ya vitambulisho vilivyozalishwa na kusambazwa hadi Machi, 2021 kufikia 7,028,567 katika wilaya 34 za Tanzania Bara na Zanzibar. Kazi za uzalishaji vitambulisho katika wilaya 116 zilizobaki inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2021.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi, *NIDA* imeendelea kuunganisha taasisi za umma na binafsi katika Kanzidata yake. Lengo ni kuwezesha wadau kuhakiki taarifa za watu wanaopata huduma na hivyo kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa jamii na kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi. Katika mwaka 2021/2022, *NIDA* itaendelea na zoezi la usajili na utambuzi katika wilaya na mikoa yote nchini na jumla ya shilingi bilioni 10.08 zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inashughulikia pia masuala ya Jumuiya za Kidini na Zisizo za Kidini. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ina jukumu la kusajili Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini, kufuatilia utendaji, uendeshaji na kushiriki katika utatuzi wa migogoro ya jumuiya zilizosajiliwa. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, jumla maombi ya usajili wa jumuiya 331 yalipokelewa. Jumuiya 124 zilisajiliwa ambapo 10 ni za kidini na 114 sio za kidini. Maombi matatu yamekataliwa kwa kutokutimiza vigezo vya usajili na 104 yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, migogoro tisa imesuluhishwa kati ya 11 iliyokuwepo. Nitoe wito kwa vikundi

ambavyo havijasajiliwa vifike katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya kwa ajili ya kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya, Sura Namba 337.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itafungua ofisi nne za usajili wa jumuiya katika Kanda ya Mashariki, Mkoa wa Dar es Salaam, Kanda ya Ziwa mkoa wa Mwanza, Nyanda za Juu Kusini Mkoa wa Mbeya na Kanda ya Kaskazini Mkoa wa Kilimanjaro. Lengo ni kurahisisha utoaji huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu; katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na wadau imefanikiwa kuwaokoa na kuwasaidia jumla ya wahanga 165 waliokuwa wanatumikishwa kinyume na sheria. Kati yao, wahanga 163 walikuwa wakitumikishwa hapa nchini na wahanga wawili walikuwa nchini Iraq na Malaysia. Wahanga wote walipewa huduma muhimu kama chakula, matibabu, msaada wa kisheria na wa kisaikolojia.

Vilevile Wizara iliratibu zoezi la kutambua familia za wahanga 77 raia wa Tanzania na kuwaunganisha na familia zao. Katika kipindi hicho, wahalifu 26 wanaojihusisha na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu walikamatwa na jumla ya kesi saba zilifunguliwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Sekretariati ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu imepanga kufanya kazi za kipaumbele zifuatazo zikiwemo: Kukamilisha uandaaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu mwaka 2021 - 2024 na kuanza utekelezaji wake; Kuimarisha ulinzi, usalama na uhifadhi wa wahanga; Kuendelea kuandaa na kutekeleza miongozo kwa ajili ya kutambua wahanga na kuwawezesha kupata huduma mbalimbali; Kuandaa utaratibu wa kitaifa wa kutoa huduma kwa wahanga; na Kuandaa mfumo wa kitaifa wa kuratibu masuala ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, Huduma kwa Wakimbizi; hadi kufikia mwezi Machi, 2021 Serikali ilikuwa ilikuwa inawapa hifadhi waomba hifadhi na wakimbizi 273,252. Pia, huduma za kijamii ziliendelea kutolewa kwa wakimbizi na waomba hifadhi kwa kushirikiana na *UNHCR*, *WFP*, pamoja na mashirika ya hisani ya kimataifa na ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi, Serikali kwa kushirikiana na *UNHCR* na *IOM* imewahamishia nchi ya tatu jumla ya wakimbizi 1,047 ambao walipelekwa katika nchi za Australia, Canada, Ireland, Marekani, Ubelgiji na Ufaransa. Aidha, Wakimbizi 31,432 walirejeshwa kwa hiari nchini Burundi.

Mheshimiwa Spika, shukrani; nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii, pamoja na maelekezo na miongozo yake kwangu na kwa Wizara ninayoiongoza. Mwenyezi Mungu amjalie Rais wetu neema ya uhai na afya njema ili aweze kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa Miaka Mitano na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kwa mafanikio makubwa huku nchi yetu ikiwa na amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na miongozo yao wanayotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, akiwemo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa *Comrade* Mussa Azzan Zungu na wajumbe wa Kamati hiyo kwa kutoa ushauri na kuboresha mambo mbalimbali katika Wizara ikiwemo kupitia na kuchambua makadirio na mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nitoe shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, almaarufu "Chiro", Mbunge wa Jimbo la Uzini, Kusini Unguja kwa kusaidia kusimamia majukumu ya Wizara ikiwemo kujibu maswali hapa Bungeni kwa umahiri mkubwa na kutoa ufafanuzi wa hoja zinazowasilishwa hapa Bungeni. Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu Ndugu Christopher Derick Kadio na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ramadhan Komboi Kailima kwa usimamizi wao madhubuti wa utekelezaji wa kazi za Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee pia, shukrani zangu za dhati nazitoa kwa Wakuu wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, nikianza na Inspekta Jenerali wa Polisi, bwana Simon Nyankoro Sirro; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Polisi, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza; Meja Jenerali Suleiman Mzee; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Makakala; na Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Bwana John Masunga ambao wamewezesha upatikanaji wa mafanikio makubwa katika Wizara pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na amani na utulivu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile namshukuru Profesa Suffian H. Bukurura, Mwenyekiti wa Bodi pamoja na Wajumbe wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi na Meja Jenerali Mstaafu Raphael M. Muhuga, Mwenyekiti wa Bodi na Wajumbe wa Shirika la Uzalishaji Mali wa Jeshi la Magereza. Aidha, nawashukuru kwa dhati Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Makamishna, Makamishna Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Maafisa na Askari na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuendelea kutekeleza vema shughuli za Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nazishukuru Jumuiya za Kidini na zisizo za kidini, vyombo vya habari na wananchi wote wa Tanzania kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau wa maendeleo tulioshirikiana nao katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nchi hizo ni Botswana, Burundi, Ethiopia, Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Korea Kusini, Malaysia, Seychelles, Ujerumani pamoja na Mashirika ya Kimataifa kama *UNDP, UNHCR, UNICEF, IOM, UN – Women, RECSA* pamoja na Taasisi ya *TRI* na Kampuni ya *GGML* kwa kuendelea kutoa misaada ya kifedha, kijamii na kiufundi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, namshukuru sana mke wangu mpenzi Mariana William Naano, ndugu na jamaa kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Aidha, kwa namna ya pekee sana kwa uzito mkubwa nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kibakwe kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika kuendeleza umoja na mshikamano wa kuchangia shughuli za maendeleo katika jimbo letu. Nawashukuru sana na tuendelee kushikamana kwa ajili ya ustawi wa jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini kabla sijaomba fedha naomba nikiri kuwa Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi walio wengi wanaishi kwenye makazi yasiyoridhisha na yasiyotosheleza. Aidha, katika wilaya nyingi kuna changamoto ya kutokuwepo kwa Vituo vya Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Ofisi za Uhamiaji. Kwa kutambua changamoto hii, Wizara iko mbioni kuandaa Mpango Kabambe wa Ujenzi wa Nyumba, Ofisi na Vituo kwa ajili ya Vyombo vyote vya Usalama vilivyoko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mpango huu umeanza kufanyiwa kazi katika ngazi ya wataalam na utakapokamilika utawasilishwa katika mamlaka husika ili kupata mwongozo kwa ajili ya kuendelea na hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka 2021/2022. Katika mwaka 2021/2022, Wizara imepanga kukusanya mapato ya jumla ya

Sh.494,917,473,000 kutoka vyanzo mbalimbali. Ili kufikia lengo hili Wizara itatekeleza mikakati mbalimbali ya kukusanya mapato ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi kama magari na pikipiki, kuendelea kuunganisha na kutumia mifumo ya kieletroniki katika kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha; katika mwaka 2021/2022, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya Sh.939,089,045,000 kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2021/2022. Kati ya fedha hizo, Sh.389,750,394,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.521,868,651,000 ni Mishahara na Sh.27,470,000,000 ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha za Maendeleo zinazoombwa, Sh.27,390,000,000 ni fedha za ndani na Sh.80,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, baada ya maombi haya ya fedha naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHE. GEORGE BONIFACE SIMBACHAWENE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2020/2021 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2021/2022.

**2. Mheshimiwa Spika**, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima na afya njema pamoja na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba yangu katika Bunge hili la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**3. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2020/2021, nchi yetu imepita katika matukio makubwa yenye huzuni ambayo hayataweza kusahaulika kwenye historia ya Nchi yetu.

Kwanza, tulimpoteza mwana mageuzi, mpendwa wa wananchi wa Tanzania na aliyekuwa mbeba maono mapana ya maendeleo, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Vyombo vyake vya Usalama imekuwa ni miongoni mwa wanufaika wakubwa wa miradi iliyojengwa na inayoendelea kutekelezwa kutokana na juhudi za Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ikiwemo ujenzi wa ofisi za Makao Makuu ya Vyombo hivyo na ujenzi wa makazi ya Askari. Wizara itaendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi inayoendelea kama ilivyokusudiwa ikiwa ni kumuenzi Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

**4. Mheshimiwa Spika,** pili, tulimpoteza Kiongozi shupavu na mwanamageuzi mahiri aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Hayati Maalim Seif Sharif Hamad na tulimpoteza Mtumishi wa Umma nguli Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Mhandisi John William Kijazi. Mwenyezi Mungu azilaze mahala pema peponi roho za wapendwa wetu. Amina! Aidha, ni katika kipindi hiki tuliwapoteza Waheshimiwa Wabunge wenzetu wawili, Mhe. Martha Jachi Umbulla na Mhe. Mhandisi Atashasta Justus Nditiye. Vifo hivi ni huzuni kwa Bunge hili na kwa wananchi wa majimbo yao.

**5. Mheshimiwa Spika,**tarehe 19 Machi, 2021 Mhe. Samia Suluhu Hassan aliapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama. Mhe. Rais ameweka historia ya kuwa Mwanamke wa kwanza kuliongoza Taifa letu. Ninatumia nafasi hii kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kumpongeza kwa dhati kushika nafasi hii ya juu katika uongozi wa nchi yetu. Ninaomba Mwenyezi Mungu amwangazie baraka na neema zote ili aliongoze Taifa letu kwa amani, utulivu na mafanikio makubwa ya maendeleo.

**6. Mheshimiwa Spika,** Hotuba za Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan alizozitoa tangu kushika Madaraka ya Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, zimempambanua na kumuonesha ni kwa namna gani alivyo

na Uzalendo, Umahiri, Ubunifu, Uadilifu, Ujasiri na Uwezo Mkubwa wa kuliongoza vema Taifa letu. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inatumia nafasi hii, kuahidi kutekeleza maelekezo na maagizo yake wakati wote. Watanzania watarajie makubwa toka kwa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan.

**7. Mheshimiwa Spika,** ninamshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kuendelea kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Ninamuahidi kutekeleza majukumu yangu kwa uaminifu, weledi na umakini mkubwa. Aidha, nitaendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM na maagizo yote ya Serikali kwa kushirikiana na Mawaziri wenzangu, Viongozi wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Dini, Wafanyakazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, vyombo vya habari pamoja na wananchi kwa ujumla.

**8. Mheshimiwa Spika,** pongezi zangu pia ninazitoa kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango kwa kupendekezwa na Mhe. Rais kushika nafasi hiyo na baadae kuthibitishwa na Bunge baada ya kuchaguliwa kwa kura 363, sawa na **asilimia 100** ya kura zote. Hii imeonesha wazi kuwa Waheshimiwa Wabunge wana imani kubwa na Makamu wa Rais katika kusaidiana na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kuliongoza Taifa letu.

**9. Mheshimiwa Spika,** pongezi nyingine ninazitoa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ushindi wa kihistoria wa **asilimia 76.27** alioupata katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2020. Ushindi huo ni wa kihistoria na ni uthibitisho kwamba wananchi wa Zanzibar wanamkubali sana Kiongozi wao na kweli ameanza kuonesha nia na dhamira ya dhati ya kuvibadilisha Visiwa vya Zanzibar.

**10. Mheshimiwa Spika,**mwisholakini si kwa umuhimu, nitoe pongezi kwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), kwako binafsi na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwenu tena kuendelea na nyadhifa hizo. **Ninaamini hii imetokana na uongozi wenu mahiri, hongereni sana!**

## B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2020/2021 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022

### Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2020/2021

**11. Mheshimiwa Spika,**katika mwaka 2020/2021 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Shilingi 902,637,666,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 481,504,753,000 ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi 382,837,810,000 ni za Matumizi Mengineyo na Shilingi 38,295,103,000 ni za Miradi ya Maendeleo.

**12. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya Shilingi 707,165,670,874 zilipokelewa na Wizara. Kati ya fedha hizo, Shilingi 372,544,541,048 zilikuwa ni za Mishahara, Shilingi 294,274,639,436 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 40,346,490,390 ni za Miradi ya Maendeleo. Fedha zilizopokelewa ni sawa na **asilimia 78** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**13. Mheshimiwa Spika,** malengo ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yaliyowekwa kwa mwaka 2020/2021 ni jumla ya Shilingi 488,569,883,000. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya Shilingi 170,364,392,063.50 zilikusanywa kutoka vyanzo mbalimbali. Ukusanyaji wa maduhuli umepungua kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo: ugonjwa wa COVID – 19, upungufu wa vitendea kazi muhimu kama magari na pikipiki, kutokuunganishwa kwa mifumo ya ki-elekroniki kama e-immigration na GePG katika baadhi ya ofisi na upungufu wa watumishi.

### Mafanikio yaliyopatika katika Mwaka 2020/2021

**14. Mheshimiwa Spika,**katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo: kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha

Bidhaa za Ngozi kilichopo Gereza Karanga – Moshi; kukamilika kwa Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Magereza katika eneo la Msalato Jijini Dodoma; kukamilika kwa ujenzi wa Jengo Jipya la Ofisi ya Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dar es Salaam; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 79 za makazi zenye uwezo wa kukaa familia 152 katika vituo vya magereza nchini; na kukamilika nyumba 19 za kuhudumia familia 38 za askari wa Jeshi la Polisi katika mikoa ya Arusha, Geita na Mwanza.

**15. Mheshimiwa Spika,** mafanikio mengine ni:kujengwa kwa Kiwanda Kipya cha Ushonaji wa Sare za Askari katika eneo la Kurasini – Dar es Salaam; kutekelezwa kwa **asilimia 90** ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Chamwino – Dodoma; kujengwa kwa kambi ya mafunzo ya Idara ya Uhamiaji iliyopo eneo la Boma Kichakamiba Wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga; kuzalishwa na kusambazwa vitambulisho 925,342; kuokolewa kwa wahanga 165 wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu; kupatikana kwa suluhisho la kudumu kwa wakimbizi ambapo 31,432 walirejea kwa hiari nchini Burundi na 1,047 walipelekwa katika mataifa mbalimbali; na kutoa mafunzo kwa watumishi 2,087 wa Jeshi la Polisi, 227 wa Jeshi la Magereza, 259 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na 354 wa Idara ya Uhamiaji.

## Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2021/2022

**16. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeweka kipaumbele katika kutekeleza maeneo yafuatayo: kuendelea kudumisha amani na usalama nchini; ujenzi wa ofisi na makazi ya askari; usajili na utambuzi wa watu 1,438,735; kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani; kuendelea kutekeleza Mkakati wa Mapinduzi ya Kilimo kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa na mahabusu; kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata Ngozi katika eneo la Gereza Karanga – Moshi; kukamilisha uunganishaji wa Mfumo wa Udhibiti wa Mipaka (eborder) katika ofisi za uhamiaji za mikoa na wilaya.

**17. Mheshimiwa Spika,** maeneo mengine ya kipaumbele ni:kufanya operesheni maalum na za kawaida, kufanya doria na misako; kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara; kuendelea kudhibiti biashara haramu ya usafirishaji binadamu; kusimamia jumuiya za kidini na zisizo za kidini ili zizingatie masharti ya usajili; kuendelea kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi waliopo nchini; na kutekeleza mikakati ya ukusanyaji mapato ili kufikia lengo lililowekwa.

## HALI YA USALAMA NCHINI

**18. Mheshimiwa Spika,**kwa ujumla nchi yetu imeendelea kuwa katika hali ya amani, utulivu na usalama na kuwezesha wananchi kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Vyombo Vingine vya Usalama nchini viliwezesha kufanyika kwa amani na utulivu Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwezi Oktoba, 2020.

**19. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya makosa makubwa ya jinai yanayojumuisha makosa dhidi ya binadamu, maadili ya jamii na kuwania mali yaliyotolewa taarifa katika Vituo vya Polisi nchini yalikuwa 37,230 ikilinganishwa na makosa 44,277 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Hii inaonesha kuwa makosa 7,047 yamepungua sawa na**asilimia 15.9.**

**20. Mheshimiwa Spika**, kupungua kwa makosa hayo kumetokana na ushirikiano mzuri baina ya Jeshi la Polisi na Vyombo Vingine vya Ulinzi na Usalama, wananchi na wadau wengine, upatikanaji wa taarifa za kiintelijensia kuhusu uhalifu, kuimarika kwa doria, kufanyika kwa misako na operesheni maalum za kitaifa na kimataifa, sambamba na kuendelea kutoa elimu kwa umma. **Ninatoa pongezi za dhati kwa Vyombo Vyote vya Ulinzi na Usalama ambavyo vimeendelea kutimiza majukumu yao ya kuhakikisha nchi inaendelea kuwa salama na tulivu wakati wote.**

**21. Mheshimiwa Spika,** katika kushughulikia makosa yaliyotolewa taarifa katika Vituo vya Polisi, jumla ya kesi 13,842 upelelezi wake ulikamilika na watuhumiwa 8,973 walifikishwa mahakamani, ambapo kesi 2,252 zilishinda na kesi 364 zilishindwa. Katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Polisi litahakikisha kesi zinapelelezwa kwa haraka na litaboresha utendaji kwa kuwajengea uwezo Maafisa, Wakaguzi na Askari ndani na nje ya nchi.

## HALI YA USALAMA BARABARANI

**22. Mheshimiwa Spika,**hali ya usalama barabarani nchini imezidi kuimarika kutokana na usimamizi mzuri wa Jeshi la Polisi kuhusu Sheria za Usalama Barabarani, ushirikiano na wadau mbalimbali, kuongezeka kwa utii wa sheria bila shuruti kwa madereva na makundi mengine ya watumiaji wa barabara na hivyo kuwezesha kupungua kwa matukio ya ajali, vifo na majeruhi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya matukio makubwa ya ajali 1,228 yalitolewa taarifa katika Vituo vya Polisi ikilinganishwa na matukio 1,920 katika kipindi kama hicho mwaka 2020 ikiwa ni sawa na kupungua kwa matukio ya ajali kwa **asilimia 36.04**.

**23. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani limeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi salama ya barabara na elimu ilitolewa katika vipindi 84 kwa njia ya runinga na 1,874 kupitia redio. Elimu hiyo pia imetolewa kwa wanafunzi 760,953 wa shule za msingi, madereva 275,768 wa bodaboda na abiria 5,361,859. Pamoja na kutolewa kwa elimu, hatua kali zilichukuliwa dhidi ya madereva waliokiuka Sheria za Usalama Barabarani zikiwemo kufungiwa leseni kwa Madereva 71. Hatua hizi zimesaidia kuongeza utii wa sheriakwa watumiaji wa barabara.

**24. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Polisi litaendelea kutoa elimu kwa umma, kuchukua hatua kali kwa wanaokiuka sheria, kuanzisha kanzidata ya kuwatambua madereva wa bodaboda na hivyo kuongeza ufanisi katika usimamizi wa usalama barabarani. **Ninatoa wito kwa watumiaji wote wa barabara kuendelea kutii sheria za barabarani ili kuhakikisha usalama wao.**

**Operesheni za Kupambana na Uhalifu**

**25. Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti na kupambana na uhalifu wa aina zote hapa nchini, Jeshi la Polisi limefanya operesheni mbalimbali kwa kushirikiana na taasisi nyingine. Operesheni hizo ni pamoja na kudhibiti upatikanaji wa silaha na risasi za moto na Nyara za Serikali kinyume cha sheria, ukamataji wa dawa za kulevya za viwandani na mashambani na kudhibiti uingizaji wa bidhaa za magendo kutoka nje ya nchi.

**26. Mheshimiwa Spika**, katika operesheni hizo risasi 280 na silaha 134 zilikamatwa zikiwemo SMG (AK 47) nne (4), Shortgun 17,G3 moja (1),Rifle mbili (2),Mark IV moja (1), Pistol 12 na Magobole 97. Aidha, jumla ya watuhumiwa 138walikamatwa na kufikishwa mahakamani na kesi zao zinaendelea. Jeshi la Polisi pia lilifanikiwa kukamata Nyara za Serikali 986 zenye uzito wa kilo 9,862 na gram 375.5 zikiwa na thamani ya Shilingi 1,374,890,427 na watuhumiwa 441 walifikishwa mahakamani. Jeshi la Polisi katika mwaka 2021/2022 litafanya ukaguzi kwa wamiliki wa silaha ili kujiridhisha kuwa wametekeleza kwa ukamilifu matakwa ya sheria husika pamoja na kudhibiti wizi wa Nyara za
Serikali.

**27. Mheshimiwa Spika,** vilevile,Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama limeendelea kufanya operesheni katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji ili kudhibiti vitendo vya uhalifu. Kwa sasa hali ya mipaka hiyo inaendelea kuwa ya amani na utulivu na shughuli za kijamii na kiuchumi zinaendelea kama kawaida.

**28. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha maeneo yote yako salama, Jeshi la Polisi limefanya operesheni za majini katika Ziwa Victoria, Nyasa, Tanganyika na uwanda wa Bahari ya Hindi ili kudhibiti vitendo vya kihalifu. Kupitia operesheni hizo, bidhaa zenye thamani ya Shilingi 249,520,000zilizoingizwa nchini kinyume cha sheria zilikamatwa na watuhumiwa 274 walifikishwa mahakamani. Aidha,ili Jeshi la Polisi liweze kutekeleza operesheni hizo kwa ufanisi zaidi linahitaji vitendea

kazi vya kisasa na vya kutosha. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imelipatia Jeshi hilo jumla ya magari 17 na imetoa jumla ya Shilingi 5,717,242,846.88 kwa ajili ya ununuzi wa magari 16 ya kusindikiza misafara ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Pia, kupitia kwa wadau Jeshi limepata msaada wa magari 12 kutoka UNHCR (10), USAID moja (1) na mtu binafsi moja (1).

**29. Mheshimiwa Spika,** katika utendaji kazi na operesheni mbalimbali kumekuwa na matukio ya Askari kuumia au kupoteza maisha. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 Serikali imelipa fidia ya Shilingi 1,171,725,000 kwa Askari wa Jeshi la Polisi walioumia na waliopoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu yao. Kati ya fedha hizo, Shilingi 856,725,000 zimelipwa kwa Askari 197 walioumia na Shilingi 315,000,000 zimelipwa kwa wasimamizi wa mirathi kwa Askari 21 waliopoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu yao. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za mashujaa wetu hawa mahali pema peponi, Amina!

**Miradi ya Ujenzi wa Makazi, Vituo vya Polisi na Majengo ya Ofisi**

**30. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na makazi ya askari, utekelezaji wa miradi ya ukarabati na ujenzi wa nyumba za makazi, Vituo vya Polisi na majengo ya ofisi unaendelea. Ujenzi wa majengo mawili (2) yaliyoko eneo la Mabatini Jijini Mwanza yenye uwezo wa kuhudumia familia 24 za Askari unaendelea, ambapo jengo moja limekamilika na jingine liko katika hatua za umaliziaji. Jumla ya Shilingi 310,784,594.51 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Aidha, kazi za umaliziaji zinaendelea katika mradi wa ujenzi wa nyumba mbili (2) za kuishi familia nne (4) za Askari Wilayani Meatu - Simiyu kwa gharama ya Shilingi 50,000,000.

**31. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani na fedha za wadau limekamilisha ujenzi wa nyumba 13 za kuishi familia 26 za Askari. Kati ya hizo, nyumba nne (4) zimejengwa eneo la Oljoro Jijini Arusha kwa gharama

ya Dola za Marekani100,000 na nyumba tisa (9) Mkoani Geita kwa gharama ya Shilingi 562,000,000. Aidha, ujenzi wa nyumba 12 za kuishi familia 22 za Askari unaendelea katika maeneo ya Kaskazini Pemba nyumba nne (4), Kusini Pemba nyumba mbili (2), Wilayani Rombo – Kilimajaro nyumba nne (4) na nyumba moja (1) ya Mkuu wa Kituo cha Polisi Uyui (OCS).

**32. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa Vituo vya Polisi na majengo ya ofisi. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Serikali imetoa jumla ya Shilingi 2,978,973,079 kwa ajili ya ujenzi huo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,500,000,000 zitatumika kujenga mabweni na hospitali katika Chuo cha Polisi Kurasini – Dar es Salaam, Shilingi 209,014,249 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "C'' Mkokotoni – Kaskazini Unguja, ambapo kazi za umaliziaji zinaendelea, Shilingi 50,000,000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja ''B'' Wilayani Mbalizi mkoani Mbeya na kwa sasa kazi zinazoendelea ni ujenzi wa vyumba vya mahabusu,Shilingi 347,275,050kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A" katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma ambao hadi sasa ujenzi umefikia hatua ya kumwaga zege ghorofa ya kwanza na Shilingi 899,481,533 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja 'A' Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Kipolisi Temeke ambapo taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea.

**33. Mheshimiwa Spika,** vilevile, Vituo vinne (4) vya Polisi Daraja "C" vimekamilika ambavyo ni Kisiwani wilayani Same, Zembwela na Nyakalilo Wilaya Nyamagana na Keko Mwanga Wilaya ya Temeke. Vituo vitatu (3) vya Daraja "C" vya Ngoyoni Wilaya ya Rombo, Isimani Wilaya ya Iringa Vijijini na Kipili Wilaya ya Sikonge viko katika hatua za umaliziaji. Kituo cha Polisi Daraja "A" Ruangwa mkoani Lindi kimejengwa na wadau na kazi za kuezeka zinaendelea. Pia, jumla ya Shilingi 666,412,620 zimetumika kutoka kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo wa Jeshi la Polisi kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Ushonaji Bohari Kuu ya Polisi, Dar es Salaam ambao umefikia

hatua ya umaliziaji. Aidha, Shilingi 38,370,000 zimetumika kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya Polisi Mkoa wa Simiyu.

**Miradi ya Kipaumbele ya Jeshi la Polisi katika mwaka 2021/ 2022**

**34. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Polisi limepanga kutekeleza miradi ya kipaumbele ambayo ni: kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja 'A' Lushoto Mkoani Tanga kwa Shilingi 250,000,000; kumalizia ujenzi wa jengo la Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara kwa gharama ya Shilingi 450,000,000; kumalizia ujenzi wa kituo cha Polisi Daraja 'C' Ludewa - Njombe kwa gharama ya Shilingi 300,000,000; kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A" Mtumba katika Mji wa Serikali, Dodoma kwa gharama ya Shilingi 601,109,901; kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A" Kigamboni, Dar es Salaam utakao gharimu Shilingi 899,481,533; kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "C'' Nyakanazi, Kagera kwa gharama ya Shilingi 60,000,000; na kukarabati jengo la ofisi Kikosi cha Polisi Anga kwa gharama ya Shilingi 120,000,000.

**35. Mheshimiwa Spika,** pia, ujenzi wa nyumba sita (6) za makazi Ludewa mkoani Njombe za kuhudumia familia 12 za Askari utaendelea kwa gharama ya Shilingi 600,000,000. Vilevile, miradi iliyoanza kutekelezwa kwa nguvu za wananchi itakamilishwa ambapo Shilingi 200,000,000 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa nyumba 12 za makazi, Kaskazini Pemba na Shilingi 200,000,000 zitatumika katika mradi wa nyumba 14 za makazi, Kusini Pemba. Aidha, Shilingi 600,000,000 zimetengwa na Kampuni ya Geita Gold Mine Limited (GGML) kuanza mradi wa ujenzi wa nyumba tano (5) za kuhudumia familia 10 za Askari mkoani Geita.

**36. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Polisi litaendelea kuwashirikisha wadau katika ujenzi wa Vituo vya Polisi, majengo ya ofisi na makazi ya Askari nchini kote, pamoja na kumalizia miradi ya ujenzi iliyosimama. **Hivyo, ninatumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi**

**katika ujenzi wa vituo vya polisi na nyumba za makazi ya Askari ili kuimarisha hali ya ulinzi na usalama nchini.**

### Mafunzo katika Jeshi la Polisi

**37. Mheshimiwa Spika**, kwa lengo la kuimarisha utendaji, Jeshi la Polisi limeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake. Hadi mwezi Machi, 2021 jumla ya watumishi 2,087 walipata mafunzo katika mbinu za upelelezi, sheria, fani ya afya, mafunzo ya utayari, uchunguzi wa makosa ya kimtandao, uchunguzi wa kisayansi, mawasiliano ya Polisi na medani za kijeshi. Kati ya hao, Askari 2,050 na Watumishi raia 24 walipata mafunzo ndani ya nchi na askari 13 nje ya nchi. Aidha, Askari 1,714 wanaendelea na mafunzo ya upandishwaji vyeo ngazi ya Sajini katika Shule ya Polisi Moshi. Katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha utendaji kazi wa watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya kuwajengea uwezo kiutendaji, upandishwaji vyeo pamoja na kuendelea kuwaruhusu watumishi kujiendeleza kitaaluma.

**38. Mheshimiwa Spika**, katika kutoa motisha kwa Askari, Jeshi la Polisi limetoa tuzo na zawadi kwa jumla kwa Askari 94, kati yao saba (7) walipewa barua za pongezi, 41 walipewa vyeti, 33 walipewa jumla ya Shilingi 3,430,000 na Askari 13 walipandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali. Aidha, hatua za kinidhamu zilichukuliwa kwa Askari 287 waliokiuka maadili ya Jeshi na sheria za nchi.

### Kushiriki katika Kuimarisha Ulinzi wa Amani katika Nchi Mbalimbali

**39. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika kuimarisha Ulinzi wa Amani kwenye Mission katika nchi mbalimbali duniani. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Februari, 2021 jumla ya Maofisa, Wakaguzi na Askari 63 wanaendelea kushiriki katika mission ya Ulinzi wa Amani kupitia United Nations African Union Mission in Darfur Sudan Darfur(UNAMID) watendaji 28; United Nations Mission in South Sudan(UNMISS) - 16; United Nations Interim Security Force for

Abyei (UNISFA) - 09 naUnited Nations Organization Stabilization Mission in the Democratic Republic of Congo(MONUSCO) – 10. Aidha, Maofisa wa Polisi watatu (3) wanafanya kazi kwa muda maalum (Secondment) kwenye Ofisi za Umoja wa Mataifa katika nchi za Sudan – Abyei Afisa (1); Sudan Khartoum (1) na Ethiopia (1).

## JESHI LA MAGEREZA

### Hali ya Ulinzi na Usalama Magerezani

**40. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Magereza limeendelea kuwapokea, kuwalinda na kuwapatia huduma muhimu wahalifu wanaoletwa magerezani kwa mujibu wa sheria za nchi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya wafungwa na mahabusu 33,570 walikuwepo katika magereza yote nchini ambapo wafungwa walikuwa 16,850 na mahabusu 16,720.

**41. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarishwa katika magereza nchini, vifaa vya kisasa vya kielektroniki vimefungwa katika Gereza Isanga Jijini Dodoma, kujenga ukuta wa ngome katika Gereza Mkono wa Mara mkoani Morogoro, Gereza Rombo Mkoa wa Kilimanjaro na Gereza Ileje mkoani Songwe na kununua silaha na vifaa vya mawasiliano. Katika mwaka 2021/2022, vifaa kama hivyo vinatarajiwa kufungwa katika Magereza ya Butimba Mkoa wa Mwanza, Ruanda Mkoa wa Mbeya na Gereza Maweni mkoani Tanga pamoja na kukarabati miundombinu ya Magereza ya Isanga, Kondoa, Lindi, Maweni, Mbozi, Mkuza, Mpanda, Kibondo na Songwe.

**42. Mheshimiwa Spika,** kutokana na msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani, Jeshi la Magereza limeendelea kutumia utaratibu wa kifungo cha nje (Extra Mural Labour – EML) ambapo katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya wafungwa 881 walitolewa magerezani (wanaume 689 na wanawake 192). Aidha, wafungwa 3,319 waliachiliwa huru kwa Msamaha wa Mhe. Rais na hivyo kufanya jumla ya wafungwa wote waliotoka gerezani katika kipindi hicho kufikia wafungwa 4,200.

**Programu ya Huduma kwa Jamii na Huduma za Uangalizi**

**43. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeendelea kutekeleza Programu ya Huduma kwa Jamii na Huduma za Uangalizi. Programu hizi zinalenga kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani, kuokoa fedha za Serikali ambazo zingetumika kuwalisha na kugharamia mahitaji ya wafungwa waliopo magerezani, kuwaepusha wafungwa wasio wazoefu kuiga tabia za kihalifu kutoka kwa wafungwa sugu, kuzipatia taasisi za umma nguvu-kazi ya wafungwa badala ya kuajiri vibarua, kuishirikisha jamii kuwarekebisha wafungwa wakiwa ndani ya jamii na kusaidia familia za wafungwa zisitengane kutokana na mzazi au wazazi kufungwa gerezani.

**44. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Wizara ilifanya Uchunguzi wa Kijamii (social enquiries) na kuandaa taarifa za uchunguzi 3,097 zilizowasilishwa mahakamani kwa ajili ya kuiwezesha Mahakama kutoa maamuzi ya kuwaweka wafungwa kwenye vifungo vya nje. Kupitia taarifa hizo jumla ya wafungwa 2,253 walihukumiwa kutumikia adhabu zao kwenye jamii ambapo wanaume walikuwa 1,792 na wanawake 461. Pia, wafungwa 2,365 walimaliza kutumikia vifungo vyao na kurudishwa kwenye jamii kuungana na familia zao.

**45. Mheshimiwa Spika**, kutokana na wafungwa hao kutekeleza adhabu zao nje ya magereza, Serikali imeweza kuokoa Shilingi 1,520,775,000 ambazo zingetumika kuwalisha wafungwa hao kama wangeendelea kukaa gerezani (kwa wastani wa Shilingi 2,500 kwa mfungwa kwa siku moja). Aidha, wafungwa hao wamefanya kazi kwenye taasisi za umma ambazo kama zingeajiri vibarua zingeigharimu Serikali jumla ya Shilingi 1,622,160,000 sawa na wastani wa malipo ya Shilingi 4,000 kwa kibarua kwa siku.

**46. Mheshimiwa Spika**, vilevile, wigo wa utekelezaji wa Sheria ya Huduma kwa Jamii, Sura ya 291 na Sheria ya Huduma za Uangalizi na Ujenzi wa Tabia, Sura ya 247 umeongezeka

baada ya kujumuisha Mikoa ya Lindi, Ruvuma na Katavi. Hatua hii imewezesha mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kupata huduma ya vifungo vya nje. Katika mikoa hiyo mitatu (3) jumla ya wafungwa 35 waliweza kutumikia vifungo vyao nje ya magereza. Aidha, elimu imetolewa katika mikoa yote ya Tanzania Bara ili kujenga uelewa wa wadau kuhusu utekelezaji wa sheria hizo.

**47. Mheshimiwa Spika**, wafungwa waliopo kwenye Programu ya Huduma kwa Jamii na Huduma za Uangalizi wameendelea kusimamiwa na kufuatiliwa kwenye maeneo wanapofanyia kazi na kwenye makazi wanayoishi ili kuzuia wasiendelee kutenda vitendo vya kihalifu. Programu za urekebishaji zilifanyika kwa wafungwa hao kulingana na mahitaji ya kila mfungwa, ambapo wafungwa 621 walifundishwa stadi za kazi na maisha na wafungwa 2,005 walipewa ushauri nasaha ili kuwasaidia kuishi maisha yasiyo tegemea uhalifu. Wafungwa 73 waathirika wa dawa za kulevya na tisa (9) waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI waliunganishwa na taasisi zinazotoa huduma za matibabu na ushauri nasaha.

**48. Mheshimiwa Spika,**kwa mwaka 2021/2022, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itawasimamia na kuwafuatilia wafungwa 5,000 wanaotegemewa kutumikia adhabu chini ya Programu ya Huduma kwa Jamii na Huduma za Uangalizi. Kazi zitakazofanyika ili kufikia azma hii ni: na kutoa elimu ya utekelezaji wa adhabu mbadala kwa Majaji, Mahakimu, Makarani wa Mahakama, Watendaji wa Mahakama, Waendesha Mashtaka, Maafisa wa Polisi na Magereza, Maafisa wa Probesheni na jamii kwa ujumla.

**49. Mheshimiwa Spika,** kazi nyingine zitakazofanyika ni: kufanya uchunguzi wa kijamii na kuandaa taarifa; kutekeleza programu za urekebishaji; na kukagua taasisi zinazowatumia wafungwa wa kifungo cha nje kufanya kazi za vibarua ili kujiridhisha kama zimekidhi vigezo vya kupokea wafungwa hao. Kiasi cha Shilingi 1,245,586,000 kimetengwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022 kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo.

**Kujitegemea kwa Chakula cha Wafungwa na Mahabusu**

**50. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Magereza linaendelea kutekeleza Mpango wa Mapinduzi ya Kilimo wa 2020/2021 – 2024/2025 kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa na mahabusu. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020 Jeshi la Magereza lililima ekari 4,200 za mahindi, 975 za mpunga, 433 za maharage na ekari 661 za alizeti na kufanikiwa kuvuna tani 4,720 za mahindi, tani 1,120 za mpunga, tani 298 za maharage na tani 43.6 za alizeti.

**51. Mheshimiwa Spika,** katika msimu wa mwaka 2020/2021, Jeshi limelima na kupanda jumla ya ekari 11,185, ambapo 5,465 zimepandwa mahindi, 2,511 mpunga, 1,331 maharage na 1,490 zimepandwa alizeti kwa matarajio ya kuvuna tani 5,530.73 za mahindi, tani 1,478.63 za mpunga, tani 299.60 za maharage na tani 458.70 za alizeti. Katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Magereza limetengewa Shilingi 6,000,000,000 kwa ajili ya kuendelea kutekeleza Mkakati wa Mapinduzi ya Kilimo. Fedha hizi zitatumika kuongeza zana za kilimo, pembejeo na kujenga maghala nane (8) ya kuhifadhia mazao katika Magereza ya Arusha, Kitai mkoani Ruvuma, Kitengule mkoani Kagera, Mollo Mkoa wa Rukwa, Pawaga Mkoa wa Iringa, Songwe Mkoa wa Mbeya, Ubena mkoani Pwani na Ushora Mkoa wa Singida.

**52. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Magereza limepata kibali cha kuzalisha mbegu bora kutoka Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania (Tanzania Official Seed Certification Institute – TOSCI) kwa ajili ya matumizi yake na kusambaza kwa wakulima. Mbegu za mahindi aina ya UH 615 zimelimwa katika Gereza Kitai Mkoa wa Ruvuma ekari 50, mpunga aina ya TXD 88 ekari 50 Gereza Idete Mkoa wa Morogoro, maharage aina ya Jesca Gereza Kisongo Mkoa wa Arusha ekari 33 na alizeti aina ya record Gereza Ushora Mkoa wa Singida ekari 50.

**53. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha shughuli za kilimo na kudhibiti upotevu wa mazao mashambani wakati wa uvunaji, Jeshi la Magereza limenunua matrekta mawili (2) na

mashine tatu (3) za kuvunia mazao ya kilimo (Combine harvester). Aidha, Serikali imetoa jumla ya Shilingi 1,515,000,000 kwa Jeshi la Magereza kwa ajili ya ununuzi wa zana za kilimo yakiwemo matrekta nane (8) na Shilingi 2,100,000,000 kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji Gereza Idete mkoani Morogoro.

**54. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza juhudi za Serikali za kufufua zao la chikichi nchini, Jeshi la Magereza limeotesha zaidi ya miche 179,000 ya mbegu bora za chikichi na kulima ekari 520 katika Gereza Kwitanga mkoani Kigoma, kati ya hizo ekari 370 zimeshapandwa mbegu mpya ya michikichi na upandaji unaendelea katika eneo lililobaki. Katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo (TARI)linatarajia kulima na kupanda ekari 2,000 za chikichi, kuzalisha mbegu bora za zao hilo na kuzisambaza kwa wakulima wadogo.

**Uboreshaji wa Mazingira ya Kazi na Makazi ya Maafisa na Askari Magereza**

**55. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya kazi, Jeshi la Magereza limekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu katika eneo la Msalato Dodoma ambayo ilizinduliwa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 04 Februari, 2021. Aidha, jumla ya Shilingi 2,500,000,000 zilitolewa kwa ajili ya kuendelea na kazi zote katika eneo hilo ambazo zinahusisha: ujenzi wa uzio wenye urefu wa mita 1,046 ambapo mita 802 zimeshajengwa; ujenzi wa nyumba za walinzi; usanifu wa mazingira; ujenzi wa tanki kubwa lenye uwezo wa kuhifadhi maji lita 130,000 kwa ajili ya matumizi ya ofisi na nyumba za Maafisa na Askari zitakazojengwa eneo hilo; na ujenzi wa ukumbi na viwanja vya michezo.

**56. Mheshimiwa Spika**, vilevile, ujenzi wa Ofisi ya Magereza Mkoa wa Dar es Salaam umekamilika. Aidha, Serikali ilitoa Shilingi 3,500,000,000 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa nyumba 173 zenye uwezo wa kukaa familia 326 zilizokuwa zimeanza kujengwa kwa kutumia rasilimali zinazopatikana

katika maeneo ya magereza. Kati ya hizo, nyumba 79 za kuishi familia 152 zimekamilika na nyumba 94 za kuishi familia 174 zinaendelea kukamilishwa.

**57. Mheshimiwa Spika**, mwezi Februari, 2021 Serikali imetoa Shilingi 7,280,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za maafisa na askari 119 za kuishi familia 210 katika maeneo ya magereza nchini. Kati ya fedha hizo, Shilingi 3,960,000,000 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 58 za kuishi Maafisa na Askari 98 wa Makao Makuu ya Jeshi la Magereza eneo la Msalato, Dodoma na Shilingi 3,320,000,000 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 61 za kuishi familia 112 za Maafisa na Askari katika mikoa mbalimbali. Ujenzi wa nyumba hizo umeanza na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**58. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2021/2022, Jeshi la Magereza linatarajia kujenga nyumba 129 za makazi ya maafisa na askari kulingana na rasilimali zinazopatikana katika magereza husika. Ujenzi huo utasaidia kupunguza changamoto ya nyumba za makazi ambapo kwa sasa zipo nyumba 5,057 ikilinganishwa na mahitaji ya nyumba 12,500 zinazohitajika.

**59. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha utendaji kazi wa Jeshi la Magereza, Serikali imelipatia Jeshi hilo magari tisa (9) kwa ajili ya shughuli za utawala. Magari hayo yamesaidia kupunguza changamoto ya usafiri kwa Viongozi Waandamizi wa Jeshi la Magereza. Aidha, kwa mwaka 2021/2022, kiasi cha Shilingi 4,661,416,000 kimetengwa kwa ajili ya kununua magari 23 ya shughuli za Jeshi la Magereza.

**Utekelezaji wa Lengo la Uchumi wa Viwanda**

**60. Mheshimiwa Spika,** katika kusaidia kufikiwa kwa lengo la uchumi wa viwanda, Jeshi la Magereza linakamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kiwanda cha Samani Msalato na ufungaji wa mashine. Ujenzi huo ulioanza mwezi Machi, 2020 umefikia zaidi ya **asilimia 90**na utakamilika mwezi Juni, 2021. Jiwe la msingi la ujenzi wa kiwanda hicho liliwekwa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 04 Februari, 2021.

**61. Mheshimiwa Spika,** kazi zinazoendelea katika ujenzi wa kiwanda hicho ni uwekaji wa mifumo ya umeme, majisafi na majitaka na kuboresha mazingira yanayozunguka kiwanda (landscaping). Gharama za ujenzi na ufungaji wa mashine katika kiwanda hicho ni Shilingi 2,000,000,000. Katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Magereza limepanga kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa kiwanda cha samani kwa kujenga jengo la kuuzia samani (Show room) eneo la Isanga – Dodoma na ununuzi wa malighali kwa ajili ya kuanza uzalishaji wa samani, ambapo jumla ya Shilingi 1,000,000,000 zimetengwa.

**Shirika la Magereza**

**62. Mheshimiwa Spika,** kupitia Shirika la Magareza, Jeshi limefanikiwa kujenga kiwanda kipya Mjini Moshi cha kuzalisha bidhaa za ngozi (Kilimanjaro International Leather Industry Co. Ltd) kwa ubia na PSSSF. Ujenzi huo umegharimu Shilingi 9,637,282,548. Kiwanda hiki chenye uwezo wa kuzalisha jozi 3,000 za viatu kwa siku kilizinduliwa tarehe 22 Oktoba, 2020 na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Vilevile, ujenzi wa kiwanda kingine cha kuchakata ngozi katika eneo hilo umefikia **asilimia 75** na umepangwa kukamilika mwezi Mei, 2021. Aidha, ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza soli za viatu umekamilika na ufungaji wa mashine unaendelea.

**63. Mheshimiwa Spika,** Shirika limekamilisha ujenzi wa majengo mbalimbali ya Kiwanda cha Sukari cha Kampuni Hodhi ya Mkulazi. Majengo hayo ni: jengo la utawala ambalo lina thamani ya Shilingi 1,085,915,768; jengo la zahanati lenye thamani ya Shilingi 270,584,513.80; nyumba saba (7) za watumishi zenye thamani ya Shilingi 664,924,108.85; na ujenzi wa uzio wa kiwanda wenye thamani ya Shilingi 323,931,243 kuzunguka eneo la kiwanda.

**Kampuni ya Ulinzi ya Shirika la Magereza (SHIMA Guard)**

**64. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Magereza limeanzisha Kampuni Tanzu ya Ulinzi ijulinakayo kama SHIMA Guard ambayo ilisajiliwa na BRELA tarehe 23 Oktoba, 2020. Kampuni

hiyo imeanza kutoa huduma sehemu mbalimbali kuanzia tarehe 01 Februari, 2021. Taasisi zilizoanza kupatiwa huduma ya ulinzi ni: Kampuni ya Mkulazi Morogoro walinzi 58; Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Dodoma walinzi saba (7); GPSA Dodoma walinzi watatu (3); Kampuni ya Kilimanjaro International Leather Industries walinzi 10; Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti walinzi saba (7); Shule ya Sekondari Bwawani walinzi sita (6); na Eneo la biashara Gereza Isanga walinzi wawili (2). Aidha, Menejimenti ya SHIMA Guard inaendelea kupeleka maombi ya zabuni ya kutoa huduma ya ulinzi sehemu mbalimbali za taasisi, mashirika ya umma na ya watu binafsi.

**65. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza thamani ya mazao ya mifugo, Shirika la Magereza linajenga Kiwanda kidogo cha Maziwa katika Shamba la Mifugo la Magereza Kingolwira mkoani Morogoro na ujenzi wa jengo la kiwanda umefika **asilimia 90** na utakamilika kabla ya mwezi Juni, 2021. Kiwanda hiki kitakapokamilika kitachakata wastani wa lita 1,000 za maziwa kwa siku kwa ajili ya kutengeneza bidhaa za maziwa. Maziwa hayo yatatoka kwenye shamba hilo na mengine kutoka kwa wananchi. Kwa sasa, taratibu za ununuzi wa mashine za kuchakata mazao yatokanayo na maziwa kwa ajili ya kiwanda hicho zinaendelea.

## Mafunzo na Ajira kwa Watumishi

**66. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza weledi wa utendaji kazi kwa Jeshi la Magereza, jumla ya Maafisa na Askari 227 walipata mafunzo ya uongozi wa ngazi za juu na taaluma ya urekebishaji katika Vyuo vya Magereza vilivyopo Ukonga Mkoa wa Dar es Salaam, Kingolwira Mkoa wa Morogoro, Ruanda na Kiwira Mkoa wa Mbeya. Aidha, Maafisa na Askari wengine 553 wanaendelea na mafunzo ya taaluma mbalimbali katika vyuo vya ndani na nje ya Jeshi. Katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Magereza litatoa fursa za masomo kwa watumishi wenye sifa za kujiendeleza. Vilevile, Jeshi litaendesha mafunzo kwa Maafisa na Askari 3,250 kwa lengo la kuwaweka tayari kutekeleza majukumu yao.

**67. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Magereza lina jumla ya Maafisa na Askari 12,767 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Maafisa na Askari 29,796 ikiwa ni upungufu wa Askari 17,029. Katika kukabiliana na upungufu huo, kwa mwaka 2021/2022, Jeshi la Magereza linatarajia kuajiri askari 853watakaopatiwa mafunzo ya awali katika Chuo cha Magereza Kiwira kilichopo Mkoani Mbeya.

**JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

**68. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi, ambapo limefanya ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto katika magari na maeneo mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya maeneo 36,703 yalikaguliwa, ambapo kiasi cha Shilingi 5,257,551,500 kilikusanywa kutokana na ukaguzi huo. Aidha, Jeshi limefanikiwa kuzima moto na kufanya uokoaji katika matukio 2,172.

**69. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha huduma za zimamoto na uokoaji, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchiimekamilisha taratibu za ununuzi wa magari matatu (3) mapya ya kuzima moto ambayo yataundwa na Shirika la Nyumbu (TATC). Gharama ya magari hayo ni Shilingi 2,977,500,000 ikiwa ni sawa na Shilingi 992,500,000 kwa kila gari na yatakamilika mwezi Juni, 2022. Kwa sasa Shilingi 2,233,125,000 zimelipwa kwa Shirika hilo ikiwa ni sehemu ya malipo ya awali (advance payment) ya **asilimia 75**. Pia, magari 26 ya kuzima moto yaliyoharibika yalipelekwa Shirika hilo kwa ajili ya matengenezo. Matengenezo ya magari saba (7) yamekamilika na magari mengine 19 yanatarajiwa kukamilishwa katika mwaka 2021/2022.

**70. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepata msaada wa magari 10 ya utawala kutoka kwa wadau wa ndani, gari moja (1) la kuzima moto na vifaa mbalimbali vya kuzima moto na uokoaji kutoka nchini Ujerumani. Aidha, katika mwaka 2021/2022, Jeshi limepanga kununua magari mawili (2) ya kuzima moto na magari nane (8) ya utawala pamoja na vifaa vya kuzima moto na uokoaji.

## Miradi Inayotekelezwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

**71. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2020/2021, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatekeleza miradi ya maendeleo inayohusu kuongeza huduma za zimamoto na uokoaji pamoja na ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari. Miradi hiyo inatekelezwa kwa utaratibu wa Force Account nahatua za utekelezaji ni kama ifuatavyo:

### Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maafisa na Askari Eneo la Kikombo Jijini Dodoma

**72. Mheshimiwa Spika,** ujenzi huu unahusisha majengo nane (8) ya kuishi familia 80 za Askari kwa gharama ya Shilingi 6,388,760,000. Fedha za ujenzi wa nyumba hizo ilikuwa ni ahadi ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mradi ulianza kutekelezwa tarehe 06 Julai, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2021. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa majengo sita (6) yenye ghorofa tano (5), ambapo jumla ya Shilingi 2,972,074,000 zimetumika. Aidha, misingi ya majengo mengine mawili (2) imekamilika.

### Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto Wilaya ya Chamwino na Nzuguni – Dodoma

**73. Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa kituo hicho ulianza kutekelezwa tarehe 10 Agosti, 2020 kwa gharama ya Shilingi 1,193,000,000 zilizotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mfuko wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Jiji la Dodoma. Ujenzi umefikia **asilimia 75** ambapo kazi zilizofanyika ni kujenga majengo manne (4) ambayo ni: jengo la utawala; mawasiliano; Kantini na maliwato. Ujenzi wa kituo hicho utakamilika tarehe 30 Juni, 2021. Vilevile, taratibu za ujenzi wa kituo cha zimamoto na uokoaji katika eneo la Nzuguni Jijini Dodoma zinaendelea. Mradi huo unatarajiwa kugharimu Shilingi1,250,000,000 hadi kukamilika kwake.

**74. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Jeshi la Zimamoto na Ukoaji litakamilisha mradi wa ujenzi wa Nyumba

za Maafisa na Askari katika eneo la Kikombo Jijini Dodoma, Kituo cha Zimamoto na Uokoaji, Nzuguni Jijini Dodoma na kukarabati Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Ilala, Jijini Dar es Salaam.

**Mafunzo na Ajira kwa Watumishi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**75. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa Rasilimaliwatu, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kuajiri Askari 340 katika mwaka 2021/2022. Askari watakaoajiriwa watapatiwa mafunzo ya awali ya kuzima moto nauokoji katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo (Handeni) Mkoani Tanga. Aidha, katika kipindi hicho, Maafisa na Askari 956 watapandishwa vyeo. Vilevile, katika kuboresha utendaji wa watumishi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kutoa mafunzo kwa Maafisa na Askari 658, ambapo katika mwaka 2020/2021 lilitoa mafunzo kwa Maafisa na Askari 259.

**IDARA YA UHAMIAJI**

**76. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uhamiaji imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya utoaji wa huduma kwa wageni na raia kupitia mfumo wa kielektroniki. Kwa sasa usimikaji wa mfumo wa usimamizi na udhibiti wa mipaka (eborder system) unakamilishwa katika ofisi za Uhamiaji za Mikoa. Kwa ujumla, matumizi ya mfumo wa kieletroniki umeiwezesha Serikali kupata faida nyingi ambazo ni pamoja na: kuimarika kwa ulinzi na usalama wa nchi kwa kudhibiti uingiaji, ukaaji na utokaji wa watu; kupungua kwa gharama za ununuzi wa malighafi na vitendea kazi; kutoa huduma za kiuhamiaji katika viwango na ubora wa kimataifa; na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

**77. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali, zoezi la kuunganisha mfumo wa malipo ya Serikali (GePG) linaendelea katika ofisi za uhamiaji za mikoa, wilaya na vituo vyote vya mipakani. Hadi kufikia mwezi

Machi, 2021 mfumo huo umeunganishwa katika ofisi za uhamiaji za mikoa 29 kati ya mikoa 31, vituo 16 kati ya 42 vya kuingia na kutoka nchini na ofisi 44 za Ubalozi wa Tanzania. Katika mwaka 2021/2022 zoezi la uunganishaji wa mfumo huo litaendelea katika mikoa na vituo vya uhamiaji vilivyobaki.

**Udhibiti wa Uingiaji, Ukaaji na Utokaji wa Wageni**

**78. Mheshimiwa Spika**, kuanzia mwezi Julai 2020 hadi Machi, 2021 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Uhamiaji imesimamia uingiaji wa jumla ya wageni 511,243 ikilinganishwa na wageni 1,158,022 waliongia katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Aidha, jumla ya wageni 421,687 walitoka nchini ikilinganishwa wageni 1,048,149 waliotoka kwa mwaka 2019/2020. Katika kipindi hicho jumla ya wageni 201 walizuiliwa kuingia nchini kutokana na sababu za kiusalama na kutokidhi vigezo vya kiuhamiaji. Idadi ya wageni waliongia na kutoka nchini kwa mwaka 2020/2021 imepungua ikilinganishwa na mwaka 2019/2020 kutokana na ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID19).

**79. Mheshimiwa Spika,** vilevile, jumla ya vibali vya ukaazi 12,676 (Daraja "A" 2,353; Daraja "B" 7,007; na Daraja "C" 3,316) vilitolewa kwa wageni walioingia nchini kwa madhumuni mbalimbali ikilinganishwa na vibali 14,202 (Daraja A 1,964, Daraja B 8,644 na Daraja C 3,594) vilivyotolewa kwa mwaka 2019/2020. Idadi ya vibali hivyo imepungua kwa**asilimia 10.74** kutokana na COVID - 19 ambapo wageni wengi hawakuingia nchini. Jumla ya Hati za Mfuasi 2,694 zilitolewa ikilinganishwa na Hati 2,078 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Aidha, Hati za Msamaha 1,299 zilitolewa ikilinganishwa na Hati 1,624 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020.

**80. Mheshimiwa Spika,** jumla ya visa 224,544 zilitolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2021 ambapo visa za matembezi ni 203,324, biashara 20,929 na kidiplomasia 291 ikilinganishwa na visa 337,411 zilizotolewa kwa mwaka 2019/2020. Kati ya hizo,visaza matembezi zilikuwa 313,744, biashara 22,235, wanafunzi 908 na kidiplomasia 524.

**Pasipoti na Hati Nyingine za Safari**

**81. Mheshimiwa Spika**, Idara ya Uhamiaji ilitoa jumla ya Pasipoti 54,072 kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali. Kati ya hizo, Pasipoti za Kidiplomasia ni 133; Kiutumishi ni 22 na za Kawaida ni 53,917. Vilevile, jumla ya Hati za Safari za Dharura 164,506 zilitolewa. Aidha, Watanzania 310 waliokwenda nje ya nchi kinyume na taratibu za uhamiaji walirudishwa nchini.

**Misako, Doria na Ukaguzi wa Vibali vya Ukaazi**

**82. Mheshimiwa Spika**, shughuli za misako, doria na kaguzi zimeendelea kufanyika kupitia Idara ya Uhamiaji hasa katika maeneo ya mipakani, migodini, viwandani, hotelini na kwenye mashamba makubwa kwa lengo la kudhibiti wahamiaji haramu ikiwa ni pamoja na kuwabaini wageni wanaofanya kazi kinyume na sheria. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya watuhumiwa 15,786 wa makosa ya kiuhamiaji walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Katika kuimarisha shughuli za misako na doria Serikali imetoa magari 16 kwa Idaraya Uhamiaji. Aidha, ununuzi wa magari sita (6) umekamilika kati ya hayo mawili (2) yamepokelewa na magari manne (4) yanatarajiwa kupokelewa kabla ya mwezi Juni, 2021.

**83. Mheshimiwa Spika**, vilevile, zoezi la kuwatambua na kuwasajili wahamiaji walowezi kwa kutumia Mfumo wa Udhibiti wa Mipaka limeanza katika Mkoa wa Tanga ili kuwapatia vibali stahiki. Hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya walowezi 4,700 walisajiliwa katika mfumo huo.

**Wageni Walioomba na Kupewa Uraia wa Tanzania**

**84. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya wageni 52 walipewa uraia wa Tanzania. Wageni waliopewa uraia wa Tanzania kwa kipindi hicho ni kutoka mataifa ya Cameroon (1), Ghana (1), India (20), Kenya (3), Lebanon (2), Pakistani (4), Somalia (2), Uganda (1), Uingereza (2), Uturuki (1), Yemeni (12) na wasiokuwa na utaifa – Stateless (3).

**Watanzania Waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine**

**85. Mheshimiwa Spika,** Watanzania 57 waliukana uraia na kupata uraia wa mataifa mengine kama ifuatavyo: Afrika Kusini (1), Australia (2), Austria (1), Botswana (3), Canada (9), India (5), Italia (2), Kenya (3), Lebanon (1), Marekani (10), Namibia (1), Netherland (1), Oman (1), Rwanda (2), Uganda (1), Uingereza (5), Ujerumani (8) na Yemen (1).

**Mafunzo, Ajira na Upandishwaji Vyeo kwa Askari na Watumishi wa Idara ya Uhamiaji**

**86. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya Maafisa na Askari 322 na watumishi raia 42 walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo kiutendaji ndani na nje ya nchi. Jumla ya Maafisa na Askari 300 walihitimu mafunzo ya uongozi katika Kambi ya Mafunzo ya uhamiaji Boma kichakamiba mkoani Tanga. Aidha, jumla ya Askari 54 walipandishwa vyeo. Katika mwaka 2021/2022, Idara ya Uhamiaji itaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa, Askari na watumishi raia ili kuwaongezea ujuzi na weledi. Pia, Idara ya Uhamiaji inatarajia kuajiri Askari 312 na kuwapandisha vyeo Askari 466.

**Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Askari wa Uhamiaji**

**87. Mheshimiwa Spika**, Idara ya Uhamiaji inatekeleza mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu Jijini Dodoma. Mradi huo unatekelezwa na SUMA JKT kwa gharama ya Shilingi 20,283,000,000. Jengo hilo litakuwa na ghorofa nane (8) na hadi kufikia mwezi Machi, 2021 ujenzi ulifikia katika ghorofa ya nne (4). Pia, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Chato lenye ghorofa moja (1) unaendelea na umefikia **asilimia 60** na utakamilika mwezi Juni, 2021.

**Miradi na Maeneo ya Kipaumbele ya Idara ya Uhamiaji katika Mwaka 2021/2022**

**88. Mheshimiwa Spika,** katikamwaka 2021/2022,Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Uhamiaji

itaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu Jijini Dodoma. Wizara pia itakamilisha ujenzi wa majengo ya ofisi zilizopo katika Mikoa ya Geita kwa gharama ya Shilingi 813,493,813; Mtwara Shilingi 878,667,544; na Lindi Shilingi 297,322,483. Aidha, makazi ya Maafisa na Askari wa Uhamiaji yataboreshwa kwa kufanya ukarabati wa nyumba katika Mikoa ya Tabora na Pwani ambapo jumla ya Shilingi 300,000,000 zimetengwa; kukarabati Ofisi ya Uhamiaji Kurasini - Dar es Salaam kwa Shilingi 100,000,000.

**89. Mheshimiwa Spika,** miradi mingine itakayotekelezwa ni:ununuzi wa nyumba 12 za makazi katika eneo la Msamala mkoani Ruvuma na bajeti iliyotengwa ni Shilingi 250,000,000; ujenzi wa madarasa katika Kambi ya Mafunzo ya Uhamiaji Boma Kichakamiba mkoani Tanga Shilingi 900,000,000; ujenzi wa nyumba ya Kamishna Jenerali Jijini Dodoma kwa Shilingi 400,000,000; ukarabati wa majengo mbalimbali katika Mikoa ya Pwani na Tabora Shilingi 110,516,159; na ununuzi wa magari sita (6) ambayo yametengewa Shilingi 960,000,000.

## MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)

### Usajili na Utambuzi wa Watu

**90. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ina wajibu wa kuhakikisha watu wote wenye sifa wanasajiliwa na kupewa Vitambulisho vya Taifa. Vitambulisho hivyo hutolewa kwa raia wa Tanzania, wageni wakaazi na wakimbizi. Vilevile, NIDA inajukumu la kuunganisha taasisi za umma na binafsi zinazotoa huduma kwa wananchi katika mfumo wa usajili na utambuzi.

**91. Mheshimiwa Spika,**hadi kufikia Machi, 2021 usajili wa wananchi umeongezeka na kufikia watu 22,345,948 ikilinganishwa na lengo la kusajili watu 25,237,954. Jumla ya wageni wakaazi 32,170 na wakimbizi 213,251 wamesajiliwa. Pia, hadi Machi 2021 Namba za Utambulisho (NIN) 18,762,822 zimezalishwa na kugawiwa kwa wananchi. Aidha, Mamlaka ipo katika maandalizi ya ujenzi wa ofisi ya usajili na utambuzi

katika eneo la mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere Hydroelectric Power (JNHPP) utakaogharimu takribani Shilingi 100,000,000.

**92. Mheshimiwa Spika,** NIDA imezalisha na kusambaza vitambulisho 925,342 na hivyo kufanya idadi ya vitambulisho vilivyozalishwa na kusambazwa hadi Machi, 2021 kufikia 7,028,567 katika wilaya 34 za Tanzania Bara na Zanzibar. Kazi ya uzalishaji vitambulisho katika wilaya 116 zilizobaki inaendelea na inatarajiwa hadi kufikia mwezi Julai, 2021 watu wote wenye Namba za Utambulisho watapata vitambulisho. Aidha, Namba za Utambulisho 13,932,455 zilitumika katika usajili wa simu kwa lengo la kuimarisha usalama. Mamlaka pia, imenunua magari manne (4) kwa ajili ya kuwezesha shughuli za usajili na utambuzi.

**93. Mheshimiwa Spika,**ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi, NIDA imeendelea kuunganisha taasisi za umma na binafsi katika Kanzidata yake. Lengo ni kuwawezesha wadau kuhakiki taarifa za watu wanaopata huduma na hivyo kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa jamii na kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi. Kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021 Mikataba 45 ya ushirikishanaji taarifa (Data Sharing Agreement) imesainiwa namaombi mengine 22 ya wadau yanashughulikiwa. Kupitia mikataba hiyo, NIDA iliweza kuvuka lengo kwa kukusanya jumla ya Shilingi 10,373,757,867 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya Shilingi 8,165,310,500 sawa na **asilimia 127**.

## Kuboresha Mtandao wa Mawasiliano katika Ofisi za NIDA

**94. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ipo katika hatua za mwisho za kuweka mtandao wa mawasiliano katika ofisi tisa (9) za NIDA za wilaya ambazo tayari zimefikiwa na Mkongo wa Taifa. Wilaya hizo ni Gairo, Kalambo, Kiteto, Nyang'hwale, Serengeti, Siha, Sikonge, Simanjiro na Wanging'ombe. Uunganishwaji wa wilaya hizo utakamilika ndani ya mwezi Mei, 2021 na hivyo kubaki wilaya 14 ambazo bado hazijaunganishwa na mtandao wa mawasiliano.

**Kazi za Kipaumbele kwa Mwaka 2021/2022**

**95. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, NIDA itaendelea na zoezi la usajili na utambuzi katika wilaya na mikoa yote nchini na jumla ya watu 1,438,735 wanatarajiwa kusajiliwa. Sanjari na zoezi hilo, elimu kwa umma itaendelea kutolewa kuhusu umuhimu wa usajili na utambuzi na itasaidia katika kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi pamoja na uchumi shirikishi.

**96. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia NIDA itakamilisha upembuzi yakinifu ili kupata njia mbadala ya kuunganisha ofisi za wilaya 14 ambazo hazijafikiwa na Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa. Wilaya hizo ni Ngorongoro mkoani Arusha, Mbulu – Manyara, Micheweni – Kaskazini Pemba, Mbogwe – Geita, Uyui – Tabora, Kyerwa – Kagera, Magharibi 'B' – Mjini Magharibi, Mlele – Katavi, Kusini – Kusini Unguja, Buhigwe – Kigoma, Malinyi na Ulanga – Morogoro, Kaskazini 'A' na Kaskazini 'B' – Kaskazini Unguja. Mamlakapia, inatarajia kuunganisha taasisi nyingine 43 za umma na binafsi katika Kanzidata ya Mamlaka ili kuendelea kurahisisha utoaji wa huduma za utambuzi kwa wananchi.

**97. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imetenga jumla ya Shilingi 10,080,000,000 kwa ajili ya shughuli za usajili na utambuzi. Kati ya fedha hizo Shilingi 10,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 80,000,000 ni fedha za nje kutoka Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini.

**USAJILI NA USIMAMIZI WA JUMUIYA ZA KIDINI NA ZISIZO ZA KIDINI**

**98. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ina jukumu la kusajili Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini, kufuatilia utendaji, uendeshaji na kushiriki katika utatuzi wa migogoro ya jumuiya zilizosajiliwa. Kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla maombi ya usajili wa jumuiya 331 yalipokelewa. Jumuiya 124 zilisajiliwa kati ya hizo, 10 ni za kidini na 114 zisizo za kidini. Maombi

matatu (3) yamekataliwa kwa kutokutimiza vigezo vya kusajiliwa na 104 yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, migogoro 11 imesuluhishwa, kati ya hiyo migogoro tisa (9) ni ya Jumuiya za Kidini na miwili (2) ni ya Jumuiya zisizo za Kidini.

**99. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msajili wa Jumuiya inafuatilia utendaji na uendeshaji wa jumuiya zilizosajiliwa ili kuhakikisha zinazingatia sheria. Uhakiki wa takwimu umefanyika kwa jumuiya zote zilizosajiliwa kuanzia mwaka 1955 hadi 2021, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2021 jumla ya jumuiya 9,836 zimesajiliwa. Kati ya hizo, Jumuiya za Kidini 992 na zisizo za Kidini 8,844. Aidha, Uhakiki wa jumuiya katika Kanda ya Kaskazini ulifanyika katika wilaya 17 kati ya 20 katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga, ambapo jumla ya jumuiya 125 zilizosajiliwa zilihakikiwa.

**100. Mheshimiwa Spika**, kupitia uhakiki huo, jumla ya watu 425 walipatiwa elimu kuhusu aina ya vikundi vinavyopaswa kusajiliwa, taratibu za usajili wa jumuiya na kazi zinazofanywa na Ofisi ya Msajili wa Jumuiya. Vilevile, elimu imetolewa kwa vikundi vya wajasiriamali, vijana na wanawake juu ya umuhimu wa kusajiliwa ili viweze kuingia katika mfumo rasmi utakaorahisisha vikundi hivyo kufikiwa na programu mbalimbali za maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 127 ya Ilani ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025. **Ninatoa wito kwa vikundi ambavyo havijasajiliwa vifike Ofisi ya Msajili wa Jumuiya kwa ajili ya kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337.**

**101. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya imetenga jumla ya Shilingi 310,048,000 kwa ajili ya shughuli za kuhakiki, kusajili na kufuatilia utendaji wa jumuiya kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337; kufungua Ofisi nne (4) za Msajili wa Jumuiya katika Kanda ya Mashariki kwenye Mkoa wa Dar es Salaam na Kanda ya Ziwa mkoani Mwanza, Nyanda za Juu Mkoa wa Mbeya na Kanda ya Kaskazini Mkoa wa Kilimanjaro kwa lengo la kurahisisha utoaji huduma kwa jamii. Kazi nyingine zitakazofanyika ni: kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kusajili vikundi na vyama

mbalimbali vya kijamii; kukamilisha na kuanza kutumia Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Jumuiya (Registration of Societies Management Information System – RSMIS) utakaokuwa wa ki-elektroniki.

**USHUGHULIKIAJI WA MALALAMIKO DHIDI YA VYOMBO VYA USALAMA CHINI YA WIZARA**

**102. Mheshimiwa Spika,** malalamiko ya wananchi kuhusu utendaji wa Idara na Vyombo vya Usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yanapokelewa na yanaendelea kushughulikiwa. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 jumla ya malalamiko 202 yalipokelewa kutoka kwa wananchi na watumishi. Malalamiko hayo yalihusu Jeshi la Polisi (168), Jeshi la Magereza (14), Jeshi la Zimamoto na Uokoaji matano (5), Idara ya Uhamiaji sita (6) na Makao Makuu ya Wizara moja (1). Aidha, malalamiko nane (8) yalihusu Taasisi zilizo nje ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hivyo yaliwasilishwa katika mamlaka husika kwa hatua za kupatiwa ufumbuzi. Malalamiko 72 yamepatiwa ufumbuzi na walalamikaji wamejulishwa na pia malalamiko 130 yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi.

**103. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kupokea malalamiko ya wananchi na watumishi na kuhakikisha ufumbuzi wa malalamiko hayo unapatikana kwa wakati. Aidha, itaanzisha Madawati ya Kushughulikia Malalamiko katika Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamotona Uokoaji, Idara ya Uhamiaji na NIDA ili kuongeza kasi ya kushughulikia malalamiko. Vilevile, Wizara itaanza kutumia Mfumo wa Ki-elektroniki wa Kupokea Maoni na Kushughulikia Malalamiko Serikalini. Jumla ya Shilingi 156,975,000 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

**UDHIBITI WA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI WA BINADAMU**

**104. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha 2020/2021, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na wadau imefanikiwa kuwaokoa na kuwasaidia jumla ya wahanga 165

waliokuwa wanatumikishwa kufanya kazi kama vile kuomba mitaani, kazi za majumbani, kutumikishwa kingono na kazi ngumu kwenye mashamba na migodi. Kati yao, wahanga 163 walikuwa wanatumikishwa hapa nchini na wahanga wawili (2) walikuwa wanatumikishwa nchini Iraq na Malaysia. Wahanga wote walipewa huduma muhimu kama chakula, matibabu, msaada wa kisheria, msaada wa kisaikolojia, elimu ya ujasiriamali, stadi za maisha na ujuzi. Vilevile, Wizara iliratibu zoezi la kutambua familia za wahanga 77 Raia wa Tanzania na kuwaunganisha na familia zao.

**105. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho, wahalifu 26 wanaojihusisha na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu walikamatwa na jumla ya kesi saba (7) zilifunguliwa mahakamani. Idadi hii ya kesi imepungua ikilinganishwa na kesi 44 zilizofunguliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019/ 2020. Kupungua kwa kesi hizo kunatokana na ushirikiano mzuri baina ya Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu, wadau pamoja na jamii kuelimika kuhusu uhalifu huu na kutoa taarifa mapema ambazo husaidia kuzuia uhalifu huo kutendeka.

**106. Mheshimiwa Spika**, Sekretarieti ilitoa mafunzo kwa wadau 174 wakiwemo Mahakimu, Waendesha Mashtaka, Polisi, Maafisa Uhamiaji, Maafisa Ustawi wa Jamii, Watendaji wa Kata na watoa huduma kutoka taasisi zisizo za Serikali katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma, Mwanza, Singida, Tanga na mikoa mitatu ya Unguja – Zanzibar. Mafunzo hayo yalilenga kutoa elimu juu ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu ya mwaka 2008 na kuboresha mbinu za utambuzi na usimamizi wa wahanga, upelelezi na uendeshaji wa mashtaka yanayohusiana na makosa ya usafirishaji wa binadamu.

**107. Mheshimiwa Spika**,elimu kwa umma juu ya madhara ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu imetolewa kupitia vyombo vya habari, semina za uhamasishaji na maadhimisho ya Siku ya Kupinga Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu Duniani yaliyofanyika kitaifa tarehe 11 Agosti 2020 Jijini Dodoma. Vilevile, Wizara kupitia

Sekretariati ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu imefanya makongamano na jamii kuhusu madhara ya biashara hiyo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kigoma, Simiyu na mikoa mitatu (3) ya Zanzibar. Makongamano hayo yalihusisha wadau mbalimbali wakiwemo Madiwani, Viongozi wa Serikali za Mitaa, Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, Wawakilishi kutoka Vyombo vya Habari, Viongozi wa Dini, Wajumbe wa Kamati za Kupinga Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto, wananchi pamoja na wadau wa michezo.

**108. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Ofisi ya Taifa ya Huduma za Mashtaka inaendelea kushirikiana na nchi ya Msumbiji na Botswana kushughulikia kesi za biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu zilizofunguliwa katika nchi hizo ambazo zinahitaji msaada wa kisheria kutoka Tanzania yaani mutual legal assistance. Vilevile, kwa kushirikiana na Serikali ya Burundi ilifanikiwa kuwaunganisha na familia zao wahanga 15 raia wa Burundi waliookolewa hapa nchini. Pia, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Kenya inafanya taratibu za kuwarudisha nchini wahanga watano (5) Raia wa Tanzania waliokuwa wakitumikishwa nchini Kenya.

**109. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Sekretariati ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu imepanga kufanya kazi za kipaumbele zifuatazo: kukamilisha uandaaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu (2021 – 2024) na kuanza utekelezaji wake; kuimarisha ulinzi, usalama na uhifadhi wa wahanga (Victim Protection); kuendelea kuandaa na kutekeleza miongozo (Standard Operating Procedures) kwa ajili ya kutambua wahanga na kuwawezesha kupata rufaa ya huduma mbalimbali; kuendelea kuwajengea uwezo wadau na Vyombo vya Dola hususani katika kutoa huduma kwa wahanga; kuandaa utaratibu wa kitaifa wa kutoa rufaa kwa wahanga (National Referral Mechanism); na kuandaa mfumo wa kitaifa wa uratibu wa masuala ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

**110. Mheshimiwa Spika,** kazi nyingine zitakazofanyika kupitia Sekretarieti hii ni: kufanya utafiti katika mikoa 10 iliyoathirika na biashara hii; kutoa huduma kwa wahanga; na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kupambana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. kufanya uchunguzi, operesheni maalum na kuendesha mashtaka yanayohusiana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu; kuanzisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa zinazohusiana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu; na kuendelea kutoa elimu na mafunzo kuhusu biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kwa umma hususani wanafunzi wa shule za msingi na Sekondari, wazazi, Viongozi wa Dini na Viongozi wa Serikali za Mitaa. Jumla ya Shilingi 130,913,000 zimetengwa kwa ajili ya kutekelezwa kazi hizo.

## HUDUMA KWA WAKIMBIZI

**111. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu lake la kimataifa la kuhifadhi wakimbizi na waomba hifadhi nchini, Serikali inawahudumia wakimbizi kutoka nchi mbalimbali, ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2021 Tanzania ilikuwa inahifadhi waomba hifadhi na wakimbizi 273,252. Kati ya hao, 223,685 wapo makambini, 27,726 wapo katika Makazi ya Ulyankulu mkoani Tabora, Katumba na Mishamo Mkoa wa Katavi, 150 wapo Chogo Mkoa wa Tanga, 21,508 wanaishi katika vijiji 73 vya Mkoa wa Kigoma na 183 wapo maeneo ya mijini kwa vibali maalum.

**112. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kupokea waomba hifadhi ya ukimbizi ambapo hadi mwezi Machi, 2021 maombi ya hifadhi kutoka familia 34 zenye watu 66 yamepokelewa na kujadiliwa na Kamati ya Kitaifa ya Kujadili Maombi ya Hifadhi (NEC). Maombi ya waomba hifadhi 15 yalikubaliwa na 51 yalikataliwa kwa kutokidhi vigezo. Aidha, huduma za kijamii zinatolewa kwa wakimbizi na waomba hifadhi kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) na Mpango wa Chakula Duniani (WFP) pamoja na mashirika ya hisani ya kimataifa na ya ndani ya nchi.

**113. Mheshimiwa Spika**, katika kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi, Serikali kwa kushirikiana na UNHCR na IOM imewahamishia nchi ya tatu (resettlement) jumla ya wakimbizi 1,047. Nchi walizopelekwa wakimbizi hao ni Australia, Canada, Ireland, Marekani, Ubelgiji na Ufaransa. Aidha, Wakimbizi 31,432 walirejeshwa kwa hiari nchini Burundi katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Idadi hii inafanya jumla ya wakimbizi wote waliorejeshwa nchini Burundi tangu kuanza kwa zoezi hili mwezi Septemba, 2017 kufikia 116,652. Vilevile, wakimbizi wa Burundi wanahamasishwa kurejea kwa hiari nchini kwao kwa kuwa hali ya usalama na amani imeimarika. Pia, Serikali inafanya maandalizi ya kuanza zoezi la urejeaji kwa wakimbizi wa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Zoezi hilo litafanyika baada ya vikao vya pande tatu baina ya Serikali ya Tanzania, DRC na UNHCR kukamilika.

**Utunzaji wa Mazingira katika Kambi za Wakimbizi**

**114. MheshimiwaSpika**, kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira katika kambi za wakimbizi na maeneo yanayozunguka kambi hizo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na UNHCR imesimamia zoezi la upandaji miti katika maeneo hayo. Jumla ya miti 555,058 imepandwa katika kambi za Nyarugusu Wilaya ya Kasulu, Nduta Wilaya ya Kibondo, Mtendeli Wilaya ya Kakonko na maeneo yanayozunguka kambi hizo. Miti hiyo imepandwa katikakipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Upandaji wa miti umeambatana na doria za kudhibiti uharibifu wa mazingira ili kuzuia ukataji wa miti na kuhakikisha uhifadhi wa misitu katika maeneo yanayozunguka kambi za wakimbizi.

**115. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kuwahudumia wakimbizi na kuwatafutia suluhisho la kudumu, kushughulikia maombi ya waomba hifadhi na kusimamia ulinzi na usalama katika kambi za wakimbizi. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kuhakikisha utunzaji wa mazingira kwa kushirikiana na wadau katika kutoaelimu kwa wakimbizi kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria mbalimbali za nchi.

Fedha zilizotengwa kwa kazi hizo ni jumla ya Shilingi 640,968,000.

**C. SHUKURANI**

**116. Mheshimiwa Spika,** ninaomba nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, akiwemo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mhe. Mussa Azan Zungu (Mb.) na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kutoa ushauri wa kuboresha mambo mbalimbali katika Wizara ikiwemo kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2021/2022.

**117. Mheshimiwa Spika,** vilevile, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Khamis H. Khamis na Mbunge wa Jimbo la Uzini, Kusini Unguja kwa kunisaidia kusimamia majukumu ya Wizara ikiwemo kujibu maswali ya Wabunge na kutoa ufafanuzi wa hoja zinazowasilishwa hapa Bungeni. Aidha, ninawashukuru Katibu Mkuu Ndugu Christopher D. Kadio na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ramadhan K. Kailima kwa usimamizi wao madhubuti wa utekelezaji wa kazi za Wizara.

**118. Mheshimiwa Spika,** pia, shukrani zangu za dhati ninazitoa kwa Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Simon N. Sirro; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Suleiman M. Mzee; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John W. Masunga; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala; na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Dkt. Arnold M. Kihaule ambao wamewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika Wizara pamoja na kuhakikisha kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini.

**119. Mheshimiwa Spika,** vilevile, ninawashukuru Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi Prof. Suffian H. Bukurura, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Magereza Meja

Jenerali Mstaafu Raphael M. Muhuga, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Makamishna, Makamishna Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Maafisa, Askari na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuendelea kutekeleza vema shughuli za Wizara. Aidha, ninavishukuru Vyombo vya Habari, Jumuiya za Kidini na zisizo za Kidini pamoja na wananchi kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**120. Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatoa shukrani kwa wadau wa maendeleo zikiwemo nchi za Botswana, Burundi, Ethiopia, Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Korea Kusini, Malaysia, Seychelles, Ujerumani pamoja na Mashirika ya Kimataifa ya UNDP, UNHCR, UNICEF, IOM, UN – Women, GGML, RECSA na TRI kwa kuendelea kutoa misaada ya kifedha, kijamii na kiufundi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**121. Mheshimiwa Spika**, mwisho, ninaishukuru familia yangu, ndugu na jamaa kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kibakwe kwa ushirikiano wanaonipa kwa kuendeleza umoja na mshikamano katika kuchangia shughuli za maendeleo ya Jimbo letu.

**D. HITIMISHO**

**122. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na wadau itaendelea kudumisha hali ya ulinzi na usalama ili kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii kwa maendeleo yao na ya Taifa letu kwa ujumla.

**123. Mheshimiwa Spika,** kabla sijatoa hoja ya kuomba fedha, ninaomba nikiri kuwa, Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi walio wengi wanaishi kwenye makazi yasiyoridhisha na yasiyotosheleza. Aidha, katika wilaya nyingi

kuna changamoto ya kutokuwepo kwa Vituo vya Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Ofisi za Uhamiaji. Kwa kutambua changamoto hii, Wizara iko mbioni kuandaa **Mpango Kabambe waUjenzi wa Nyumba, Ofisi na Vituo** kwa ajili ya Vyombo Vyote vya Usalama. Mpango huu umeanza kufanyiwa kazi katika ngazi ya wataalam na utakapokamilika utawasilishwa katika mamlaka husika ili kupata mwongozo kwa ajili ya kuendelea na hatua ya utekelezaji.

**Makadirio ya Ukusanyaji Mapato kwa Mwaka 2021/2022**

**124. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara imepanga kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 494,917,473,000 kutoka vyanzo mbalimbali. Ili kufikia lengo hili Wizara itatekeleza mikakati mbalimbali ya ukusanyaji mapato ikiwemo: ununuzi wa vitendea kazi kama magari na pikipiki; kuendelea kuunganisha na kutumia mifumo ya kieletroniki katika kutoa huduma; kuanzisha ofisi nne (4) za Msajili wa Jumuiya zitakazo saidia kuhamasisha usajili wa vikundi na vyama vya kijamii na kiuchumi, kurahisisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza tija katika usimamizi na ukaguzi wa jumuiya.

**Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2021/2022**

**125. Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 939,089,045,000** kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2021/ 2022. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 389,750,394,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **Shilingi 521,868,651,000** ni Mishahara na **Shilingi 27,470,000,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha za Maendeleo zinazoombwa, **Shilingi 27,390,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 80,000,000** ni fedha za nje.

**126. Mheshimiwa Spika,** ninaomba kutoa Hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na hoja imeungwa mkono nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa George Simbachawene kwa kuweka mezani hoja yako ambayo Waheshimiwa Wabunge wameisikiliza kwa umakini mkubwa sana, nakushuru sana sana sana.

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Ndani ya Nchi Kamati ya Kudumu ya Bunge Mheshimiwa Chumi kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. COSATO D. CHUMI - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati yetu naomba kusoma taarifa ya kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba taarifa hii iingie kwenye taarifa rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani mapema asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa kuwa jukumu kubwa la Kamati yetu ni kuisimamia Serikali kwa niaba ya Bunge kuhusu masuala yanayohusu Usalama wa Raia na Mali zao, naomba kuvipongeza vyombo vyote vya Dola kwa kusimamia hali ya ulinzi na usalama tangu nchi yetu ilipopata msiba wa mpendwa wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli hadi tulipompata Rais wa Awamu ya Sita na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Hali hii inaendelea kutoa Taswira nzuri kuwa nchi yetu ni kitovu cha amani barani Afrika na duniani kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 kanuni ndogo ya (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato

na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha Kifungu cha 6(3) na Kifungu cha 7(1)(a), cha Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kujadailiwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117(1) hadi 117(2) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda ya Taarifa hii, nitangulie kulikumbusha Bunge hili kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inajumuisha Mafungu matano ya kibajeti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 14 Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, Fungu 28 Jeshi la Polisi, Fungu 29 Jeshi la Magereza, Fungu 51 Wizara, kwa maana ya Makao Makuu ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa – NIDA na Fungu 93 Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu sehemu nne zifuatazo:-

(a) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kama ambavyo itaoneshwa katika ukurasa wa pili hadi wa sita;

(b) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ambayo inapatikana ukurasa wa sita hadi 16;

(c) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ukurasa wa 16 hadi wa 23 na maoni na ushauri wa Kamati ukurasa wa 24 hadi wa 34.

Mheshimiwa Spika, najielekeza kwenye matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo.

**SPIKA:** Sasa naomba ujielekeze kwenye maoni na ushauri wa Kamati moja kwa moja kwasababu ni bajeti ya siku moja leo leo tunajaribu kuokoa muda Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa maelekezo yako najielekeza moja kwa moja kwenye maoni na ushauri wa Kamati.

Kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa maoni na ushauri wa jumla na mahsusi kama ifuatavyo:-

(i) kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa umma na Utawala Bora kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa watumishi katika Idara na majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutokana na umuhimu wake katika usalama wa Raia na Mali zao;

(ii) Kama ilivyofanyika kwa ujenzi wa nyumba za Watumishi na Askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania, Serikali ione umuhimu wa kuwa na Mpango Mkakati wa kujenga nyumba za makazi kwa ajili ya Watumishi na Askari wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hii itaondoa changamoto ya muda mrefu ya makazi kwa askari ambao wengi wao wanakaa uraiani jambo ambalo si zuri kiusalama;

(iii) Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani yameendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya vyombo vya usafiri na usafirishaji. Kwa mara nyingine Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuyawezesha Majeshi yake kwa kuyapatia vyombo vya usafiri na usafirishaji ili kuweza kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi;

(iv) Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo yanaendelea kukua kutokana na kutokulipwa kwa stahiki mbalimbali za Wastaafu, Watumishi na madeni ya wazabuni na watoa huduma. Aidha, Serikali kupitia Hazina ilipe madeni yote yaliyohakikiwa, kipaumbele kitolewe kwa Wastaafu;

(v) Serikali itoe fedha za maendeleo kwa wakati kwa mafungu yote ya Wizara ili kutekeleza kwa ufanisi miradi inayopangwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri mahsusi, Fungu namba 14 Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2020/2021 Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Zima Moto lililopo katika eneo la Mchicha, Wilayani Temeke Jijini Dar es Salaam ambalo ujenzi wake ulisimama tangu mwaka 2013. Kwa mara ya mwisho jengo hili lilitengewa Shilingi Bilioni Mbili katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo fedha hizo hazikutolewa. Pamoja na ushauri huo, mradi huu haukuwahi kutengewa fedha katika mwaka wa fedha 2019/2020, 2020/ 2021 wala katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa Serikali haijalipa umuhimu wa kipekee suala hili. Hivyo, Kamati inaushauri kwa Serikali kuwa kwa mara nyingine kuwa katika mwaka 2021/2022 fedha zitengwe kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo na litumike kuimarisha huduma za Zima Moto na uokoaji katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kulipatia Jeshi hili magari ya kuzima moto na

kununua vifaa vya kuzima moto na uokoaji. Hata hivyo fedha zinazotengwa haziendani na mahitaji halisi na fedha hizo huwa hazitolewi kwa Wakati. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Jeshi la Zima Moto na Uokoaji lilitengewa shilingi bilioni 3.5 lakini hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ni asilimia 46 tu ya fedha hizo ndizo zilizokuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaushauri Serikali kuongeza ukomo wa bajeti ya maendeleo ya Jeshi la Zima Moto na Uokoaji na kutoa fedha hizo kwa ukamilifu kuendana na mahitaji halisi ya Jeshi. Hii italiwezesha Jeshi hili kutatua changamoto za uhaba wa magari ya kuzima moto na uchache wa vituo vya zima moto na uokoaji katika maeneo mbalimbali nchini jambo linalosababisha wananchi wengi kukaidi kulipa tozo kutokana na kukosekana kwa huduma za zima Moto.

Mheshimiwa Spika, tatu, pamoja na ushauri wa jumla uliotolewa awali, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele katika kuajiri askari wa kutosha kulingana na miradi ya kimikakati inayoendelea ambayo itahitaji huduma za Zima Moto na uokoaji. Miradi hiyo ni pamoja na ile ya upanuzi wa viwanja vya ndege, miradi ya umeme na gesi na bomba la mafuta.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali katika kuongeza mapato ya Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, Wizara iangalie upya tozo zilizopangwa kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa vya Zima Moto ambapo gharama yake ni kubwa kulingana na hali halisi ya vipato vya wananchi, jambo hili linachangia wananchi wengi kushindwa kulipa na hivyo kusababisha Serikali kupoteza mapato yatokanayo na tozo hizo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 28 - Jeshi la Polisi Serikali itoe fedha za Maendeleo kwa miradi ya muda mrefu iliyokuwa imeidhinishwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Hii ni pamoja na Mradi wa kukamilisha kituo cha Polisi cha Mkokotoni ambapo ujenzi wake umesimama tangu mwaka

2013 licha ya kuwa mradi huo ulikwishatekelezwa kwa asilimia 60.

(ii) Pamoja na juhudi za Jeshi la Polisi za kutekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya vituo vya Polisi na nyumba za Askari kwa mfumo wa nguvu kazi kwa maana ya *force account* kupitia Mfuko wa tuzo na tozo na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, bado suala la makazi kwa Askari limeendelea kuwa changamoto ambayo inatakiwa kupewa uzito wa kipekee hasa kwa kuzingatia usalama wa Askari wanapoishi uraiani.

(ii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali iongeze na kuendeleza juhudi za kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayowasilishwa Bungeni na fedha zake kuidhinishwa na Bunge. Kufanya hivyo, kutaiwezesha Bunge kuongeza tija katika ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za umma inavyostahili.

(iii) Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Kamati inaishauri Serikali kushughulikia changamoto za kimkataba zilizojitokeza katika mradi wa ujenzi wa nyumba 353 za Maafisa na Askari kwa ubia na Mwekezaji wa Sekta Binafsi katika eneo la Msasani na Kunduchi jijini Dar es Salaam ili nyumba hizo zianze kutumika.

(vi) Ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia, Kamati inaishauri Serikali kutenga Bajeti ya kutosha na kutoa fedha hizo kwa ajili ya kuwawezesha Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi kukabiliana na makosa mbalimbali yakiwemo makosa ya kimtandao na makosa yanayovuka mipaka. Aidha, kitengo cha uchunguzi kiwezeshwe kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 29 - Jeshi la Magereza, Kamati inampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kutoa Msamaha kwa Wafungwa zaidi ya 5,000 katika Sikukuu ya Muungano tarehe 26 Aprili, 2021. Msamaha uliotolewa kwa Wafungwa umeipunguzia Serikali gharama

ya takribani shilingi 4,000,000 kwa siku ambapo kwa Mwaka ni shilingi bilioni 1.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zote zitakazoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka 2021/2022 kwa jili ya vikao vya Taifa na za Mikoa za *Parole* ili wafungwa wengi zaidi wanaostahili kupewa msamaha wapunguzwe magerezani na hatimaye kuokoa fedha za Serikali zinazotumika kuwatunza ambapo kwa sasa takribani shilingi 26,000,000 hutumika kwa siku sawa na shilingi bilioni tisa kwa Mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali katika kujenga Magereza mapya ili kutatua tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani, bado Jeshi la Magereza linakabiliwa na changamoto hiyo ambapo uwezo wa magereza yaliyopo ni kuhifadhi wahalifu 29,000 kisheria kwa siku ikilinganishwa na wahalifu 32,000 waliopo kwa siku katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa Magereza mapya. Kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya Shilingi 840,000,000 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Magereza Makuu na hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Magereza mapya.

(iii) Serikali iliwezeshe jeshi la Magereza kupata magari hususan kwa ajili ya kusafirisha mahabusu ambapo kwa sasa mahitaji halisi ni 480. Upatikanaji wa magari hayo, pamoja na mambo mengine, utasaidia mahabusu kupata nafasi ya kusikiliza kesi zao kwa wakati uliopangwa na hivyo kuamuliwa mapema. Hii itapunguza msongamano wa wafungwa na Mahabusu Magerezani lakini pia itaondoa changamoto ya mahabusu kukaa muda mrefu magerezani bila kesi zao kuamuliwa. *(Makofi)*

(iv) Tangu Mwaka 2016 Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali na jiko katika Gereza la Segerea. Hata hivyo ushauri

huo haujawahi kuzingatiwa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha hizo ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali hiyo ambayo ni muhimu kwa Gereza la Segerea.

(v) Serikali itoe jumla ya shilingi milioni 840 zilizotengwa katika Mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kukarabati mabweni na miundombinu ya Magereza 12 nchini. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

(vi) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa shilingi bilioni 3.6 zilizotengwa katika mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la mpunga la gereza la Idete na ununuzi wa zana za kilimo. Aidha, kwa Mwaka 2021/2022 Serikali imetenga shilingi bilioni sita kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora za mazao mbalimbali na kununua zana za kilimo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula. Pamoja na juhudi hizo za Serikali, Kamati inashauri Jeshi kuwa na mpango mkakati wa kuanzisha na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Magereza mengine ili Jeshi hilo liweze kujitosheleza kwa chakula na kuzalisha kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Spika, Fungu 51 Wizara, Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kurekebisha Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 na Kutunga Sheria ya Sekta Binafsi ya Ulinzi kwa Mwaka 2021 tangu Bunge la Kumi na Moja. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Mapendekezo ya Sheria hizo, hata hivyo, kamati inashauri;

(i) Serikali kuhakikisha kuwa Mchakato wake unapewa umuhimu unaostahili ili Sheria hizo zipatikane mapema;

(ii) Serikali ihakikishe inazalisha vitambulisho vyote kulingana na idadi ya namba za utambulisho ambazo zimekwisha tolewa kwa wananchi ifikapo Mwezi Juni 2021 kama ilivyokuwa imepangwa;

(iii) Serikali iongeze jitihada za kuwafikia kwa urahisi watu wote wenye vigezo vya kusajiliwa na kutambuliwa wanaoishi mbali na makao makuu ya wilaya. Hii ni pamoja

na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari ili kuwezesha wataalamu kuwafikia walengwa wengi zaidi;

(iv) Mikataba ya Manunuzi ya Mitambo ya uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa ijumuishe mafunzo ya muda mrefu kwa Wataalamu wa ndani bila ya gharama ya ziada ili kuwezesha Serikali kumiliki, kuendesha, kuhudumia na kukarabati mitambo hiyo jambo ambalo litaepusha gharama kubwa zinazotumika kwa kutegemea wataalamu kutoka nje;

(v) Serikali ikamilishe Mfumo wa kielektroniki wa usajili wa Jumuiya ili kuwezesha malipo ya kiektroniki kupatikana mahali popote nchini. Hii, pamoja na mambo mengine, itaongeza mapato ya makusanyo yanayotokana na usajili wa Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, Fungu - 93 Idara ya Uhamiaji, Idara ya Uhamiaji imeendelea kutokupelekewa fedha za maendeleo kwa mtiririko unaostahili. Kamati inaishauri Serikali itoe fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo hadi kufikia Mwezi Februari, shilingi 400,000,000 sawa na asilimia 8.99 tu ya shilingi bilioni 4.45 zilizoidhinishwa na Bunge ndio zilikuwa zimetolewa. Kutokutolewa kwa fedha hizo kutaendelea kuchelewesha utekelezaji wa Miradi ya maendeleo iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, pili, pamoja na Sheria ya Marekebisho ya Utumishi wa Umma Na. 18 ya mwaka 2007 kuiondoa Idara ya Uhamiaji kutoka katika usimamizi wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kupelekwa kwenye usimamizi wa Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, bado Idara ya Uhamiaji pamoja na mambo mengine, haipati stahiki za kimaslahi na huduma za msamaha wa kodi kama vyombo vingine vya Jeshi katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuipa haki Idara ya Uhamiaji kama Majeshi mengine yaliyo chini ya

Wizara hii. Hii itaiwezesha masuala ya stahiki mbalimbali za Maafisa na Askari wa Uhamiaji kushughulikiwa kikamilifu na kuiwezesha Idara kutekeleza majukumu yake ya kisheria na kimuundo kwa ufanisi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa tangu Mwaka 2007 Idara ya Uhamiaji ilianza kutumia Muundo wa Utumishi wa Maafisa na Askari wa Uhamiaji wenye vyeo vya Kijeshi sawa na vyombo vya Ulinzi chini ya Wizara ya mambo ya Ndani ya Nchi, Kamati inashauri Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 Rejeo la Mwaka 2016 ifanyiwe marekebisho ili Idara hiyo itambulike rasmi kuwa ni Jeshi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Idara ya Uhamiaji inachangia kwa asilimia kubwa katika mapato ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Idara hii bado inakabiliwa na uchache wa vyombo vya usafiri ambavyo pamoja na mambo mengine vinasaidia katika doria ya kuwabaini wageni wanaoishi bila vibali vya ukaazi. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Idara kupata vyombo vya usafiri ili kuwabaini wahamiaji wasio na vibali na kuwachukulia hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuwalipisha ada husika na faini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge; Naibu Waziri Mheshimiwa Hamis Hamza Hamis, Mbunge; Katibu Mkuu, Ndugu Christopher Kagio; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ramadhani Kailima pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na

mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Mbunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Jerad Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (FUNGU 14, 28, 29, 51 NA 93) KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, kwa kuwa jukumu kubwa la Kamati yangu ni kuisimamia Serikali kwa niaba ya Bunge kuhusu masuala yanayohusu Usalama wa Raia na Mali zao, naomba kuvipongeza vyombo vyote vya Dola kwa kusimamia hali ya ulinzi na usalama tangu nchi ilipopata Msiba wa Mpendwa wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli hadi tulipompata Rais wa Awamu ya Sita na Amiri

Jeshi Mkuu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Hali hii inaendelea kutoa Taswira nzuri kuwa nchi yetu ni kitovu cha amani barani Afrika na duniani kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kujadailiwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Noamba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) hadi 117 (2) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda (scope) ya Taarifa hii, nitangulie kulikumbusha Bunge hili kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inajumuisha Mafungu matano (5) ya kibajeti yafuatayo:-

a) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

b) Fungu 28 - Jeshi la Polisi;

c) Fungu 29 - Jeshi la Magereza;

d) Fungu 51 - Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - NIDA; na

e) Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu sehemu nne (4) zifuatazo:-

a) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

b) Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

c) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na

d)Maoni na Ushauri wa Kamati.

## MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRAD1 YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo minne (4) katika Mikoa ya Singida na Arusha ambayo ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii. Sehemu hii ya Taarifa inaeleza mambo makuu mawili:

a) Muhtasari wa maelezo ya Miradi iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021; na

b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.
Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa fedha lilizoidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii.

### Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara hii ilipaswa kutekeleza jumla ya miradi 13 katika mikoa

mbalimbali nchini. Hata hivo, kwa madhumuni ya ukaguzi wa miradi hiyo, Kamati ilitembelea Mradi mmoja kati ya hiyo 13 na Miradi mingine mitatu (3) katika Mikoa ya Singida na Arusha. Muhtasari wa maelezo kuhusu miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

**a) Miradi iliyotekelezwa kupitia Utaratibu wa Mfuko wa Tuzo na Tozo chini ya Jeshi la Polisi**

Miradi hii inajumuisha ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida na Jengo la Ofisi ya Mkuu FFU na Ghala la kuhifadhia Silaha, Singida. Miradi hii inatekelezwa chini ya Fungu 28- Jeshi la Polisi.

**b) Mradi uliotekelezwa kupitia ufadhili wa Serikali na Wadau**

Mradi huu unahusu ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari-Arusha unaotekelezwa na Jeshi la Polisi (Fungu 28).

**c) Mradi Na. 6501- Vitambulisho vya Taifa**

Mradi huu unahusu uunganishaji Mtandao wa Mawasiliano kati ya Vituo vya Usajili na Makao Makuu na unatekelezwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani Makao Makuu, (Fungu 51).

**Matokeo ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa miradi ya maendeleo sasa naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo kwa kutaja yafuatayo:-

i) Miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mfumo wa nguvukazi yaani *Force account* inakamilika mapema ikilinganishwa na miradi ambayo fedha zake huidhinishwa na Bunge. Kwa mfano, ujenzi wa ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida ambao ulianza kutekelezwa tarehe 20/02/2021 na unatarajiwa kukamilika tarehe 30/06/2021 ambapo hadi kamati ilipofanya ziara yake

ujenzi wa msingi ulikuwa umekamilika. Mradi huu unatarajia kugharimu jumla ya shilingi 1,214,862,300/= utakapokamilika.

ii) Juhudi zinazofanywa na Serikali za kushirikiana na Wadau kufadhili miradi ya maendeleo hususan nyumba za makazi ya askari zinapunguza tatizo la changamoto za Ofisi na makazi ya askari nchini. Mfano wa Mradi huu ni ujenzi wa Makazi ya Askari unaohusisha jengo moja lenye nyumba sita (06) kwa ajili ya makazi ya askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) Oljoro Mkoani Arusha.

iii) Kuhusu uzingatiaji wa masuala ya jinsia, mradi wa ujenzi wa miundombinu ya ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida umefanya vizuri kwa kuzingatia umuhimu wa majengo kuwa na sehemu za matumizi ya watu wenye mahitaji maalum.

**Maoni ya jumla kuhusu Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

i) Ili idhini ya Bunge kwa bajeti ya kugharimia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iwe na tija, upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati na kwa kadiri inavyostahili, ni jambo muhimu kufanikisha utekelezaji huo kwa muda uliopangwa;

ii) Utaratibu wa Serikali kutekeleza miradi yake kwa mfumo wa nguvukazi (Force Account) na chanzo cha fedha kikiwa ni mfuko wa Tuzo na Tozo ni jambo linaloongeza ufanisi na upatikanaji wa tija inayokusudiwa;

iii) Ushirikishaji wa wadau katika ujenzi wa nyumba za askari chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi unasaidia kwa kiasi kikubwa kutapunguza changamoto ya uhaba wa makazi ya askari nchini; na

iv) Masuala ya Jinsia hususan kuona umuhimu wa kuzingatia matumizi ya Watu wenye mahitaji maalumu katika ujenzi na

miradi mingine ni jambo la kupewa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi nchini;

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kutekeleza miradi kwa utaratibu wa tuzo na tuzo na ufadhili wa wadau, Kamati inasisitiza kuwa Serikali iongeze na kuendeleza juhudi za kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayowasilishwa Bungeni na fedha zake kuidhinishwa na Bunge.

## UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipofanya uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, ilizingatia makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo lililokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mafungu yote Matano ya Wizara. Vilevile, Kamati ilizingatia taarifa muhimu na za ziada zilizopatikana kupitia mahojiano wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

### Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ikijumuisha Mafungu yake yote matano ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **488,569,880,319/=** ikilinganishwa na Shilingi **471,894,244,600/=** zilizokadiriwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia Mwezi Februari 2021, kiasi kilichokusanywa kilikuwa ni Shilingi **bilioni 149.65** sawa na asilimia **30.63** tu ya lengo la Mwaka lililopangwa. Kamati

ilibaini kuwa makusanyo hayo yamepungua kwa asilimia 35 ikilinganishwa na makusanyo yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo yalikuwa Shilingi **Bilioni 229.81 sawa na** asilimia **48.7** ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kufanya uchambuzi wa kina, Kamati ilibaini kuwa Mafungu yote matano ya Wizara yalikusanya kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hiki kwa kila Fungu katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu mwenendo wa makusanyo kwa kipindi cha miaka mitano na kufanya ulinganisho wa Makusanyo hayo kwa miaka mitano kuanzia Mwaka 2016/2017. Kamati ilibaini kuwa makusanyo ya Mapato yamekuwa yakiongezeka kila Mwaka hadi Mwaka 2019/2020 na kupungua katika Mwaka huu wa fedha 2020/2021. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na COVID- 19 ni kati ya sababu zilizochangia makusanyo hayo kupungua.

Mwenendo huo wa Makusanyo unadhihirika katika Jedwali Na. 1& 2 na Grafu Namba 1 hapa chini.

**Jedwali Na. 1: MWENENDO WA MAKUSANYO YA WIZARA 2016/2017- 2020/2021**

| MWAKA | 2016/2017 | 2017/2018 | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| MAKUSANYO | 156.53 | 160.69 | 185.53 | 229.81 | 149.65 |


**Grafu Na. 1: MWENENDO WA MAKUSANYO YA WIZARA 2016/2017- 2020/20**




**Chanzo: Randama za Wizara 2016/2017- 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati ilifanya uchambuzi na kuainisha mchanganuo wa makusanyo kwa kila Fungu hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ikilinganishwa na lengo la Mwaka lilowekwa. Aidha, Kamati ilifanya ulinganisho wa Makusanyo yaliyopatikana hadi kufikia Mwezi Februari 2021 na Makausanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho, Mwaka 2020 kama inavyoonekana katika Grafu na Jedwali Na. 2 hapa chini.

**GRAFU NAMBA 2: ULINGANISHO WA MAKUSANYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 NA 2020/2021**




Chanzo: **Randama ya Wizara 2020/2021**

**Jedwali Na. 2: MCHANGANUO WA MAPATO HADI KUFIKIA FEBRUARI 2021**

| FUNGU | MAKADIRIO 2020/2021 | % YA JUMLA YA LENGO | MAKUSANYO FEB 2021 | % YA JUMLA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|
| 14 - Zimamoto | 9,250,000,000 | 1.89 | 4,664,131,500 | 3.17 |
| 28 – Polisi | 127,031,856,000 | 26 | 55,923,139,929 | 37.37 |
| 29 – Magereza | 2,000,002,000 | 0.4 | 399,446,628 | 0.27 |
| 51- Wizara | 226,606,600 | 0.04 | 92,314,107 | 0.06 |
| 93-Idara ya Uhamiaji | 350,061,418,319 | 71.65 | 88,571,271,968.54 | 59.18 |
| **JUMLA** | **488,569,882,925** | | **149,650,304,132.54** | |

Chanzo: **Randama ya Wizara 2019/2020- 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

i) Makusanyo ya Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 1.89 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 14 limechangia kwa asilimia 3.17 ya kiasi kilichokusanywa;

ii) Makusanyo ya Fungu 28- Jeshi la Polisi, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 26 na Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 28 limeshachangia kwa asilimia 37.37 ya kiasi kilichokusanywa;

iii) Makusanyo ya Fungu 29- Jeshi la Magereza, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.4 na Fungu hilo limechangia kwa asilimia 0.27 ya kiasi kilichokusanywa;
iv) Makusanyo ya Fungu 51- Wizara, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.04 na Taarifa ya Makusanyo ilionesha Fungu hilo limechangia kwa asilimia 0.06 ya kiasi kilichokusanywa;

v) Makusanyo ya Fungu 93- Jeshi la Uhamiaji, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 71.65 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu hilo limeshachangia asilimia 59.18 ya kiasi kilichokusanywa.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho huo wa makadirio ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na mapato halisi ya kila fungu, umeisaidia Kamati kubaini kuwa Idara ya Uhamiaji ndio iliyochangia kwa asilimia kubwa katika makusanyo yote ya Wizara. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa kutofikiwa kwa lengo la makusanyo kumechangiwa na mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na COVID-19, hali iliyopelekea kupungua kwa uingiaji na utokaji wa wageni na Raia.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi uliofanyika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo kwa Mwaka huu wa fedha si wa kuridhisha kwani kiujumla Wizara kwa mafungu yote imekusanya asilimia 30.63 tu ya lengo lililowekwa. Aidha, Fungu 14- Jeshi la Zimamoto pekee ndilo limeweza kufikia nusu ya makadirio yake ambapo hadi kufikia Mwezi Februari 2021 lilikuwa limekusanya asilimia 50 ya makisio yaliyowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mwenendo usioridhisha wa makusanyo ya Mapato kwa Mwaka huu ni dhahiri kuwa lengo lililowekwa litakuwa gumu kufikiwa. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali izingatie changamoto zilizoathiri ukusanyaji wa mapato na kupanga makadirio ya makusanyo kwa kuzingatia uhalisia katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Wizara hususan fedha za maendeleo umendelea kuwa changamoto ya muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Bunge la Kumi na Moja Kamati iliendelea kuishauri Serikali kupitia Hazina kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo utengwaji wa fedha za maendeleo na mtiririko wa upatikanaji wa fedha hizo uliendelea kuwa si wa kuridhisha na hivyo kuathiri ratiba ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan iliyohusu ujenzi wa Ofisi, nyumba za Askari

na Watumishi pamoja na ununuzi wa magari yakiwemo ya doria na zimamoto.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia changamoto hiyo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2021. Kupitia uchambuzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

i) Hadi kufikia mwezi Februari 2021, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 66.48 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara.

ii) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari 2021, asilimia 49 ilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na asilimia 4.54 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.


iii) Hadi kufikia mwezi Februari 2021, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 62.64 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo na asilimia 76.74 ya bajeti ya Maendeleo ya Fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

iv) Hadi kufikia mwezi Februari 2021, Asilimia ya fedha za maendeleo zilizotolewa kwa kila Fungu ilikuwa: Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji- asilimia 46.23; Fungu 28- Jeshi la Polisi- asilimia 75; Fungu 29- Jeshi la Magereza-asilimia 89.1; Fungu 51- asilimia 58.18 na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji ilipokea asilimia 8.99;

v) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, Mafungu mawili tu, 14 Jeshi la Zimamoto na 93- Idara ya Uhamiaji ndiyo yalipokea chini ya asilimia 50 ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa ajili ya mafungu hayo.

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa upatikanaji wa fedha za Mishahara, Matumizi Mengineyo na Maendeleo, umeoneshwa dhahiri katika Grafu Na. 3 hapa chini.

**Grafu Na. 3: MCHANGANUO WA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021 KWA MATUMIZI MATATU YA WIZARA**




**Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Mishahara, Mengineyo na Maendeleo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ni wa kuridhisha kwani matumizi yote yamepokea zaidi ya asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa zaidi ya Asilimia 50 kwa ajili ya Jeshi la Magereza, Jeshi la polisi na Wizara. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu 93- Idara ya Uhamiaji si wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** Ili idhini ya Bunge kwa bajeti ya kugharimia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iwe na tija, upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati na kwa kadiri inavyostahili, ni jambo muhimu kufanikisha utekelezaji huo kwa muda uliopangwa. Hivyo, ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe fedha hizo kwa Mafungu yote kwa ukamilifu kufikia tarehe 30 Juni, 2021 ili kutoathiri ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

## Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka

wa Fedha 2020/2021, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo kwa Mafungu yote matano.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika masuala yaliyotolewa ushauri, yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, baadhi yanaendelea kuzingatiwa na mengine ambayo hayajazingatiwa kikamilifu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti kama inavyoonekana katika Kiambatisho Na. 1 cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya ushauri uliozingatiwa kikamilifu na Serikali ulihusu kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya umwagiliaji katika Magereza ili kuliwezesha Jeshi hilo kuwekeza katika kilimo. Taarifa iliyotolewa na Wizara ilieleza kuwa ushauri ulizingatiwa ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021 Fungu 29- Jeshi la Magereza limepokea kiasi cha Shilingi Bilioni 2.10 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika Gereza la Idete.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia iliridhishwa na utekelezaji wa ushauri wake kuhusu Serikali kuliwezesha Jeshi la Magereza kujenga nyumba kwa ajili ya Makazi ya Maafisa na Askari. Taarifa iliyotolewa ilieleza kuwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali imekamilisha ujenzi wa nyumba 79 zenye uwezo wa kuchukua familia 152. Aidha, kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imelipatia Jeshi la Magereza kiasi cha Shilingi Bilioni 7.28 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 148 za Maafisa na Askari katika eneo la Msalato, Isanga na maeneo mengine nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu ushauri unaoendelea kuzingatiwa, Taarifa iliyowasilishwa ilionesha kuwa Serikali imeendelea kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusu upatikanaji wa Suluhisho la Kudumu kwa Wakimbizi waliopewa Uraia wa Tanzania ili kuhakikisha Usalama katika Maeneo wanayoishi na yale yanayowazunguka. Taarifa iliyotolewa mbele ya Kamati ilionesha kuwa Serikali inaendelea na mpango wa kutafuta suluhisho la kudumu la wakimbizi waliopewa Uraia wa Tanzania (Raia Tajnisi) wanaoishi katika Makazi ya Wakimbizi

ya Katumba, Mishamo na Ulyankulu ikiwemo hatima ya makazi hayo ya wakimbizi. Aidha, maelezo yaliyotolewa yalionesha kuwa katika kuimarisha usalama wa makazi na maeneo yanayozunguka, operesheni za mara kwa mara zinazoshirikisha Vyombo vya Ulinzi na Usalama zimekuwa zikifanyika kwa lengo la kuwabaini na kuwachukulia hatua wahalifu wanaoishi katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu ushauri ambao haujazingatiwa kikamilifu ulihusu Serikali kutoa kikamilifu Shilingi bilioni 4.45 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Idara ya Uhamiaji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Maelezo yaliyotolewa na Serikali yalionesha kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, Shilingi milioni 400 sawa na asilimia 8.99 tu ya fedha zote ndizo zilikuwa zimetolewa.

## UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo. Majukumu hayo ni pamoja na:

i) Kuendelea kusimamia uwepo wa amani na usalama wa Raia na mali zao;

ii) Kuendelea kusajili na kutoa vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania, wakimbizi na wageni;

iii) Kuendelea kuzuia na kupeleleza makosa ya jinai na makosa ya usalama barabarani;

iv) Kuimarisha shughuli za kilimo na mifugo ikiwa ni pamoja na kutekeleza mkakati wa kujitosheleza kwa chakula; na

v) Kuendelea kudurusu na kutunga Sera na Sheria mbalimbali zinazohusu Wizara ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopitia majukumu hayo kwa kulinganisha na Bajeti inayoombwa, ilibaini kuwa utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake utaimarika endapo Serikali itatenga fedha za kutosha na kutoa fedha hizo kadri ambavyo zimeidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara.

**Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **494,917,473,719/=.** Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la asilimia 1.01 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa Shilingi **488,569,880,319/=.** Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 28- Jeshi la Polisi ambapo lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa asilimia 5. Ongezeko hilo linatarajiwa kuwa katika tozo za barabarani, ada ya umiliki wa silaha na marejesho ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilirejea sababu zilizochangia Wizara kutofikisha lengo la makusanyo kwa Mwaka 2020/2021 na kubaini kuwa elimu ya usalama barabarani ilikuwa mojawapo ya sababu zilizochangia kupungua kwa makusanyo yatokanayo na tozo za barabarani. Hata hivyo, Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2021/ 2022 Makadirio ya makusanyo ya tozo za barabarani yameongezwa hadi kufikia shilingi **124,868,593,500** ikilinganishwa na makadirio ya shilingi **118,316,470,682** kwa mwaka 2020/2021 huku idadi ya makosa yanayokadiriwa ikibaki kuwa milioni 3.1. Ni maoni ya Kamati kuwa, pamoja na nia njema ya kuongeza makusanyo ya Wizara, ni vyema Serikali ikalenga uhalisia katika kupanga makisio hayo.

Mchanganuo wa lengo la makusanyo kwa Mafungu yote unaonekana katika Jedwali Na. 3 hapa chini.

**Jedwali Na. 3: MAKADIRIO YA MAPATO**

| FUNGU | MAKADIRIO 2020/2021 | %YA JUMLA YA LENGO | MAKADIRIO 2021/2022 | %YA JUMLA YA LENGO |
|---|---|---|---|---|
| Fungu 14 - Zimamoto na uokoaji | 9,250,000,000 | 1.89 | 9,250,000,000 | 1.86 |
| Fungu 28 - Jeshi la Polisi | 127,031,856,000 | 26 | 133,383,448,800 | 26.95 |
| Fungu 29 - Jeshi la Magereza | 2,000,000,000 | 0.41 | 2,000,000,000 | 0.40 |
| Fungu 51 – Wizara | 226,606,000 | 0.05 | 226,606,600 | 0.045 |
| Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji | 350,061,418,319 | 71.65 | 350,057,418,000 | 70.73 |
| **Jumla** | **488,569,880,319** | **100** | **494,917,473,719** | **100** |

Chanzo**: Randama ya Wizara 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo:-

i) Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linategemewa kukusanya asilimia 1.86 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 1.89, ki-uwiano ikiwa ni pungufu kwa asilimia 0.03;

ii) Fungu 28- Jeshi la Polisi linategemewa kukusanya asilimia 26.95 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 26 kiasi ambacho ki-uwiano ni ongezeko kwa asilimia 0.95;


iii) Fungu 29- Jeshi la Magereza linategemewa kukusanya asilimia 0.40 ya makusanyo ambayo ki-uwiano ni pungufu ya asilimia 0.01 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 0.41;

iv) Fungu 51- Wizara linategemewa kukusanya asilimia 0.045 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 0.05; Kiasi hiki ni pungufu katika uwiano kwa asilimia 0.005;

v) Fungu 93- Idara ya Uhamiaji linategemewa kukusanya asilimia 70.73 ya makadirio ya makusanyo ikiwa ni pungufu katika uwiano kwa asilimia 0.92 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo lilitegemewa kukusanya kwa asilimia 71.65.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ufafanuzi huo, ni dhahiri kuwa Fungu 28- Jeshi la Polisi na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji, ndio yanayotegemewa katika makusanyo ya Wizara hii kama inavyoonekana katika Grafu Na. 4 ya Taarifa hii. Kamati imebaini kuwa kwa miaka minne mfululizo mafungu hayo yamekuwa yakikadiriwa na kukusanya asilimia nyingi zaidi ikilinganishwa na Mafungu mengine.

**Grafu Na. 4: ULINGANISHO WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2020/2021- 2021/22**




Chanzo: **Randama ya Wizara 2020/2021 na 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Mafungu hayo kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa na muhimu katika makusanyo. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizi, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Fungu 93- Idara ya Uhamiaji bado haijapewa uzito unaostahili katika kupelekewa fedha za maendeleo licha ya kuwa ndio inakusanya zaidi ya Mafungu mengine ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa Fungu 93 lipewe uzito unaostahili katika kutengewa na kupelekewa fedha za maendeleo ili kutekeleza miradi yake ya maendeleo ikiwa ni pamoja na Miradi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mikoa

ya Lindi na Mtwara ambayo utekelezaji wake umesimama tangu mwaka 2015 na 2017 mtawalia.


**Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mhesimiwa Spika,** maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwa kwa mafungu yote matano ni Shilingi bilioni **939.08.** Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni **521.86** sawa na asilimia **55.57,** ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi bilioni 389.75 sawa na asilimia **41.5** ni Matumizi Mengineyo na Shilingi bilioni **27.47** sawa na asilimia **2.93** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, Shilingi bilioni **27.39** sawa na asilimia 99.7 ni fedha za ndani na Shilingi milioni **80** sawa na asilimia 0.3 ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho na bajeti kuu ya Serikali na kubaini kuwa wakati Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ni asilimia 2.93 tu ya Bajeti yote, asilimia 37 ya bajeti kuu imeelekezwa kwenye matumizi ya maendeleo**.** Aidha, Kamati ilibaini kuwa, wakati Bajeti ya Maendeleo ya Bajeti kuu ya Serikali imeongezeka kwa asilimia nne (4) ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Bajeti ya Wizara iliyotengwa kwa ajili ya Maendeleo imepungua kwa asilimia 20.4 ikilinganishwa na Bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara hii ili kufanikisha miradi yake muhimu yenye tija kwa vyombo vyake vya Dola na Taifa kwa ujumla.

**Chati Na. 1: MGAWANYO WA FEDHA ZA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**




Chanzo: **Randama ya Wizara 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Katika Mwaka wa fedha 2020/2021, fedha za nje za maendeleo zilikuwa asilimia 2.5 ambazo hata hivyo hazikutolewa. Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kupunguza utegemezi kwenye fedha za Wahisani ambapo mara nyingi huwa hazitolewi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma, Vifungu na Mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha unaoishia. Katika uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

i) Bajeti inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 imeongezeka kwa asilimia 10.6 ikilinganishwa na Bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Ongezeko hili lipo katika Mishahara kwa asilimia 8.38 na imeongezeka kwa asilimia 1.97 katika Matumizi Mengineyo;

ii) Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo imepungua kwa asilimia 20.4 ikilinganishwa na Bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

iii) Upungufu wa Bajeti ya Maendeleo inayoombwa imepungua kwa kwa asilimia 46.2 kwa Fungu 29- Jeshi la Magereza, asilimia 8.9 kwa Fungu 93- Idara ya Uhamiaji; asilimia 7.19 kwa Fungu 51- Wizara na kwa Fungu 28- Jeshi la Polisi imepungua kwa asilimia 1.7;

iv) Bajeti ya Maendeleo inayoombwa kwa Idara ya Zimamoto ni kiasi kilekile kilichoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, jumla ya Shilingi Bilioni 3.5; na

v) Fedha za Matumizi Mengineyo zimeongezeka kwa Mafungu yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo: Fungu 14 Jeshi la Zimamoto- imeongezeka kwa asilimia 2.49, Fungu 28- Jeshi la Polisi imeongezeka kwa asilimia 1.4, Fungu 29- Jeshi la Magereza imeongezeka kwa asilimia 0.9, Fungu 51- Wizara kwa asilimia 0.9, na Fungu 93- Uhamiaji kwa asilimia 3.47.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo yaliyoainishwa hapo juu yanatokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia na kujadili Randama za Mafungu matano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mapema leo hii.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa maoni na ushauri wa jumla na mahsusi kwa kila Fungu kama ifuatavyo:-

### Ushauri wa Jumla

i) Kamati ilipopitia na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilibaini

kuwa upungufu wa Rasilimali watu umeendelea kuwa changamoto inayohitaji kupewa umuhimu wa kipekee katika kuishughulikia. Suala hili limekuwa likishauriwa na Kamati mara kwa mara hata hivyo halijapewa uzito unaostahili[1].
Kwa mara nyingine, Kamati inashauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa Watumishi katika Idara na Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutokana na Umuhimu wake katika usalama wa Raia na Mali zao;

ii) Kama ilivyofanyika kwa ujenzi wa nyumba za Watumishi na Askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania, Serikali ione umuhimu wa kuwa na Mpango Mkakati wa kujenga nyumba za makazi kwa ajili ya Watumishi na Askari wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hii itaondoa changamoto ya muda mrefu ya makazi kwa askari ambao wengi wao wanakaa uraiani jambo ambalo si zuri kiusalama;

iii) Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani yameendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya vyombo vya usafiri na usafirishaji. Kwa mara nyingine Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuyawezesha Majeshi yake kwa kuyapatia vyombo vya usafiri na usafirishaji ili kuweza kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi;

iv) Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo yanaendelea kukua kutokana na kutokulipwa kwa stahiki mbalimbali za Wastaafu, Watumishi na madeni ya wazabuni

[1] Jeshi la Zimamoto linauhitaji wa Watumishi 7,076 ikilinganishwa na watumishi 2039 waliopo; Jeshi la Polisi lina uwiano duni wa askari na wananchi wanaowahudumia ambapo uwiano uliopo ni 1:1,100 badala ya ule wa Kimataifa wa 1:450; na Idara ya Uhamiaji inajumla ya Watumishi 3,108 na mahitaji halisi ni Watumishi 19,320.

na watoa huduma[2]. Aidha, Serikali kupitia Hazina ilipe madeni yote yaliyohakikiwa, kipaumbele kitolewe kwa Wastaafu;

v) Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hazipatikani kwa wakati, jambo linaloathri ufanisi na tija ya miradi. Kamati inashauri Serikali kutenga na kutoa fedha za maendeleo kwa wakati kwa Mafungu yote ya Wizara ili kutekeleza kwa ufanisi miradi inayopangwa.

**Ushauri Mahsusi**

**Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

i) Kwa miaka minne mfululizo kuanzia Mwaka wa Fedha 2017/2018 hadi 2020/2021 Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Zimamoto lililopo katika eneo la Mchicha, Wilayani Temeke Jijini Dar es Salaam ambalo ujenzi wake ulisimama tangu Mwaka 2013. Kwa mara ya mwisho jengo hili lilitengewa Shilingi Bilioni Mbili (2) katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambapo fedha hizo hazikutolewa. Pamoja na ushauri huo, Mradi huu haukuwahi kutengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, 2020/2021 wala 2021/2022.

Kamati inamaoni kuwa Serikali haijalipa umuhimu wa kipekee suala hili. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kwa mara nyingine kuwa katika Mwaka 2021/2022 zitengwe fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo na litumike kuimarisha huduma za zimamoto na uokoaji katika Mkoa wa Dar es Salaam;

---

[2] i) Madeni ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji:- Watumishi Shilingi 1,619,368,892.18, Wazabuni Shilingi 209,369,122.88. ii) Madeni ya Jeshi la Polisi: Watumishi- madeni yaliyohakikiwa Shilingi 33,540,672,572.32, madeni yasiyohakikiwa shilingi 40,382,368,351.47-, Wazabuni- madeni yaliyohakikiwa Shilingi 342,920,138,358.55, yasiyohakikiwa Shilingi 193,742,163,031.12; Watoa huduma – madeni yaliyohakikiwa Shilingi 12,116,697,119.89, yasiyohakikiwa Shilingi10,076,396,223.69; Wastaafu- Shilingi 3,201,290,521.33. iii)Jeshi la Magereza: Shilingi 34,441,508,793.43- Wazabuni, Shilingi 37,689,347,522.67- Watumishi, Shilingi 14,793,434,809.73- Watoa huduma. iv)Idara ya Uhamiaji: Watumishi, madeni yaliyokubaliwa-5,830,902,394.80, madeni yaliyokataliwa 656,132,252; Madeni ya kusafirisha mizigo ya wastaafu na waliofariki Shilingi 54,674,600.

ii) Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kulipatia Jeshi hili magari ya kuzima moto na kununa vifaa vya kuzima moto na uokoaji. Hata hivyo fedha zinazotengwa haziendani na mahitaji halisi na fedha hizo huwa hazitolewi kwa Wakati. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Jeshi lilitengewa shilingi bilioni 3.5 lakini hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 ni asilimia 46 tu ya fedha hizo ilikuwa imetolewa.

Kamati inaishauri Serikali kuongeza ukomo wa bajeti ya maendeleo ya Jeshi la Zimamoto na kutoa fedha hizo kwa ukamilifu kuendana na mahitaji halisi ya Jeshi. Hii italiwezesha Jeshi hili kutatua changamoto za uhaba wa magari ya kuzima moto na uchache wa vituo vya zimamoto na uokoaji katika maeneo mbalimbali nchini jambo linalosababisha wananchi wengi kukaidi kulipa tozo kutokana na kukosekana kwa huduma za zimamoto na uokoaji;

iii) Pamoja na ushauri wa jumla uliotolewa hapo juu, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele katika kuajiri askari wa kutosha kulingana na miradi ya kimikakati inayoendelea ambayo itahitaji huduma za zimamoto na uokoaji. Miradi hiyo ni pamoja na ile ya upanuzi wa viwanja vya ndege, miradi ya umeme na gesi na ujenzi wa bomba la mafuta;

iv) Pamoja na nia njema ya Serikali katika kuongeza mapato ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Wizara iangalie upya tozo zilizopangwa kwa ajili ya ukaguzi wa vifaa vya zimamoto ambapo gharama yake ni kubwa kulingana na hali halisi ya vipato vya wananchi, jambo linalochangia wananchi wengi kushindwa kulipa na hivyo Serikali kupoteza mapato yatokanayo na tozo hizo.

## Fungu 28- Jeshi la Polisi

i) Serikali itoe fedha za maendeleo kwa miradi ya muda mrefu iliyokuwa imeidhinishiwa fedha katika Mwaka wa Fedha 2020/ 2021. Hii ni pamoja na Mradi wa kukamilisha kituo cha Polisi cha Mkokotoni ambapo Ujenzi wake umesimama tangu mwaka 2013 licha ya kuwa mradi huo ulikwishatekelezwa kwa asilimia 60;

ii) Pamoja na juhudi za Jeshi la Polisi za kutekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya vituo vya Polisi na nyumba za Askari kwa mfumo wa nguvu kazi (force account) kupitia Mfuko wa tuzo na tuzo na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, bado suala la makazi kwa Askari limeendelea kuwa changamoto ambayo inatakiwa kupewa uzito wa kipekee hasa kwa kuzingatia usalama wa Askari wanapoishi uraiani. Kamati inaendelea kuishauri Serikali iongeze na kuendeleza juhudi za kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayowasilishwa Bungeni na fedha zake kuidhinishwa na Bunge. Kufanya hivyo, kutaiwezesha Bunge kuongeza tija katika ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za umma inavyostahili;

iii) Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Kamati inaishauri Serikali kushughulikia changamoto za kimkataba zilizojitokeza katika mradi wa ujenzi wa nyumba 353 za Maafisa na Askari kwa ubia na Mwekezaji wa Sekta Binafsi katika eneo la Msasani na Kunduchi jijini Dar es Salaam ili nyumba hizo zianze kutumika;

iv) Ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia, Kamati inaishauri Serikali kutenga Bajeti ya kutosha na kutoa fedha hizo kwa ajili ya kuwawezesha Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi kukabiliana na makosa mbalimbali yakiwemo makosa ya kimtandao (cyber crime) na makosa yanayovuka mipaka (transnational crime). Aidha, kitengo cha Uchunguzi (forensic unit) kiwezeshwe kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Fungu 29- Jeshi la Magereza**

i) Kamati inampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kutoa Msamaha wa Wafungwa 5000 katika Sikukuu ya Muungano tarehe 26 Aprili, 2021. Msamaha uliotolewa kwa Wafungwa umeipunguzia Serikali gharama ya takribani Shilingi 4,075,000[3] kwa siku ambapo kwa Mwaka ni shilingi 1,487,375,000.

[3] Gharama ya kumhudumia mfungwa/mahabusu mmoja ni Shilingi 815 kwa siku

Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zote zitakazoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka 2021/2022 kwa jili ya vikao vya Bodi ya Taifa na za Mikoa za *Parole* ili wafungwa wengi zaidi wanaostahili kupewa msamaha wapunguzwe magerezani na hatimaye kuokoa fedha za Serikali zinazotumika kuwatunza ambapo kwa sasa takribani Shilingi 26,363,620 hutumika kwa siku sawa na Shilingi 9,622,721,300 kwa Mwaka;

ii) Pamoja na jitihada za Serikali katika kujenga Magereza mapya ili kutatua tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani, bado Jeshi la Magereza linakabiliwa na changamoto hiyo ambapo uwezo wa magereza yaliyopo ni kuhifadhi wahalifu 29,902 kisheria kwa siku ikilinganishwa na wastani wa wahalifu 32,348 waliopo kwa siku katika kipindi hiki.

Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga fedha za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa Magereza mapya. Kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya Shilingi 840,000,000.00 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Magereza Makuu na hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Magereza mapya;

iii) Serikali iliwezeshe jeshi la Magereza kupata magari hususan kwa ajili ya kusafirisha mahabusu ambapo kwa sasa mahitaji halisi ni magari 480. Upatikanaji wa magari hayo, pamoja na mambo mengine, utasaidia mahabusu kupata nafasi ya kusikiliza kesi zao kwa wakati uliopangwa na hivyo kuamuliwa mapema. Hii itapunguza msongamano wa wafungwa na Mahabusu Magerezani lakini pia itaondoa changamoto ya mahabusu kukaa muda mrefu magerezani bila kesi zao kuamuliwa;

iv) Tangu Mwaka 2016 Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali na jiko katika Gereza la Segerea. Hata hivyo ushauri huo haujawahi kuzingatiwa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha hizo ili kukamilisha ujenzi wa Hospitali hiyo ambayo ni muhimu kwa Gereza la Segerea;

v) Serikali itoe jumla ya shilingi milioni 840 zilizotengwa katika Mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kukarabati mabweni na miundombinu ya Magereza 12 nchini. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa;

vi) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa Shilingi 3,615,000,000.00 zilizotengwa katika mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la mpunga la gereza la Idete na ununuzi wa zana za kilimo. Aidha, kwa Mwaka 2021/2022 Serikali imetenga Shilingi Bil 6 kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora za mazao mbalimbali na kununua zana za kilimo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula. Pamoja na juhudi hizo za Serikali, Kamati inashauri Jeshi kuwa na mpango mkakati wa kuanzisha na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Magereza mengine ili Jeshi hilo liweze kujitosheleza kwa chakula na kuzalisha kwa ajili ya biashara.

**Fungu 51- Wizara**

i) Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kurekebisha Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 (The Road Traffic Act Cap 168 R.E 2002) na Kutunga Sheria ya Sekta Binafsi ya Ulinzi ya Mwaka 2021 tangu Bunge la Kumi na Moja. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Mapendekezo ya Sheria hizo, hata hivyo, kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa Mchakato wake unapewa umuhimu unaostahili ili Sheria hizo zipatikane mapema;

ii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa kiasi cha shilingi 6,319,692,308 kwa ajili ya Mradi wa Vitambulisho vya Taifa ikiwemo kununua kadi ghafi kwa ajili ya vitambulisho. Hata hivyo, Kamati inaendelea kushauri Serikali kuwa ihakikishe inazalisha vitambulisho[4] vyote kulingana na idadi ya namba za utambulisho ambazo zimekwisha tolewa kwa wananchi ifikapo Mwezi Juni 2021 kama ilivyokuwa imepangwa;

---

[4] Takribani vitambulisho 11,937,628

iii) Serikali iongeze jitihada za kuwafikia kwa urahisi watu wote wenye vigezo vya kusajiliwa na kutambuliwa wanaoishi mbali na makao makuu ya wilaya. Hii ni pamoja na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari ili kuwezesha wataalamu kuwafikia walengwa wengi zaidi;

iv) Mikataba ya Manunuzi ya Mitambo ya uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa ijumuishe mafunzo ya muda mrefu kwa Wataalamu wa ndani bila ya gharama ya ziada ili kuwezesha Serikali kumiliki, kuendesha, kuhudumia na kukarabati mitambo hiyo jambo ambalo litaepusha gharama kubwa zinazotumika kwa kutegemea wataalamu kutoka nje;

v) Serikali ikamilishe Mfumo wa kielektroniki wa usajili wa Jumuiya ili kuwezesha malipo ya kiektroniki kupatikana mahali popote nchini. Hii, pamoja na mambo mengine, itaongeza mapato ya makusanyo yatokananayo na usajili wa Jumuiya.

**Fungu 93- Idara ya Uhamiaji**

i) Idara ya Uhamiaji imeendelea kutokupelekewa fedha za maendeleo kwa mtiririko unaostahili. Kamati inaishauri Serikali itoe fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo hadi kufikia Mwezi Februari, Shilingi 400,000,000.00 sawa na asilimia 8.99 tu ya Shilingi 4,450,000,000 zilizoidhinishwa na Bunge ndio zilikuwa zimetolewa. Kutokutolewa kwa fedha hizo kutaendelea kuchelewesha utekelezaji wa Miradi ya maendeleo iliyokusudiwa;

ii) Pamoja na Sheria ya Marekebisho ya Utumishi wa Umma Na. 18 ya mwaka 2007 (The Public Service Ammendment Act, 2007) kuiondoa Idara ya Uhamiaji kutoka katika usimamizi wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kupelekwa kwenye usimamizi wa Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, bado Idara ya Uhamiaji pamoja na mambo mengine, haipati stahiki za kimaslahi na huduma za msamaha wa kodi kama vyombo vingine vya Jeshi katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Kamati inaishauri Serikali kuipa haki Idara ya Uhamiaji kama Majeshi mengine yaliyochini ya Wizara hii. Hii itaiwezesha masuala ya stahiki mbalimbali za Maafisa na Askari wa Uhamiaji kushughulikiwa kikamilifu na kuiwezesha Idara kutekeleza majukumu yake ya kisheria na kimuundo kwa ufanisi ndani na nje ya nchi;

Aidha, kwa kuwa tangu Mwaka 2007 Idara ya Uhamiaji ilianza kutumia Muundo wa Utumishi wa Maafisa na Askari wa Uhamiaji wenye vyeo vya Kijeshi sawa na vyombo vya Ulinzi chini ya Wizara ya mambo ya Ndani ya Nchi, Kamati inashauri Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 Rejeo la Mwaka 2016 ifanyiwe marekebisho ili Idara hiyo itambulike rasmi kuwa Jeshi;

iii) Pamoja na kuwa Idara ya Uhamiaji inachangia kwa asilimia kubwa katika mapato ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Idara hii bado inakabiliwa na uchache wa vyombo vya usafiri ambavyo pamoja na mambo mengine vinasaidia katika doria ya kuwabaini wageni wanaoishi bila vibali vya ukaazi. Kamati inaishauri serikali kuiwezesha Idara kupata vyombo vya usafiri ili kuwabaini wahamiaji wasio na vibali na kuwachukulia hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuwalipisha ada husika na faini.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard):-

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb. - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb. - **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb. - Mjumbe
4. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb. - Mjumbe
5. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb. - Mjumbe
6. Mhe. Janeth Mauris Masaburi, Mb. - Mjumbe

7. Mhe. Cosato David Chumi, Mb. - Mjumbe
8. Mhe. Stela Alex Ikupa, Mb. - Mjumbe
9. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb. - Mjumbe
10. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb. - Mjumbe
11. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb. - Mjumbe
12. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb. - Mjumbe
13. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb. - Mjumbe
14. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb. - Mjumbe
15. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb. - Mjumbe
16. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb. - Mjumbe
17. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb. - Mjumbe
18. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb. - Mjumbe
19. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb. - Mjumbe
20. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb. - Mjumbe
21. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb. - Mjumbe
22. Mhe. Emmanuel Godwin Kunambi, Mb. - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. George Boniphace Simbachawene (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Christopher Kadio, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ramadhan Kailima pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya

Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
Mei, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chumi kwa kupitia kwa ufasaha mkubwa kabisa taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa niaba ya Kamati. Tunakushukuru sana.

Sasa Waheshimiwa Wabunge tunaingia moja kwa moja kwenye uchangiaji na kama tulivyosema kwa sababu leo ni siku moja hebu nijaribu kuanza na dakika saba saba kwanza halafu huko mbele tutaona, nikiona kama naanza kubanwa tutarudi kwenye tano tano. Kengele ni moja tu itakayopigwa kwenye hizo dakika saba. Tuanze na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2020/2021 Mheshimiwa Waziri alieleza mafanikio makubwa sana juu ya bajeti hasa kwenye kipengele cha *NIDA* kwa asilimia 86. Kumekuwa na shida kubwa sana ya Vitambulisho vya Taifa hususan watu wa vijijini. *NIDA* walisema wana mpango wa kusajili watu takriban 25,000 leo hii Waziri anasema wamesogea wamefika watu 23,000 lakini waliopata Vitambulisho vya Taifa hawazidi milioni saba.

Mheshimiwa Spika, kuna watu walipata namba wakati ule akizungumzia bajeti hii walikuwa watu milioni 17 leo wameongeza wamekuwa 18. *Deadline* ya kupata Vitambulisho vya Taifa kwa mwaka huu ni tarehe 8 Juni, 2021 lakini kuna watu wanakaa zaidi ya mwaka mmoja hawajapata hivyo vitambulisho ijapokuwa wana hizo namba ambazo wamepewa hivyo kuwapa ugumu kuendelea kufanya shughuli za kitaifa kwa sababu wanavitegemea vitambulisho hivyo.

Waziri alisema kuna mashine mpya mbili wamenunua ambazo zina uwezo wa kutoa vitambulisho takriban 144,000. Naomba kupata maelekezo yake kama kweli mashine hizo zipo na vitambulisho vinapatikana. Leo Waziri ameeleza vizuri kwamba amejitahidi kutafuta taasisi zaidi ya 39 za umma na binafsi ili ziweze kujiunga na vitambulisho hivi vya taifa kama chanzo cha mapato ili watu waweze kutumia vitambulisho hivyo. Umuhimu wa vitambulisho ni mkubwa tunaomba Waziri atuambie mwisho wa changamoto hii ya upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa utakuwa lini.

Mheshimiwa Spika, nikija eneo la polisi, bajeti iliyopita walikuwa wajengewe nyumba 431 lakini leo hii tuna polisi wanakaa mitaani. Kamati imeshauri vizuri unapokuwa na polisi mtaani na yeye kazi yake anayoifanya wakati mwingine ni ya kugombana na hao raia kwa maana inategemea ni maeneo gani wanafanyakazi ni hatari sana kwa askari huyu. Polisi hawa wanakaa uraiani maana nyumba ni chache. Tunaomba bajeti hii waweze kuongezewa ili polisi wajengewe nyumba.

Mheshimiwa Spika, Rais amezungumzia suala la upandishwaji madaraja, naomba sana wakati huu madaraja hasa kwa askari wadogo utiliwe maanani. Hata hizo nyumba tulizozisema tuachane na viongozi wenye vyeo vikubwa kwani wanaopata shida ni maaskari wadogo ambao na wao wanahitaji kukaa kwenye makazi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya kipolisi, nilishawahi kufika Chuo cha cha Polisi Kidatu, mazingira wanayosomea

siyo rafiki kabisa. Majengo yale yalijengwa siku nyingi na ni chakavu, kwa hiyo, watu wale wanasoma katika mazingira magumu sana. Hivyo basi naomba Wizara hii safari hii isimamie na kuwatizama.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie makampuni binafsi ya ulinzi ambayo naamini yanasimamiwa na Wizara hii. Nataka kujua ni namna gani Wizara inasimamia hasa silaha za moto kwa makampuni haya binafsi. Wanawasimamiaje kuhakikisha wanatunza na kuwa waaminifu katika matumizi ya silaha hizi za moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, makampuni mengi binafsi yanaajiri wafanyakazi toka nje ya nchi. Ukienda kwenye hoteli nyingi za *Five Stars, Three Stars* utakuta walinzi wale wengi wanatokea Kenya wakilinda kwenye makampuni haya. Mimi nafikiri ni wakati sasa kuhakikisha SUMA JKT wanapewa kazi ya kulinda mahoteli hayo badala ya kutumia makampuni binafsi kwa sababu vijana wetu wengi hawana ajira, tunafikiri wao wanaweza wakatusaidia kupunguza ajira kwa kutumia makampuni ya nyumbani na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie masuala ya Zimamoto. Mara nyingi huwa nasema hapa Zimamoto ni jeshi la mwisho. Nikisema la mwisho nina maana hii, ni kweli kabisa ukiangalia *uniform*, dawa na nyumba za Zimamoto ni jeshi ambalo limekuwa likipata bajeti ndogo kulinganisha na majeshi haya mengine. Kama Kamati ilivyosema tunahitaji kuwekeza kwenye Jeshi hili. Si hivyo tu wamezungumzia Jengo la Mchicha shilingi bilioni 2 ziliwekezwa pale, ile ni pesa iliyolala mahali pale, najua hapa tumekwishajenga lakini bado kuna haja ya kuongeza fedha na kuhakikisha lile jengo linaisha hata tukalipa matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, suala la magari, bajeti iliyopita walisema watapata magari matano kutoka Nyumbu. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kama magari hayo yamepatikana kwa kutoa taarifa mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, magari ya Zimamoto, mikoani hakuna magari na kama yapo wafanyakazi ni wachache. Tunaomba ikama ya wafanyakazi katika idara hii iongezwe.

Mheshimiwa Spika, nikienda Magereza, leo hii watu walioko magerezani wafungwa ni nusu na mahabusu ni nusu. Tulisema wakati uliopita ni bora kukawa kuna kesi zile ambazo zinapunguza idadi ya mahabusu ili tuweze kupata nafasi ya kuwaweka wafungwa kwenye nafasi ya kutosha. Kama wafungwa ni zaidi ya milioni iliyotajwa, nusu 16 ni wafungwa waliohukumiwa na nusu 16 ni mahabusu. Kwa hiyo, mahabusu ni wengi tunaomba kesi zifanywe haraka haraka ili kusudi hawa mahabusu waweze kutoka na magereza yaweze kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kimsingi magereza mengi ni magereza yaliyojengwa enzi za ukoloni. Mimi sipendi watu wetu wafungwe lakini wafungwe katika staha, wakae kwenye magereza ambayo yana vyoo vya kutosha na wanawake waliokuwa kule magereza wapate stara ya kutosha. Tukiwa na magereza yenye maeneo madogo kama ni mahabusu kisaikolojia unakuwa umeshamfunga.

Mheshimiwa Spika, tumesema magereza itengeneze chakula. Gereza la Songwe ni kubwa na lina ekari nyingi lakini hawana vifaa vya kuwawezesha kulika. Ili ulime na uzalishe chakula lazima uwe na matrekta, wataalamu na fedha ya kununulia mbegu. Mmesema mmetenga mbegu lakini ni lini zitapatikana kwa sababu kila mwaka mnazungumzia kutenga mbegu. Songwe wana eneo kubwa lakini hawana trekta, vifaa vya kutosha na wataalamu, naomba Wizara itazame suala hilo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Sylivia Sigula na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Kwanza nianze kumpongeza sana Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu Waziri na *IGP* Sirro pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya za kutulinda sisi pamoja na mali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo kama mawili na la kwanza vitambulisho hivi vya *NIDA* ni tatizo kubwa sana katika maeneo mbalimbali hususan katika Jimbo langu la Makambako. Watu wameandikisha, wengine wamepata namba lakini vitambulisho vyenyewe hawajapata, kila wanapofuatilia havipatikani. Wengine wanakaa mbali vijijini kwenda wilayani kule nenda rudi nenda rudi, jambo hili limekuwa lina usumbufu mkubwa, nina imani na majimbo mengine katika nchi hii tatizo hili ni kubwa. Kwa hiyo, tunaomba sana katika bajeti hii Waziri aone namna ya kuhakikisha anaondoa usumbufu kwa wananchi juu ya kupata haki zao za vitambulisho vya *NIDA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, pamoja na kwamba nimewapongeza kwa kazi nzuri ya ulinzi wanayofanya katika nchi hii, wanafanya kazi nzuri sana lakini hivi sasa vibaka wameanza kunyemelea kurudi taratibu na majambazi wameanza kuteka magari. Nikuombe Waziri na timu yako na *IGP* Sirro, kama mlivyosimamia jambo hili awali msimamie na sasa ili likome kabisa wananchi waishi kwa amani katika nchi yao na mali zao kwa sababu sasa vibaka wameanza kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine liko kwenye Jimbo langu na ni tatizo la muda mrefu. Kituo cha Polisi cha Mji wa Makambako kuna wananchi takriban sita wako ndani ya eneo la polisi; hawaruhusiwi kufanya kitu chochote hata choo kikibomoka hawaruhusiwi kutengeneza. Siku ukipita pale tu hata wewe mwenyewe utawaonea huruma; choo

zimebomoka na nyumba zao ziko katika hali mbaya. Niombe fidia ambayo walikuwa wanaidai walipwe ili waweze kuondoka. Nimwombe sana Waziri na *IGP* Sirro waone namna ya kulipa wananchi hawa sita na tathmini ilishafanywa ili waweze kwenda kutafuta mahala pengine na wao waishi kwa amani katika nchi yao. Chonde chonde sana naomba jambo hili walichukulie kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, Makambako ni *center* na ni lango kuu la kwenda Songea au Mbeya na sehemu nyingine hata baadhi ya matukio ni watu waliotoka sehemu mbalimbali kuja pale. Kuhusiana na vitendea kazi naomba atenge gari maalum kuja katika kituo cha Makambako ili askari wangu pale waweze kufanya kazi kwa uhakika kulinda wananchi na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine tunashukuru kwa kujengewa nyumba za polisi katika eneo letu la Kituo cha Makambako. Haijawahi kutokea kuwa na nyumba pale sasa hivi wametujengea nyumba kwa kweli lazima tushukuru wamefanya vizuri na wananchi ndiyo maana waliunga mkono kujenga nyumba zile za polisi ili walinde mali zao vizuri na mimi Mbunge wao niliunga mkono kuhakikisha nyumba zile zinajengwa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu tuendelee kuwajengea nyumba zingine katika bajeti hii ambayo wameitenga ili askari wetu pale waweze kupata nyumba nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo sikuwa na mambo mengi ya kuchangia katika Wizara hii kwa sababu inafanya vizuri ni changamoto ndogo ndogo hizi tulizozizungumzia. La mwisho Mungu aniongoze kwa busara kuna jambo umelisema sasa na mimi kulisema tena siyo vizuri.

**WABUNGE FULANI:** Sema.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga, ni mmoja wa wazee wetu katika Bunge hili ambao tunawathamini sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Sylivia Sigula atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia na kwa sababu ya muda moja kwa moja naomba nijielekeze kuzungumzia Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, katika Jeshi la Polisi kozi mbalimbali zinatolewa na tunafahamu wazi kwamba kozi hizi ni nzuri kwa sababu zinawajenga askari wetu. Hata hivyo, kuna hii *refresher course* kwa ajili ya kuwajenga uwezo askari na utaratibu wa sasa hivi ni kwamba ni lazima ifanyike kwenye vyuo vya askari ambavyo viko Zanzibar, Moshi pamoja na Kidatu.

Mheshimiwa Spika, kozi hizi ni nzuri lakini utaratibu unaotumika sasa hivi si rafiki sana na hauleti tija. Katika kozi hizi askari wanajitegemea chakula na tunafahamu kabisa mishahara ya askari au watumishi mingi ni midogo lakini pia inakuwa na makato mbalimbali. Askari wetu wengi wanategemea sana posho lakini wanapokuwa kwenye mafunzo haya inawalazimu kukatwa Sh.7,000 kwa siku kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Spika, jambo hili si jambo rafiki sana kwa sababu kwanza linazuia tija ya kozi ile badala ya askari ku-*concentrate* na kozi anakuwa anawaza kwamba anatakiwa achangie pesa hiyo na inakatwa moja kwa moja kwenye posho. Tunafaahamu kwamba kwa siku posho ya askari anapewa shilingi 10,000, kwa hiyo, tunapokata shilingi 7,000 tunamlazimisha abaki na shilingi 3,000 ili aweze kuitumia na familia yake.

Kwa hiyo, jambo hili linamfanya awe na mawazo lakini pia atashindwa ku-*concentrate* kwenye mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe tu ushauri, utaratibu wa zamani ulikuwa ni mzuri, hizi *refresher course* zilikuwa zinafanyika kwenye mikoa husika kwa maana kwamba zilikuwa hazina makato ya gharama za chakula.

**TAARIFA**

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mchangiaji kwamba kozi hiyo inaitwa ya utayari na ilianza kutolewa kwa muda wa wiki mbili, wiki tatu, mwezi mmoja sasa hivi inatolewa kwa muda wa miezi mitatu. Akimaliza kozi hiyo baada ya wiki moja imeanzishwa tena kozi nyingine, kwa hiyo, ni tabu kidogo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa unapokea taarifa hiyo?

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo kwa sababu hiyo miezi mitatu kama askari akiwa kozi atakatwa Sh.7,000 kila siku.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naendelea na utaratibu wa zamani ambapo kozi hizi zilikuwa zinafanyika kwenye mikoa husika hizi gharama za chakula hazikuwepo. Askari wali-*concentrate* kwenye kozi kwa sababu mwisho wa siku walirudi nyumbani kwenye familia zao. Kwa hiyo, naishauri Serikali aidha utaratibu huu wa zamani ufuatwe au basi kama itawezekana Serikali ichukue gharama hizi za chakula kwa sababu haiwezekani tumpe mafunzo polisi halafu ajigharamie chakula. Kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali aidha ichukue changamoto hii ya chakula igharamie au urudishwe mfumo ule wa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze sana Wizara pamoja na Kamati imetoa ushauri mzuri lakini bado kuna changamoto kubwa ya vitendea kazi pamoja na *stationeries*.

Hivi navyoongea sasa hivi Kituo cha Polisi Kigoma Mjini hakina gari la askari. Sasa unaweza ukaona ufanisi utatoka wapi kama vitendea kazi vinakuwa adimu hasa tukijua kabisa Kigoma Mjini pale kuna bandari, benki na mambo mengi ambayo yangehitaji ulinzi wa raia na mali zao lakini mpaka sasa hatuna gari la askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini imekuwa ni utamaduni bajeti hizi zinazotengwa hazitoshelezi kuendesha haya magari ya askari. Leo hii ukipata tatizo ukipiga simu polisi utaambiwa gari haina mafuta, mbovu au haipo. Kwa hiyo, napenda kuishauri sana Wizara iingilie kati jambo hili hasa kwenye mfumo wa bajeti ya mafuta ili askari wetu hawa wawezeshwe vizuri na tutakapokuwa tunahitaji huduma tuzipate kwa wakati kwa sababu imekuwa ikileta shida sana kwa wananchi wanapotaka huduma ya kipolisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 12, ameeleza namna ambavyo wanashughulikia makosa na taarifa zinazotolewa Polisi, lakini kumekuwa na mlundikano mkubwa sana wa mahabusu katika Vituo vya Polisi. Utaratibu huu tunaona ni kinyume na sheria. Sheria inatutaka tusizidishe masaa 48 mtu awe ameshafikishwa Mahakamani, lakini utaratibu huu haufwatwi, vijana wanawekwa ndani, ukiulizia unaambiwa upelelezi unaendelea au unaambiwa maelezo hayajachukuliwa. Kwa kweli hali hii inawatesa sana wananchi. Kwa hiyo, naiomba Wizara ione namna nzuri ya kushughulikia jambo hili, kupunguza msongamano wa mahabusu katika Vituo vya Askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona kabisa na ni wazi kwamba katika majeshi mengine kumekuwa na utaratibu mzuri wa kuwa-*handle* hawa Askari wa kike, wamekuwa wakipatiwa fedha ya kujikimu katika mazingira yao ya kike hasa ya hizi *pads,* lakini katika Jeshi la Askari Polisi, Askari wa kike hawapatiwi. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara, kama yote ni majeshi, kwa nini wengine wapatiwe, wengine wasipatiwe? Kwa hiyo, naomba sana jambo hili liweze kuchukuliwa *serious,* kwani Askari hawa wanafanya kazi ngumu, nzito na pia

wanafanya kazi ambayo inaleta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA F. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Neema, endelea.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA F. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kutoa taarifa kwamba jambo hili la uhitaji wa taulo za kike siyo tu kwa watumishi maskari wanawake, pia kwa wafungwa na mahabusu wanawake.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imekuwa ikitenga bajeti ndogo kwa ajili ya kuwawezesha wafungwa na mahabusu wanawake, lakini bajeti hii imekuwa haitoki na matokeo yake hawa wanawake walio mahabusu na wafungwa wanatumia magodoro na magazeti wanapokua kwenye siku zao jambo ambalo ni hatarishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Sylivia hujaendelea, hii inanikumbusha wakati wa vita vya Kosovo na Herzegovina palikuwa na vita moja kule Yugoslavia ya zamani ambayo ilikuwa mbaya sana. Sasa baada ya vita ile kwisha, wakawa wanamhoji mtu mmoja, raia wa kule kwamba katika vita hii, kitu gani kilikuwa ni shida kubwa sana katika kipindi cha vita? Yule mtu akasema, yaani hebu *imagine* wakati ule kulikuwa hakuna *toilet paper*. Yaani kwake katika shida kubwa wakati wa vita, kulikuwa hakuna *toilet paper* kabisa. Sasa *you can imagine* matatizo makubwa kama haya! Endelea Mheshimiwa Sylivia. *(Kicheko)*

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naipokea taarifa.

**SPIKA:** Nafikiri siyo kwa Polisi peke yake, itakuwa na Magereza, Uhamiaji na Zimamoto labda. Ahsante, endelea. *(Makofi)*

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimalizie kama nilivyokuwa naeleza. Kwa hiyo, jambo hili linabidi lichukuliwe kwa uzito wake, wanafanya kazi ngumu, lakini pia mazingira siyo Rafiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kabisa, kwenye hizo *stationary*, sisi tunaotokea mikoa ya pembezoni, mgao huu wa *stationaries* unachelewa kutufikia. Leo Kigoma na mikoa mingine ya pembezoni, nafikiri hata na Rukwa, tunachelewa kupata vitendea kazi *(stationary).* Unakuta hizi *log book* pamoja na mambo mengine havitufikii kwa wakati. Tunaomba sana Wizara izingatie mgawanyo huu, hat sisi wa mikoa ya pembezoni tuzipate basi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunapozungumzia suala la vitendea kazi ambavyo nimesema, ilikuwa ni ajabu sana, juzi nilipigiwa simu na mwananchi, amefika Kituo cha Polisi hajapata *PF3,* anaambiwa zimekwisha, akatoe *copy* nje. Nadhani tuweke utaratibu mzuri, kama hizi *document*... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylivia Sigula. Tunakupongeza sana. Ni Mbunge kijana, kwa kweli mchango wake ni mkubwa na mzuri. Tunakutia moyo, utaendelea ku-*improve* na *ku-improve* zaidi na zaidi. Ila unalijua sana Jeshi la Polisi, umetokea huko nini? Ahsante sana, hakuna neno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, lile la taulo za kike *is very serious*. Mwakani mkirudi na bajeti yenu hilo halijawa *addressed*, Wabunge akina mama wote humu ndani wakishika shilingi ya Waziri, sijui bajeti yako itapitia wapi? Mwakani, siyo leo. Kwa hiyo, mliangalie kipekee, kwa kweli ni hitaji ambalo ni la lazima, tuangalie tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami napenda kuchangia kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambayo ni muhimu sana.

Kabla sijaanza kuchangia, napenda kujua kwa kweli hatima ya vijana wawili; Wilson Thomas na Richard Kayanda ambao walipotea wakati wanatoka nyumbani kwangu; walikuwa kwenye timu yangu ya kampeni siku tarehe 26 mwezi wa Kumi, mpaka leo hawajulikani walipo. Hawa vijana wana wake zao, wana watoto wadogo na ndiyo walikuwa tegemeo kwenye familia. Mheshimiwa Waziri unalifahamu hili, *IGP* analifahamu, *RPC* analifahamu, *OCD* analifahamu, *DC* analifahamu; tungependa kujua hatima ya hawa ndugu, kama wameshafariki mtuambie tuweke matanga; na kama wapo gerezani tuweze kwenda kuwatembelea tuwaone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee sasa. Ukisoma hotuba au ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu waliotoa Machi, 2021 wameonyesha ni jinsi gani Jeshi la Polisi linakiuka Haki za Binadamu na wakaainisha baadhi ya mambo ikiwepo raia kufia mikononi mwa Jeshi la Polisi, pia ukamataji usiokuwa na staha; na huu ninaweza nikakiri kwamba ni mimi mhanga mmojawapo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020 mwezi wa Kumi nilivamiwa na Jeshi la Polisi, wakaja kunikamata na video ilizunguka sana. Tena Jeshi la Polisi wanaume, wakati mwanamke anatakiwa akamatwe na Polisi wa kike. Mbaya zaidi, kijana yule Polisi alionekana kabisa akinipapasa kwenye makalio. Kwa hiyo, ni wengi sana wanafanyiwa hii kero.

Unapoenda kukamata una-*harass* kitu ambacho ni kinyume cha haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunashuhudia watuhumiwa wanapokua kwenye Jeshi la Polisi vituoni wanapigwa na kuteswa. Kuna baadhi ya Polisi wanawatesa wakiwalazimisha wakiri makosa ambayo hawajayatenda na ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu imeainisha haya. Kwa hiyo, Waziri naomba myafanyie kazi ili sasa Jeshi la Polisi, isiwe *Police Force* kama ilivyo, liweze kuwa ni Jeshi ambalo linatoa huduma kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa spika, kitu kingine ni jinsi ambavyo watuhumiwa kwa maana ya wafungwa na mahabusu wanavyokaguliwa kwenye Magereza yetu. Juzi wakati Mheshimiwa Ole-Sendeka anaongea kwa machungu sana kuhusu Mererani, kwamba watu wanakaguliwa uchi, ikanikumbusha sana wakati niko Segerea. Mnavyoingia pale, mnavuliwa nguo zote, mnaambiwa mnakaguliwa na hata kama mama yuko kwenye siku zake, utaruka kichurachura ili waone kama una kitu umeficha huku chini. Mwaka 2020 nilizungumzia hili jambo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukipiga picha, siku hizi wanakamata hata familia. Leo unamkamata baba ana mkwelima wake, labda mkwelima ana shemeji yake pale, wakifika Gerezani wanavuliwa nguo zote wanabaki uchi wote! Uchi kabisa wa mnyama, anakalishwa kwenye ndoo analazimishwa kwamba ajisaidie haja kubwa ili waone kama kuna kitu ameingia nacho Gerezani. Nadhani hii ni kinyume kabisa na haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru Waziri Mkuu juzi alitoa kauli hapa kwamba wataenda kuangalia, ikiwezekana waweke *mashine*. Tuwe na *modern tools* za ku-*screen*, mahabusu akipita au akiingia anakuwa *screened* tu, kama kuna kitu ameweka tumboni kitaonekana, kuliko wanavyofanya sasa hivi. Ni udhalilishaji. Yaani kila unapotoka kwenda Mahakamani, ukirudi lazima uvue nguo zako zote, ukaguliwe, ni udhalilishaji sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine kwenye *NIDA*, vitambulisho vya Taifa ni muhimu sana. Mosi, vingeweza kuwa ni pato hata kwa Taifa letu. Tunajua kwamba makampuni mbalimbali yanatumia kama *data* na wanalipa, bima, ukienda benki, ukienda kwenye simu, lakini pia hata Watanzania wengi hasa walivyosema ukiwa na simu ni lazima usajili kwa kutumia Kitambulisho cha Taifa, wengi walihangaika sana. Utakuta hata mwingine anamsajilia ndugu yake.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo uliainisha kwamba kufikia Juni, 2021 tutakuwa tumeandikisha na kutoa vitambulisho kwa Watanzania milioni 21, kitu ambacho kimekuwa kinyume. Hata leo hapa Mheshimiwa Waziri anakiri tumeshamaliza Mpango wa Pili, kwamba ni milioni saba tu ndiyo wana vitambulisho. Pamoja na kwamba kulikuwa na kanuni ya 7(1) inaelekeza wale Maafisa Uandikishaji wanapoandikisha wahakikishe wanatoa vitambulisho ndani ya miezi sita. Mheshimiwa Waziri amesema hapa kuna watu wana namba, ambao ni zaidi ya milioni 18. Hao kwa mujibu wa hii Kanuni walitakiwa wawe na vitambulisho, lakini hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine, ukisoma ripoti ya *CAG* amesema haya yote yamefanyika kwa sababu ya upungufu wa rasilimaliwatu na fedha. Ukiangalia mwaka wa fedha 2016/2017 waliweza kuandikisha 4% tu ya lengo ambalo lilikuwa limewekwa. Kwa hiyo, utaona kwamba hatutoi kipaumbele. Hii inasikitisha. Kama tunaweza tukahuisha na wapiga kura wakapata kadi zao, tunashindwa nini kwenye hiki kitu muhimu sana ambapo Kitambulisho cha Taifa unatembea nacho kila sehemu! Nimesema, kwa hicho kitambulisho unapata mapato kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine *CAG* ripoti imeonyesha kulikuwa hakuna viashiria ambavyo vingeweza kufuatilia ufanisi wa hii kazi, lakini mbaya zaidi kadi zaidi ya 427,000 ziliweza kuharibika ambazo *is worth* shilingi bilioni 3,400. Sasa shilingi bilioni 3,400 zimeharibika ambazo hata ukisema ujenge madarasa ya shilingi milioni ishirini ishirini ni zaidi ya madarasa 170 watoto wetu wangeacha kukaa kwenye miti, lakini

zimeharibika. Kwa hiyo, naomba sana tuone umuhimu wa *NIDA,* watu wapewe Vitambulisho vyao vya Taifa. Kwanza hata inaweza kupunguza uhalifu, maana unaweza uka-m-*trace* mtu popote pale. Pia hata kwenye haya mambo ya *Loan Board* wanaweza waka-*trace* wakajua ni vipi watakupata; na sehemu nyingine zote Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kingine, napenda kuongelea kuhusu maslahi ya hawa Askari Magereza na Askari wengine kwa kweli. Hawa watu wanafanya kazi. Mimi nazungumzia Magereza kwa sababu nimeishi nao. Namshukuru Mungu nilivyoenda Gerezani miezi minne ile, nimeweza kujifunza mengi sana. Askari Magereza leo, mwenye *degree* analipwa shilingi 770,000/= lakini hapewi asilimia 15 za taaluma kama wanavyopewa wenzao Askari Polisi. Kwa mfano, Askari Polisi mwenye *degree* analipwa shilingi 860,000/=, anapewa asilimia 15 ya taaluma ambayo ni shilingi 129,000/=, anapewa shilingi 61,000/= ya pango, lakini wenzao huku hawapati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi hawa watu hawajapandishwa vyeo kwa takribani ya miaka sita. Hakuna ajira ambazo zimefanyika kwenye Jeshi la Magereza na kwingine kote. Tunajua kuna watu wanakufa, watu wanaacha kazi, kuna watu wanalemaa na mambo mengine mengi, sasa tusipoajiri kwenye hii kada tunasababisha utendaji kazi kuwa na udumavu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine, *uniform,* nimelipigia sana kelele hili. Hawa maaskari wanajinunulia wenyewe. Fedha zilitoka mathalani, naambiwa fedha zilitoka kidogo wakaambiwa wanunue *baret,* lakini ni wajibu wa Serikali kuhakikisha yule Askari anapewa kama ni *baret*, anapewa shati, anapewa mkanda, suruali, sketi, kiatu *everything!* Sasa wamekuwa wakijinunulia muda wote. Sasa kama ni hivyo kwamba Serikali inashindwa kuwanunulia, basi waweke *package* kwenye mshahara wao ili wakiwa wanapata na wawaelekeze ni wapi wanaenda kununua. Ukiwa-*align* hapa utakuta kila Askari ana-*uniform* yake tofauti tofauti. Huu pia ni udhalilishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kwenye zimamoto. Lazima tujue kama Taifa majanga ya moto yameongezeka. Umeme wenyewe unakatikakatika kila mara, mengine yanatokea ni hitilafu tu; mtoto amewasha kiberiti, pasi ya umeme na nini; lakini ukiangalia kiuhalisia, hatuna magari ya zimamoto kwenye Majimbo na Wilaya, achilia mbali ofisi. Hapa Mheshimiwa Waziri amesema anajenga Chamwino, kwa sababu hapa kuna Ikulu, lakini huko ukienda wilayani ukikuta gari, ni lile dogo ambalo halina *capacity.* Kwa mfano, lile gari lililoko Tarime, ikitokea dharura yoyote haliwezi kwenda Mori ichote maji irudi. Kwa hiyo, badala ya kununua magari ya washa washa, tununue magari ya zimamoto.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Esther Matiko. Huyo ni shuhuda wa mapito. Halafu baada ya mapito hayo, anatokea mtu mmoja anafukuza wenzie utafikiri vibaka. *Is not fair* duniani hapa. Duniani ni lazima uwe na kumbukumbu.

Mheshimiwa Kamishna Fakharia Shomar Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Athuman Maige. Mheshimiwa Kamishina, tafadhali.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na pia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia na kuipongeza Wizara; Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote waliokuwepo Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia magari ya doria ya Polisi pamoja na Magereza na magari yanayochukua mahabusu. Magari ya doria ya Polisi ndiyo kiini kikuu kwa Polisi kuweza kuwakamata au kufuatilia majambazi na aina zote za tatizo litakalotokea katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Viongozi Wakuu wanapokwenda ziara, magari ya doria ndiyo yanayoshughulikia, lakini Mheshimiwa Waziri alipokuja kuzungumzia hapa ukurasa wake wa 37, kasema anatoa

magari tisa na hayo anawapa Magereza kwa ajili ya utawala. Hiyo kweli sikatai, lakini kwanza tutizame katika utendaji. Kamati yetu ilikwenda ziara, tukapewa gari ya doria, kila mkoa tulikuwa tunabadilishiwa na ndiyo utaratibu. Ilikuwa likifika kwenye kilima, gari inatoa moshi utafikiri chetezo. Haliwezi kwenda, halina nguvu. Sasa ina maana hizi gari ni mbovu na haziwezi kukidhi mahitaji. Unamfukuza jambazi kwa gari kama hiyo utampata? Humpati. Sasa kwa vyovyote mjitahidi baada ya gari kutumia ninyi utawala au viongozi, mtafute gari za doria kwa ajili ya maskari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukichukua Magereza wakati mahabusu wako Magereza, tatizo linakuwepo hapo, hawapelekwi Mahakamani kwa wakati, maana hakuna gari na Magereza yapo mbali na Mahakama. Ina maana tunawapa tatizo wafungwa wale walioko ndani au mahabusu kuweza kufika kwa wakati Mahakamani. Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie, magari ndiyo uti wa mgongo katika kazi zao, maana bila hayo magari hao Polisi hawataweza kufanya kazi zao kwa ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija na ajenda ya pili, nataka kuzungumzia kwa upande wa Zanzibar kidogo. Zanzibar kuna kituo kinaitwa *Ng'ambo Police Station.* Nakumbuka wakati mimi mdogo ndiyo kwanza nazaliwa, bibi yangu nilimsikia anakiita kibiriti ngoma, ambalo ndilo jina la awali, baadaye likabadilishwa, likawa Ng'ambo. Kituo kile kiko katikati ya mji pale Mkoa wa Mjini Wilaya ya Mjini, ambapo kipo katika katika Jimbo la Mheshimiwa Abdulwakil. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza, kituo kile hakina uzio na kituo cha mwanzo kikubwa kile; hicho Madema kimefuatia baadaye, lakini kituo kile ndiyo kilikuwa kituo mama na kimezungukwa na barabara. Unaweza kupita ukakuta ndani kuna kuku anaranda, mara ndani kaingia mbuzi anaranda. Sasa Polisi na hivyo vitu vinaendaje? Unaweza ukapita ukaona kinachofanyika ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale pale pana kituo kingine tu cha Serikali wamejengea uzio wa matofali. Sasa na nyie

naomba kile kituo kwa sehemu kilipokuwepo kipate uzio wa matofali ili kiweze kujisitiri, baadaye na kile kituo mtaweza kukikarabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiendelea, kuna tatizo hili la Magereza. Magereza wanapokea mahabusu, lakini mahabusu wanaopokea wengine na kwa wale wakimbizi ambao wamechukuliwa kama 100 au 50. Sasa baada ya kupelekwa Mahakamani inabidi warejeshwe mahabusu. Wanaporudi mahabusu kwa kweli tunawaonea wale Jeshi la Magereza. Mnawapeleka, wale hawako kwenye bajeti, hawana chakula na wale wako wengi, mnategemea kule Magereza watakula nini? Ina maana sasa wajibane.

Mheshimiwa Spika, Magereza itafute mbinu wewe Polisi umekamata, kazi yako imekwisha; Mahakama kuhukumu, kazi yake imekwisha; lakini wakati mwingine hukumu inatoka inabidi watolewe wale na wakitolewa inatoka faini ili watoke, lakini ile faini haiendi Magereza, inakwenda Serikalini. Sasa yeye ile bajeti yake ya chakula aliyoitumia akiwalisha wale itakuwaje? Mngefanya basi wakati wao wanapita njia za panya nanyi mkawakamata, basi wajilishe, japo ni mahabusu wajilishe wenyewe, lakini uzito huo msiwape Jeshi la Magereza ambao wanapata usumbufu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye zimamoto, nawapongeza. Wana *club* ambayo wanafundisha katika katika *school* za sekondari jinsi ya kuzima moto ili ukitokea moto waweze kujihami wenyewe, lakini wanakwenda kidogo kidogo. Maana toka wameanza, ndiyo kwanza sekondari 10. Nawaomba wajitahidi wafanye kila mkoa angalau sekondari tatu, nne na siku hizi majanga ya moto kwa mashule yako mengi, halafu tena kama wao watakuwa hawafanyi hii club, siyo vibaya kuwa na club, lakini wafanye haraka ili zisambae kwa Tanzania nzima, vijana wetu wawe na weledi wa kuweza kuhami moto kabla haujawaathiri.

Mheshimiwa Spika, nikija kwa Polisi wastaafu, hawa kila siku wanaongeza ingawa suala hili mama kaligusia jana,

lakini kwa nini hawafanyi wakati mtu unamjua tarehe fulani anastaafu. Kwa nini hawamfanyii ili akiondoka pale, aende na *cheque* yake, unajua umemtumia toka kijana, ujana wake kamalizia pale mpaka anakuwa mtu mzima, leo unamtoa haki yake humpi na nina hakika kwa viongozi wa juu, wakiondoka wanaondoka na *cheque* zao au wanaondoka pesa imeshaingia kwenye akaunti, lakini hawa wanyonge ndio wanaowahangaisha.

Mheshimiwa Spika, sasa hawa wanyonge wajaribu kuwapa, ikiwa wanatoa cheki au *cash,* tena wanawapingia tunajua tarehe fulani mwaka fulani, fulani atastaafu, anajijua mimi naondoka pale naagwa na changu tayari, la sivyo tutakuta wanapata malazi ya *pressure*, wanakufa mapema, ameshazoea kutumia, ana familia wanawaangaliaje, ina maana kila siku wawafuate, bora wampe chake. Nalishukuru Bunge, unaondoka, unaondoka na chako, tena mwenyewe utajijua. Kwa hilo Bunge halina mjadala. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, Ahsante naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Bunge mambo yanakuwa mazuri kwa sababu ya Makamishina kama Fakharia, wanahakikisha mambo yanakuwa sawasawa.

Mheshimiwa Almas Athumani Maige nilishakutaja, Mheshimiwa Ravia Idarus Faina atafuata.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Leo nifuate mwongozo wako au ushauri wako kwamba uongee jambo moja linaloeleweka. Leo nataka kuongelea sekta ya ulinzi binafsi. Sekta ya ulinzi binafsi hapa imeanza mwaka 1980 na kampuni mbili na ilianzishwa na Mheshimiwa Rais aliyekuwepo madarakani kwa kumwita *IGP* kwamba sasa tunarudisha makampuni yote na mali zote za wenyewe hatuwezi kuendelea kuzilinda na mgambo, Jeshi la Polisi. Kwa hiyo yakaanzishwa makampuni mawili *Group*

*Four* na bahati nzuri sana *IGP* aliyekuwepo akaomba *share* kwenye *Group Four* lakini pia *Ultimate Security* nayo pia Kamishna wa Polisi Rashid akaomba nae awe kwenye *group* hilo.

Mheshimiwa Spika, leo tuna makampuni 3,500 yameajiri askari walinzi laki tano, Jeshi la Polisi hawazidi elfu 60. Kwa hiyo sehemu kubwa ya ulinzi nchi hii inafanyika na sekta ya ulinzi binafsi. Hata hivyo, hakuna *GN* wala sheria wala mwongozo wowote ulioanzisha sekta hii nchi. Sekta hii imeendelea kukua, matokeo yake mambo mabaya sana yanafanywa kwenye sekta hii, lakini pia Serikali inakosa kodi, haina idadi kamili ya makampuni kwa sababu hakuna mwongozo wowote.

Mheshimiwa Spika, duniani, mimi nina sheria tatu hapa za sekta ya ulinzi binafsi, tulikoiga sisi; *Private Security Services Act,* lakini tuna Sheria ya *Common Wealth,* hii ni ya Jumuiya ya Madola, Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi, lakini kuna sheria nyingine muhimu sana inaitwa *Data Protection Act* ya sekta ya ulinzi binafsi, lakini pia kuna sheria nyingine *Regulatory of Investigatory Power Act.* Zote sheria tatu zinadhibiti makampuni ya ulinzi kwa sababu yanalinda raia na mali zao lakini wana silaha.

Mheshimiwa Spika, sekta ya ulinzi binafsi hapa nchini imesaidia kueneza silaha nchi nzima *shotgun* na udhibiti hakuna kwa sababu makampuni haya yalipoanzishwa mwaka 1980 na Jeshi la Polisi, viongozi wote wa Polisi wana makampuni ya ulinzi. Asilimia 75 makampuni ya ulinzi nchi yanaongozwa au yanadhibitiwa na polisi. Matokeo yake Polisi hawa viongozi waliokuwa na uwezo mwaka 1980, miaka 40 baadaye wamezeeka au wamefariki.

Mheshimiwa Spika, sasa makampuni haya yanaendeshwa na watu ambao hawana uwezo wowote, yamerithiwa kama mali ya mtu binafsi, watoto wamerithi, wake zao wamerithi na ndugu zao wamerithi. Mabunduki yako uvunguni, hivi karibuni naomba nitaje maslahi yangu, nilikuwa Mwenyekiti wa Sekta ya Ulinzi Binafsi, tulianzisha

chama ili kuweza kuji-*control* sisi wenyewe. Nikamsaidia Mheshimiwa *IGP* Mwema kuanzisha *at least* kanuni ndogondogo ambazo sio sheria wala haziko kwenye sheria yoyote.

Mheshimiwa Spika, leo hii makamppuni yana hasara huku na huku. Kwanza makampuni yenyewe haya baada ya miaka 40 na kurithiwa na watu ambao hawana taaluma, yanaendeshwa yanapata mambo yafuatayo kama changamoto:-

Mheshimiwa Spika, Askari wanaiba mali za watu ambao wanawalinda, mnakumbuka kesi ya Kasusura aliyetumwa kwenda kuchukua milioni mbili dola akatoweka nazo; Wizi wa mishahara ya benki ya *NMB,* walitumwa wagawe hela, walinzi wakavua nguo pale Kawe wakachukua hela, wakaacha silaha na kila kitu; Wizi wa *CRDB* Azikiwe mabilioni; Wizi wa kule Moshi mabilioni pia; na Walinzi wanakufa na hakuna uhakika na hawapati haki zao.

Mheshimiwa Spika, Temeke *NMB* ilivamiwa, kulikuwa na Polisi na kampuni za ulinzi binafsi, walinzi wote wakafa, huyu Polisi wa cheo cha chini akazikwa na bendera ya Taifa na huyu mlinzi aliyekuwa *Sergent* wakati anastaafu akazikwa kawaida kabisa, hii sio haki. Vilevile walinzi wote waliopiga risasi majambazi wameshtakiwa kwa mauaji. Pale Tabora majambazi yanataka yambake mtoto, samahani lugha chafu, wanataka kumbaka mtoto wa kike, yule mlinzi amekamata silaha wanamsukuma mwisho akafyatua risasi, baadae amekamatwa kwa mauaji. Naye yupo kazini, hii ni kwa sababu hakuna sheria.

Mheshimiwa Spika, haya naweza kuyasema kwa uchungu sana. Mimi nilipoingia madarakani nilitoka sekta ya ulinzi binafsi, nimeleta mfano wa sheria, Serikali ikasema itaileta. Leo hii hakuna chochote kilichokuja humu Bungeni. Sheria itaanzisha mamlaka inaitwa *Public Security Authority* kama *EWURA, TCRA, TRA* na kadhalika, ndivyo ilivyotoka duniani kule, hiyo mamlaka itakuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani sio Jeshi la Polisi, lakini polisi hawa

wanashindwa kuleta sheria hiyo kwa sababu sasa wenyewe ni wenyewe, wanajisimamia wenyewe.

Mheshimiwa Spika, limezuka jambo lingine ambalo linasikitisha sana, kutokuwa na mamlaka yoyote tunakosa *local content* kwenye migodi au kwenye mashirika makubwa ya kidunia, kwa sababu hatuna viwango. Makampuni ya Tanzania hayana viwango, hayana cheti wala hayajapangiwa kiwango gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuchukulie zabuni itangazwe ya kujenga barabara, si lazima mtu wa *civil* ndio afanye *quotation* kule na ufundi umeme naye ana-*quote* kwenye barabara; tunatangaza zabuni ya ulinzi wana-*quote* makampuni yote, kumbe kwenye sekta hii kuna *man guarding,* kuna mitambo, lakini kuna upelelezi na vilevile kuna wanaosindikiza mali wanajiita *CIT.* Sasa inatangazwa zabuni vurugu tupu, ni ya nani hiyo zabuni. Kungekuwa na mamlaka itapanga kwanza kazi hii daraja la ngapi.

Mheshimiwa Spika, tunapotangaza kazi ya ujenzi wa jengo hili tunasema mkandarasi daraja kadhaa, makampuni hayo huko yalikotokea yana madaraja la kwanza mpaka la saba, lakini pia yana taaluma hapa tunaenda fujo tu. Hivi karibuni kumekuwa na usemi wa *Auxiliary Police* wanasema haya makampuni yote ni *Auxiliary Police,* sio kweli, *Auxiliary Police* ni watu wengine na sekta ya ulinzi.....loh!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja hii nitaandika *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige. Kwa kweli katika sekta hii umetupa *lecture,* Mheshimiwa Waziri basi mtafuteni mzee Maige hapa ili awamegemegee zaidi ya hayo na tuweze ku-*improve*. Mheshimiwa *IGP* nilisikia profesa mmoja *retired professor* wa pale Usa River, nafikiri na nyie Wabunge mmemsikia kwenye mitandao, yule profesa sijui

Meena sijui nani, amefanyiziwa vitu vya ovyo sana, tena na baadhi ya askari wetu ambao walimpeleka mpaka kituoni, ile ni picha mbaya mbaya kabisa. Nadhani lile lifanyiwe kazi angalau Taifa tujue ni nini kinatokea, kama wastaafu wetu wanaweza kufanyiwa mambo ya kihuni namna ile tena na askari wetu kabisa, inakuwa haipendezi kabisa.

Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, sasa tunarudi kwenye dakika tanotano.

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. Kwanza nataka kupata ufafanuzi juu ya Serikali kwa nini haijajenga Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Zanzibar na hii inapelekea kwamba Waziri na Naibu Waziri wanapofika Zanzibar wanapata tabu sana, wapi watafikia. Kwa hiyo naiomba Serikali ilete ufafanuzi juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa vile muda ni mchache...

**SPIKA:** Hebu fafanua hilo likoje.

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, hadi hii leo Zanzibar hakuna Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa hiyo ni lini Serikali itajenga hiyo Ofisi hili Waziri na Naibu Waziri wanapokuja Zanzibar wawe na sehemu maalum ambayo wanafikia.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba Serikali itupatie Ofisi ya *NIDA* pamoja na Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Kusini Unguja ambayo tunakosa huduma hiyo, ukizingatia wananchi wa Wilaya ya Kusini wanakosa huduma nzuri ambayo wanaihitaji kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu Jeshi la Polisi; hapa nisipopata ufafanuzi mzuri natarajia kushika shilingi.

Kwanza naomba nipate ufafanuzi, ni kwa nini askari polisi anasoma na ahahitimu *degree* yake ya kwanza na

anapomaliza *degree* yake anapelekwa kozi ya *sergent* na anapata cheo cha *sergent.* Je, huyu ambaye kasoma *diploma* na *form six* yeye atapewa cheo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeweka utaratibu mzuri tu wa *PGO,* lakini *PGO* inatumika katika baadhi ya maeneo, baadhi ya maeneo haifanyi kazi. Inakuwaje Askari Polisi anakaa miaka 15 hajapata *rank.* Jeshi la Polisi linawapeleka askari, *rank* pamoja na faini, lakini cha kushangaza mpaka kufikia mwaka 2013 hawana stahiki zao ambazo wanazipata.

Mheshimiwa Spika, vilevile Askari Polisi wanapewa jukumu la kuwachukua watuhumiwa kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine lakini hakuna stahiki zao ambazo wanapata, wanaishia kujaza fomu na hizo fomu zinabakia kwenye mafaili hadi leo hawapati stahiki zao. Hii inaleta usumbufu kwamba huyo ambaye anaenda kumchukua mtuhumiwa ni yeye mwenyewe amuhudumie mtuhumiwa, sijui pesa anaitoa wapi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa suala ambalo alichangia Mbunge mwenzangu kwamba, Askari Polisi wanahitaji kupatiwa vitendea kazi, haipendezi kuona *documents* muhimu za Jeshi la Polisi zinapelekwa kwenye vibanda vya kawaida tu kutolewa *photocopy* ili ifanyike hiyo kazi, hiyo haipendezi kwa kweli. *Photocopy machine* thamani yake sio kubwa kwamba askari apate tabu kwenda kutoa yeye hiyo *photocopy.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, hoja zako ni za msingi sana. Kwa kweli kulikuwa na umuhimu wa kuweza dakika kumikumi leo, lakini bahati mbaya sana, *insha Allah* mwakani tutakumbuka jambo hili.

Mheshimiwa Nicholaus Ngassa atafuatiwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Assa Makanika.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba muhimu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kabla ya kuchangia naomba ku-*declare interest* mimi kabla ya kuwa Mbunge nilikuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa miaka kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefanya kazi na Mheshimiwa Simbachawene, nimefanya kazi na Mheshimiwa Mwigulu na Mheshimiwa Masauni. Kwa hiyo, baadhi ya *development* ambazo nitazichangia hapa ni jitihada ambazo zimeanza siku nyingi naamini wataendelea kuzifanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa nitachangia maeneo matatu kutokana na muda. Eneo la kwanza, nitachangia kuhusu makazi na nyumba za askari; eneo la pili, nitachangia kuhusu Jeshi la Polisi na Jeshi la Zima Moto na Uokoaji; na eneo la tatu, kwa mapana nitachangia kuhusu vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa katika upande wa makazi na nyumba za askari, Wabunge wengi wamechangia hiyo *concern* kuhusu kuboresha nyumba za makazi. Kwa kweli kwa mfano mimi kwenye jimbo langu la Igunga, tuna nyumba zimejengwa mwaka 1993 mimi nilikuwa darasa la kwanza, mpaka leo hazijawahi kufanyiwa maboresho. Kwa hiyo kama Wizara ijaribu kuangalia kuja na *package* ambayo itasaidia kuanza kuboresha nyumba za askari.

Mheshimiwa Spika, katika hilo nina wazo ambalo naweza kulitoa. Kwa mfano tunaangalia tunapopata fedha ya barabara tunapotoa kwenye mafuta, sasa kuna faini na tozo mbalimbali ambazo zinatoka kwenye taasisi za Wizara ya Mambo ya Ndani, inaweza Wizara ikajenga hoja Serikalini na ikaja hapa ikipitishwa na tukakubaliana, katika tozo na faini mbalimbali angalau kila asilimia kumi basi ikaingizwa kwenye Mfuko Maalum kwa ajili ya kuboresha nyumba za makazi ya askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakapotoka hii fedha itakuwa na Mfuko Maalum halafu itaenda kufanya kazi kwa

mfumo wa *force account* kupitia hata Jeshi la Magereza kwa maana itatusaidia sana kuboresha nyumba za askari na kujenga nyumba mpya.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni kwenye suala la Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, kama alivyosema Waziri wamepanga kununua magari mawili lazima pia wawe na wilaya za kimkakati. Kwa mfano Wilaya yetu ya Igunga, pale bomba la mafuta kutoka Uganda linapita na litakuwa na kituo kikubwa cha koki, sasa wilaya ina ofisi ya zima moto lakini haina gari la zimamoto. Kwa hiyo tunaomba Waziri maeneo kama haya ambayo ni ya kimkakati kwa sababu lile bomba ni kubwa, ni la gharama kubwa, ikitokea *eruption* ya moto bila kuwepo na gari pale tutatafutana na tutauwa wananchi wengi. Kwa hiyo maeneo kama haya, yawe ya kimkakati kwa Wizara ili waweze kuyapa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, suala lingine katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni suala la motisha kwa wafanyakazi. Wale wafanyakzi wanafanya kazi wakati mwingine katika mazingira magumu ya kuokoa watu kwenye moto, kwenye majanga, kwenye maji. Sasa unashangaa, inabidi Wizara waweke mfumo mzuri pia wa motisha itakayowasaidia hawa watumishi wa jeshi la zimamoto wote kwa ujumla. Tusiwe tunasubiri kwamba mtu amefanya *wonderfully deeds,* kaokoa mtoto au kafanya nini, ikishaanza kusambaa kwenye ma-*group* ya *WhatsApp* ndio anatafutwa awe *awarded.* Kwa hiyo naomba tubadilishe huo mfumo hili tuweze kuwapa motisha askari wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo napenda kulichangia kwa upana kidogo ni suala la vitambulisho vya Taifa. Kwa kweli wakati *design* ya *National ID* inafanyika, *NIDA* imeanzishwa mwaka 2008, moja ya jambo kubwa ambalo lilikuwa ni lengo lake, ukiacha la kiusalama, ni kuhakikisha inatusaidia kutambua walipa kodi wa nchi hii, *taxpayer identification.* Kwa kipindi kile walipa kodi walikuwa milioni mbili lakini walikuwa wanatakiwa kuwa milioni 14, sasa kama Wizara ifanye tathmini hili limetusaidia vipi katika kuongeza walipa kodi mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kuzalisha vitambulisho, lazima itoke kwenye hili suala la namba, twende tukazalishe ili watu wengi waweze kutambulika. Sasa hivi katika moja ya vitu ambavyo inakwenda ni *digital economy.* Watu wanalipa kwa kutumia kadi, hizi kazi za vitambulisho vya Taifa, hata katika *design* yake ni kwamba baadaye tunasema tutumie kama *e- wallet* ambayo maana yake ni kwamba, malipo haya yanayofanyika katika huduma mbalimbali, mtu anaenda na kitambulisho cha Taifa na ile namba yake ya utambulisho, analipa anatoa kadi inachanga malipo yanafanyika. Tukifikia hivyo, Serikali itapata kodi lakini tutakuwa tumebadilisha pia mfumo wa kutembea na pochi kubwa hiizi mifukoni zenye hela nyingi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kumshauri Waziri na Wizara wasaidie, *NIDA* wakati inafanyiwa *design* na sasa hivi ilipo, nyaraka nyingi zimekuwa za kipindi kile *NIDA* bado ina watumishi zaidi ya 100. Sasa hivi *NIDA* ina-*oparate* nchi nzima, ina ofisi nchi nzima na ndio maana ugumu unakuja kufanya kazi, mtumishi wa *NIDA* aliyepo Kongwa akihitaji kununua kalamu, lazima awasilisane na Makao Makuu Dar es Salaam, ni ngumu sana kufanya kazi na kutoa matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba wabadilishe, kwenye majeshi mengine yaliyoko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, wanaona namna tunavyo-*oparate* kupitia Makamanda wa Mikoa, sasa na *NIDA* tubadilishe ili mamlaka katika wale Maafisa wa *NIDA* wa Mikoa wawepe nguvu ya kuweza kusimamia maafisa walioko katika maeneo yao. Sio mtumishi anahitaji pini ya kubana fomu ya usajili, anatakiwa aombe Dar es Salaam ndio ipelekwe kule Wilayani. Hilo waliangalie sana.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni la muhimu, naomba Mheshimiwa Waziri akalifanyie kazi kulikuwa na mikataba miwili, naomba waiangalie vizuri, ambayo baadaye itawasadia. Kulikuwa na mkataba wa ujenzi wa ofisi za *NIDA* nchi nzima, walijenga awamu ya kwanza,

wanatakiwa kwenda awamu ya pili wakaangalie wamefikia wapi. Mkataba mwingine wa muhimu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, Mbunge wa Igunga, mengine muandikie Mheshimiwa Waziri, itatusaidia.

Mheshimiwa Assa Makanika atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia Wizara hii muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuchangia sehemu moja katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani, suala la uraia. Wizara hii ni Wizara muhimu sana katika ujenzi wa uchumi wa nchi yetu, na ni Wizara ambayo hakika ikilegalega kidogo tu inaweza ikatikisa misingi ya uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina-*deal* na mambo ya *home affairs.* Na ukiweza kuangalia raia yeyote yule katika nchi yoyote ili, ili aweze kujenga uchumi wa nchi hiyo, lazima aji-*feel proud* ya nchi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, tarehe 26, vyombo vya ulinzi na usalama viliendesha operesheni moja pale maeneo ya Mabwepande. Katika operesheni ile kweli inawezekana kukawa kuna moja wapo ya watu ambao ni wahalifu na watu ambao siyo raia wa nchi yetu ambao wanaweza kuwa waliingia katika nchi yetu kimakosa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika operesheni ile namna ilivyoendeshwa, hususan kwa watu wetu wa Kigoma, kwa kweli haikuwa inatuonesha *pride* kusikia kama na sisi ni sehemu ya nchi hii. Kulikuwa kuna maswali mengi ambayo yalikuwa yakiulizwa, nikiwa mmoja wapo wa mashuhuda. Wananchi wa Mkoa wa Kigoma kutoka sehemu mbalimbali walinipigia simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifika pale Dar es Salaam, Oysterbay, nilivyofika pale moja wapo ya maswali yaliyokuwa yakiulizwa yalikuwa yanatwezwa na kuonesha kwamba watu fulani wana haki kamili ya kuwa raia wa nchi hii na wengine ni Daraja B. Jambo ambalo siyo jema katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana – Mheshimiwa Waziri nilikupigia simu na tukazungumza sana, asilimia 80 ya watu waliokamatwa katika operesheni ile walikuwa ni watu wa Kigoma, na sana maswali waliyokuwa wakiulizwa wanatwezwa utu wao, maana utaambiwa sema namba nne, sema namba tano, kana kwamba ni vitu ambavyo mtu anaji-*feel inferior* sana.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yangu, niiombe Serikali Sikivu iweze kuangalia historia ya ujirani mwema na nchi hizi husika haiwezi ikaondoa uraia wa watu wa Kigoma. Sisi tumekuwa ni majirani na nchi hizo. Ni vyema zaidi Serikali iangalie *approach* nyingine ya kuweza kutu-*treat* sisi watu wa Kigoma ili tuji-*feel* tuna hatimiliki ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe kitu kimoja, kwa kupitisha tu kidogo katika historia ambayo tunayo na muunganiko wa nchi jirani; sisi tuna historia ambayo inatusema kana kwamba tumekuwa hata katika historia ya kiuongozi. Ukiangalia mwaka 1888 Mjerumani amekuja kutawala hapa kwetu, sisi Kigoma ilikuwa ndiyo makao makuu yake akitawala Rwanda na Burundi, lakini makao makuu ikiwa ni Kigoma. Sasa ukisema historia ituhukumu sisi mtakuwa mnatuonea. Hayo ni masuala ya Mwenyezi Mungu, niombe na sisi tuweze kumiliki haki sawa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tuna historia ambayo haiwezi kufutika, mfano vijiji vyetu vingi vinafanana. Ukiangalia pale kwetu Kigoma tuna Kijiji kinaitwa Kalinzi, lakini ukienda hata Ngara kuna Kijiji kinaitwa Inkarinzi; ukienda hata Burundi, kuna Kijiji pia kinaitwa Karinzi. Hiyo inaonesha ni namna gani historia yetu inavyofanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hapohapo kwetu Kigoma, mojawapo tuna Vijiji vinaitwa Mnanira, hata ukienda Burundi pia kipo Kijiji cha Mnanira; ukienda Rwanda kipo Kijiji cha Mnanira. Sasa historia hii isije ikawa ni mhukumu kwetu. Hivyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia hii Idara ya Uhamiaji iweze kuangalia namna ya kutu-*treat* sisi watu wa Kigoma ili na sisi tuji-*feel* kwamba ni sehemu ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nitoe ushauri mdogo sana; ukija ukaangalia suala hili la uraia linaua sana na kudororesha hali ya uchumi katika Mkoa wetu wa Kigoma. Nilikuwa nikiongea na Rafiki yangu mmoja, yeye ni mtu wa Ubelgiji, na nimesoma naye, lakini akawa anashangaa sana, anasema Ubelgiji imejengwa na mali inayotoka katika nchi Jirani ya watu wa Kigoma, Nchi ya Kongo, lakini sisi hiyo mali inapita katika anga la watu wa Kigoma, lakini kulingana na changamoto ya uraia katika Mkoa wetu wa Kigoma...

**SPIKA:** Mheshimiwa Makanika, kengele imeshalia.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, lakini niseme tu ya kwamba Serikali iangalie suala hilo kwa umakini, nitaweka mchango wangu kwa njia ya maandishi kumalizia hili. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Kuna baadhi ya maeneo umetuacha kidogo hatukupata sana, lakini siku zijazo labda tutakuelewa vizuri zaidi. Kwamba mtu akiambiwa aseme nne ametwezwa kivipi? Lakini baadaye labda, nafikiri atasema ine, ahaa. Ni *methodology* tu za watu wa Uhamiaji, unajua tena, sasa hapo kasema Mheshimiwa Makanika, angeongea Mheshimiwa Semuguruka hapa, *Masha Allah,* ingekuwa hatari; malalamiko yao yanafanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kwa namna ya pekee, kwa vile nimesimama kwa mara ya kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia nimpongeze kwa hotuba anazoendelea kuzitoa tokea kuapishwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa namna ya pekee nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ya juzi, Mei Mosi, kwa kuongeza umri wa wategemezi kutoka miaka 18 hadi miaka 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiendelea, nataka nizungumzie kuhusu suala la upungufu wa askari. Moja kwa moja nataka nijielekeze katika Mkoa wetu wa Kaskazini Pemba. Tunafahamu kwamba askari wanafanya kazi kubwa sana na wanatusaidia kwa njia moja au nyingine katika kulinda raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, katika mkoa wetu, askari ni wachache na uchache huo umetokana na kwamba wengi wamestaafu, wengine wamepandishwa vyeo, wengine wamefariki na wengine wamepata uhamisho kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine, na hata nje ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa askari hawa, kutokana na umuhimu wa mahitaji tuliyonayo ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba, ingawaje wengi wamechangia katika maeneo au kwa nchi nzima kwamba askari ni wachache, lakini kwasababu nimejielekeza Mkoa wa Kaskazini Pemba, niseme tu kwamba tunaomba tuongezewe askari katika maeneo yetu kwa sababu askari ni wachache.

Mheshimiwa Spika, suala la nyumba za watumishi; naipongeza sana Serikali kwa kuongeza bajeti ya kuendelea kujenga nyumba za watumishi. Ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba, yapo majengo ambayo Serikali kupitia Wizara hii imeendelea kujenga lakini bado askari wetu wana upungufu wa makazi; askari wetu wengi wanakaa uraiani. Niiombe sana Serikali kuongeza bajeti au kuweka uharaka katika kuendelea kujenga majengo haya ili askari wetu waendelee kuondokana na changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la *OC; OC* bado ni ndogo, lakini hata hiyo inayotengwa bado haiwafikii walengwa. Niiombe sana Serikali kwa vile kupitia Wizara ya Afya pamoja na Elimu, fedha zinaelekezwa moja kwa moja kwenye vituo, basi niiombe sana Serikali fedha hizi za *OC* ziende moja kwa moja kwenye vituo husika ili kuondosha changamoto kwa sababu madeni yamekuwa ni mengi.

Mheshimiwa Spika, wana madeni mengi ya mafuta, hawawezi kutekeleza majukumu yao kutokana na uchache wa mafuta, uchache wa vifaa. Kama *OC* itakwenda moja kwa moja na itakwenda kwa wakati, basi wataweza kulipia madeni yao kwa wakati, lakini pia wataweza kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kuhusiana na suala la fedha ambazo zilikuwa zinatengwa kwa ajili ya kuwahudumia askari hawa, zile shilingi laki tatu kwa miezi mitatu, na hii ni kutokana na uanzishwaji wa maduka ya *duty free.* Askari hawa walikuwa wanapatiwa huduma katika maduka haya kuweza kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi Serikali imesitisha lakini kutokana na hilo Serikali ikawa imetenga kila mwezi angalau askari hawa waweze kupewa laki moja kwa ajili ya kujihudumia kiuchumi. Pamoja na hilo, fedha hizi zikawa zinatengwa shilingi laki tatu kwa miezi mitatu, yaani ili kufidia kwamba hatuwezi kuwapelekea kila mwezi lakini tuwe tunawapelekea kwa miezi mitatu; hata hilo pia limekuwa na changamoto. Muda mrefu hawakuwa wakipokea fedha hizi,

naomba sana Serikali askari hawa tunajua kazi wanazozifanya, hizi lakini tatu ziweze kuwafikia kwa haraka ili waweze kutekeleza majukumu yao.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru.

**SPIKA:** Nashukuru sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, na Mheshimiwa Omar Ali Omar ajiandae.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ukiukwaji mkubwa sana wa haki za binadamu ambao umekuwa ukifanywa na Jeshi la Polisi na ukiukwaji huu umefanyika hasa pale Polisi wanapokuwa wakiwakamata watuhumiwa, wamekuwa wakikiuka hizi haki ikiwa na pamoja na kuwafanyia vitu vya hovyo ambavyo pia vinakiuka kabisa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Haki za Binadamu iliyotolewa Aprili, 2021, imesema wazi kabisa, ripoti hiyo ilikuwa ni ya mwaka 2019/2020, imesema wazi kabisa kwamba matukio manne ya mauaji ya raia yamefanyika mikononi mwa polisi. Na matukio haya yalifanyika tu kutokana na polisi kuwakamata watuhumiwa kwa kutumia nguvu kubwa sana ambayo ilisababisha pia watuhumiwa kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, Ibara ya 13(6)(b), nitainukuu, inasema wazi kabisa kwamba; *"Ni marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo;"(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini haya mambo tumekuwa tukiyashuhudia wazi kabisa, raia wetu wakitendewa mambo ya ajabu, kana kwamba wameshakutwa na makosa wakati huo bado Mahakama inakuwa haijathibitisha makosa yao, jambo ambalo linakiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, sheria hiyohiyo Ibara ya 13(6)(e), inasema; ***"****Ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili tumeliona likifanywa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, lakini mbali na hayo, tunajua wazi kabisa, wakati mwingine watuhumiwa wanapokamatwa na kupelekwa katika vituo vya polisi kule hakuna bajeti ya chakula, lakini watu wamekuwa wakikamatwa, wakijazwa katika vituo vya polisi na sheria inasema mtu akikamatwa anatakiwa akae kwenye kituo cha polisi saa zisizozidi 48. Lakini watu wanakaa mpaka wiki mbili wako mikononi mwa polisi, jambo ambalo limekuwa likikiuka kabisa sheria za…

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa; mwenye taarifa aendelee.

**T A A R I F A**

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hata matendo ya kikatili kwa watoto wa kike na wanawake yanafanyika katika vituo vyetu vya polisi, wanavyokamatwa watu wanafanyiwa mpaka ubakaji kwenye vituo vyetu vya polisi.

Mheshimiwa Spika, nampa taarifa hiyo kwasababu vipo na kama utakuwa unatakiwa uthibitisho watu waende wakaulize mahabusu ambao wamekaa zaidi ya mwezi vituo vya polisi na wakapelekwa magerezani.

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea taarifa hiyo kwasababu hata mwaka jana, mwezi Agosti nilipokamatwa na Jeshi la Polisi, nilitishiwa kumwagiwa tindikali usoni. Kwa hiyo hivyo ni vitendo ambavyo vinafanywa na Jeshi la Polisi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella, yaani kidogo nishtuke kwamba na wewe ilikuwa... endelea kuchangia Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, suala la wananchi wetu kukosa dhamana; leo hii suala la dhamana limekuwa kama tu ni zawadi ya polisi. Wananchi wamekuwa wakikosa dhamana kwa makosa ambayo yanadhaminika kisheria. Na jambo hili limesababisha magereza mengi kujaa sana. Jambo hili la wananchi wetu kunyimwa dhamana limesababisha wananchi wetu kujaa sana huko magereza bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo, kumekuwa na matukio mengi sana ambayo yanasababisha kunyima uhuru wa watu wetu, ikiwa ni pamoja na watu kukaa muda mrefu gerezani, mtu anakaa mpaka miaka kumi, mitano, mitatu, kesi yake bado haijasikilizwa. Akiuliza anaambiwa upelelezi bado haujakamilika. Lakini mwisho wa siku huyu mtu inakuja kutolewa hukumu hajakutwa na hatia, amekaa gerezani miaka kumi, hiki tunawanyima wananchi wetu haki zao za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali iweze kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Makosa ya Jinai, tufanye marekebisho ya sheria hizo ili kuwapa uhuru wananchi wetu. Kwasababu mwisho wa siku tunayajaza tu magereza bila kuwa na masuala ya msingi kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa; ndani ya magereza kumekuwa na mambo mengi sana ambayo wengine wameyazungumzia lakini ntayazumgumzia hapa.

Pamoja na changamoto ambayo ameizungumzia dada yangu, Mheshimiwa Esther, magerezani kiukweli kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, leo hii magereza wanachanganywa na watoto wa miaka 13, 14 hadi 15. Mwanamke wa miaka 60 anakaguliwa mbele ya mtoto wa miaka 14; hili jambo kiukweli linahuzunisha sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Stella, muda hauko upande wetu.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Omar Ali Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa fursa hii ya kuchangia katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na *cabinet* yake kwa kutuletea Bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba katika askari ambao wanastahili kupongezwa ni Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi linafanya kazi kubwa sana nchini kwetu. Lakini Jeshi la Polisi linafanya kazi katika mazingira magumu mno. Jeshi la Polisi toka mwaka wa 2015 hawajapata nyongeza ya mishahara; Jeshi la Polisi halijapata *increment;* halijapata kupandishwa vyeo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa *IGP* na Waziri wa Mambo ya Ndani, hongera sana; huyo ni Mbunge wa ACT – Wazalendo.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, lakini kwa kweli kwa masikitiko makubwa, tena makubwa mno, ukienda hata majengo wanayokaa askari polisi ni majengo ambayo

hayastahiki. Kwa mfano Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambapo natoka mimi, Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba hata nyumba ya kukaa hana. Mpaka sasa hivi tunavyoongea hana nyumba ya kukaa kwasababu ya kwamba nyumba ile imekuwa mbovu kabisa, hawezi kuishi. Kwa hiyo, hii ni kuonesha kwamba Jeshi la Polisi hatujalipa kipaumbele katika utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna nyumba za maafisa ambazo zimejengwa kule Finya, Mkoa wa kaskazini Pemba, mpaka sasa hivi nyumba zile hazijamalizwa. Hata Naibu Waziri aliwahi kufika katika eneo lile na akaona majengo yale hali halisi yalivyo na akashindwa kushughulikia lile suala mpaka leo hii. Kwa hiyo, tunataka sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie, je, nyumba ile itamalizwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukitoka maeneo hayo, Ofisi ya Polisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba haikaliki, inavuja kama pakacha. Kwa kweli inasikitisha sana, kuna vyumba ambavyo ndani ya ofisi ile hawafanyi kazi tena askari polisi kwasababu vimekuwa vichakavu na kwasababu ofisi inavuja sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenyewe binafsi tarehe 1 Machi nilifika katika Ofisi ya Makao Makuu ya Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba na kujionea kwa macho yangu kwamba lile eneo liko katika hali ya hatari. Jengo liko hatarini, toka mwaka wa 1970 mpaka kaja kalifungua Mheshimiwa Hayati Moringe Sokoine mwaka 1979, jengo lile mpaka leo halijafanyiwa ukarabati wa aina yoyote. Hii ni kuonesha kwamba askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kwa hiyo, hilo tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama wanavyosema Waswahili, kidonda kikioza sana basi hata nzi hakitaki. Hii ni kuonesha kwamba hata lile jengo lenyewe la polisi, Kamanda wa Polisi hana hata pa kuishi, kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika eneo lingine la askari polisi; Kisiwa cha Pemba kina bandari bubu 16. Kutokana na muda sitaweza kuzitaja, lakini Pemba ina bandari bubu 16. Kwa hiyo, hizi bandari bubu ndiyo bandari ambazo zinatuhatarishia amani katika Kisiwa cha Zanzibar. Kwasababu kama tunavyojua kwamba mipaka yetu inahitaji kulindwa na askari polisi ni moja katika jamii ambao wanastahiki kulinda mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu hayo makubwa lakini askari polisi hawana vitendea kazi. Mkoa mzima wa Kaskazini Pemba una gari moja tu la Kamanda wa Polisi, magari yote yamelala, kwa sababu ya ukosefu wa vipuri, mafuta na upungufu pia wa askari. Kwa taarifa tu Mheshimiwa Maida alinifilisi kidogo lakini napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Kaskazini pekee una mahitaji ya askari 150 na hii ni kutonana na kwamba kumetokea mambo mengi; askari wameumwa, wengine wamestaafu na wengine wamefukuzwa kazi.

Kwa hiyo, kutokana na hali hiyo ya ukosefu wa askari, bandari hizi bubu ndizo ambazo zinatumika katika kuingiza uharamia wa kila aina ikiwemo madawa ya kulevya. Kule Zanzibar mahakama zetu zina kesi nyingi ambazo zinahusiana na madawa ya kulevya. Hii ni kuonesha kwamba maeneo ambayo yanatumika kupitisha madawa ya kulevya ni bandari bubu na idadi ndogo ya askari ambao tunao katika vituo vya polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha sana Kamanda ana dhamana ya kuwalisha mahabusu badala ya dhamana ile kuwa ya Serikali. Kwa kweli wanapata misaada kutoka kwa wasamaria wema, wenyewe wanawaita wafanyabiashara werevu wanaojua athari...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Omar Ali Omar, dakika tano ni chache, lakini nakushukuru sana.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, lakini mngetuongeza tuko wachache. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Omar Ali Omar. Mnaona jinsi ambavyo ni Mbunge wa ACT-Wazalendo lakini anachangia *very very objectively*, matatizo halisi ya askari wetu na jinsi wanavyofanya kazi katika mazingira magumu. Ahsante sana Mheshimiwa unatuonyesha jinsi ya kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Tunaendelea na nilishamtaja Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo na Mheshimiwa Dkt. Kiruswa ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi na mimi niungane na wenzangu kupongeza Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na vyombo vyake kwa ulinzi mzuri wa nchi yetu. Tunajua tunajivunia tunu za Taifa na mahsusi kwenye upande wa amani tunajua Wizara ya Mambo ya Ndani pamoja na vyombo vyake wanachangia sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo kuna mambo kadhaa ambayo yanahitaji kuboreshwa ndani ya Wizara yetu hiyo ili ustawi wa wananchi uweze kuwepo katika sehemu mbalimbali za nchi yetu. Najua ni bahati kwa nchi au mkoa kuwa na ujirani na nchi zingine. Kwa mfano, Mkoa wa Kagera tunapakana na nchi tano; Uganda, Rwanda, Burundi, DRC na Sudan Kusini. Hata hivyo, wananchi wa Mkoa wa Kagera wamekuwa ni wahanga na hasa katika kutambuliwa na kupewa Vitambulisho vyao vya Taifa ili waweze kupata huduma zingine ambazo wanastahili kupewa kwa mfano kusajili simu zao. Pia tumeona Wizara ya Kilimo imekuja na utaratibu wa kusajili wananchi kulipwa fedha zao kupitia simu zao, huduma hizo wamekuwa wakizikosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Wilaya ya Misenyi, Kyerwa, Karagwe, Ngara wote tumekuwa wahanga wa kukosa vitambulisho na wananchi wanaishi kwa tabu kama vile hawapo ndani ya nchi yao. Suala hili limesababisha Mkoa

wa Kagera ukadorora katika maendeleo. Mtu hawezi kufanya kitu kizuri, hawezi kulima shamba zuri, hawezi kujenga nyumba nzuri kwa sababu kesho ataambiwa wewe siyo raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijikite sana kwenye Wilaya ya Misenyi ambapo ndiyo jimbo langu. Kuna familia baba ameambiwa siyo raia, mama ni raia, mtoto wa kwanza ni raia, wa pili siyo raia. Sasa mpaka tunaleta mtafaruku katika familia, watu wanaenda kutafuta hata vinasaba maana baba anamuuliza mama huyu sasa ambaye siyo raia ni wa nani?

Mheshimiwa Spika, kwa Wilaya yetu ya Misenyi ukitaka kumpima mwananchi kwa kuongea Kiswahili au kuimba Wimbo wa Taifa sisi wote siyo raia. Hii ni kwa sababu mimi naongea Kihaya, Mnyankole akiongea Kinyankole tunaelewana bila shida. Sasa unaponipima kwa kusema kwamba niongee Kiswahili au niimbe Wimbo wa Taifa, hatuwatendei haki. Sisi wote ni mashahidi tukipangana kwenye mstari kila mmoja umpime anaimba Wimbo wa Taifa mpaka mwisho kuna wengine watateleza katikati, sasa hicho ndiyo kipimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote ni mashuhuda Wilaya ya Misenyi umekuwa ni uwanja wa vita ya Uganda na Tanzania. Sisi ndiyo tulikuwa wahanga, mwingiliano wa kabila mbalimbali kutoka Uganda umekuwepo na tukaishi kama jamii moja. Sasa leo kigezo cha Wizara cha kusema kwamba imba Wimbo wa Taifa, ongea Kiswahili, watu wanaongea Kinyankole, Kihaya, tunaongea Kiganda vizuri kabisa na wao wanaongea hivyo hivyo. Kwa kweli suala la vitambulisho katika Wilaya ya Misenyi kwa kweli limekuwa ni janga la kitaifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wameanza kujitahidi wanapata namba, hivi kinachoshindikana ku-*print* kale kakadi ni nini? Tumekuwa kwenye halmashauri kule tuna-*print* kadi za wazee za bima za afya kuna mashine Sh.25,000, una-*print* vile vitambulisho unampa mtu anaendelea na

maisha yake. Ile namba ukishaingiza kwenye *computer* kule kwako unakotaka itasoma, lakini hata kitambulisho kile ambacho unaweza ku-*print* kwa Sh.200, kwenye Wizara yetu imeshindikana, shida ni nini?

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu wamepata shida sana kuhusiana na jambo hili. Cha ajabu wakati wa uchanguzi wote ni raia lakini ikija kwenye kuwatambua kama Watanzania siyo raia. Mimi wamenituma, kupitia Kiti chako watuambie kama sisi siyo raia tupelekwe kwenye nchi ambayo tunastahili twende kuishi huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini Watanzania ndiyo wanatakiwa kufaidi maziwa na asali ndani ya nchi yetu. Sasa kumwambia Mtanzania halisi kwamba hajaongea Kiswahili, Kiganda, Kihaya hicho siyo kipimo. Waende waangalie maana zile kaya zipo. Ukienda kule kwetu Bukoba sisi tunapojenga boma ni kama uwanja wote huu wa ofizi za Bunge, ni mtu ana mji wake na migomba yake imemzunguka, ukivuka hapo unaenda mji mwingine tunahesabika kirahisi, mtu yupo tangia mwaka 1920 leo uamwambia siyo raia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri wanayofanya Wizara ya Mambo ya Ndani kwenye eneo hilo bado hawajafanya vizuri. Hii inasababisha wakati mwingine majeshi yao wanaitumia kama *loophole* kwamba nikuite raia au siyo raia, unasemaje? Kwa hiyo, niombe sana Wizara ya Mambo ya Ndani ilichukulie kwa uzito suala hili ili wananchi waweze kuwa na raha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo. Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, tafadhali, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye

hii hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nianze kwa kumpongeza Waziri na timu yake yote, Naibu Waziri na Watendaji katika Wizara hii kwa kazi nzuri na muhimu wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni nyeti na ukiangalia maslahi ya watenda kazi katika Wizara hii yanasikitisha na kutia huruma. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Longido sisi ni wilaya ambayo karibu ina miaka 25 sasa tangu ianzishwe lakini hakuna Kituo cha Polisi cha Wilaya, kuna kituo kidogo kilichojengwa tangu enzi ya ukoloni na nyumba za maaskari pale ukiziangilia zinatia huruma. Naomba katika bajeti hii Waziri hebu aangalie kule Longido atatusaidiaje.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukienda Kwamwanga kuna Kituo cha Polisi ambacho zamani kilikuwa barabarani, barabara ya lami ikafika pale kutoka Rombo, wananchi wakajiongeza wakajenga kituo kingine pembezoni, imebakia *finishing* tu. Waziri aliyepita nilishamuomba angetuchangia tu kama milioni 20 tunafanya *finishing* nzuri.

Mheshimiwa Spika, pia maaskari pale wanalala nje, ukiona nyumba wanazolala zinatia huruma. Naomba sana pia katika bajeti hii hebu muangalie hali ya usalama katika Wilaya ya Longido inayopakana na nchi ya jirani yenye kilometa zaidi ya 350.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tulishahamisha wananchi kwa sababu alisema kwenye hotuba yake kwamba na sisi tunaweza tukachangia ili tupate vituo vingine zaidi vya polisi, tumefanya hivyo. Kule Mndala tumeanzisha kituo, Serikali haiweki hata mkono. Tarafa ya Kitumbene yenye vijiji zaidi ya 19 tulishapendekeza tuwe na kituo lakini hamna juhudi yoyote ya Serikali katika kuhakikisha kwamba tuna vituo hivyo vya polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili la miundombinu ya polisi kuwafanya wafanye kazi katika mazingira rafiki na makazi yao lizingatiwe sana nchi nzima lakini katika Wilaya

yangu ya Longido basi nilisemee maana ndiyo nyumbani kwamba kwa kweli hali ni mbaya, hata ya magari ni mbaya. Kila wakati mimi kama Mbunge ndiyo nachangia tairi, matengenezo ya gari na unakuta kuna magari mengine yamekaa juu ya mawe kwa sababu hamna bajeti inayotolewa kutoka Wizarani kusaidia uendeshaji wa operesheni za polisi katika wilaya yangu. Hata Zimamoto lakini ni jina tu, hawana hata gari ya kukimbia kwenye matukio yakitokea kwenda kushuhudia licha ya gari ya kuzima moto unapotokea mahali popote. Naomba haya masuala yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu dakika ni chache naomba nijielekeze kwenye suala la wafungwa na mahabusu. Tunashida kubwa sana na sijui Wizara ya Mambo ya Ndani itatusaidiaje. Kuna kikosi kinachodhibiti ujangili wa nyara za Serikali kinachofanya kazi katika wilaya hizi zenye wanyamapori, kuna vitendo viovu vinafanyika. Naomba tu nimjulishe Waziri na ajue namna ya kufanya kwa sababu ndiyo wanaolinda mali na raia wa nchi yetu kwamba watuhumiwa wanapokamatwa kuna mazingira ya rushwa na kuna mahabusu wanaokaa magerezani mpaka miaka mitano hawahukumiwi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano, kuna mtu anaitwa Taraiya Paulo alikamatwa kwa sababu tu kwenye simu yake alikutwa amefanya mawaliano na mtu ambaye anafanya biashara ya ujangili lakini alikuwa anamfuata kwa deni lake la mbuzi aliyomuuzia. Akakaa mahabusu miaka mitatu, ametoka juzi tu ndiyo anaeleza kwamba yeye alikamatwa kwa sababu simu yake imekutwa na mawasiliano ya mtuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna mwingine anaitwa Luka Olokwen, yeye alikamatwa na mguu wa swala ambaye ameliwa na chui akabakiza, kwa sababu sisi jamii ya kifugaji hatuli nyama pori akabeba ule mguu ampelekee mbwa wake nyumbani, akakamatwa akaambiwa usipotoa milioni tano hatukuachii. Familia ikauza tena walewale ng'ombe aliokuwa anachunga akalipiwa milioni tano baada ya

mwaka mmoja amekuja amechukuliwa juzi amefungwa miaka 20, kwa sababu tu alikutwa na mguu wa swala aliyeliwa na mnyama pori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mwingine anaitwa Daniel Saitot, yeye alikamatwa tangu tarehe 1/9/2018. Kesi yake haijasikilizwa mpaka leo, alikutwa sijui ana ngozi ya chui. Hiyo ni kusema kwamba hebu Wizara hii ya Mambo ya Ndani iangalie mazingira ya kusaidia raia wa Tanzania wasio na hatia wanaopewa kesi mbalimbali za uhujumu uchumi. Sambamba na hilo, mimi naomba hizi kesi za uhujumu uchumi ziwekwe kwa *category,* ziwekwe ambazo zinadhaminika watu wadhaminiwe waendelee na kesi zao wakiwa majumbani ili kupunguza msongamano katika magereza yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kuna hili suala la uhamiaji, kipengele kinachotukera kidogo sisi watu wa mipakani ni ile hati ya kusafiria ya *Single Entry Permit*. Mtu ana shida kubwa labda anamuuguza mgonjwa yupo Nairobi anahitaji kwenda kila wiki anadaiwa akate hiyo *permit* kila wiki. Naomba *passport* za muda mrefu zitengenezwe na kuwa zinapatikana pale pale mpakani kuwaondolea raia wetu adha ya kulazimika kununua *passport* mpya ya muda wa dharura kila wakati wanapohitaji kusafiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kiruswa. Nilishakutaja Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mimi leo sitawapongeza, nitawaombea, namuombea Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri Mwenyezi Mungu awape nguvu na afya kwa kuwatetea wananchi wa Tanzania. Pia nichukue nafasi hii kumuombea Mheshimiwa Sirro na Kamishna wa Zanzibar kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kuwatetea wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, askari wetu wanafanya kazi ngumu sana, kwa kweli ni kazi ya kusikitisha. Asilimia kubwa ya Askari wa Jeshi la Polisi wanaostaafu ni nadra kuwakuta ni wazima. Askari wetu hawa wanafanya kazi ngumu wakistaafu wengi wana-*paralyze.* Hawa watu wanafanya kazi kubwa sana na ngumu na maeneo yao ya kazi siyo rafiki.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye vituo vya polisi Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza vipo kwenye hali ngumu lakini hata mazingira yao ya kazi wanapokuwa barabarani ni magumu. Wewe ni shuhuda leo ukiondoka kuanzia Dodoma kufika Dar es Salaam ni askari lakini jua, mvua wanapigwa askari wetu. Kazi yao ni ngumu sana, tutakaa tutawalaumu lakini askari wetu wanafanya kazi ngumu na kipato chao ni kigumu sana. Wapo askari siyo wazuri lakini kuna askari ni wazuri sana akiwemo Kamanda Sirro na Kamishna wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushahidi tosha ni wakati tunapofanya chaguzi. Askari wetu wanafanya kazi ngumu sana ya kudhalilishwa, kutukanwa, ni nusu kujuta kufanya kazi hii lakini hawana lingine la kufanya kwa sababu waliiomba kazi hii. Namuomba Mheshimiwa Waziri wawaone askari wetu kwa posho zao lakini na vitendea kazi. Sasa hivi unakwenda kwenye vituo kuripoti kesi ya ubakaji lakini unaambiwa hakuna gari wala hakuna askari kutoka pale kwenye kituo akamfuata mtuhumiwa, unaambiwa wewe kama unayo pesa utoe mafuta upeleke kule akachukuliwe mtuhumiwa. Mimi nahisi yote haya ni kwa sababu bajeti ni ndogo. Sababu ya vituo vyetu kuwa chakavu bajeti ni ndogo kwa sababu polisi si maskini wa wafanyakazi; wana wajenzi, watu wa umeme, nafikiri wana kila *design* ya mafundi, kwa nini wasipewe bajeti kubwa ya kufanya kazi zao wanakuwa ni watu wanyonge sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, turudi katika wale wanaostaafu, askari wetu wengi wanastaafu hawapati haki zao mapema. Unakuta askari kastaafu kama mwaka au miezi sita unamkuta ni omba omba. Haipendezi, inakera, inauma na wao ni

binadamu kama sisi na wao ni wafanyakazi kama sisi, lazima askari wetu watunzwe wana kazi ngumu kutulinda sisi na mali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bora aombe kuliko kuiba. Wengi tunasema askari wanapenda rushwa lakini mimi nasema wasiombe rushwa ila kuomba ni haki kwa sababu hawaibi. Wanaomba kwa sababu wapo kwenye hali ngumu lazima tuungane bajeti ya watu hawa iwe kubwa, ni haki yao. Mimi nasema pesa hizi angekuwa nazo Sirro angewapa askari wote wakaneemeka au angekuwa Kamishna wa Zanzibar anazo pesa hizi angewapa askari wake wote wakaneemeka kwa sababu hataki waombeombe wala waombe rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini leo unawakuta askari wapo kwenye ...

**T A A R I F A**

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**SPIKA:** Taarifa, endelea

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji anayeendelea kuchangia kwamba kuomba ama kutoa rushwa ni mwiko na ni kinyume kabisa cha sheria bila kujali mazingira uliyopo. Naomba Mheshimiwa mzungumzaji awatetee askari lakini asitee rushwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Pokea hiyo taarifa Mheshimiwa Mwanakhamis.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, sitetei rushwa, natetea askari wetu. Wengi tumezungumza hapa, wamesemwa wana vitendo vibaya, wanabaka, wanakera, wanaudhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri ni mwaka wa ishirini au na zaidi nipo kwenye siasa lakini sijawahi kukamatwa

kupelekwa kituo cha polisi wala sijapelekwa magereza. Suala la magereza mimi sijui najua utendaji wa kazi wa askari wetu, kwa sababu sote humu tunapogombea wanatulinda askari polisi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana muda umeisha.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona muda wetu hauwezi kutupeleka zaidi ya hapo, tutakaporudi jioni wale ambao nina majina yenu kwenye karatasi naamini wote mtapata nafasi. Cha muhimu ni kuwahi kurudi ataanza Mheshimiwa Rashid Abdalla Rashid, Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mheshimiwa Eng. Samweli Hhayuma, wote jioni mtapata nafasi ya kuchangia mjiandae tu.

Nawashukuru sana Waheshimiwa kwa jinsi ambavyo tunaendelea kuchangia kwa amani na utulivu, kwa kweli mmetoa hoja nyingi nzuri sana na tuendelee kufanya hivyo. Mimi nakumbuka babu yangu upande wa mama alipokuwa amekaribia kufika miaka mia akawa dakika zake za mwisho za kufariki zimefika akaniambia mawili matatu lakini kimoja nakikumbuka sana. Aliniambia mjukuu wangu naona mimi miaka yote hii nadhani Mungu anaweza kuniita wakati wowote lakini sijawahi kupelekwa kituo cha polisi. Sentesi hiyo tu ilikuwa ni moja ya urithi niliyopata. Sasa nikajiuliza kumbe kutokupelekwapelekwa kule ni jambo linaloonyesha uungwana wa hali ya juu lakini pia wakati mwingine si kwamba unaweza ukaenda kule kwa kutaka mwenyewe unaweza ukapelekwa lakini tujitahidi kufuata sheria bila shuruti.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana, nasitisha shughuli zetu hadi jioni ya leo saa 10.00.

*(Saa 07.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na kikao chetu jioni ya leo. Majadiliano yanaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na dakika tano tano zetu zile zile. Mheshimiwa Abdalla Rashid Abdalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Makame Mlenge. Mheshimiwa Abdalla.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia Wizara yetu hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Napenda sana kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao kwa ujumla kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kutengeneza bajeti hii na hadi kuikamilisha kuileta ndani ya Bunge letu hili Tukufu kwa ajili ya kujadiliwa. Lazima tuthamini nguvu zao, jitihada zao kwa sababu sote tunajua kwamba utayarishaji wa bajeti ya Wizara kama hii unahitaji umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika michango yangu katika Jeshi la Polisi na muda ukiruhusu nitaingia katika idara yetu ya Uhamiaji. Naomba Mheshimiwa Waziri akubali kwamba, Wizara hii kwa maana ya Jeshi la Polisi kwenye Wilaya ya Mkoani ilichukua zaidi ya miaka 20; lilikosa utetezi. Nasema kwamba jeshi hili lilikosa utetezi kwa sababu, majengo yote ya vituo vya Polisi pamoja na Makao

Makuu ya Wilaya, basi kimsingi majengo haya hayakubaliki kufanya kazi yakitumika kama ni majengo ya ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukianza na Kituo cha Polisi Kengeja hiki kimeoza kabisa na hakifai. Hata Kituo cha Polisi Mtambile nacho kadhalika, hakifai. Tukija kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Polisi Mkoani, hii ndiyo kabisa hayafai kabisa. Kwa sababu, majengo haya yalijengwa kabla ya uhuru. Ni majengo yaliyokuwa yakitumika na Masultani kwa kule Zanzibar. Sasa nilisema yamekosa utetezi kwa sababu majengo haya yalikosa watu wa kuwatetea kwa sababu majimbo hayakuwepo kwenye watu ambao ni makini kwa ajili ya kutetea Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi lilikuwa linaonekana kama ni maadui, kwa hiyo, hata makazi yao yalikuwa yanaonekana vile vile ni ya kiadui adui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mvua sasa zinaendelea kunyesha katika Wilaya ya Mkoani, tena ni mvua kubwa, ofisi hazikaliki, zinavuja. Hapa niliposema kwamba walikuwa na kazi kubwa ya kufanya bajeti ya Wizara, ni kwa sababu walikosa hadidurejea ya kuangalia kwamba bajeti iliyopita kulikuwa na makosa gani? Kulikuwa na mahitaji gani katika Wilaya ya Mkoani? Ndiyo maana hapa Mheshimiwa Waziri katuambia kwamba atajenga nyumba 14 katika Mkoa wa Kusini Pemba, lakini kama angekuwa na hadidurejea za bajeti iliyopita, nadhani angelielekeza kwenye ujenzi wa angalau ile ofisi ya Wilaya ya Mkoani badala ya nyumba 14 kwenye Mkoa wa Kusini Pemba.

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Waziri ni mtu mmoja mkakamavu, makini sana, kwa sababu katika Wizara ambayo alikuwepo aliwahi kufanya ziara ya kuja kukagua mambo mbalimbali ambapo naamini alipotoshwa, lakini alipokuja na akaupata ukweli, mambo yakaenda vizuri. Sasa hapa nayeeleza haya siyo kwa upotoshaji. Nayaeleza ili aandae ziara na nitaomba tuambatane pamoja twende katika Kituo cha Polisi Kengeja, Kituo cha Polisi Mtambile na Makao Makuu ya Wilaya ya Polisi Mkoani, tuone hali zao zilivyo, wanatia Imani. Hili wakati mwingine linasababisha hata ufanyaji kazi unakuwa ni wa kudorora dorora.

Mheshimiwa Spika, mwezi mmoja uliopita, Makamu wa Pili wa Rais alifanya ziara kwenye Wilaya ya Mkoani, akataka kujua kuna kesi ngapi ziko Mahakamani, ngapi ziko Polisi na ngapi ziko *DPP*, lakini jibu lililotoka pale ni kwamba kuna kesi 21 bado ziko Polisi zikiwa na miezi tisa zinasubiri ushahidi. Kuna ushahidi mwingine hauhitaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Abdalla Rashid Abdalla. *(Kicheko)*

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Haya. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ndiyo ubaya wa dakika tano. *(Kicheko)*

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Spika, nitamwasilishia kwa maandishi na ninaunga mkono hoja...

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** ...lakini ni lazima Mheshimiwa Naibu Waziri apange ziara kwenda kukagua Wilaya ya Mkoani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, shukrani. Mheshimiwa Haji Makame Mlenge nilishakutaja na Mheshimiwa Bidyanguze ajiandae.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nikiwa mmoja wa mchangiaji katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani. Kwanza, nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya afya na uzima. Namwomba Mwenyezi Mungu kwa wale ambao wana afya mgogoro, basi awaponyeshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende katika mchango wangu katika Wizara hii. Nianze tu na Polisi. Niseme tu kwamba, Polisi

ndio ambao wanatufanya tuendelee na vikao vyetu tukiwa huru na salama kutokana na kazi zao. Nawashukuru kwa hilo kwa sababu tumeondoka mitaani kwetu lakini bado hatujapata migogoro kutokana na kazi zao nzuri, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kutokana na umuhimu wao wa kazi, japokuwa na wenzangu wamesema sana suala la ajira, lakini naomba, ili waweze kufanya kazi vizuri, basi suala la ajira lisiachwe nyuma, liangaliwe kwa umakini na umahiri mkubwa. Kwa sababu ndilo ambalo litasababisha kuweza kufanya kazi zao vizuri. Sitakaa sana hapa kwa sababu watu wengi wamezungumza.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la usafiri. Suala la usafiri ni changamoto kubwa katika Jeshi la Polisi, pia tukizingatia kwamba hawa ndio ambao wanatufanya tuweze kukaa kufanya kazi kwa amani na usalama, lakini wanaposhindwa kupata usafiri wa kutosheleza, maana yake huenda tukaja tukawalaumu siku moja lakini watakuwa hawana tatizo la kulaumiwa.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, ndani ya Jimbo langu nina vituo viwili vya Polisi; nina Kituo cha Chwaka lakini pia nina Kituo cha Jozani. Vituo hivi viwili vyote vinafanya kazi, lakini vikiwa havina usafiri wa aina yoyote. Sijui wanapangaje kazi zao mpaka waweze kufanya kazi vizuri. Kituo cha Chwaka, eneo lake hili lina mahoteli yasiyopungua 18 kwa wale wa Shirika la Umeme, wanaita mahoteli makubwa ambapo wameweka katika ngazi ya kushughulikia maalum, lakini hawana usafiri. Sasa sijui, kazi hizo zinaweza zikafanywa vipi iwapo wataendelea kukosa usafiri? Ikiwa Serikali wanaelekeza sana nguvu zao na tunapiga kampeni kila siku kuona utalii unaongezeka, lakini hatuwapatii usafiri katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, la kushangaza zaidi; na nimsemee ndugu yangu Naibu Waziri, kwa sababu hana nafasi nzuri ya kusema maana yeye ni mtetezi wa Serikali ndani ya Jimbo lake. Kile kituo hakina usafiri na kinapokea kesi nyingi sana.

Kwa hiyo, suala la usafiri ni jambo muhimu sana ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo suala la maslahi. Suala la maslahi nalo lina changamoto. Niiguse suala la maslahi ya wastaafu, kwa sababu wenzangu wamesema, sitaki niende sana hapa ili muda wangu usije ukamalizika, lakini nazungumza zaidi kuhusiana na utaratibu mzuri wa Askari Polisi pale ambapo linatokezea tatizo la kufiwa na mfanyakazi, wanakuwa na utaratibu mzuri sana. Pengine unapotaka kuchukua maiti unaweza kuwajulisha wakakwambia hata, usimguse maiti, tunakuja wenyewe kumchukua na kumpeleka katika sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, hiyo ilinitokea mimi mwenyewe, pale marehemu ndugu yangu alipofariki. Wakati nawajulisha na nilikuwa nimeshatafuta usafiri, nikaambiwa kwamba wanakuja kumchukua wenyewe na ikabidi usafiri ule niutumie kwa mambo mengine na nisiutumie kwa kumpeleka marehemu. La kushangaza ni kwamba, anapofariki mtu, basi wanachukulia kwa umuhimu, wanamshughulikia, lakini kwanini wasishughulikie maslahi yao?

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwa jeshi la Polisi waone kwamba huyu Askari wanapokuwa naye ni mtamu na anapokufa wana hamu sana ya kwenda kumzika. Pia, wawe na hamu ya kuona mafao yao yanapatikana kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri katika tarehe 19 nilikuwa na swali la msingi la kuhoji kutokana na Askari ambaye amefariki toka mwaka 2003 hadi leo warithi hawajapata mafao; mpaka na wao wafe! Kwa hiyo, siyo jambo zuri. Kama uliweza kwenda kumchukuwa wakati amefariki na ulikuwa unamtumia, basi ni vizuri na kuona maslahi yao yanapatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali yangu hapa, tuone kwamba watu wote siyo sawa, kwa hiyo Askari Polisi wawe wanachukua jukumu la kuwashauri wale wafiwa.

Wengine hawana uwezo wa kufika. Sisi tulipata maslahi yetu kwa kupitia wakubwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. HAJI MAKAME MLENGE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nakushukuru sana Mheshimiwa. Nilishakutaja Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani. Mheshimwia Nashon hayupo, namruka. Ahsante, Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nfasi hii nami niweze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ambayo ni muhimu sana.

**SPIKA:** Atafuatia Mheshimiwa Condester.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nitachangia mambo machache kwa sababu ya dakika tano. Nisipotambua mchango wa Askari wetu nitakuwa naidanganya nafsi yangu. Tunatambua mchango wa Askari wetu hasa kwa kujitolea kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna changamoto kadhaa ambazo zinawakumba Askari wanaojitolea hasa wa chini kabisa. Nitatolea mfano tu kwenye uchaguzi uliopita. Mheshimiwa Naibu Waziri nimezungumza nawe sana na jambo hili liko Wizarani. Siku ya uchaguzi siyo Jimboni kwangu, labda wanaweza wakafikiri nazungumza kwa sababu ni Jimboni kwangu. Askari amevunjika mguu siku ya uchaguzi akiwa kazini, mpaka leo nazungumza hakuna mchango wa

Wizara hata kidogo. Askari wenzake wale wa chini ndio wanaojichangisha na mimi Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo kwa sababu, Wizara haijachangia, isipokuwa inaleta picha mbaya kwa Askari wengine siku nyingine kujitolea. Inaleta picha mbaya sana na watarudi nyuma, kwa sababu wataamini kwamba nikiumia, itakuwa ni mzigo wangu mimi na familia yangu. Jambo hili haliko sawa, tuwatie moyo Askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Vituo kwa maana ya *Ma-OCD,* wale ni viongozi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unaweza ukamtaja jina la huyo Askari ili...

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri nafikiri anajua, kwa sababu anajua jina na ameshafanya naye mawasiliano, anajua vizuri.

**SPIKA:** Lakini *Hansard* haijui.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nikikumbuka nitalitaja, lakini hapa sina kumbukumbu nzuri.

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Wakati mwingine ni vizuri kutaja maana tutakapofuatilia baadaye...

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, haya.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Askari hao wachache ndio wanaopata mateso makubwa; lakini *Ma-OCD,* wale ni maaskari ambao wana

vyeo hivyo. Ukiangalia ofisi zao, wale sio wafungwa, wanastahili kupewa hizo nafasi na angalau mazingira yao yafanane. Kwa hiyo, tunapozungumzia kuboresha makazi ya askari, hata ofisi zao zifanane, angalau nao wakiwa mle ndani wajue wako ofisini, angalau watimize majukumu yao. Siyo wanapita huku kuna kunguni, kuna panya na nini. Yaani ifikie mahali kwa kweli tuwatie moyo askari wetu. Pamoja na kwamba kuna shida ya maslahi na nini, basi angalau mazingira yafanane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya dakika tano, nitakwenda kuzungumzia pia habari ya vitambulisho vya Taifa. Alipokuwa anazungumza Mbunge wa Kigoma, yawezekana alisomeka kwamba ni Kigoma. Mikoa yote ya pembezoni tuna changamoto hiyo. Mimi natokea Wilaya ya Nkansi, sisi tunapanda boti tu kwenda Kongo pale. Ikifika wakati wa uchaguzi, wale wote wanaoonekana wana mtazamo tofauti na CCM, wanaambiwa wewe sio raia. Hili jambo siyo zuri, linaleta unyanyasaji. Siyo jambo jema kabisa. Pamoja na kwamba bado tuna changamoto ya utekelezaji wa vitambulisho, basi mikoa ile ya pembezoni ipewe kipaumbele ili kumaliza hizi changamoto ambazo zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu ambao walipewa namba toka mwaka 2020, sasa kama namba wameshapata, vile vitambulisho vinachukua muda gani? Hili jambo ni lazima tulitazame. Kwanza tunawakwamisha kwenye mambo mengi. Leo unapokwenda kwenye sijui usajili wa *line* na vitu gani, kote unahitaji kitambulisho cha Taifa. Kwa hiyo, tunawakwamisha sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuishauri Serikali yangu ya Tanzania, sisi wote ni Watanzania. Leo hawa watu ambao wanaitwa wahamiaji au wageni ambao wamekuja kufanya shughuli mbalimbali Tanzania, tunatambua kwamba ipo sheria ya wageni wanapotaka kufanya kazi. Kipindi cha nyuma ilikuwa ni shilingi milioni sita kwa miaka miwili. Leo watu wengi hawana hivyo vibali vya

kufanya kazi, wakiwemo watu wachache tu ambao wanafanya kazi saluni, hizi shughuli ndogo ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuishauri Serikali kwenye jambo hili, imekuwa ni kama upenyo wa baadhi ya watu wa uhamiaji, wanakwenda kufika kule wanawaambia nipe shilingi 500,000/= ili nikuachie, kwa sababu sasa hawana vibali. Kwa hiyo, naishauri Serikali, ni vizuri mkawatambua wale wanaofanya kazi nchini ambao ni wageni, wako wangapi? Je, wana vibali vya kufanya kazi hizo? Yawezekana hata idadi yao hatuijui. Kwa hiyo, Serikali inakosa mapato, ila watumishi wachache wanakwenda kwa kukosa uaminifu, anaomba shilingi milioni moja, wanamalizana; naomba shilingi laki mbili, wanamalizana.

Mheshimiwa Spika, sasa hawa watu, kama kweli kuna vibali, tuangalie aidha kuna shida kwenye sheria yenyewe, tuifanyie maboresho. Ila kabla ya kufanya maboresho, tuwatambue wako wangapi? Je, kweli hizo kazi wanazofanya wanafanya kwa mujibu wa sheria? Yawezekana tukiwatambua itasaidia sasa hata kile kiasi ambacho tunakitaka kama ni kikubwa kipunguzwe. Lengo ni kwamba kifike Serikalini, kisipotee huko mtaani kama kinavyopotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kwa hiyo, pia kwako kuna shida ya uhamiaji?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, eeh, wapo wengi tu.

**SPIKA:** Hebu tamka nne! Tunaendelea Waheshimiwa. Mheshimiwa Condester Sichalwe. *(Kicheko)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa. Kwanza kabisa nianze kwa kusema kwa kuwa muda ni mfupi namwomba baba yangu Mheshimiwa Waziri Simbachawene pamoja na Naibu Waziri,

wapate nafasi ya kutembelea Jimbo la Momba ili kwa haya ambayo nitayaainisha kutokana na muda mfupi, sitaweza kupata nafasi ya kuelezea kwa kina, watakuja kujionea kwa uhalisia wenyewe nitakachokiongea hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kwanza ambayo nataka kueleza hapa ambayo inawapata Jeshi la Polisi na wanashindwa kutekeleza majukumu yao vizuri kwa wananchi wa Jimbo la Momba, jambo la kwanza ni usafiri. Jimbo la Momba ni Jimbo ambalo ni pana sana, lina *square meter* za mraba 5,856; vijiji 72 na vitongoji 302. Unaweza kuona ni kwa kiasi gani Askari hawa wanawezaje kufanya kazi; kutoka kijiji kimoja kwenda kingine wakati mwingine ni zaidi ya kilomita 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uhalifu unapotokea mfano labda Kijiji cha Itumba, Kata ya Nzoka mpaka Askari huyu afike eneo la tukio kwenda kuwasaidia wananchi hawa, nasi tuko kwenye Jimbo la mpakani, unakuta wahalifu hawa wameshakimbia, wameondoka, wametokomea Zambia. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali na Wizara hii itutazame, tupatiwe gari ili Askari hawa waweze kufanya kazi yao vizuri. Wakati mwingine hata lambalamba tu wanatusumbua sana. Hatuwezi hata ku-*deal* na lambalamba.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Taarifa Mheshimiwa.

**SPIKA:** Endelea wa taarifa. Mheshimiwa Condester, kuna taarifa unapewa. Upande gani?

## TAARIFA

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hali iliyoko kule Momba ni sawa sawa na Nyang'hwale, tuna magari mawili *Landcruiser* lakini hayana matairi. *(Kicheko)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo, lakini sisi hatuna kabisa hiyo gari.

**SPIKA:** Pokea taarifa hiyo Mheshimiwa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, hatuna kabisa hilo gari, hata pikipiki hakuna; hata baiskeli hakuna.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Jimbo la Momba, yaani Halmashauri ya Wilaya ya Momba ndiyo Jimbo ambalo linabeba Makao Makuu ya Wilaya ya Momba, Majimbo mawili ya uchaguzi...

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Amar Hussein afadhali wewe una magari hayana matairi, mwenzako hata baiskeli hana. Sijui yupi zaidi sasa hapo. Endelea Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni kuhusiana na kwamba Jimbo la Momba yaani Halmashauri ya Momba ndio jimbo ambalo Makao yake Makuu inabeba Wilaya ya Momba, lakini hatuna kituo cha polisi ambacho kinafanana na hadhi ya wilaya. Tuna *outpost* mbili tu ambayo ni kituo kidogo cha Kamsamba ambacho kina askari nane, kituo kidogo ambacho kipo Chitete ambako ndio makao makuu, kina askari wanne, yaani hata ukipata ya Uchaguzi jamani askari huyu hana baiskeli, hana pikipiki anakwenda kumkamata nani.

Mimi kuna wakati nimefanya kampeni na lambalamba, maana yake nimekuta lambalamba anafanya mkutano wake na hawezi kuja kunisikiliza, wananchi wanafanya pale, kwa hiyo ikabidi tuwaombe kwa sababu hatuwezi kuwapigia Jeshi la Polisi watakuja na nini, watembee kilomita 50.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester, lambalamba ndio nini?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, lambalamba ni mkusanyiko. Ulinde dakika zangu Mheshimiwa Spika tafadhali, nitakapotoa ufafanuzi wa lambalamba.

Mheshimiwa Spika, lambalamba ni hawa wanajiita, sijui tusemeje! Sijui waganga wa kienyeji, kwa hiyo wakifika kwenye Kijiji wanahamasisha kwamba tumtafute mchawi na kitu kama hicho. Sasa vile vinaleta mgongano kwenye jamii, kwa hiyo utakuta wakati mwingine wananchi wanataka hata wakaague shule. Nimefika mahali nimewaambia Serikali haitambui uchawi, wananchi wanasema hapana si tunataka Mbunge ambaye anayetutetea, tunaumwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba sana, naamini kungekuwa na gari na kungekuwa na Kituo cha Polisi kizuri, kina Afisa mwenye nyota tatu, akapewa askari wa kutosha wangeweza kufanya *patrol* na kuzunguka, wananchi katika hali ya kawaida tunaogopa sana askari. Kwa hiyo kuona askari wanapitapita, wanalinda wanaona kwamba kuna usalama wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine hatuna askari wa kike, nafikiri kwa sababu hatuna kituo ambacho kina hadhi ya wilaya ili Afisa mwenye nyota tatu akikaa pale kuna mwongozo wa Jeshi la Polisi ambao wanabidi awe na askari wa idadi fulani. Sasa tunajiuliuza sisi wananchi wa Jimbo la Momba sisi wote ni wanaume? Hapana, sasa tunakaguliwa na nani kama askari wote hawa ni wanaume? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, hakuna nyumba za maaskari na wakati mwingine hata Kituo cha Polisi chenyewe huwezi ku-*identify* kama ni Kituo cha Polisi. Askari hawa wanalala wapi, wanajichanganya huko, wanapanga huko mitaani. Sasa kama ilivyo kuna imani za kishirikina, wakati mwingine wanaweza kuamini hata askari mwenyewe ni mchawi. Kwa hiyo akachomewa nyumba, kwa sababu kule watu wanakatana mapanga kwa hizi imani za kishirikina.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namwomba baba yangu Mheshimiwa Simbachawene afike kule tu, kwa sababu muda hautoshi nisije nikasitishwa hapa, ili akajionee, tukatembee nimfikishe kule Katumba, nimpeleke kule Chole, Siliwiti na kule Kichangani Kamsamba. Akishaenda kuona tu, baada ya mwezi mmoja ataniletea askari hata 40 na atanipa gari.

Mheshimiwa Spika, ahsante san ana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa matumizi mazuri ya muda, Mheshimiwa Condenster Sichalwe. Nitamshangaa sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani asipokubali hiyo *offer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Santiel Kirumba atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Samweli Hhayuma. Mheshimiwa Santiel Kirumba, hayupo. Mheshimiwa Hhayuma. *(Makofi)*

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuaminiwa. Pia niipongeze wizara nzima kwa kazi nzuri inayofanyika.

Mheshimiwa Spika, niongelee maeneo mawili, eneo la kwanza ni eneo la Vitambulisho vya Taifa. Hili suala limesemwa sana jimboni kwangu, wazee wananiuliza hivi tumechukuliwa alama za vidole, ilikuwa ni maonyesho tu, hivi vitambulisho mbona haviji? Kweli hivyo vitambulisho ni muhimu sana kwa ajili ya watu kufanya shughuli zao na kwa ajili ya kujitambulisha katika maeneo mbalimbali. Ukienda kwa watendaji kuomba barua, siku hizi katika maeneo mengine hizo barua za watendaji hazitambuliki, vitambulisho vile ni muhimu kwa watu kupata huduma na kufanya shughuli za kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze upande wa huduma hasa za Jeshi la Polisi. Nawapongeza kwa kazi nzuri inayofanyika, kazi ya kuhakikisha kwamba usalama na ulinzi wa raia na mali zao. Vijana wetu wanajituma sana na sisi ambao tunafanya siasa huwa tunatembea usiku na njiani tunaona jinsi wanavyopigwa na baridi, wanavumilia. Ninachoomba, ili wafanye kazi kwa moyo Wabunge wenzangu wamesema sana, tuangalie maslahi yao, wawe na furaha na kazi wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwenye maslahi hasa na kwenye vifaa ambavyo wanavitumia kwa ajili ya kutenda kazi; magari na *service* za magari, kwa sababu wakati mwingine wanakuwa watumwa kwa viongozi wengine, Polisi katika Halmalshari hawana mafuta wanakwenda kuomba kwa Mkurugenzi. Wakati mwingine wana kazi ya kwenda kufanya au kwenda kukamata, mhalifu, yule aliyelalamika analazimika kuombwa mafuta. Sasa hapo haki inakuwa ngumu kutendeka. Naomba tuwatendee haki tuwape vitendea kazi ili wafanye kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo linguine ni eneo la ulinzi shirikishi, Polisi Jamii. Hii inakwenda wakati mwingine inafifia, naomba eneo hilo tulikazie ili angalau sasa wananchi wakishiriki usalama unakuwa mzuri zaidi. Namie niombe ulinzi shirikishi au Polisi Jamii itanuliwe kidogo ifike kwenye upande wa kutekeleza Sheria hizi za Usalama Barabarani hasa inayowagusa vijana wetu wa bodaboda, ambao wengi wao wanaendesha vyombo vile bila mafunzo yaliyokamilika. Kumekuwa na utamaduni sasa kwa sababu anajua kabisa ana makosa, akisimamishwa hasimami anakimbia. Sasa Polisi wanachukua hatua za ziada za namna ya kuhakikisha wanaweza kuwakamata, wakati mwingine wanawachapa fimbo. Sasa ukifanya hivyo maana yake unahatarisha maisha ya yule anayeendesha, lakini na watumiaji wengine wa barabara.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza ajali ambazo zinaweza kuzuilika, naomba katika eneo hili, polisi jamii tuwatengenezee utaratibu mzuri, kwa sababu wana vikundi vyao vile vikundi tuviimarishe ili washirikiane vizuri na Jeshi la Polisi. Kwenye jimbo langu ukienda kimya kimya kama hawajui gari vijana wanaanza kukimbia, maana yake kidogo kuna ile sintofahamu, hilo eneo tukikaa nao, tukalirekebisha angalau tutawasaidia hao vijana kufanya shughuli zao kwa kufuata taratibu na sheria za nchi. Badala ya kuweka nguvu nyingi katika kuwakamata, wakiwa na vitambulisho vya uraia wanafahamika wote wanatoka maeneo gani, wana-*register* nzuri kwenye eneo lile, inakuwa rahisi kumfuata hata baada ya kuwa umeshajua kuwa kuna kijana huyo amekimbia.

Unamfuta kwenye eneo ambalo anaishi hakuna sababu ya kukimbizana.

Mheshimiwa Spika, tuliongea sana na eneo pia la faini wanayopigwa vijana wa bodaboda, pikipiki zile sio zao, kwa siku mapato labda shilingi elfu nane, lakini akipatikana na kosa elfu thelathini. Anaanza kukimbizana na ndugu zake, hii kweli inawaumiza vijana, hatuwajengei uwezo wa kujikwamua kiuchumi. Tutafute namna ya kuwawezesha ili watekeleze sheria na wafanye shughuli zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa kwa sababu najua kuna *limitation* ya muda, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hhayuma. Mheshimiwa Innocent Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la *NIDA*, suala hili kwa kweli limekuwa ni kero. Mimi kama Mbunge naunga mkono Serikali kusema kila raia awe na kitambulisho cha *NIDA,* lakini ni jambo ambalo linashangaza, Serikali inatangaza wananchi hao wawe na vitambulisho, lakini ninachokiona hiki kilichotangazwa, Serikali ilikuwa haijajiandaa. Hawa wananchi wanasema sisi tupo tayari, mtupe vitambulisho, wanakwenda kwenye Ofisi za *NIDA* hawapati vitambulisho wanaambiwa shida ni mtandao, kwa kweli hili jambo halijakaa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali iliangalie na nishauri kama Serikali katika hili bado haijajipanga vizuri, ni afadhali kulisitisha kuliko wananchi kuendelea kukosa huduma. Kwa sababu limekuwa ni kero kubwa sana na ukilinganisha kwa mfano mazingira ya kule kwetu Kyerwa,

wananchi wanatoka maeneo ya mbali anakwenda wilayani zaidi ya kilomita 30, anashinda pale, hajapata kitambulisho anarudi nyumbani, imekuwa ni kero kubwa sana. Kwa hiyo niiombe sana Serikali ili iliangalie, ikiwezekana kama bado haijajipanga isitishe.

Mheshimiwa Spika, kule kwangu kuna shida, ukienda kwenye Ofisi za *NIDA* wanasema shida ni mtandao, mtandao mpaka wafuate Wilaya nyingine ya Karagwe. Kwa hiyo niombe zile wilaya ambazo zipo pembezeni na hakuna mtandao wangeacha hili jambo kwa sababu limekuwa ni kero kubwa sana, yaani kule kwetu ukiongelea *NIDA* wanasema hii ni hatari. Kwa hiyo niombe sana hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la watu wa Uhamiaji, kubainisha wale ambao ni raia na sio raia. Mazingira ya kule kwetu ukisema mwananchi aende wilayani ni kero kubwa. Ushauri wangu ninaotoa, Maafisa hawa wa Uhamiaji wawatumie Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji. Waende kule *site* wakawatumie hawa ndio wanaweza kutambua raia ni nani, haiwezekani Afisa Uhamiaji umetoka Dar es Salaam au Dodoma, unafika Kyerwa unasema huyu siyo raia, hili sio sawa. Wawatumie viongozi ambao wananchi wamewachagua Maafisa Watendaji, Wenyeviti wa Vijiji ili waweze kujua ni nani ambaye ni raia au siyo raia, vinginevyo hii biashara ni kama kuwaneemesha watu. Kwa hiyo hilo niombe sana tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni kuhusu hawa mapolisi wetu, pamoja na mambo mengine ambayo yanazungumzwa lakini wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Ukifika kule kwangu, sasa hivi wilaya ina zaidi ya miaka saba hawana ofisi, wanafanyakazi kwenye Ofisi ya Kijiji. Tulivyomaliza uchaguzi nilikwenda kuikagua ile ofisi inadondoka wakati wowote, imebidi nichukue fedha niwape milioni 10 angalau tuweze kuboresha ile ofisi ambayo ni ya kata. Kwa hiyo niombe sana, hili liangaliwe. Pia hawana nyumba, wanaishi

kwenye mazingira magumu, yaani ni kama kundi fulani ambalo limetelekezwa. Kwa hiyo niombe sana tuliangalie, tuweze kuboresha mazingira wanayofanyia kazi, kwa sababu wanafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninaloomba, kule kwetu kuna kitu kinaitwa gongo, ile gongo inatokana na ndizi, hizi ndizi zinatengenezwa wanapata gongo. Serikali tunaomba ifanye utafiti hii gongo iweze kuhalalishwa. Kama tunaruhusu ndizi na hiki kitu kinatokana na ndizi, kwa sababu kuna gongo nyingine inatokana na vitu vya ajabu ajabu, lakini hii inatokana na ndizi. Kwa hiyo, naomba kwa Mheshimiwa Waziri, Wanakyerwa wamenituma, hili jambo liangaliwe. Kwa sababu imekuwa ni biashara ya watu...

**SPIKA:** Yaani hiyo hoja ni muhimu sana, kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mchungaji anaomba gongo hii.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**SPIKA:** Na kuna taarifa juu ya hayo. Taarifa ipo upande gani! Haya endelea.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpe taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Bilakwate, wanachotengeneza Kagera sio gongo ni *enkonyagi* au *Kaliinya*. Kwa hiyo, *enkonyagi* ni tofauti na gongo, gongo ni haramu *enkonyagi* sio haramu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, Ahsante hiyo taarifa nimeipokea kwa kweli inaitwa *enkonyagi*. Kwa hiyo hili niombe sana, Serikali iliangalie namna gani wanaweza kutafiti kwenye kinywaji hiki ili kiweze kuruhusiwa kwa sababu hata ukimuuliza Mheshimiwa Mwijage na Waheshimiwa wengine wanaotoka Kagera, wote wamesomeshwa kutokana na hiyo *akaguri*, *akakonyagi*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine niongelee suala la bodaboda. Hawa vijana wamejiajiri, hebu niombe sana Polisi wetu wajikite kuwapa elimu kuliko kukimbizana nao kila sehemu. Wanafanya kazi kwenye mazingira ambayo ni magumu, unamkamata bodaboda ambaye kwa siku akipata faida kubwa ni shilingi 30,000, unamtoza shilingi 50,000, unamtoza shilingi 200,000; hili kundi tutaendelea kulifanya kuwa maskini. Kwa hiyo niombe sana hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Innocent Bilakwate. Mheshimiwa Ester A. Bulaya sasa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wewe utakuwa shahidi, duniani watumishi ambao wanatoa huduma kwa wananchi na hasa kazi zao ngumu wamekuwa wakilipwa vizuri sana. Ukienda Marekani, Uingereza, Afrika Kusini na maeneo mengine, Walimu, Madaktari, Manesi na Polisi na vyombo vingine vya usalama wamekuwa wakilipwa vizuri, mazingira yao ya kazi yakiwa mazuri, pamoja na makazi yao kutokana na kazi ngumu wanazozifanya lakini na *risk* wanazoweza kukutana nazo kwenye kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, mbali na changamoto za kiutendaji, lakini Polisi wetu wamekuwa wakilipwa mishahara midogo, hasa Polisi wa chini. Lakini sio tu, nyumba zao, ofisi zao ni aibu kulingana na mzigo waliopewa wa ufanyaji kazi katika Taifa letu.

Nikitolea mfano pale Buhigwe, najua sasa hivi watakwenda kufanya kwa sababu ndio anakotoka Makamu wa Rais. Kuna muda Polisi walikuwa anafanyakazi kwenye matenti, kuna muda walikuwa wanatumia Ofisi ya Mtendaji wa Kata, lakini kuna wakati mwingine walikuwa wanakwenda kuchapisha *documents* mtaani. Hivi kuna siri za nchi au za kiupelelezi zinazoweza kuwa salama! Lazima tuboresha mazingira ya Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumesema tunataka jeshi letu liwe la kidijitali lakini leo *computer* imekuwa anasa, sio hitaji la msingi. Unaweza ukakuta Makao Makuu ya Polisi, nenda Wilayani, nenda mkoani kwa Bunda pale jimboni kwetu, maana nikisema langu italeta mgogoro, Jimboni kwetu pale Bunda, utakuta ofisi ya *OCD* ndio kuna *computer*, kwa *OC-CID* na *traffic* ziko *computer* tatu. Leo sisi hapa tuna Ipad kwa sababu tunataka twende na teknolojia na wenzetu duniani wanavyokwenda. Tubadilike tufanye jeshi letu liwe la kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye Jimbo la Bunda Mjini. Pale Jimbo la Bunda Mjini ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Bunda ambayo ina majimbo matatu, Bunda Mjini, Bunda Vijijini na Mwibara. Kituo cha Polisi cha Jimbo la Bunda Mjini ni aibu, hakuna nyumba, wanakaa mtaani, hata hizo nyumba chache tu zilizokuwepo ni aibu. Hivi leo Sajenti anapewa labda chumba kimoja kwa sababu cheo chake kidogo hatakiwi kuwa na familia! Akiwa na watoto walale wapi, sebuleni? Wanandugu wakija. *Please,* tuwatendee haki hawa askari wetu ambao wanalinda Taifa hili kwa jasho na damu.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa Mbunge wa Jimbo *at least* kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo niliwasaidia jengo la upelelezi; nilipokuwa Mbunge wa Vijana, niliwapa mabati katika kujenga bwalo lao, tangu nilipofanya mimi kimya! *Please*, naomba Wizara iboreshe kile kituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu na mahabusu, uzuri nami nililala pale, kwa Mkoa wa Mara labda kama sijalala mahabusu ya Serengeti. Mahabusu ile ni ndogo na mbaya yaani haina hadhi, inawezekana mahabusu hiyo watu 10 ikawa ni shida, hewa hakuna. *Please*, tunaomba pia Wizara ikarabati mahabusu ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kile Kituo kiendane na hadhi ya wilaya, Wizara ipeleke na magari. Hivi leo hii akitokea mwizi Nyamswa, kukitokea uhalifu Mwibara, mafuta yenyewe shida, katika Wilaya yetu ya Bunda ambayo

inaunganisha majimbo hayo matatu kama nilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie gereza la Jimbo la Bunda Mjini. Nilipokuwa Mbunge niliwakarabatia mahabusu moja, nikawapelekea na *tv* pale, ile mahabusu inatia aibu, nyumba za magereza Bunda Mjini ni shida.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mradi umeanza tangu nilipochangia kidogo leo nyumba zipo kwenye lenta. Mpaka sasa hivi bado kuna shida kubwa mahabusu ile ya gereza la Bunda pale ni shida, lakini hata dawa kwenye Gereza la Bunda hakuna. Mdogo wangu kwenye uchaguzi alikamatwa, ilikuwa anaandika dawa ndiyo nampelekea. Je, wafungwa wengine wanakuwaje wasiokuwa na ndugu na wanatoka kwenye maeneo mbalimbali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, jambo lingine mlipe madeni ya polisi ya kuhamisha na mnapowapeleka kozi muwalipe kama watu wengine sio mnawakata kwenye mishahara yao wakati mnaenda kuwaongezea ujuzi. Ni aibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya. Tunakushukuru sana kwa mchango wako, nafikiri Waheshimiwa walikuwa hawajui, unasikia uzoefu huo? Selo zote za Mkoa wa Mara wamelala, magereza wanayajua halafu mtu mmoja huyo anafukuza tu kama vibaka. Yaani anafukuza halafu baadhi mnaunga mkono, hapana! Wamesota hawa watu jamani. *(Kicheko)*

Lakini pia wamejifunza kwamba huko hakufai, mbele ya safari ni kuangalia upya. La sivyo wafanye *reconciliation,* lah! Basi tu.

Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo. Basi tukubaliane Waheshimiwa awe mchangiaji wa mwisho, bado ninayo orodha ya majina ya watu hapa lakini hali ndiyo hiyo. Mheshimiwa Tadayo tumalizie dakika tano za mwisho.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ya mwisho kuchangia. Mchango wangu ni mfupi sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niungane na wote ambao wamepongeza kazi nzuri iliyofanywa na Wizara hii pamoja na changamoto nyingi ambazo tunazifahamu zinazoikabili Wizara hii lakini kwa kweli kazi ni nzuri na hata ukisoma takwimu *crime rate* yetu sio mbaya kama nchi zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili niungane pia na wote waliozungumza juu ya suala la hali mbaya ya miundombinu ya vitendeakazi na majengo ya polisi hata Jimboni kwangu Mwanga tuna tatizo hilo kiasi ambacho askari wetu wakati mwingine, nilipita siku moja pale kituoni nikakuta wanachangishana kupiga rangi kwenye jengo la polisi jambo ambalo lina moyo mzuri kwa kweli nawapongeza lakini tunahitaji kuwasaidia kwasabbau kimsingi sio kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nishauri sasa kuhusu masuala yote yanayohusiana na ujenzi katika majeshi yetu. Kwa bahati ni kwamba Wizara hii ina nafasi ya kuwa na nguvukazi yenye ujuzi mbalimbali ambao ni wenzetu wale wafungwa. Iko teknolojia ya matofali haya ya *hydra form* ambayo *National Housing* wanafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nina hakika kabisa tukiipeleka hii teknolojia kwenye maeneo ya megereza yetu na kwa ujumla kwenye majeshi mbalimbali ambayo iko chini ya Wizara hii wana uwezo wa kutengeneza matofali na tukamaliza kabisa tatizo la ujenzi wa nyumba za askari pamoja na maeneo mbalimbali ya maofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo pengine hata sisi tunaweza tukashirikiana ni kwamba hata tunapozungumzia hizi fedha za *CSR* kwenye wawekezaji mbalimbali ni vizuri pia tukakumbuka vituop vyetu vya polisi kwenye mambo ya *furniture n.k. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilipenda kuzungumzia ni juu ya suala la majanga ya moto. Mwishoni mwa mwaka jana Jimbo langu lilipata tatizo la kuunguliwa na shule inaitwa Nyerere Sekondari, moto ambao ulitokea karibu mara tatu mfululizo ukaunguza mabweni mawili kwa kiasi kikubwa sana. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama viliitikia kwa haraka sana, navipongeza. Lakini nadhani tunahitaki kwenda mbele kidogo kwenye tatizo hili iwe ni sehemu ya kuwaelimisha wanafunzi wetu shuleni na kuwapatia vifaa vya kuzimia moto. Endapo wale wanafuzni wangekuwa na elimu ya kutosha ya kupambana na moto halafu wakawa na vifaa vya kisasa, nina hakika majanga haya yangeweza yakadhibitiwa kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tuliweza kukimbia mchaka mchaka kila asubuhi tukiwa wanafuzni sidhani kama leo tukiamua kwamba kila Jumamosi tuna zoezi la kudhibiti moto, la kuzima moto kwa wanafunzi wetu sidhani kama itashindikana. Naamini itawezekana na tutaweza kuzuia haya majanga kwa sababu hata tungekuwa na magari mengi bado janga linapotokea ni vizuri wasije kuzima moto ila moto udhibitiwe, usitokee au usiendelee pale ambapo umeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mfupi tu. Naomba kuunga mkono hoja ya Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kwa kuwa ameokoa muda, Mheshimiwa Kihenzile malizia hizo dakika.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na pengine nipongeze kazi kubwa ambayo unafanya na wenzetu kuanzia Waziri mwenyewe pamoja na majeshi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilitaka tu kuongelea kwenye maeneo machache lakini moja wapo wa maeneo nataka kuzungumzia ni mazingira ya kazi kwa wenzetu wa Jeshi la Polisi. Ni vyema Serikali ikatazama kwa kina mazingira yale

ya kazi, leo ukiingia kwa *OCD* au ofisini pale Polisi wakati mwingine mazingira hayatoshi, *furniture* ni za hovyo. Ni vizuri tukalitazama hilo ili kulipa heshima Jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili tumeona jinsi ambavyo tumekabidhi dhamana kwa wenzetu wa Jeshi la Polisi, wanafanya kazi kubwa ya usalama wa nchi yetu. Na hili nafikiri Mheshimiwa Waziri ni vizuri ukalitazama vizuri sana hili tutakapokuwa tunapitisha huko baadaye kwasababu haiwezekani Polisi wanafanya operesheni za ulinzi na usalama wa watu wetu na sisi kipaumbele cha kwanza ni ulinzi na usalama wa watu wetu na mali zao halafu *OCD, OCS,* wanaomba mafuta kwa wadau ambao miongoni mwao watageuka kuwa wahalifu, heshima ya Jeshi iko wapi hapo? Hii sio sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kupendekeza tuweke mkakati mzuri ili kulipa heshima jeshi letu angalau wanapofanya shughuli zao wawe na bajeti ya kutosha. Tunawapa *inferiority complex* n ahata uwezo wa kusimamia sheria na kanuni inakuwa ni changamoto.

Pili, tunajikuta tunalazimisha vitendo vinavyoitwa rushwa, yue mtu anawapa mafuta kila siku, kesho unakuja kumuambia ni mhalifu, kibinadamu inakuwa ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wenzetu wa Jeshi la Polisi iko changamoto kubwa sana kwenye dhamana. Ni vyema mkalitazama nchi nzima kwenye vituo vyetu. Mfumo wetu wa utoaji dhamana ukoje? Kwa nini mtu akikamatwa Ijumaa anakaa mpaka Jumatatu wakati Jumamosi na Jumapili kazi inafanyika, tunafanya haya yote kwa faida ya nani? Ni vyema tukalitazama jambo hili pia kwa kina ili kusaidia watu wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi hapo hapo ulipo jaribu na wewe kuchangia dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, sasa nichukue fursa hii, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa Mbingu na Ardhi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nichukue fursa hii tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako hili Tukufu kwa kuwa wametoa michango mizuri, michango ambayo kitaalam tunaita *very constructive ideas,* michango ambayo ni michango jengefu. Michango ambayo sisi tutaichukua tunakwenda kuifanyia kazi ili kuona namna ambavyo tunaboresha utoaji wa huduma au tunaboresha Wizara yetu au tunaboresha vyombo vyetu katika kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo sasa nianze kutoa majibu ya baadhi ya michango ambayo Waheshimiwa wameichangia lakini pia wameulizia ndani yake wametaka kujua baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Spika, kuna michango mbalimbali ambayo imetolewa, kiujumla ni kwamba kuna Kituo cha Polisi cha Ng'ambo *Station* Zanzibar kimezungumzwa hiki, kiukweli kituo hiki ni cha zamani maana binafsi ninafungua macho yangu kile kituo nakiona vile vile. Kama Serikali tunao wajibu wa kukifanyia maboresho lakini kwa wanaokifahamu kituo kile hatuwezi kukipanua kwasababu ni kituo ambacho kimezungukwa na barabara. Pande zote ukizitazama kimezungukwa na barabara. Kwa hiyo, kikubwa ambacho tunakifanya ni kwamba kama Serikali tunakwenda kukiboresha zaidi katika utoaji wa huduma ili kiweze kutoa huduma zaidi lakini sio kukitanua na kukijenga upya kwa mazingira kilipo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna hoja nyingine ilikuja hapa Mheshimiwa Omar Ali Omar alizungumzia suala la

nyumba za Polisi Finya. Ni kweli nyumba zile nimewahi kufika, nimetembelea pale, nimeona hatua ambayo nyumba zile zimefikia na nimeona waliniambia idadi ya fedha ambazo zinatakiwa ili kumaliza nyumba zile.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee Serikali ilitoa maelekezo na tukalichukua lile jambo na tayari tumeshatoa maelekezo kunakohusika kwamba tuweze kupatiwa zile fedha ili tukamalize kituo kile.

Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba asiwe na wasiwasi nyumba zile zitamalizwa na askari wa eneo lile na maeneo ya Jirani watapata mahali pazuri pa kuweza kukaa na familia zao.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Maida Hamad naye ameeleza suala zima la upungufu wa wafanyakazi wa Jeshi la Polisi hasa katika kisiwa cha Pemba. Ni kweli upuingufu upo lakini kama ambavyo mara nyingi huwa nazungumza hasa nikisimama hapa huwa naelekeza kwamba upatikanaji wa ajira una *some procedures* lazima zifuatwe, sio kwamba tukurupuke tu tuajiri kwasababu tuna uhitaji, kuna mambo lazima tuyafuate, lazima tupate kibali cha kuajiri ambacho tunakiendea mbio sasa hivi kukipata, lazima tuangalie bajeti tuliyonayo, lazima tuangalie uhitaji wa hawa wanaotaka kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kikubwa nimuambie Mheshimiwa ndani ya bajeti hii tunategemea kuajiri askari wasiopungua 400 ambao hao sasa wataenda ku-*cover* hizo nafasi. Mheshimiwa asiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, limezungumzwa suala la *OC,* amesema kwamba *OC* ziende moja kwa moja vituoni. Utaratibu umeshawekwa wazi hasa kwenye *PGO* kwamba fungu alinalo mwenye Fungu ni *IGP* na *RPC.* Kwa hiyo, hilo la kusema kwamba ziende vituoni moja kwa moja hapa inabidi tuje tukae tena tujue namna ya kufanya lakini utaratibu uko wazi hivyo kwamba linatoka kwa *IGP,* linakuja *RPC, RPC* ana-*distribute* kwenye *OCD's* na vituoni.

Mheshimiwa Spika, kingine Mheshimiwa Ravia Idarus Faina na yeye amezungumzia suala la je, ni lini sasa Serikali itajenga ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Zanzibar? Hili tuseme kwamba tunalichukua kwa umuhimu wa kipekee sana. Ni jambo ambalo tumeliona na limetugusa na tumeona sasa tuna haja ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa asiwe na wasiwasi na hilo, tunakwenda kujenga ofisi nzuri ya kisasa ambayo itakuwa ni Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Waziri akienda atafikia pale, Naibu Waziri na shughuli nyingine za Kiwizara zitafanyika hapo. Hilo asiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, lakini akaja na hoja ya *PGO,* akasema kuna baadhi ya vipengele vinaepukwa, kuna baadhi ya taratibu hazifuatwi, maeneo hayafuatwi. Ni vyema Mheshimiwa angejaribu kueleza yale maeneo ambayo anahisi kwamba hayakufuatwa na sisi tukajua namna ya kuyaweka sawa kwasababu ukituambia haifuatwi na wakati taratibu zipo, zinafuatwa zote tunakuwa hatujui tufanye nini lakini vizuri tungepata kujua yale maeneo ambayo bwana kwenye maeneo fulani na fulani hapa *PGO* imekengeuka kidogo haikufuatwa.

Mheshimiwa Spika, kingine kulikuwa kuna jambo la zile tunaita *fire clubs.* Hapa nataka niseme katika suala hili la zimamoto hatuwezi kuzima moto kwa uzoefu tu kwamba tunauzima moto lazima kuna mambo *automatic* tuelezane. Kwanza tuwaeleze wananchi kwamba wachukue tahadhari katika suala la ku-*control* majanga.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, sisi tuna wajibu wa kutoa elimu kwa jamii kitu ambacho tunakifanya mara kwa mara katika Jeshi letu la Zimamoto lakini cha tatu ambacho tunakifanya na tayari tumeshakifanya, hivi karibuni tulifanya makubaliano pale, tulisaini makubaliano baina ya Jeshi hili la Zimamoto na wale watu wa *scout* ili sasa waweze kutufikishia ujumbe hata mashuleni na maeneo mengine ili hata likitokeza tatizo au janga lolote la moto waweze kuli-*save* wakati Jeshi la Zimamoto wanakuja kuhami hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika hili tumejipanga vizuri na tuwaambie tu wananchi kwamba tutaendeleza kutoa elimu kwasababu kitu kimoja kikubwa ambacho kitawafanya watu waweze ku-*control* haya majanga ni taaluma ambayo tuanenda kuwapa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna jambo jingine ambalo limeulizwa. Mheshimiwa Faina ameuliza suala zima la Ofisi ya *NIDA* Wilaya ya Kusini. Ofisi ipo! Tunachokiangalia sisi ni utoaji wa huduma. Hatuangalii kuwepo kwa ofisi kwasababu inawezekana Ofisi ikawa ipo kubwa ya ghorofa lakini huduma zikawa hazipatikani. Lakini sisi huduma inatolewa, ukienda Makunduchi Ofisi ipo pamoja na kwamba ni ndogo lakini huduma zinatolewa na wananchi wanapata huduma kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kikubwa niwaambie tu kwamba Ofisi zinatoa lakini kikubwa ambacho tumeshakubaliana kwamba tunakwenda kujenga Ofisi ya Kisasa ya *NIDA,* Serikali itajenga pale Kusini Makunduchi ili wananchi waweze kupata huduma za upatikanaji wa vitambulisho kwa muda ambao umekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwaambie tu kwamba wasiwe na wasiwasi tumeshajipanga vizuri, mwanzoni ama mwishoni mwa mwezi wa tano tunategemea maeneo mengi ya Tanzania watu watakuwa tayari wameshapata vitambulisho vya *NIDA.*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna changamoto nyingine zimeelezwa za magari ya Polisi, wengine hawana, wengine zipo lakini mbovu, wengine hazina maringi, wengine hawana kabisa.

Pia kumezungumzwa masuala ya upandishwaji vyeo, hayo yote ni mambo ambayo tuko nayo na tunaenda kuyafanyia kazi. Kikubwa ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono bajeti hii ili ipite ikatatue changamoto zinazokabili baadhi ya vyombo vyetu ambavyo mmeviorodhesha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis. Sasa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene aweze kuhitimisha hoja yake dakika 20.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri waliyochangia na kusema ukweli michango pamoja na kwamba ni siku moja lakini michango ni mingi mno. Umetuendesha vizuri na tumepata wachangiaji 25 waliopata kusema. Lakini pia tumepata wachangiaji wengi walioweka kwa maandishi. Niseme tu kwa kweli michango yote tunaithamini na tutaichukua yote kwa ajili ya kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nafahamu pia wako ambao hawakusema lakini pia hawakuandika ila kwa namna moja ama nyingine tumekuwa tukikutana wakieleza yao. Nataka niseme tu wote michango yenu tutaitumia katika kuhakikisha kwamba tunaboresga utendaji kazi na kuleta mabadiliko katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, nianze na mchangiaji wa kwanza ambaye ni Kamati yenyewe ya Nje, Ulinzi na Usalama. Michango na maoni yote ya Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama kamati inayoongozwa na Mheshimiwa Zungu, yote kabisa tunaichukua kama ilivyo na sisi kwetu ni suala la kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ina watu wenye weledi, tunafanya nao kazi kwa karibu na tukijifungia kule tunafundana kweli kweli. Ndiyo maana mengi hapa hayajasemwa lakini hata ambayo hayakuja hapa sisi tunayafahamu na tunayafanyia kazi kwa kadri walivyotuelekeza. Kwa hiyo, nawashukuru sana Wajumbe

wa Kamati wote kabisa na hotuba yenu yote sisi tumeichukua na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, sio rahisi sana kujibu hoja zote zilizosemwa hapa kwa maandishi na wale waliosema na kwa hivyo nitajaribu kusema baadhi ya zile ambazo kwa mujibu wa uzito wake basi zinapaswa kutolewa majibu hapa.

Mheshimiwa Spika, zimezungumzwa changamoto za vyombo vyote, Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto, juu ya changamoto ya vitendeakazi, changamoto ya makazi ya askari, ofisi zenyewe (vituo) au makambi ya magereza. Yamezungumzwa hapa masuala ya maslahi ya watumishi, upungufu wa watumishi kwa maana ya askari. Yote haya ukiyaangalia kwa namna yalivyo, ni suala la fedha. Kama bajeti ikiruhusu tunaweza tukamaliza matatizo haya yote na tufahamu kuwa nchi yetu hii ni kubwa, Wilaya nyingi bado hazina huduma muhimu, hatuna vituo vya polisi, hatuna makambi kwa ajili ya magereza na nchi inapanuka na kila siku tunaanzisha maeneo ya utawala mapya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme changamoto hii tunaichukua kama Serikali na kadri bajeti zinavyokwenda tutakuwa tunapungua changamoto na mtaona hata katika kitabu chetu cha hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani tumeweka fedha nyingi sana kwenye *development* sasa. Kubwa ni kwamba fedha hizo zipatikane na tuweze kutekeleza miradi hiyo, inayoendelea na ile ambayo itatekelezwa kwa fedha hizi ambazo tunaziomba safari hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, changamoto ni nyingi, zote mlizozisema, nyingi zinahitaji fedha. Kama fedha hakuna, hakuna muujiza hapo. Na siwezi kusema kwamba nitafanya kwa sababu ni fedha ndiyo itakayofanya. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge mtuelewe, kadri Serikali itakavyokuwa inapata fedha tutaendelea kupunguza changamoto mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tunayo magari takribani 357 ambayo yataingia wakati wowote kwa ajili ya Jeshi la Polisi. Tutajitahidi tugawane kwa kuangalia uzito wa maeneo yetu mbalimbali. Safari hii tutaangalia maeneo ya vijijini zaidi na ya mipakani ambako huko ndiko kuna changamoto nyingi sana. Nimeongea na *IGP* amesema kweli kabisa *this time* tutayapeleka magari haya vijijini zaidi kuliko hata mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia katika ujenzi wa makazi ya askari katika kila jeshi tumepanga kiwango cha fedha ambazo zitakwenda. Kuna ambao wana shilingi bilioni sita, bilioni tatu, bilioni mbili; zitatusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto hii ikiwemo na kusaidia miradi inayoendelea sasa. Tumepewa fedha nyingi sana ambazo kusema kweli zitatusaidia sana, Dodoma tu hapa tunajenga nyumba nyingi tu, lakini na mikoa kadhaa tutajenga nyumba nyingi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaambie Waheshimiwa Wabunge changamoto hizi tunazifahamu kama Serikali na kusema ukweli askari wetu wanaishi katika makazi ambayo hayafai ukilinganisha na mabadiliko ya uchumi na kadiri tunavyokwenda kwenye uchumi wa kati, haiwezekani sekta nyingine zimekuwa sana elimu, afya lakini sekta hii ya ulinzi bado hatujaikuza kulingana na mazingira tunayokwenda nayo. Bado kuna majengo ya kikoloni yanaonekana, *lock up* za kikoloni, *cell* za kikoloni, bado tuna kazi kubwa ya kufanya. Mimi niseme natambua sana michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, yako mengine ambayo yamezungumzwa ni *very specific.* Kuna hili lilizungumza juu ya mafunzo yale ya utayari ya askari polisi. Yale mafunzo siyo mafunzo kama mtu anaenda kusomea kazi mpya. Ni mtu anaenda kufanya mafunzo ya utayari, ukakamavu, sasa ile ni sehemu ya kazi. Hizi Sh.10,000 ambazo wanapewa kila siku kama *ration allowance* huwa ni kwa ajili ya askari huyo kupata chakula. Kwa hiyo, awe yuko ofisini, barabarani, likizo

au ypo kwenye *training* ya mafunzo hayo ni hela hiyohiyo ndiyo anayotakiwa kula.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sasa ukisema unamlipa nyingine wakati ana hela ya kula na ameenda kwenye mafunzo ya utayari, jamani, unajua kuna utofauti kati ya vyombo hivi vya kijeshi na *civil service* ya kawaida. Hawa wanajeshi utayari ni sehemu ya kazi yao, yaani kunyakua, kuruka kichura na kadhalika ni sehemu ya shughuli yao sio mafunzo kama mafunzo mapya. Kwa hiyo, anapokwenda pale anahama na ileile Sh.10,000 yake anaenda kuila akiwa kule kwenye yale mafunzo kwa sababu ukimlipa utakuwa umemlipa *double payment* na kwa mujibu wa sheria za Serikali ni makosa mtu kumlipa malipo mara mbili kwa ajili ya jambo hilohilo. Kwa hiyo, chakula hicho atakula akiwa nyumbani, kwenye mafunzo au akiwa popote. Hiyo ndiyo *PGO* inavyosema na ndiyo sheria ya nchi inavyosema. Sasa kama ni suala la huruma ya kwangu mimi Simbachawene ningesema tu kwamba walipwe lakini sasa ni sheria kwamba amepewa *ration allowance* ataila popote pale atakapokuwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni juu ya kazi ya Jeshi la Polisi na lawama ambazo wamekuwa wakipewa. Nataka niwaambie ndugu zangu, ukiangalia katika takwimu na ukiangalia *level* ya uhalifu katika nchi yetu tuna nafuu kubwa sana. Leo katika hotuba yangu nimesema makosa ya usalama barabarani yamepungua kwa asilimia 36.4 na makosa ya jinai za kawaida yamepungua kwa asilimia 15.9. Hii maana yake ni kwamba vyombo hivi vinafanya kazi vizuri kwa kushirikiana na wadau wengine. Lawama za mtu mmoja-mmoja kwa tabia yake na hulka yake hizo haziwezi kuepukika zipo katika kila sekta. Hawa askari polisi ni binadamu, ni watoto wetu tuliowalea wenyewe na tunawajua wanavyofanana; tunawajua kwa sababu ni ndugu zetu, kwa hiyo, siyo kosa la mtu mmoja lifanye jeshi zima la polisi likawa halina maana.

Mheshimiwa Spika, hapa nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao

kwa kweli mmesema sana juu ya hali za maisha ya vijana hawa wanaofanya kazi nzuri na kwamba zinatakiwa kuboreshwa pengine tutawatoa kwenye utendaji mbovu, mtu anaingia ana -*stress,* anakuja pale badala ya kum-*arrest* mtu vizuri anam-*arrest* vibaya kwa sababu yuko *traumatized* kiasi kwamba akili yake haiko vizuri. Kwa hiyo, tushirikiane kwa pamoja na mimi nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mfano, sisi Jeshi letu la Polisi limejitahidi sana kufanya kazi vizuri kwa kushirikiana na majeshi mengine na wadau wengine. Ukiangalia takwimu, kwa mfano, kuna namna ambayo unaweza uka-*rate* ukaangalia jinai ikoje na makosa yakoje, Kingereza wanasema *incarceration rate. Incarceration rate* ni pale unapohesabu katika *population* ya watu laki moja ni watu wangapi wako magerezani au wamezuiwa wanasubiri aidha kesi au wamehukumiwa.

Sasa ukiangalia Marekani *incarceration rate* ni 727, Kenya 81, Uganda 124, Brazil 193, Tanzania 59. Maana yake katika Watanzania laki moja wanaokuwa wamezuiwa magerezani ni wachache. Hii maana yake ni kwamba vyombo hivi vinafanya kazi nzuri na ndiyo namna pekee ya kuweza kutathmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na nieleze kwamba kwa yale ya marekebisho waliyosema tutaendelea kuchukua hatua kwa wale ambao hawana uadilifu. Mambo yote yanafanyika kwa mujibu wa utaratibu, mtu anapokiuka taratibu kusema kweli tutachukua hatua kali. *IGP* hapa kila siku lazima kuna watu wanakuja ofisini kwangu kukata rufaa amewafukuza. Ukitaka kuwarudisha anakwambia haiwezekani huyu mimi najua hafai kuwa askari polisi. Ninyi wenyewe Wabunge ndiyo mnaonipigia simu Mheshimiwa Mbunge ndugu yangu amekuwa hivi, amekuwa hivi, huku tunakwenda kwa mujibu wa sheria na hili ni jeshi, huku ni *discipline* asilimia 100. Kwa hiyo, tutajitahidi na tutachukua hatua kuhakikisha tunakuwa na jeshi lenye weledi lakini lenye nidhamu pia.

Mheshimiwa Spika, limezungumziwa suala la ucheleweshaji wa malipo ya wastaafu na hapa ni kwa majeshi yote. Nataka niwaambie malipo ya wastaafu sasa hayachelewi sana, kama yanachelewa ni pamoja pia na malipo ya wastaafu wengine. Mimi nizungumzie ile ya kufungasha mizigo na kumrudisha askari aliyestaafu kwao; hii ilikuwa ina tatizo kwa muda wa miaka kadhaa, kwa kweli ilikuwa haijalipwa, lakini Mama yetu Mheshimiwa Rais Samia Hassan Suluhu alipoingia tu kama kuna *document* ya kwanza niliyompelekea ofisini kwake ilikuwa ni kumuomba fedha hizi na sasa ameruhusu na zimeanza kutoka. Uhamiaji wameshapata shilingi milioni 65, Polisi wamepata shilingi bilioni 3 na Magereza wamepata shilingi milioni 812, tumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Sasa tutaanza kuwalipa wale wastaafu ambao walikuwa hawajapewa fedha zao kwa ajili ya kufungasha mizigo na kurudi nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lilizungumzwa jambo ambalo lilikuwa *sensitive* kidogo kwa sababu ni *gender sensitive;* suala la taulo za kike kwa askari na kwa wafungwa. Bado jambo hili si la kukurupuka na kulisemea kwa sababu tukisema kwa askari ambao wana mshahara na wana malipo mengine kama hizo *allowance, ration allowance* na vitu kadhaa, wataibuka na walimu hapa, watasema kwani sisi walimu wa kike hizi taulo na sisi vipi? Kwa hiyo, maeneo mengine na sekta nyingine wataibuka, lakini acha tulichukue kwa sababu ni jambo la *gender* kwa sababu pia kuna jeshi mojawapo hapahapa nchini linafanya hivyo. Tujiulize wenzetu wamefanyaje, wamechukua wapi, basi tutaelewana na tunaweza tukaja na suluhisho lakini ni muhimu zaidi kwa wafungwa magerezani. Kwa wafungwa magerezani hili nadhani tulichukue tuone namna tunavyoweza kuwashirikisha wadau kuweza kutatua tatizo hili kwa sababu wale hawana *alternative means,* wamefungiwa mle hawana njia, asiyekuwa na uwezo anafanyaje? Hili tunalichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ilizungumzwa juu ya *Graduate Sergeant* kufanya kozi ya *graduate. Sergeant* huyu kama ni *graduate* ukienda moja kwa moja ukawa *Inspector* umeruka

sana. Zamani utaratibu ulikuwa ni huu uliorudi sasa wa kwamba lazima apitie kwenye *Sergeant course* ndiyo aende kwenye *Inspector.* Ukimaliza *Sergeant course* siyo mtu mdogo anaongoza askari 30. Kwa hiyo, mimi niseme tu utaratibu huu mpya acha tuuone unavyokwenda, lakini hata watakaokuwa na diploma wanaweza wakafanya hii *Sergeant course* kwa sababu majukumu yale hawezi kushindwa kubeba mtu mwenye diploma. Kama anaweza kubeba mwenye *degree* na mwenye diploma anaweza kubeba.

Mheshimiwa Spika, kwa harakaharaka nizungumzie suala la tozo za zimamoto, ukaguzi wa majanga ya moto na kutoa ithibati. Tozo hii ni kweli imelalamikiwa ni kubwa na Kamati ime-*raise concern* kubwa sana kwamba ukaguzi ukifanywa gharama zile ni kubwa. Tunafikiri na kwa sababu ni suala la Kanuni zilizo chini ya Waziri tutajaribu kuona, tupitie upya, tutashirikiana na Kamati yenyewe ili tuweze kuja na Kanuni rafiki ili tupanue na wigo wa watu wanaoweza kulipa. Hili hatuwezi kulifanya ndani ya mwaka huu, tulifanye kwa mwaka huu kwa ajili ya mwaka wa fedha unaokuja kwa sababu Kanuni za Fedha zinatukatalia.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililozungumzwa ni upekuzi magerezani. Upekuzi huu unafanyika kwa mujibu wa sheria. Kama kuna wanaofanya kinyume na sheria inavyotaka, wanafanya makosa na pale tutakapopata taarifa za malalamiko mahsusi tuna uwezo wa kuchukua hatua kwa wale waliofanya upekuzi huo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililozungumzwa ni suala la Uhamiaji. Uhamiaji na hasa mipakani ambapo wamelalamika sana, niseme tu hata inapozungumzwa habari ya Kitambulisho cha Taifa cha *NIDA* unaweza ukapata kitambulisho lakini bado ukawa...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Waziri anapoongea hapa ni elimu kubwa sana kwenu ambayo itawasaidia hata ninyi kufafanua baadhi ya mambo kwa wananchi. Sasa mtu unakuwa uko hapa hapa unapiga *story* wakati yanatolewa

majibu ambayo ndiyo kero za wananchi, ni vizuri sana mkakaa mkasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, wamesema kwamba maeneo ya mipakani kuna ubaguzi, wanahojiwa waseme nne, waimbe wimbo wa Taifa; hizi ni *technique* tu za kutaka kujua huyu ni nani na huyu ni nani. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wa mikoa ya mipakani tunafahamu kwamba wakati mwingine kati ya nchi hii na nchi hii kutofautisha ni kitu kigumu sana, lakini ni kautaratibu tu fulani siyo *conclusively* kwamba kenyewe kanatosha kuweza kumtia mtu hatiani. Kinachofanyika ni zaidi ya hapo, tunataka kujua pia umezaliwa wapi, wazazi wako walikuwa wapi, hayo tumekuwa tukifanya na ndio kazi ya Idara ya Uhamiaji. Tukifanya hivyo tunagundua kabisa, mtu mwingine anakwambia mimi mama yangu alifia hapa lakini tukienda nchi ya pili tunaenda kukuta mpaka mama yake na kwao mpaka tunajua kila kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya tunayafanya kwa weledi mkubwa na Waheshimiwa Wabunge naomba mtuamini. Kwa sasa tunadhani pengine tukipata vitambulisho hivi vya Taifa ndiyo tumepata uraia wa Tanzania; uraia wa Tanzania una Sheria yake ya Uraia na unamchakato wake. Kitambulisho hiki ni *procedure* tu ya kuwatambua na vinatolewa hata kwa wakimbizi na wahamiaji wa kazi. Kwa hiyo, ukipata kitambulisho hiki siyo muarobaini kwamba wewe umeshamaliza sasa hutaulizwa, hapana! Utaulizwa na utanyang'anywa hata hicho kitambulisho kama umepewa tukigundua kwamba wewe siyo raia wa Tanzania kwa sababu ziko haki za Mtanzania na ziko pia haki za mtu anayeishi Tanzania ambaye siyo raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la *NIDA.* Kwa sasa tulikuwa tunamalizia vitambulisho vya *first generation* kwa maana ya ile *backlog* ya zamani. Ndiyo maana kasi yetu pamoja na kufunga mashine haijawa kubwa kwa sababu kwa sasa tunazalisha vitambulisho kama 32,000 kwa siku. Lengo letu

lilikuwa ni kuzalisha vitambulisho 140,000 kwa siku endapo tungekuwa tunatumia vitambulisho vya *second generation.* Sasa vile vya *first generation* bado tulikuwa na *backlog* ya vitambulisho kama 4,500,000 *(raw card)* ambazo ni lazima tuzimalize, tusipozimaliza ile ni fedha tutapata hasara. Kwa hiyo, mtaona *speed* inasuasua lakini badaye tutatoa vitambulisho kwa *speed* kubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nina uhakika kwamba hadi Julai, August, *backlog* yote iliyokuwepo ya 25,000,000 tutakuwa tumemaliza kabisa. Kwa *target* ya 25,000,000 tumetoa vitambulisho 7,000,000, tuliokwishawatambua ni 18,000,000. Tuna uhakika kazi ya utambuzi kama imefanyika basi kazi ya kufyatua vitambulisho itafanyika kwa *speed.*

Mheshimiwa Spika, changamoto ni nyingi, ukitaka kununua wino mchakato wa manunuzi, ukitaka kununua *raw card* mchakato wa manunuzi, ukitaka kufanya sijui nini mchakato wa manunuzi. Kwa hiyo, michakato hii ya manunuzi ndiyo inayochelewesha mambo kwenda lakini sasa ndiyo sheria za nchi tutafanyaje? Hata hivyo, kwenye eneo hili nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Julai na Agosti watu wote waliokuwa wamechukuliwa alama za vidole, wametambuliwa watakuwa wamepata vitambulisho vyao.

Mheshimiwa Spika, sasa ilielezwa hapa juu ya kadi mbovu 427,000 zilizokuwa zimeonekana wakati Mkaguzi wa Hesabu za Serikali alipopita kwenye Ofisi za *NIDA.* Kadi zile zilikuja mwanzo kabisa wakati *NIDA* haijaanza kuzalisha hata kitambulisho hata hiki kimoja. Walipoangalia *specification* wakaona haziendani na zilizokuwa zimeagizwa, kwa hiyo, mkandarasi akaambiwa kadi zako hizo hatuzitaki, tunazozitaka sisi ni hizi. Kwa hiyo, ilikuwa ni yeye juu yake kuja kuchukua kadi zake kwa sababu hatuzihitaji pale lakini kwa sababu sasa zimeshafutwa kwa mujibu wa sheria na tumeandikiana tayari hakukuwa na mawasiliano mazuri kati ya Ofisi ya *CAG* na Ofisi ya *NIDA* juu ya namna ambavyo zile kadi zilikuwa *abandoned* pale maana hazina *specifications* tunazozihitaji. Kwa hiyo, zinatakiwa hata kuteketezwa yaani

hazihitajiki. Kwa hiyo, eneo hilo ndivyo ambavyo ninaweza kulisemea.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo yamesemwa ni yale ya jumla, kama nilivyosema tutajitahidi kuyafanyia kazi na kuhakikisha kwamba yote yaliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge tunayazingatia. Vinginevyo nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wachangiaji wote, nina vikaratasi hapa vina michango mingi sana lakini niseme tu tutazingatia yale waliyoshauri.

Mheshimiwa Spika, niongelee hili la mradi wa *Dar City,* zile nyumba za Kunduchi na Msasani ambapo Kamati pia na wenyewe walisema. Tulielewana na Kamati, tunamalizia mchakato wa mwisho ili *negotiation* kati ya yule mbia na Serikali uweze kumalizika kwa sababu pale ni kwamba mkataba ule unavunjika. Mnapovunja mkataba kunakuwa kuna mambo mengi, *investment* ile ilikuwa ya miaka 70, *investment* ile ilikuwa ya hela nyingi kwa hiyo, Wizara ya Fedha na Wizara yangu zinaendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba tunamaliza mkataba ule bila Serikali kuingia kwenye kesi mbaya au kuvunja mkataba kwa kukiuka taratibu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru sana wewe na Waheshimiwa Wabunge wote. Nimshukuru Naibu Waziri wangu na Maafisa wote wa vikosi vyote ambao wanafanya kazi kwa karibu sana pamoja na mimi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na kwa kweli imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo ya kujibu hoja, japo ni baadhi tu, nyingine kadiri mtakavyoona mnaweza mkazijibu kimaandishi siku zijazo ili Waheshimiwa Wabunge waweze kupata ufafanuzi wa mambo haya ambayo mengi yake yanawagusa wananchi wetu. Tunakushukuru sana kwa kazi

hiyo uliyofanya ukisaidiana na Mheshimiwa Naibu Waziri. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tuendelee, Katibu.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*........Sh.13,160,145,739

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, mshahara wa Waziri. Tuanze na Mheshimiwa Hamis Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tunamshukuru sana kwa hilo lakini kuna maeneo ambayo hakuyaweka. Sasa inaleta tabu kidogo tunataka tuzuie huu mshahara wake mtani wangu, sina jinsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo kwa mfano kama Sengerema, Wilaya ya Sengerema ina visiwa kama 34, kuna wavuvi wako kule wanafanya kazi zao za uvuvi wanaibiwa nyavu, mashine zao, tumeomba tupate boti kule na tupate Kituo cha Polisi eneo la Kanyara. Mimi binafsi nimejenga Kituo cha Polisi pale Nyakarilo lakini kituo kile hakina vifaa pia hakuna mawasiliano kule ziwani.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mwenyezi Mungu tumepata kituo kingine tumejengewa na Nyanzaga *Gold Mine* tumekabidhiwa juzi. Vituo tunavyovijenga pale kwa

nguvu ya wananchi vipo karibu vitatu lakini hatujaona msaada wowote ambao unakwenda kule kuwasaidia wale polisi waweze kufanya kazi zao. Waziri amesema ana magari 300.

Je, ananihakikishia katika magari haya mapya Sengerema tutapata magari mawili?

Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza lakini la pili...

**MWENYEKITI:** Linakuwa moja tu. Ahsante sana na umeshauliza tayari Mheshimiwa Tabasam. Mheshimiwa Waziri, kama kuna ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Tabasam, tumeongea naye sana na amekuwa akija hapa mezani kwangu mara kwa mara. Magari haya yakitoka tutampatia gari moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, jipongeze Mheshimiwa Tabasam. Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nchi yetu imekuwa ikiheshimu sana mila, tamaduni na desturi za makabila mbalimbali. Kwa mila na desturi za makabila mengi ya wafugaji, kitendo cha mfugaji kuwa na ngoma, mkuki, kuwa na usinga, kuwa na vile vijumba, Wasukuma wanaita *numba ja masamva,* sijui wanasemaje kwa Kiswahili, lakini kuwa na vibuyu ndani ni kitu cha kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwepo *operation* ya Jeshi la Polisi katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa hususan Mkoa wa Geita ambayo imekuwa ikikamata mtu yeyote wanayemkuta aidha ana nguo nyekundu, ana ngoma, ana usinga ambayo inalenga kupiga vita lamri chonganishi. Hata hivyo *operation* hii imeathiri sana wananchi wa Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, mwongozo halisi wa *operation* hii ni upi; na itaisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa suala hilo la Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida, jeshi la Polisi operesheni ndiyo shughuli yake na operesheni hizi huwa zinakuwa zimetafsiriwa vizuri na zinatolewa na *IGP* na imeelezwa sababu ya Operesheni, muda wa Operesheni; nani anafanya nini; na nani anawajibika kwa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji katika maeneo ya Kanda ya Ziwa kwa sababu za visasi na ushirikina, *rate* ni kubwa mno. Tutakuja kuleta uone halafu pengine tushauriane tunafanyaje? Katika kupambana na hali hiyo, ndiyo maana tunazifanya hizi Operesheni. Tunadhani pengine elimu ni jambo moja, lakini pia tukifanya Operesheni hata kama wanapiga ramli hizo na nini; sasa kama imetokea kwa bahati mbaya kulingana na Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba mila na desturi haziepukiki, mtu amevaa usinga, amebeba mkuki, amebeba hengo, hii sidhani kama inaingia huko. Sasa tujaribu kuona tena, nitakaa niongee na Mheshimiwa Mbunge aweze kunieleza vizuri na wataalam wangu, tumsikilize ili tuweze kupata tafsiri ya hicho anachokisema ukilinganisha na Operesheni ambazo tunaendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana pengine wamefanya vijana wetu kule isivyo, lakini bado nachelea kusema, kuna kazi na jukumu kubwa kama Serikali kuhakikisha kwamba tunapunguza mauaji ya namna hiyo katika maeneo ya Kanda ya Ziwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kanyasu kule bado kuna shida mzee, hebu dogo kama unalo.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na nia njema ya Serikali hasa wanapofanya Operesheni katika kudhibiti mauaji. Shida ya Operesheni hii wanapokwenda kule chini, wale Askari wanavyokamata watu, kukamatwa ni bure na kuachiwa ni pesa; na wanakamata ovyo ovyo. Wanakamata mtu wakimkuta nyumbani, anakwambia mimi nina ngoma, wewe ni mchawi, anakamatwa. Matokeo yake watu wanakimbia nyumba. Ila nakubaliana na Operesheni hii na ninaunga mkono kazi ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri amesikia, *IGP* amesikia. Kuanzia Tabora mpaka Mwanza kule Kanda ya Ziwa iko shida. Kuna baadhi ya vijiji; Kijiji kizima kikubwa hakina Kanisa hata moja, wala Msikiti hata mmoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, tutoe wito pia na wenzetu wa madhehebu, hebu wapeleke elimu ya dini, nayo inaweza ikasaidia. Upagani umezidi mno, watu wanauawa sana kwa sababu ya imani za kishirikina. Hili ni jambo la kweli kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndiyo maana Serikali inabidi kwa kweli ikae wima, kwa sababu watani zangu hawa bwana, yaani wakiambiwa tu na wale wapiga ramli za uchonganishi, Ndugai ndio anafanya hivyo, anatoka na panga huko moja kwa moja. Anakuwa na hukumu mkononi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kusema kabisa, nisiporidhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri nitatoa shilingi. Leo wakati nachangia asubuhi, nilielezea ni jinsi gani upekuzi unaofanyika kwenye Magereza zetu nchini, unakiuka haki za binadamu. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hapa amesema tu kiurahisi kwamba ni kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu *ni-quote* tu baadhi ya Ibara za vifungu cha Katiba. Ibara ya 12 kifungu kidogo cha (2) kinatamka: “kila mtu anastahili heshima ya

kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake." Ibara ya 16 kifungu kidogo cha (6)(b), kinatoa marufuku kwa mtu anayeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mkosaji mpaka atakapotiwa hatiani. Ibara ya 13(6)(e) inatoa marufuku kwa mtu yeyote kuteswa, kuathibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha utu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Magereza nyingi nchini, hata kabla mimi sijaenda Segerea, nilikuwa nikipokea malalamiko mengi sana kwa wananchi wa Tarime *by then*, ukaguzi wanaoufanya, wanadhalilisha utu wa binadamu. Nimesema asubuhi hapa, ukiwa Mahabusu, kila unapotoka kwenda Mahakamani na kurudi, unavuliwa nguo zote kama mnyama, yaani kama ulivyozaliwa kutoka kwenye tumbo la mama yako, unakaguliwa. Wakati mwingine wanawake mnaambiwa mruke kichurachura ili waone kama kuna vitu umeweka ndani viweze kudondoka. Ikitokea upo kwenye siku zako, unaamrishwa, ukirukaruka kichura damu zinadondoka, udeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa wanaume, nimekueleza. Siku hizi unaweza ukakamatwa baba, mtoto, mkwelima, mkalundikwa wote kwenye chumba kimoja, mnavuliwa nguo zote kama mlivyozaliwa. Unaamrishwa ujisaidie ili waone kama una kitu umekibeba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni unajua Dhahiri, Ijumaa Mheshimiwa Sendeka alielezea kule Mererani tu; fikiria Magereza yote nchini, naomba Bunge lako Tukufu lielekeze na Mheshimiwa Waziri aji-*commit* tu hapa aidha kufunga mashine ambazo mahabusu wakipita au wafungwa; hata wafungwa wakiwa wanakwenda gengeni na kurudi, *the same* lazima wakaguliwe wakiwa uchi wa mnyama. Mfunge mashine ambazo ukipita zinakuona kama umebeba kitu au hujabeba kitu. *Short of that,* waelekezwe, wakague kwa kufuata utu wa binadamu kuliko wanavyofanya sasa hivi, ni kudhalilisha utu wa binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Serikali kama ile ambayo Waziri Mkuu aliitoa kule Mererani

kwamba watakwenda kufunga mashine ambazo zitakuwa zinakagua mahabusu na wafungwa mara watokapo Gerezani na kurudi, *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaielewa *concerning* ya Mheshimiwa Esther Matiko na pengine ni kwa sababu ya muda tu, lakini nilichosema ni kwamba ukaguzi huu na upekuzi upo kwa mujibu wa sheria; siyo huo anaousema. Huo ni kinyume cha utaratibu. Ni kwamba mtu akikiuka ukaguzi ulioelezwa, kama akifanya hicho unachokisema ni kosa, anatakiwa achukuliwe hatua. Kwa sababu moja kati ya vitu vya msingi kwa Jeshi la Magereza au Magerezani ni usalama, kutokuingia na vitu ambavyo ni hatari. Yaani hilo jambo ni namba moja. Ukaguzi au upekuzi kufanyika ni kitu ambacho kimekuwa kikifanyika miaka na miaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vyumba maalum ambavyo vimewekwa kwa ajili ya kufanyika ukaguzi huo na upekuzi na anapita mtu mmoja mmoja anapekuliwa. Sasa kama kuna dai hilo analolisema, ndiyo maana nikasema wakati na-*wind* hoja yangu kwamba kama kuna dai *specific,* lije tulichunguze lenyewe limefanyika wapi? Lini? Siku hiyo alikuwepo nani? Maana sisi kwenye zamu zetu tunajua kila siku nani yupo na kwa muda gani? Tunajua nani alifanya hivyo na tutachukua hatua kwa sababu atakuwa amekiuka utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane kwamba, sasa kwa kadri ya maendeleo ya kiteknolojia ilipofikia, kupekuana kwa kufanyiana hivyo ambavyo kumefikia kutweza utu na heshima ya binadamu ni vema tukaona kumepitwa na wakati, twende kwenye vifaa vya kisasa, tuweke *spring machine*, halafu ziangalie hata mtu alivyobeba tumboni. Hata hivyo, inahitaji uwekezaji pia. Ila nakubaliana kwamba huko ndiko tunakotakiwa kwenda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, huyo anayeongea ni mzoefu. Anakupa ukweli na nina hakika haokoti haya maneno. Mheshimiwa Esther Matiko. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa sababu mwishoni Mheshimiwa Waziri amemalizia kwa kuweka *commitment* kwamba wanatakiwa waende kwenye ustaarabu zaidi wa kununua mashine. Hata hivyo kiuhalisia Mheshimiwa Waziri nikwambie, siyo kwamba ni *special case* moja au mbili, kwa siku zote miezi minne niliyokaa Segerea, kila nikitoka kwenda Mahakamani Kisutu na kurudi navua nguzo zangu zote.

**MBUNGE FULANI:** Ni Magereza gani?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarime. Hata Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Bulaya; Shinyanga, yeyote akisimama hapa ambaye ameshawahi kwenda Gerezani hata kwa upande wa CCM, Magereza yote nchini wanafanya hivi. Sasa kwa sababu umeji-*commit* kwamba Serikali inakwenda kuangalia, ukisema kwamba ni kinyume, basi miaka yote hiyo wamekuwa wakifanya *practice* ambayo ni kinyume cha Sheria na wanatakiwa Magereza yote wachukuliwe hatua, kwa sababu hii ni *practice* ambayo ipo kila Gereza. Hata leo huko waliporudishwa wafungwa na mahabusu wamefanyiwa hivyo, hapa ninapoongea sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama unaenda kufunga mashine, tu-*budget* kama anavyosema ni uwekezaji, kama nchi tuone sasa ili tusitweze utu wa binadamu tupange bajeti zetu kuhakikisha kwamba tunafunga mashine za kisasa kuondoa hiki kitu ambacho kinafanywa kwa Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa. Baadhi ya haya mambo ukiyasikiliza ni mapokeo ya taratibu za kikoloni. Ni *colonial mind set.* Tangu wakati wa ukoloni, Mwafrika hakuwa na thamani yoyote, kwa sababu hata enzi

hizo, wao kwao huko Uingereza hawakuwa wakiwafanyia watu wao uchi namna hiyo; lakini wakatufanyia hivyo, nasi tulipochukuwa, tumewaangalia wafungwa kama ni *condemned group* au wawekwa mahabusu na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba sana Wizara ya Katiba na Sheria, Mambo ya Ndani na wengine, haya mambo ya *basic human right* lazima tuyaangalie. Maana vinginevyo, tulipata uhuru wa nini sasa kama bado tunapelekana kama kima? Yaani siyo mambo madogo, lazima tuyaangalie, hata kama yana-*cost* lazima Wizara ya Fedha tuangalie, twenda mahali ambapo ni bora zaidi. Kuyasikia haya mara Mererani mara wapi, yaani haituweki mahali pazuri sana, hasa inapokuwa na wanawake nao wanafanyiwa mambo ya namna hiyo, inakuwa *even wise.*

Hata wanaume wenyewe, katika mchanganyiko huo, hata kama siyo mchanganyiko, hii habari kidogo haipendezi. Tunaogopa hata kuendelea kulisemea hili jambo, kwa sababu inabidi tulitazame kwa kweli. Wizara ya Fedha, Mambo ya Ndani wanapaswa kupewa fedha huko mbele. Kabisa! *(Makofi)*

Wanatakiwa wapewe fedha za maendeleo, wana *backlog* kubwa sana kama mlivyosikia Waheshimiwa Wabunge ambavyo wameeleza, kwenye Kitabu cha Maendeleo wanatakiwa wapate fedha ili wa-*revolutionize* vituo vya polisi, maeneo ambayo watu wanakuwa mahabusu, nakadhalika nakadhalika.

Hata *mindset* ya askari wetu, anakamatwa mtu ana anuani, ana heshima zake, lazima apelekwe mahabusu. Sasa hii ni nini? Wakati duniani kote, mtu anakuja, bwana fulani tunakuhitaji. Leo lini? Jumatatu; unaonaje kati ya Alhamisi na Ijumaa ukaja kituoni kati ya saa hizi na saa hizi. *Okay,* mimi nachagua muda huu. Basi vizuri. Siku hiyo mtu atakwenda kituoni, atatoa maelezo yake, kwa sababu ana *address,* atakwenda wapi? Mtu ambaye hana *address* ni suala lingine. Nchi hii bwana, unapigwa mtu yeyote; hata wewe unapigwa

ndani. Sasa kumweka huyu mtu ndani unataka ku-*achieve* nini? Watu wanalundikwa ndani tu, *it is not okay.* Binafsi huwa inaniuma sana. *(Makofi)*

Mimi nimefuatilia sana maisha ya Mandela. Niliwahi kuwasimulia siku moja, kwamba wakati ule karibu anakamatwa, kabla hajapelekwa Robben Island alikuwa kule Rivonia, Umkonto we Sizwe wanajificha wanafanya hujuma usiku na nini, lakini mchana wanakaa kwenye *lunch* na kwenye *lunch* ile yeye anakuwa ni mmoja wa wanaohudumu chakula kwa wale vibarua. Sasa katika kuhudumu chakula kwa wale vibarua, wale vibarua wanapotaka ile huduma kwa akina Mandela hawa, yaani hawawathamini; wewe mpuuzi lete chakula hapa, wewe mjinga nini! Yaani akagundua Waafrika hawathaminiani.

Sasa nikawa nawaza, hivi mimi nawapigania hawa, wao wenyewe hawawathamini wenzao, wana matatizo gani hao? Tuna shida hiyo sana. Yaani kumkamata mtu na kumlundika ndani, tunaona raha tu. Ukishakuwa Polisi unasema tu, nitakuweka ndani! Kweli anakutandika ndani. Unaweza ukakaa wiki au mwezi. *(Makofi)*

Bahati mbaya sheria zetu, hata ukitoka hudai chochote, huna malipo, yaani huna haki tu. Shughuli zako mwezi mzima zimekwama, hamna kinachokwenda; una heshima zako, *it is very embarrassing.* Haya mambo lazima tuyatazame huko mbele ya safari. Hii kuweka weka ndani watu ovyo ovyo hii, siyo sawa; na ukiwa ndani yenyewe ndiyo hiyo uvuliwe na nini, aah, sasa *it is even worse. (Makofi)*

Mheshimiwa Nape Nnauye atakuwa wa mwisho kwenye eneo hili.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano ya kuboresha *Passport* zetu, kwa sababu ni moja ya *Passport* bora kabisa katika ukanda wetu. *Passport* hizi ukiwa unaiomba kwa mara ya kwanza unalipa shilingi 150,000/=,

lakini ikitokea bahati mbaya *passport* hii ikapotea au ikaharibika unatakiwa kulipa shilingi 500,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, *Passport* ni haki ya raia wa Tanzania. Unapoiwekea kiwango cha shilingi 500,000 kuipata *passport* ambayo bahati mbaya labda imepotea au imeharibika, ninadhani ni kuwanyima haki Watanzania kwa sababu gharama hii ni kubwa sana. Kwa hiyo, naomba maelezo ya Waziri kwa sababu hili jambo nadhani ni la kikanuni, siyo sheria. Mheshimiwa Waziri unasemaje kuhusu jambo hili; hamwoni kwamba linanyima haki raia wa Tanzania kupata *passport* zao? Kwa sababu kwa kweli ni haki yao na asipopata, kuna mambo mengi sana anayakosa kama haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Mheshimiwa Waziri atakuwa na maelezo mazuri. Vinginevyo sina haja ya kutoa shilingi, nadhani tuwatetee Watanzania ambao kupata hiyo fedha ya kupata *passport* kwa awamu ya pili inakuwa tatizo kubwa. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi wa hili la *Passport.*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Nape kwamba ikitokea mwananchi mwenye *passport* ya Tanzania ameipoteza *passport* yake, ili kupata *passport* nyingine, utaratibu uliokuwa umewekwa ulikuwa ni shilingi 500,000/=. Hii ina sababu yake. Kulijitokeza *tendence* ya kwamba *passport* zinapotea sana, lakini wengine walikuwa wanaziweka rehani kwa mtu, anamwambia nipe fedha kiasi kadhaa halafu anaiacha *passport* pale, halafu akija huku anaomba *passport* nyingine, anasema tu ile imepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hali ile ilienda enda, lakini bahati mbaya sana ilikuwa inafanywa na vijana wadogo wadogo, siyo watu wazima. Yaani idadi kubwa ni ya vijana wadogo wadogo na unakuta hao ndio wanasafiri *South Africa*, Dubai na wapi. Sasa sitaki kulisema sana kwa

sababu ni jambo la kiusalama pia, lakini lilikuwa lina maana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wenzangu niliowakuta wakaona wafanye bei iwe kubwa kidogo na hali hiyo sasa hivi imepungua sana. Sasa kumbe tunaweza tukaanza, kwa aliyepoteza, labda kuna mtu ameunguliwa na nini, zote hizo *special cases* tunaweza tukaziangalia *differently,* kwamba mtu mzima anatoa maelezo, kwamba bwana nyumba yangu imeungua au nilikuwa nasafiri bahati mbaya niliweka kwenye begi. Maelezo ya mtu mzima yanaeleweka. Kwa sababu ile tuliyokuwa tunai-*cure*, kwa sasa ni kama vile imekuwa haipo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba tunafahamu kwamba hiyo inaweza ikasaidia, lakini *passport* kwa sasa zinapatikana kwa njia nyepesi sana. Unaingia online, una-*apply within* muda mfupi tu umepata *passport* yako na tunatoa kwenye mikoa karibu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna ugumu wa *passport* kwa sasa.

Sasa kumbe tunaweza tukaanza kwa wale waliopoteza kuna mtu kaunguliwa na mambo mengi, yaani zile *specially cases* tunaweza tukaziangalia *differently.* Mtu mzima anatoa maelezo kwamba *passport* yangu imeungua kutokana na nyumba yangu kuungua au nilikuwa nasafiri bahati mbaya niliweka kwenye begi limeibiwa. Maelezo ya mtu mzima yanaeleweka kwa sababu ile tuliyokuwa tunai-*cure* kwa sasa ni kama vile imekuwa haipo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niseme tu kwamba tunafahamu kwamba hii inaweza ikasaidia, lakini *passport* kwasasa zinapatikana kwa njia nyepesi sana, yaani kwa njia nyepesi sana unaingia *online* una-*apply, within* muda mfupi tu umepata *passport* yako na tunatoa kwenye mikoa karibu yote. Kwa hiyo hakuna ugumu wa *passport* kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape umeridhika?

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana na kwa kweli leo tunapongeza kuhusu urahisi wa kupata *passport* siyo kama ilivyokuwa zamani, hapo Wizara mmefanya maendeleo makubwa sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Accounts and Finance Unit*.......Sh. 548,922,000
Kifungu1003 – *Policy and Planning Unit*...........Sh.561,116,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 – *Probation and Community Services*...................................Sh.2,739,583,256

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Liwale

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nipate maelezo kuhusu *sub vote* 22005.

**MWENYEKITI:** 22005 ndiyo, mbona siioni, hii ya kwako mwenyewe, siyo ya Waziri.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** 22005.

**MWENYEKITI:** Haipo. *Sub Vote* ngapi Katibu?

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:** Tuko *sub vote* 1004

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Ni 003.

**MWENYEKITI:** 1004, sasa wewe unasema *twenty* ngapi

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Nimesema 22003

**MWENYEKITI:** 22003 *Fuel, Oil and Lubricants,* haya endelea

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani. Ilikuwa ni...

**MWENYEKITI:** Sawa, umekubali matokeo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*...........................................Sh.224,907,000
Kifungu 1006 – *Management Information System Unit*..............................Sh.381,680,396,000
Kifungu 1007 – *Internal Audit Unit*..........................Sh.229,374,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*.............................................Sh.307,098,000
Kifungu 1009 – *Complaints Division*...................Sh.186,915,000
Kifungu 1010 – *Legal Services Division* ...............Sh.495,342,000
Kifungu 2001 – *Registrar of Societies* ...............Sh.228,048,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 - *Refugees Unit* ..........................Sh.1,118,070,609

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, tafadhali.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimechanganya hicho kifungu nilikuwa na maana kifungu hiki 4001.

**MWENYEKITI:** Lakini nimeshahoji, bahati mbaya nimeshahoji, wameshakubali.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Hakijahojiwa.

**SPIKA:** Ndiyo hiki tulichopo? Haya basi hebu endelea.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Nilikuwa naulizia *sub vote* 22005, miaka miwili yote ilikuwa haijatengewa fedha, lakini naona mwaka huu imetengewa fedha za kutosha, kuna 380,592,000 miaka yote miwili ilikuwa haijatengewa fedha *Military Supply and services.*

**MWENYEKITI:** Ulitakiwa uangalie kwenye randama, yaani swali lako liendane na kwenye randama, uwe umeangalia halafu unatengeneza, kwa sababu maelezo mengi yako kwenye randama.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nipate maelezo hapa, kwa nini miaka ya nyuma hakijatengewa fedha sasa hivi imetengewa fedha?

**MWENYEKITI:** Randama inasemaje? Makatibu mnayo randama? Itatuchukulia muda lakini Waheshimiwa Wabunge ni kwamba unapoangalia kifungu, kwa sababu kifungu hiki hapa kiko kwenye *summary, very summarized* inataja tu *amount,* lakini kwenye randama ndiyo kunakuwa na maelezo ya jambo hilo. Kwa hiyo pale sasa ukioanisha kama kuna swali ndiyo unaweza hasa ukauliza swali. Kwa hiyo kifungu hicho kinaafikiwa. Katibu.

**FUNGU 14 – JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

Kifungu 3001 – *Fire and Rescue Services* … … Sh. 24,685,455,000
Kifungu 3002 – *Fire and Rescue Services Training Institute*..........................................Sh.520,826,000
Kifungu 3003 – *Fire Safety* … … … … … … … … Sh.131,700,000
Kifungu 3004 – *Operations*… … … … … .... Sh.711,173,000
Kifungu 3005 – *Dar es Salaam Regional Office*............................................Sh.632,260,000
Kifungu 3006 – *Arusha Regional Office*..............Sh.469,510,000
Kifungu 3007 – *Dodoma Regional Office*..........Sh.458,960,000
Kifungu 3008 – *Mwanza Regional Office*...........Sh.588,360,000
Kifungu 3009 – *Mbeya Regional Office* ...............Sh.398,760,000
Kifungu 3010 – *Kinondoni Regional Office*........Sh.493,560,000
Kifungu 3011 – Mara Regional Office..................Sh.223,560,000
Kifungu 3012 – *Kigoma Regional Office*............Sh.227,810,000

Kifungu 3013 – *Pwani Regional Office*...............Sh. 545,060,000
Kifungu 3014 - *Manyara Regional Office*..........Sh.268,810,000
Kifungu 3015 – *Geita Regional Office*................Sh.229,660,000
Kifungu 3016 – *Temeke Regional Office*............Sh.666,800,000
Kifungu 3017 – *Singida Regional Office* ............Sh.236,560,000
Kifungu 3018 – *Tabora Regional Office* … … … Sh.339,860,000
Kifungu 3019 – *Iringa Regional Office* … … … … Sh.347,860,000
Kifungu 3020 – *Rukwa Regional Office* … … … …Sh.189,460,000
Kifungu 3021 – *Ruvuma Regional Office* … … … Sh.308,560,000
Kifungu 3022 - *Kagera Regional Office* … … ……Sh.305,360,000
Kifungu 3023 – *Mtwara Regional Office* … … …Sh.301,760,000
Kifungu 3024 – *Lindi Regional Office* … … … … …Sh.282,660,000
Kifungu 3025 – *Njombe Regional Office* … … … Sh.221,160.000
Kifungu 3026 – *Shinyanga Regional Office* … … Sh.306,760,000
Kifungu 3027 - *Ilala Regional Office* … … … … … Sh.638,060,000
Kifungu 3028 – *Kilimanjaro Regional Office* … … Sh.342,060,000
Kifungu 3029 – *Morogoro Regional Office* … … Sh.431,060,000
Kifungu 3030 – *Katavi Regional Office* … … … … Sh.214,560,000
Kifungu 3031 – *Tanga Regional Office* … … … …Sh.482,260,000
Kifungu 3032 – *Simiyu Regional Office* … … … … Sh.187,160,000
Kifungu 3033 – *Songwe Regional Office* … … … Sh.216,199,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**FUNGU 28 – JESHI LA POLISI**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*..........................Sh.59,407,620,000
Kifungu 1002 – *Finance and Logistics* … … Sh.222,657,619,000
Kifungu 1003 – *Internal Monitoring & Evaluation*....................................Sh.181,784,000
Kifungu 1004 – *Legal and Research Services*… …Sh.227,944,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit* … … … …. ...Sh.243,968,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit* … … … … … …… … … ... Sh.270,144,000
Kifungu 2001 - *Police Main Force* … … … … … … … …Sh. 0
Kifungu 2002 – *Police Marine* … … .. … … ... ..Sh.1,403,283,000
Kifungu 2003 – *Railway Police Division* … … …Sh.1,842,652,000
Kifungu 2004 – *Police Signals Branch* … … … … Sh.704,458,000

Kifungu 2005 – *Police Zanzibar* … … … … … … Sh.5,231,792,000
Kifungu 2006 – *Police Airwing* .. … … … … … … Sh.1,717,104,000
Kifungu 2007 – *TAZARA Police* … … … … … … Sh.1,255,956,000
Kifungu 2008 – *Field Force Unit* … … … … … … Sh.5,902,072,000
Kifungu 2009 – *Traffic Police* … … … … .. … … … Sh.886,492,000
Kifungu 2010 – *Police Airport* … … … … … … Sh. 2,462,276,000
Kifungu 2011 - *Police Dog and Horses* … … … Sh. 946,283,000
Kifungu 2012 - *Dar es Salaam Special Zone* … Sh.3,791,440,000
Kifungu 2013 – *Police Ilala* … … … … … … … .. Sh.9,702,168,000
Kifungu 2014 – *Police Kinondoni* … … … … … Sh.14,234,376,000
Kifungu 2015 – *Police Temeke* … … … … …Sh. 7,572,004,000
Kifungu 2016 – *Police Arusha* … … … … ... ...Sh.12,727,802,000
Kifungu 2017 – *Police Iringa* … … … … ..... ...Sh. 7,797,064,000
Kifungu 2018 – *Police Kilimanjaro* … … ..... .. Sh.10,293,522,000
Kifungu 2019 – *Police Kigoma* ...… … … ... ... Sh. 8,502,972,000
Kifungu 2020 – *Police Kagera* … … ... ... ... ...Sh. 9,422,842,000
Kifungu 2021 – *Police Lindi* … … … … ... ... ...Sh. 6,238,262,000
Kifungu 2022 – *Police Mwanza* … … … ... ... .Sh.11,739,812,000
Kifungu 2023 – *Police Mara* … … … …... .... ..Sh. 7,081,606,000
Kifungu 2024 – *Police Tarime-Rorya* … ... ....Sh. 5,420,630,000
Kifungu 2025 – *Police Mbeya* … … … ... .... ...Sh. 9,974,672,000
Kifungu 2026 – *Police Mtwara* … … … ... ... ...Sh. 7,285,945,000
Kifungu 2027 – *Police Morogoro* … … ... ... ... Sh.12,383,698,000
Kifungu 2028 – *Police Manyara* … … ... ... ...Sh. 7,351,958,000
Kifungu 2029 – *Police Singida* … … ... ... ... ...Sh. 7,149,304,000
Kifungu 2030 – *Police Pwani* … … … … … ... Sh. 7,755,820,000
Kifungu 2031 – *Police Ruvuma* … … … … ...Sh. 6,698,112,000
Kifungu 2032 – *Police Rukwa* … … … … ... ..Sh. 5,404,660,000
Kifungu 2033 – *Police Shinganya* …... ... ... ...Sh. 7,431,088,000
Kifungu 2034 – *Police Tabora* … … … … ... ..Sh. 7,386,830,000
Kifungu 2035 – *Police Tanga* … … … … ... ... Sh. 9,854,322,000
Kifungu 2036 – *Police Mjini Magharibi* … ... ...Sh. 9,620,304,000
Kifungu 2037 – *Police Kusini Unguja* … … ... ...Sh. 4,292,424,000
Kifungu 2038 – *Police Kaskazini Unguja* … ... Sh. 3,338,876,000
Kifungu 2039 – *Police Kusini Pemba* … … ... ..Sh. 2,516,280,000
Kifungu 2040 – *Police Kaskazini Pemba* … ... Sh. 2,547,608,000
Kifungu 2041 – *Police Dodoma* … … … ... ..Sh.11,735,390,000
Kifungu 2042 – *Police Geita* … … … … ... ... Sh. 6,567,262,000
Kifungu 2043 – *Police Katavi* … … … … ... ... ... Sh. 4,175,394,000
Kifungu 2044 – *Police Njombe* … … … ...... ...Sh. 5,163,824,000

Kifungu 2045 – *Police Simiyu* ... ... ... ... ... ...Sh. 4,505,824,000
Kifungu 2046 – *Police Songwe* ... ... ...... ... ... Sh.4,170,011,000
Kifungu 2047 – *Police Rufiji* ... ... ... ... ... ... ..Sh. 3,924,616,000
Kifungu 2049 – *Police Bandari* ... ... ...... ... ...Sh. 2,125,670,000
Kifungu 2050 – *Police Band* ... ... ... ... ... ... ...Sh. 1,203,592,000
Kifungu 2051 – *Police Bohari* ... ... ... ... ... ...Sh. 3,067,212,000
Kifungu 3001 – *Police College Moshi*.... .... ....Sh. 3,527,386,000
Kifungu 3002 – *Police College* ... ... ... ... ... ...Sh. 1,806,654,000
Kifungu 3003 – *Operations and Training*............Sh. 981,002,000
Kifungu 3004 – *Zanzibar Police College*..........Sh. 884,109,000
Kifungu 3005 – *Mwanza Marine Police College*...Sh. 420,052,000
Kifungu 3006 – *Tanzania Police Staff College Kidatu*...........................Sh. 773,636,000
Kifungu 4001 – *Police Vehicles Maintenance*......Sh. 950,468,000
Kifungu 5001 – *Police Medical Unit* ... ... ... ....Sh.2,570,947,000
Kifungu 6001 – *Police Ujenzi* ... ... ... ... ...... ... Sh. 564,576,000
Kifungu 7001 – *Criminal Investigation Division*......................................Sh.7,106,070,000
Kifungu 7002 – *Stock Theft Prevention Unit*... Sh. 436,828,000
Kifungu 7003 – *Criminal Intelligence Bureau*... Sh.1,120,566,000
Kifungu 7004 – *Forensic Investigation Bureau*.........................................Sh.2,553,524,000
Kifungu 7005 – *Community Engagement* ... Sh. 876,375,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**FUNGU 29 – JESHI LA MAGEREZA**

Kifungu 1001 – *Prisons Headquarters* ... ... ... ...Sh. 8,159,717,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts* ... ... ... Sh. 2,109,322,000
Kifungu 2001 – *Parole Department* ... ... ... ... Sh. 830,732,000
Kifungu 2002 – *Prisons Welfare and Rehabilitation*........................Sh.148,380,644,000
Kifungu 2003 – *Resettlement of Offenders* ...Sh.4,077,152,000
Kifungu 2004 – *Prisons Arusha* ... ... ... ... ... ... ...Sh.1,005,600,000
Kifungu 2005 - *Prisons Dar es Salaam* ... ... ... ...Sh.2,695,346,000
Kifungu 2006 – *Prisons Dodoma* ... ... ... ... ... ... Sh. 952,068,000
Kifungu 2007 – *Prisons Kigoma* ... ... ... ... ... ... Sh. 616,201,000
Kifungu 2008 – *Prisons Tanga* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 801,600,000

Kifungu 2009 – *Prisons Kagera* … … … … … … Sh. 716,328,000
Kifungu 2010 – *Prisons Mwanza* … … … … ... … Sh.1,054,028,000
Kifungu 2011 – *Prisons Tabora* … … … … … … …Sh. 907,188,000
Kifungu 2012 – *Prisons Mbeya* … … … … … … Sh.1,019,076,000
Kifungu 2013 – *Prisons Singida* … … … … .. … … Sh. 607,354,000
Kifungu 2014 – *Prisons Coast* … … … … … … … Sh. 963,720,000
Kifungu 2015 – *Prisons Lindi* … … … … … … … …Sh. 742,170,000
Kifungu 2016 – *Prisons Manyara* .. … … … … … Sh. 624,966,000
Kifungu 2017 – *Prisons Mtwara* … … … … … … Sh. 701,886,000
Kifungu 2018 – *Prisons Ruvuma* … … … … .. …Sh. 620,408,000
Kifungu 2019 – *Prisons Rukwa* … … … … … .. …Sh. 615,558,000
Kifungu 2020 – *Prisons Mara* … … … … … … …Sh. 640,164,000
Kifungu 2021 – *Prisons Iringa* … … … … … … …Sh. 723,840,000
Kifungu 2022 – *Prisons Kilimanjaro* … … … …Sh. 850,584,000
Kifungu 2023 – *Prisons Morogoro* … … … … …Sh.1,851,128,000
Kifungu 2024 – *Prisons Geita* … … … … … … ..Sh. 29,950,000
Kifungu 2025 – *Prisons Katavi* … … … … … …Sh. 29,950,000
Kifungu 2026 – *Prisons Njombe* … … … … … ..Sh. 29,950,000
Kifungu 2027 – *Prisons Simiyu* … … … … … ... .Sh. 29,950,000
Kifungu 2028 – *Prisons Shinyanga* … … … ... …Sh. 563,110,000
Kifungu 3001 - *Ukonga Prisons Staff College*…Sh.2,747,948,000
Kifungu 3002 - *Kingolwira Prisons Driving School*........................................Sh. 386,236,000
Kifungu 3003 - *Ruanda Prisons Trade School* …Sh. 774,664,000
Kifungu 3004 – *Prisons College Kiwira* … … … ..Sh.1,441,438,000
Kifungu 4001 – *Prisons Building Brigade* … … … Sh.1,079,740,000
Kifungu 4002 – *Prisons Industries* … … … … … …Sh. 383,912,000
Kifungu 4003 – *Prisons Farms* … … … … … … …. Sh. 988,148,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**FUNGU 93 – IDARA YA UHAMIAJI**

Kifungu 2001 – *Immigration Zanzibar* … … … Sh. 6,113,934,000
Kifungu 2002 – *Immigration Headquarters*…Sh.53,132,124,000
Kifungu 2003 – *Immigration Ilala* … … … … ........Sh.32,346,000
Kifungu 2004 – *Tanzania Regional Immigration Training Academy* … … … … ...Sh.508,629,000
Kifungu 2005 – *Immigration Kinondoni* … … … …Sh.32,946,000

Kifungu 2006 - *Immigration Temeke* … … … ……Sh.32,346,000
Kifungu 2007 - *Immigration Arusha* … … … … … Sh.89,880,000
Kifungu 2008 – *Immigration Dar es Salaam* … … Sh.80,750,000
Kifungu 2009 – *Immigration Dodoma* … … … …Sh.74,230,000
Kifungu 2010 – *Immigration Geita* … … … … … Sh.80,180,000
Kifungu 2011 – *Immigration Iringa* … … … …. … Sh.77,030,000
Kifungu 2012 – *Immigration Kilimanjaro* … …... ..Sh.86,230,000
Kifungu 2013 – *Immigration Kigoma* … … … ….Sh.102,773,000
Kifungu 2014 – *Immigration Katavi* … … … … … Sh.78,680,000
Kifungu 2015 – *Immigration Kagera* … … … …Sh.102,430,000
Kifungu 2016 – *Immigration Lindi* … … … … ……Sh.77,380,000
Kifungu 2017 – *Immigration Mwanza* … … … ….Sh.86,230,000
Kifungu 2018 – *Immigration Manyara* … … …... .Sh.77,380,000
Kifungu 2019 – *Immigration Mbeya* … … … … ..Sh.86,230,000
Kifungu 2020 – *Immigration Morogoro* … … ….. Sh.81,080,000
Kifungu 2021 – *Immigration Mtwara* … … … …..Sh.92,230,000
Kifungu 2022 – *Immigration Mara* … … … … ….Sh.90,230,000
Kifungu 2023 – *Immigration Njombe* … … … ….Sh.74,850,000
Kifungu 2024 – *Immigration Pwani* … … … … .. .Sh.87,080,000
Kifungu 2025 – *Immigration Ruvuma* … … … …Sh. 87,080,000
Kifungu 2026 – *Immigration Rukwa* … … … …. ..Sh.87,080,000
Kifungu 2027 – *Immigration Simiyu* … … … … …Sh.72,850,000
Kifungu 2028 – *Immigration Singida* … … … …..Sh.73,480,000
Kifungu 2029 – *Immigration Shinyanga* … … … .Sh.73,480,000
Kifungu 2030 – *Immigration Tanga* … … … … …Sh.87,710,000
Kifungu 2031 – *Immigration Tabora* … … … … …Sh.88,080,000
Kifungu 2032 – *Immigration Songwe* .. … … … …Sh.74,650,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 51 – WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management…* … … … … … Sh.10,080,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 14 - JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI

Kifungu 3001 – *Fire and Rescue Services* … … Sh. 3,500,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 28 – JESHI LA POLISI

Kifungu 2023 – Police Main Force… … … … … … … … … Sh. 0
Kifungu 2025 - Police Zanzibar … … … … … … … … … Sh. 0
Kifungu 2035 – Police Air Wing … … … … … … Sh. 220,000,000
Kifungu 2035 – Police Kagera … … … … … … …Sh. 80,000,000
Kifungu 2023 – Police Mara… … … … … … … …Sh. 450,000,000
Kifungu 2025 - Police Mbeya … … … … … … … … … … …Sh. 0
Kifungu 2035 – Police Tanga … … … … … … … Sh. 250,000,000
Kifungu 2039 – Police Kusini Pemba … … … … Sh. 200,000,000
Kifungu 2040 – Police Kaskazini Pemba … … … …Sh. 150,000,000
Kifungu 2044 – Police Njombe … … … … .. … ….Sh. 650,000,000
Kifungu 2045 – Police Simiyu … … … … … … … … … … .. Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 29 – JESHI LA MAGEREZA

Kifungu 4001 – *Prisons Building Brigade* … … … Sh. 840,000,000
Kifungu 4002 – *Prisons Industries* … … … … … .. Sh. 1,000,000,000
Kifungu 4003 – *Prison Farms* … … … … … … … Sh. 6,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 93 – IDARA YA UHAMIAJI

Kifungu 2002 - *Immigration Headquarters* … …Sh. 4,050,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa tafadhali.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Hivyo, naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa kama ilivyo ada Waheshimiwa Wabunge napaswa kuwahoji kikanuni ili tuweze kuiamulia hoja hii, kwamba sasa Waheshimiwa Wabunge mkubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote wameafiki. Kwa niaba yetu nichukue fursa hii kuwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge wote kuanzia Kamati, mpaka Bunge zima kwa kushiriki katika mchakato huu wa Wizara hii kubwa ambayo tulitakiwa tufanye kwa siku mbili, lakini tumeweza kufanya kwa siku moja. Nasema ahsanteni sana Kamati,

Wabunge wote, lakini kipekee wenzetu ambao wameshughulika na bajeti hii tangu mwanzo; Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake, Wakuu wa Majeshi yetu mbalimbali Jeshi la Polisi, Magereza Uhamiaji, Zimamoto na kadhalika, tunawapongezeni sana wote kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya. *(Makofi)*

Mmeisikia michango ya Wabunge, twende tukajaribu kuyapitia na kuyachanganua yale ambayo yamependekezwa na Waheshimiwa Wabunge na sisi yale ya upande wetu hata ambayo hayakuletwa hapa rasmi lakini tunatakiwa tuyapeleke mbele niwahakikishieni sisi tutayapeleka kwenye mamlaka ili tuweze kuona namna gani ya kuboresha utendaji kazi wa majeshi yetu tunayoyapenda sana.

Nimalizie kwa kusisitiza sana suala zima la haki za binadamu. Tunashughulika na tumepewa mamlaka ya kutumia nguvu, mtu yoyote ukipewa mamlaka ya kutumia nguvu unapaswa kuwa na busara sana katika kutumia nguvu zako hizo, kwa sababu unaweza kuishia kuzitumia nguvu hizo kwa mtu mnyonge, kwa mtu ambaye hana hatia yoyote, hajui tu kujieleza na mambo mengine yanayofafana na haya.

Kwa kweli kama nilivyosema mwanzoni ni mapokeo ya tulivyotawaliwa. Wakati mwingine ile *hangover,* buibui ile ya tulivyotawaliwa, bado inatusumbua mpaka leo, bado waafrika hatuthaminiani. Tunapaswa kuongeza kuthaminiana na *curriculum* yetu tuipeleke mpaka kwenye mashule kule kwa Profesa Ndalichako tuanzie kule kuthamini utu wa mtu ipande, isonge, iende mbele kabisa. Itatusaidia katika mambo mengi, siyo tu Polisi, Magereza na kadhalika, hata katika maisha yetu ya kawaida.

Unapofanya maamuzi fulani lazima kutazama na utu wa mtu yule na kadhalika. Tuchukuliane kama wenzetu huko duniani wanavyochukuliana na kadhalika. Jambazi achukuliwe kama jambazi, jangili achukuliwe kama jangili, lakini binadamu na watu walio wengi ambao ni raia wa

kawaida kundi baya sana huwa ni asilimia moja au mbili lakini kundi kubwa amekosea, amevunja sheria kwa kujua au kwa kutokujua, lakini bado ni binadamu ambaye anarekebika na ziko namna za kuwarekebisha.

Pia mazingira ya Magereza na nini, iko kila sababu tuboreshe. Zile imani za zamani kwamba magereza hakupaswi kuboreshwa kwa sababu ni mahali ambapo watu wanakwenda kuadhibiwa, nadhani tutoke huko, kule nako wanakaa binadamu, hawakai wanyama wa porini na hata kwenye *National Park* wanakokaa wanyama wa porini tunaboresha mazingira. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sisi Wabunge tunapata nafasi ya kutembelea magereza yetu na Wabunge ambao hamjui *right* hiyo kwenye majimbo yenu ni vizuri mkafahamu lakini kuna utaratibu. Unafuata utaratibu unaihusisha Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, *DAS* na wengine, ni Afisa Magereza anapata taarifa unaandaliwa, siku ya siku unakwenda, unafika unakagua, unaona hali halisi ya mambo ilivyo, inasaidia sana katika kuweza kushauri au kuchukua hatua mbalimbali za kusaidia kuboresha hali. *(Makofi)*

Wale Maaskari Magereza wameachwa sana, ni Jeshi moja ambalo lina askari wenye nidhamu sana, hata wakipewa vifaa, toa magari kwa wakati mmoja Polisi na Magereza, Magereza watayatunza kwa miaka 20 au zaidi. Wanatunza sana vifaa, wanafanya kazi katika mazingira magumu. Unajua askari magereza anafanya kazi utafikiri naye mfungwa, maana kama kwenye mvua na yeye kwenye mvua; kama kwenye jua na yeye kwenye jua. Kama sijui nini na yeye yuko pale pale na zile tofauti ndogo ndogo za kati ya Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza na hata za majeshi, si vizuri sana tukaziendekeza, wengine wakawa wana-*feel* wana fedha za taulo za kike, ndani ya majeshi hayo hayo, lakini wengine hawastahili kuwa nayo, ndani ya majeshi hayo hayo, inakuwa haipendezi. *(Makofi)*

Hawa wote ni muhimu kwa Taifa letu, tujitahidi tunapowapa *services* tuwape wote. Sasa raia naye akidai

hiyo, tutamuuliza wewe tatizo lako ni nini. Haya ni mambo ya majeshi, kule kuna kwata na kadhalika. Nafikiri tutaelewana tu. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ni watu waelewa sana muende mkaangalie *possibility* ya vitu hivi, ni motisha fulani fulani, unajua Jeshini kuna motisha motisha zake, mojawapo ndiyo hizo.

Waheshimiwa Wabunge tunawatakia kila la kheri watu wa Mambo ya Ndani, mwendelee kufanya kazi yenu nzuri ambayo mnaendelea kuifanya mpaka sasa. Hizi lawama ndogo ndogo zisiwavunje moyo, ni sehemu ya kazi yenu. Sasa mkiona mmekosa lawama kabisa, basi sasa labda mmekuwa likizo, lakini kazi yenu *nature* yake lazima utapata lawama ya hapa na pale. Mjue mna mtihani huo kwamba mnapofanya yale na ubinadamu nao kwa kiasi kikubwa sana uweze kuingia katika utendaji wa kazi zenu.

Baada ya kufikia hapo, basi shughuli zimekamilika za siku ya leo, kwa hiyo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 4 Mei, 2021, Saa 3.00 Asubuhi)*